Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 20 Julai, 2012

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):-

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Shirika la Elimu Kibaha kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2011 *(The Annual Report and Audited Accounts of Kibaha Education Centre for the Financial Year ended 30th June, 2011).*

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:-

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka 2012/2013.

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa fedha 2012/2013.

MHE. ALLY S. AHMED (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):-

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka 2011/2012 Pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

MHE. ROSE K. SUKUM (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):-

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Juu ya Wizara ya Kilimo Chukula na Ushirika Kuhusu Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 226

Kubadili Muundo wa Kamati ya Ukaguzi ya Halmashauri

MHE. ANDREW J. CHENGE (K.n.y. MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE) aliuliza:-

Halmashauri za Wilaya/Miji zimekuwa zikishindwa kudhibiti Matumizi ya fedha za maendeleo kutokana na muundo mzima wa Kamati ya Ukaguzi (*Audit Committee*).

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati wa kubadili muundo wa Kamati hizo kwa kushirikisha hata Madiwani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati za Ukaguzi *(Audit Committees)* katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaundwa kwa mwongozo wenye kumb. Na. CHA/3/215/01 uliotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI mwezi Novemba, 2007.

Kamati hizi zina wajumbe watano wakiwemo wajumbe wawili kutokana na Wakuu wa Idara, wajumbe wawili kutoka nje ya Halmashauri katika Idara au taasisi na Mwanasheria ndiye Katibu wa Kamati. Mwenyekiti wa Kamati anatokana na Mkuu wa Idara isiyokuwa na manunuzi makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyoonekana katika muundo wake, ni kweli kwamba Kamati hii haishikirishi Waheshimiwa Madiwani kwa kuwa inaundwa na wataalam pekee. Hata hivyo Kamati kupitia kwa Afisa Masuhuli, ina wajibu wa kuwasilisha taarifa yake kwenye kikao cha Kamati ya Fedha na Mipango kwenye Halmashauri za Wilaya na Kamati ya Fedha na Uongozi kwenye Halmashauri za Miji ambapo Waheshimiwa Madiwani ni wajumbe.

Kwa jinsi hiyo Serikali inaamini kuwa Waheshimiwa Madiwani wanashirikishwa kikamilifu katika utendaji wa Kamati ya Ukaguzi kwa kupelekewa taarifa na kuijadili.

Aidha Waheshimiwa Madiwani wanayo fursa ya kujadili taarifa ya Mkaguzi wa ndani wa hesabu ambayo huwasilishwa kwenye Baraza la Madiwani kila baada ya miezi mitatu kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaamini kwamba Wahesimiwa Madiwani bado wana nafasi kubwa ya kudhibiti matumizi ya fedha na mali nyingine za Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Kamati ya Fedha na Kamati nyingine za kudumu. Majukumu ya Kamati ya Ukaguzi ni sehemu tu ya majukumu ya Kamati ya Fedha kama yalivyoainishwa katika

Memoranda ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1997, Agizo namba 3.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Waheshimiwa Madiwani waendelee kuwa katika nafasi nzuri ya kusimamia na kuhoji utekelezaji wa shughuli za Halmashauri si vema wao kuwa sehemu ya Kamati ya Ukaguz ya Halmashauri kutokana na ukweli kwamba wao ni chombo cha usimamizi na maamuzi kuhusu masuala yote yanayohusu Halmashauri zao.

Aidha kila Diwani anayo nafasi ya kukagua Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa katika Kata yake ili kuhakikisha kwamba thamani ya fedha katika miradi hiyo inakuwepo.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda niulize swali moja tu la nyongeza. Mwaka jana Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Manunuzi ya Umma na ililetwa na Serikali hapa kwa nia njema sana na moja ya mapendekezo ambayo Bunge lako lilifanya ni kwamba kwa kutambua Kamati kama hii ya *Audit Committee* na zile zinazoshughulikia manunuzi, Madiwani si wajumbe lakini Bunge lilipendekeza kwamba yafanywe marekebisho ili kabla ya mikataba yoyote ya manunuzi kufanyika pawepo na fursa ya Kamati ya Fedha na Uchumi na Mipango iweze kuyapitia hayo.

Je, swali langu kama Serikali iliona umuhimu wa Muswada huo mbona Muswada huo haujaanza kutumika ili na Kanuni zile zinapaswa kutumika ili na

Kanuni zile ambazo zinapashwa kufanyika na tuanze kuona utaratibu huo sasa hivi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, anachosema Mheshimiwa Andrew Chenge ni kweli. Nilitaka niwaweke katika *historical perspective* ya jambo hili. Wakati wa hii Sheria ilipopitishwa hapa ililetwa na Mheshimiwa Mstaafa Mkulo yeye ndiye aliileta hapa na tukazungumzia haya yote wakati AG alipokuja hapa akitaka kupitisha hapa *under miscellaneous amendment* ikawa imeonakana haikupitia katika mikondo ikaondoka na wakati ule tulikuwa na majukumu mengi hapa ya kufanya ikaonekana kwamba ije baadaye ikaja baadaye.

Baadaye ikaja ikapitishwa hapa. Mle ndani inasema Waziri wa Fedha in *collaboration* na Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa watatengeneza Kanuni na ndipo hapo swali lake linakuja na niko *conscience* kabisa na Mheshimiwa Chenge anachokisema ni kweli.

Hii Kanuni ilikuwa inasema huwezi ukaingia katika manunuzi ukaruhusu kupitia zile Kamati za zabuni na hii Kamati unayosema hapa bila kuipitisha katika Kamati ya Fedha na badae *full council* ikapita. Kwa maneno mengine ni kwamba wakishapitishwa wale wazabuni huwezi ukaenda ukakuta kijiko kwenye kata kinafanya kazi kule halafu unasema eti mmesha-*award.* Ndicho anachokisema hapa, tukasema ipite.

Sasa Kanuni hizo zimeshaandaliwa na tunakubaliana na Mheshimiwa Chenge kwamba iko hapa ya *operationalize* hii habari inayozungumzwa hapa wala tusiwe na wasiwasi hili jambo lilishakuja na Mheshimiwa AG alishalileta hapa mmeshapitisha kwa hiyo sasa ni kazi ya kuhakikisha kwamba hii Sheria inavyofanya kazi kama Mheshimiwa Chenge anavyoshauri

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameona umuhimu wa Kamati ya Fedha kushiriki katika Mipango ya Maendeleo na kwa kuwa Wabunge wa Viti Maalum ni Madiwani.

Je, Serikali itaangalia lini utaratibu wa Wabunge wa Viti Maalum kushiriki katika Kamati ya Mipango na Fedha katika maeneo yao kwa kuwa suala hili limekuwa likizungumzwa mara kwa mara na Mheshimiwa Waziri Mkuu alilitolea maelezo kwamba hakuna tatizo. Mheshimiwa Waziri mwenyewe alishawahi kuzungumzia umuhimu huo, lakini utekelezaji wake unasuasua. Ni lini sasa utakamilisha kanuni ili tuweze kushiriki Wabunge wa Viti Maalum katika Kamati ya Mipango na Fedha?

NAIBU SPIKA: Swali lilihusu *Audit Committee,* lakini Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Chiku Abwao kwa kutambua kwamba tuliwahi kulisemea jambo hili. Mimi niliwahi kusimama hapa nikasema nimezaliwa na mama na mke wangu ni mama. Kwa hiyo najua umuhimu na wala hapa sitaki kuzua mgogoro hapa tukaanza kushindana hapa umuhumi wa hawa. Mimi natambua akinamama wana umuhimu mkubwa sana katika taifa. Jana ameondoka Mheshimiwa Rais wa Liberia mwanamama, amekuja hapa tumemwona wote mizinga 21 amepigiwa pale. Kwa hiyo natambua umuhimu wao na Chama changu cha Mapinduzi kinawatambua akinamama.

Tulipokuwa tunajibu jambo hili tulisema kabisa kwamba Mbunge huyu wa namna hii kwa sababu ni wa Mkoa walau achague Halmashauri moja ambayo angetaka ashiriki. Kwa sababu hawezi akawa anatoka Rombo, anakwenda Siha anakwenda kule, anakwenda Same pamoja na kwamba anawahudumia wananchi. Ikasemwa kwa uzito mkubwa sana baadaye Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu limekuwa linajitokeza akalibeba yeye mwenyewe.

Sasa hebu jiulize Waziri Mkuu na mimi nani mkubwa? Yaani mimi nianze kukataa hapa, Waziri Mkuu alishasema analibeba na mimi nikisema nikujibu kwamba sasa tayari imekuwa, ataniambia bwana mdogo hii habari umeipata wapi. *(Makofi/Kicheko)*

Nataka nithibitishe kwako hapa kwamba jambo hili Mheshimiwa Waziri Mkuu amelichukua kwa uzito mkubwa. Kwa hiyo anaendelea kulifanyiwa kazi, tunaiona hiyo *concern* na haya mabadiliko ambayo yanatokea na nadhani kwamba tutafika mahali tutalitatua. Kwa hiyo tunakaribisha wazo hili na tunawatambua akinamama. *(Makofi)*

Na. 227

Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2012/2013

MHE. FELISTER A. BURA (K.n.y. MHE. JENISTA J. MHAGAMA) aliuliza:-

Tarehe 24/4/2012 wakati Wabunge wakijadili Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2012/2013, moja ya mambo yaliyojitokeza ni pamoja na haja ya kufundisha matumizi ya teknolojia katika uzalishaji wa chakula ili kupunguza mfumuko wa bei na njaa.

Je, ni shughuli gani zilizopangwa kufanyika katika Mpango kwenye eneo hilo kwa mwaka 2013/2014?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa elimu bora ya kilimo cha kisasa, utumiaji wa mbegu bora za kisasa pamoja na utumiaji wa zana bora za kilimo za kisasa ni baadhi tu ya maeneo yanayoongeza uzalishaji ikiwa ni pamoja na kuimarisha na kuboresha hifadhi ya chakula. Hivyo basi, kwa kuzingatia umuhimu huo, shughuli zilizopangwa kufanyika katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2012/2013 pamoja na matumizi ya teknolojia ili kukidhi azma hii, ni pamoja na:-

(a) Kupongeza kiwango cha mikopo kwa wanafunzi watakaodahiliwa katika vyuo vikuu kwa mchepuo wa uhandisi wa maji na kilimo cha umwagiliaji na uchunguzi wa hali ya hewa.

(b) Kuongeza mgao wa Bajeti wa shughuli za utafiti na uzalishaji wa mbegu bora.

(c) Kwa kushirikiana na wawekezaji binafsi katika Ukanda maalum wa Kilimo wa Kusini mwa Tanzania SAGCOT, kutoa elimu mahususi kwa wakulima walio katika makubaliano/mikataba ya kilimo cha mpunga, miwa na kadhalika.

(d) Kusaidia shughuli za taasisi za ubunifu na uendelezaji wa zana za kilimo na viwanda hususani, *CAMARTEC, TEMDO, SIDO* na Nyumba.

(e) Kuongeza mafunzo kwa ajili ya kujenga uwezo wa kutathmini na kusimamia athari za kimazingira na mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini kadhaa zilizofanyika zinabainisha kuwepo kwa uhusiano chanya kati ya mfumuko wa bei na kuyumba kwa upatikanaji wa chakula hapa nchini. Pale upatikanaji wa chakula unapopungua mfumuko wa bei huongezeka mara moja. Kutokana na hali hii, baadhi ya shughuli nilizozitaja na nyinginezo utekelezaji wake utawezesha kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula na hatimaye kudhibiti mfumuko wa bei.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja ya nyongeza. Nia ya Serikali yetu ni kila kaya ijitosheleze kwa chakula kwa kipindi cha mwaka mzima.

Je, wananchi wa Tanzania wameandaliwaje kupokea huo mpango wa kuhakikisha kwamba wakulima wote wanatumia pembejeo za kisasa hasa mbegu bora na mbolea katika ukulima na kuhakikisha kwamba wananchi wote wanajitosheleza kwa chakula kwa kipindi chote. Wananchi wameandaliwaje kutumia teknolojia hiyo mpya?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU: Mheshimiwa Spika, kwanza wakulima wote wanatambua ya kwamba wanaowajibu wa kuhakikisha kwamba wanalima na kupata chakula cha kutosha kwa ajili ya maisha yao kwa mwaka mzima. Matatizo ambayo huikumba nchi mara nyingi huwa yanatokana na ukame hasa katika maeneo ambayo si maalum sana kwa uzalishaji wa chakula hali ya hewa ikiwa nzuri wakulima hulima na kupata ziada kidogo

kwa ajili ya maisha yao. Maandalizi ni kuwafanya wakulima wote wajue wajibu wao huo.

Lakini inapotokea matatizo yanakuwepo ya upungufu wa chakula ndiyo hifadhi ya chakula hulazimika kutoa chakula katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa na kupeleka katika maeneo yenye uzalishaji mdogo.

Lakini Mpango wa Maendeleo unasisitiza juu ya ukuzaji wa kilimo kwa kutumia umwagiliaji. Hapo utakapofika hapo kama nchi tutaweza kusema tunaweza sasa kujitosheleza kwa chakula bila kuwepo matatizo makubwa kama inavyotokea sasa.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Peramiho na wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla wao, wanaelewa sana kwamba Serikali inajitahidi kuhakikisha nchi hii inajitosheleza kwa chakula kwa kupitia kilimo cha mazao ya chakula kama vile mahindi yanyolimwa sana katika Jimbo la Peramiho na kwa kuwa mara nyingi Serikali imekuwa ikitoa matamko mbalimbali yanayozuia wananchi hawa wasiuze mazao yao nje na kusababisha tatizo kubwa sana la soko.

Je, Serikali haioni kupitia dhana hii ya mpango kukubali ombi la wananchi wa Jimbo la Peramiho kuweka katika mpango maalumu wa Serikali kujenga soko kubwa la Kimataifa mpakani mwa Tanzania na Msumbiji ili wananchi waweze kuzalisha kwa wingi chakula kwa ajili ya kuhifadhi kwa matumizi ya nchi

lakini vilevile kwa kupata fedha kwa kukiuza chakula kwa utaratibu rasmi nje ya nchi, kupitia mpaka wa Tanzania na Msumbiji ndani ya mpaka wa Tanzania na Msumbuji ndani ya Peramiho?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza wazo la kuwa na masoko ya Kimataifa kwa ajili ya kuwa na biashara halali mpakani ni jambo linalokubalika.

Kinachobakia ni utekelezaji wake kwa kufuata uwezo unaokuwepo kupanga ni kuchagua tunaanza kujenga mahali pengine lakini ninaamini kwamba kwa uhusiano uliopo kati ya Msumbiji na Tanzania katika mpaka unapakana na Peramiho suala hilo linaweza kutiwa maanani, lakini suala la msingi ninaloweza kusisitiza hapa ni kwamba Serikali haina Sera ya kudumu ya kusema ni lazima wakulima wasiuze nje. Kinachogomba hapa ni kwamba una ziada kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine inakuwa ni kweli kuna tatizo kubwa la nchi ina upungufu na wakati uleule chakula kinauzwa nje. Lakini kama Waziri anayesimamia mpango mimi ninachosisitiza ni kwamba tuongeze uzalishaji ili tuwe sehemu ya soko na tusiwe sehemu ya soko la chakula badala yake tuwe ni sehemu ya wauzaji wa chakula katika masoko yanayotuzunguka. Kwa sababu nchi zote zinazotuzunguka zina upungufu wa ardhi isipokuwa Tanzania. *(Makofi)*

Na. 228

Kunusuru Kiwanda cha Kukoboa Kahawa – Kilimanjaro

MHE. BETTY ELIEZER MACHANGU aliuliza:-

Kiwanda cha kukoboa Kahawa cha Kilimanjaro kimekuwa hakijiendeshi kwa ufanisi na kinakabiliwa na deni la zaidi ya shs. 700,000,000/=.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukinusuru kiwanda hicho kinachokabiliwa na uchakavu wa mitambo na madeni?

(b) Je, Serikali inasaidiaje kiwanda hicho ili kimilikiwe na wanaushirika wenyewe ili kulinda maslahi yao na pato la Taifa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha *Tanzania Coffee Curing Company LTD. (TCCCO LTD.)* kilichoko Moshi, kinakabiliwa na madeni yanayofikia kiasi cha sh 737,223,137.7 yanayotokana na madeni ya gharama za uendeshaji kutokana na kiasi kidogo cha kahawa inayokobolewa na kiwanda hicho pamoja na uchakavu wa mitambo ambayo teknolojia yake imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshauriana na wanahisa wa Kiwanda hicho hususan Umoja wa Vyama vya Ushirika kwa upande mmoja na Umoja wa Wakulima wakubwa wa kahawa kwa upande mwingine ili kufanya tathimini ya mkakati wa muda wa kati na mrefu wa uwekezaji *(Medium and Long term STARTEGIC Finance and Investment Plan)* ili kubaini na kupendekeza hatua za kuchukua ili kukinusuru kiwanda hiki kinachokabiliwa na matatizo ya uendeshaji na uzalishaji kutokana na uchakavu wa mitambo na madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia tathimini hiyo Serikali kwa kushirikiana na wana hisa ambao wengi wao ni Vyama vya Ushirika inaangalia uwezekano kununua mitambo mipya ya kisasa ambayo itakuwa na gharama nafuu za uendeshaji kwa ama, kukopa benki au kuuza baadhi ya mali za kudumu ambazo hazitumiki na kiwanda hicho ili kupata mtaji wa fedha za kuanza kulipa deni linalokikabili.

Jumla ya mahitaji ya shilingi bilioni 1.3 zinahitajika kwa upande wa mtaji wa kuwekeza *re- investment* na shilingi milioni 750 kwa ajili ya kulipia madeni. Aidha, mkutano wa wadau uliofanyika mwaka 2011 tayari ulitoa maamuzi ya nini kifanyike na tumepokea taarifa kwamba mawasiliano na mabenki na taasisi zingine za fedha yameanza kufanyika ili kupata mkopo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wamiliki wa kiwanda hicho wengi wao ni Vyama vya Ushirika kwa asilimia 69 na *Tanzania Coffee Growers Association (TCGA)* kwa asilimia 31, Serikali inawashauri washirika

hao kuangalia uwezekano wa kununua hisa zaidi kutoka kwa *TCGA.*

Aidha, endapo watao na inafaa kubadili muundo wa umiliki uliopo na kukubaliana kumilikisha wanaushirika wenyewe kwa namna watakavyoona inafaa. Serikali haitakuwa na pingamizi kwa makubaliano yoyote watakayoafikiana. Hivyo kunahitajika mfumo wenye uwezo na uzoefu tofauti katika uzalishaji na uendeshaji bora na wenye ufanisi zaidi. Ukiwa na mitambo na usimamizi wa rasilimali na unaozingatia kanuni bora za kibiashara na kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kusaidia uzalishaji na uendeshaji wa vyama vya Ushirika kwa kutumia idara ya maendeleo ya Ushirika ambayo inakuwa na jukumu la kutoa utalaamu, usahuri na ukaguzi wa vyama hivyo ili kujiendesha kwa faida na kwa maslahi ya wanachama wa vyama hivyo. *(Makofi)*

MHE. BETTY E. MACHANGU: Mheshimiwa Naibu Spika, uhai wa viwanda vya kusindika na kukoboa kahawa unategemea sana uzalishaji wa kutosha wa kahawa. Kwa kuwa kwa sasa hivi kuna mwamko unaoendelea kujengeka wa kulima kahawa kutokana na Sera ya mwaka 2009 ilipitishwa na Bunge lako Tukufu na mkakati wa mwaka 2010/2020.

Kwa kuwa, kahawa inaliingizia Taifa hili takribani Shilingi bilioni 170 kama fedha za kigeni na nchi yetu ya Tanzania ina hekta milioni 400.8 ambazo zinaweza kuoteshwa kahawa na katika hizo hekta milioni 400 ni

hekta laki mbili tu zinatumika kwa hivi sasa kuotesha zao la kahawa.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza zao hili la kahawa ili kuinua pato la Taifa lakini pia kusaidia hivi viwanda visiendelee kufanya kazi chini ya kiwango kwa ajili ya matumizi bora ya viwanda hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, mwaka jana tulipata *barcode* ya nchi yetu ya Tanzania. Je, tangu tumepata *barcode* ya Tanzania viwanda vyetu vya *TANICA* na *TANCRIF* zina mabadiliko gani ya mauzo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ametaka kujua Serikali ina mkakati gani wa kuongeza ufanisi katika zao la kahawa hapa nchini.

Tumekuwa tukilizungumzia hili mara kwa mara na ninadhani moja katika mambo yote ambayo tunafanya kwa mazao yote ya biashahara na hata ya chakula ni kuongeza uwezo wa *agro processing* ndani ya nchi kwa maana ya uwezo wa kukoboa na kadhalika. Ndani ya nchi kwa sababu kwa sasa hivi Vyama vya Ushirika vingi tunatengeneza mkakati ili waweze kuwa na uwezo zaidi wa kufanya *curing.* Kwa kurejea suala hili la kiwanda hiki kilikuwa na uwezo wa kukoboa tani mpaka 50,000 kwa mwaka mmoja, lakini kwa sasa hivi kinakoboa tani chini ya 5,000 kwa mwaka mmoja. Kwa hivi majuzi walikoboa kama tani 3,000 tu hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *you can see the defference.* Unaweza kuona tofauti kubwa ya uwezo wa kiwanda na kinachofanya sasa. Hii ni hali inayojitokeza katika hali ya ukoboaji kwa maeneo yote ambayo yanaweza kuhamasisha soko kwa maana ya zao la kahawa. Kwa hiyo, mkakati ni kuongeza uwezo kwa kuviwezesha vyama vya Ushirika na wadau wengine kukopa ili kuboresha mitambo ya ukoboaji na kadhalika.

Katika zao la kahawa, hili la pili la *barcode* kwenye viwanda viwili vya uzalishaji naomba nirejee na suala hili tutalijibu wakati tunajibu hoja za Wizara yetu ambayo tunajibu leo kama tulivyowasilisha Randama na hotuba asubuhi ili tuweze kulijibu suala hili kwa uhakika na ufanisi zaidi. *(Makofi)*

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kuwa mwaka 1998 na 1999 kulikuwa na mdororo mkubwa wa uchumi na matatizo yaliyo katika kiwanda hiki cha kukoboa kahawa Moshi yanatokana na mdororo wa uchumi wa miaka mitatu (3) iliyopita ni pamoja na Chama Kikuu cha *KNCU* kinadaiwa shilingi bilioni 1.3.

Lakini Serikali ikaamua kwamba vyama vikuu vitafidiwa na kama *KNCU* ingefidiwa ingeweza kusaidia kiwanda cha kukoboa kahawa lakini waliopata fidia walikuwa ni wakulima wa pamba walipata fidia kutokana na mdororo wa uchumi na juzi hapa hata rafiki zangu Wamasai walifidiwa ng'ombe kutokana na hali mbaya ya hewa. Naomba kuiuliza Serikali hilo fungu la kufidiwa Chama Kikuu cha *KNCU* - Kilimanjaro

ili kiweze kusaidia kiwanda cha kukoboa kahawa, fidia hiyo itatoka lini na kama haitoki hamwoni kuwa mnatubagua? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, mdororo wa uchumi wa mwaka 2008 Tanzania ikiwa nchi tunayotegemea sana mauzo ya mazao ya kilimo yaliathiri siyo zao la kahawa tu. Yaliathiri pia zao la pamba, yalithiri kahawa, ule mpango wa Benki Kuu na Wizara ya Fedha ya kujaribu kuweka fidia kwenye zao hili haukukusudia kuondoa hasara yote iliyopatikana kwasababu hasara yote iliyopatikana ilikuwa inakwenda kwenye matrilioni na mdororo wa uchumi haukuathiri katika sekta ya kilimo peke yake. Uliathiri sekta zote, mimi ninavyofahamu ni kwamba fidia ile ilijaribu kwenda kwenye maeneo mbalimbali. Mheshimiwa Augustine Mrema, anasema kwamba kwenye Chama Kikuu cha *KNCU* haujafika.

Nilivyomwelewa ni kwamba ile fidia haikwenda kabisa naomba kwa ridhaa yako tukubaliane kwa sababu suala hili linahitaji majibu ya uhakika zaidi tuwasiliane na wenzetu wa Wizara ya Fedha na Benki Kuu ili tukupatie majibu ya uhakika. Tujue *what happened* lakini kwa ufahamu wangu ni kwamba kadri inavyowezekana pesa ile ilisambazwa japo kidogo kidogo kwa maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

MHE. ZITTO Z. KABWE: Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa kahawa wa Mkoa wa Kigoma kwa miaka mitatu mfululizo wanaongoza kwa kupata bei kubwa zaidi ya kahawa kuliko wengine wote Tanzania nzima

na kahawa ya Kigoma ndiyo ambayo imekuwa kahawa bora Kusini mwa Jangwa la Sahara katika kipindi cha miaka mitatu (3) iliyopita.

Lakini kuna tatizo kubwa sana ambapo kuna wanunuzi wa kahawa kutoka Mkoa wa Kigoma ambao wanasafirisha kahawa kabla haijakobolewa kuipeleka Kilimanjaro wakati pale Kigoma katika Kijiji cha Matazyo kuna kiwanda cha kukoboa kahawa, kiwanda cha Kanyovu. Nilikuwa ninaomba kauli ya Serikali kuhusiana na tatizo hili kwa sababu Waziri analifahamu.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yote sahihi kabisa lakini pia naomba na mimi nijipongeze maana Mkoa wa Kigoma tumefanya vizuri kwenye kahawa kama anavyosema Mheshimiwa Kbwe Zitto.

Ninachojua mimi ni kwamba kule Manyovu na maeneo yote yanayolima kahawa hata kule kwangu Kakonko tumeweka *CPUs* Sera zetu ni kwamba mazao yote tuyaongezee thamani kabla hayajauzwa. Kwa hiyo, kama kuna mtu anayebadilisha tena kwamba iuzwe ile kahawa ikiwa haijakobolewa hayo ni mambo ambayo ni ya kujitafutia tu kupata bei au kumlalia mkulima. Bado maelekezo yetu ni palepale kwamba kahawa ile ikobolewe ikipelekwa kule iende kuuzwa ikiwa imekobolewa. *(Makofi)*

Na. 229

Matrekta ya Kilimo Nchini

MHE. IGNAS A. MALOCHA aliuliza:-

(a) Je, Serikali iliingiza matrekta mangapi kupitia Wakala wake wa SUMA JKT na ni muda gani umepita tangu matrekta hayo yaingizwe nchini?

(b) Je, hadi sasa ni matrekta mangapi yamenunuliwa na wakulima?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a) na(b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wake SUMA JKT iliingiza nchini jumla ya matrekta 1,860. Matrekta hayo yalitolewa Bandarini mnamo tarehe 1 Novemba, 2010.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa matrekta wa SUMA JKT ulilenga kusaidia jitihada za Serikali kuongeza uzalishaji kwenye sekta ya kilimo na hasa uliwalenga wakulima wadogo wasiokuwa na uwezo wa kununua matrekta wenyewe.

Kutokana na lengo hilo, matrekta haya yanauzwa moja kwa moja kwa mkulima. Hadi sasa jumla ya matrekta 786 yamenunuliwa na wakulima. Vituo vya kuuza matrekta 424 yana ahadi kununuliwa na yaliyobaki yanatarajiwa kuwa yameuzwa ifikapo Desemba, 2012.

MHE. IGNUS A. MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Wakati Serikali ilipoingiza matrekta kwa maana ya *power tiller* ilijitahidi sana kuyasambaza hayo matrekta hadi kwenye *scheme* za umwagiliaji na vikundi vya SACCOS kwa nini Serikali isifanye kazi hiyo nzuri kusambaza pia matrekta ya SUMA JKT ili kuongeza uzalishaji katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ni lini Serikali itasogeza matrekta ya SUMA JKT katika Mkoa wa Rukwa ili kuwapunguzia wakulima wa Mkoa huu gharama ya kuyafuata huku na ukizingatia kwamba Mkoa wa Rukwa ni Mkoa mzuri sana wa uzalishaji?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nitambue mchango mkubwa unaotolewa na Wabunge wa Mkoa wa Rukwa na Jumamosi tulikuwa huko mimi na baadhi ya Mawaziri wenzangu *precisely* kwa ajili kuongea na wananchi kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya sekta ya kilimo.

Katika Mikoa ambayo imeonekana inataka kuchangamkia sana *mechanization* kwa maana ya matumizi ya matrekta na *Power Tillers* kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa kilimo Mkoa wa Rukwa na Katavi. Pia kuna mchango mkubwa wa viongozi wa Mkoa pamoja na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, *geographically* utaona SUMA JKT imegawa vituo baina ya Dodoma, Mwanza, Arusha na Mbeya. Kituo kingine kimefunguliwqa juzi tu, Mkoani Ruvuma, mjini Songea.

Naomba niseme kuwa palepale Rukwa tuliambiwa kuna mahitaji ya matrekta kama 80. Kwa hiyo, tumemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Rukwa na Mkuu wa Mkoa wa Katavi na Ma-*RAS* wao wawasiliane na Halmashauri kujua kuwa ni kiasi gani Halmashauri hizi zimefikia utayari ule wa kumiliki matrekta haya na mimi naomba nikuhakikishie kwenye Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itafanya kila utaratibu ili pamoja na mikakati iliyofanywa ya kupunguza gharama za kukopa trekta hizi, trekta zenyewe zifikishwe Mkoa wa Rukwa ili iwe rahisi zaidi kutekeleza azma hii ya wakulima.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge ninawaona lakini tukumbuke kuwa leo ndiyo siku ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Naomba tuvumilie maswali yetu tuyapeleke mbele kidogo. Tuendelee na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Na. 230

Ugonjwa wa Malaria Nchini

MHE. HOROUB MUHAMMED SHAMIS aliuliza**:-**

Mwanzoni mwa mwezi Februari, 2012, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alipewa tunzo nchini Ethiopia kwa Tanzania kufanikiwa kutokomeza Malaria.

(a) Je, taasisi gani na nchi gani iliyofanya tathmini na kuonyesha kuwa ugonjwa wa malaria umepungua kwa kiasi cha nchi kupewa tunzo?

(b) Je, hivi sasa ugonjwa huo upo kwa kiwango gani nchini?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Horoub Mohamed Shamis, Mbunge wa Chonga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni moja ya nchi saba Barani Afrika, zilizopata Tuzo ya heshima iliyotolewa na taasisi ya Umoja wa Viongozi wa Afrika wanaoshughulikia mapambano dhidi ya Malaria *(African Leaders Malaria Alliance (ALMA).*

Nchi nyingine ni Benin,Cameroon, Kenya, Rwanda, Burundi na Msumbiji. Tuzo hii inatolewa na taasisi ya

ALMA, kwa nchi ambazo viongozi wao wameonesha jitihada binafsi na Serikali wanazoziongoza katika kutekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na tatizo la Malaria katika nchi zao.

Tathmini hiyo inahusisha kuangalia kiwango cha utekelezaji wa viwango 14 vilivyowekwa, ambavyo ni pamoja na ugawaji wa vyandarua vyenye dawa, *(LLINs),* upuliziaji wa dawa ukoko ndani ya nyumba *(IRS),* kwa maeneo yenye uambukizo mkubwa, uwepo wa vipimo wa kuchunguza uwepo wa vimelea vya malaria kwa kutumia vipimo vya kutoa majibu haraka *(MRDT),* uwepo wa dawa ya mseto kutibu Malaria *(ACTs),* kiwango cha chanjo kwa watoto na asilimia ya wajawazito waliojifungua katika vituo vya huduma. Aidha, Mheshimiwa Rais pia alipata tuzo yeye binafsi kama Mwenyekiti mwanzilishi wa Taasisi ya Umoja wa Viongozi wa Afrika wanaoshughulikia mapambano dhidi ya Malaria (*ALMA*).

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali yetu, inaonesha malaria kupungua. Takwimu za matukio *incidence* ya Malaraia yamepungua kutoka 317 mwaka 2004 hadi 288 mwaka 2010 kwa kila watu 1000. Katika kipindi hicho pia idadi ya vifo vinavyotokana na Malaria vimepungua kutoka vifo 53 mwaka 2004 hadi vifo 29 mwaka 2010 kwa kila watu 100,000.

Taarifa ya utekelezaji wa mikakati ya kudhibiti Malaria *Tanzania Progress and Impact Report* imeonesha kuwa udhibiti wa Malaria ni mojawapo ya hatua mbali mbali zinazotekelezwa nchini ambazo

zimechangia katika kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano kwa zaidi ya asilimia 45 kutoka vifo 147 kwa mwaka 1999 hadi vifi 81 mwaka 2010 kwa kila watu 1000.

MHE. SAID SULEIMAN SAID: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Hapa nchini kuna utafiti unaendelea juu ya chanjo ya Malaria ambayo inalenga kukinga maambukizi ya ugonjwa huu.

(a) Je, ni hatua gani imefikia chanjo hiyo?

(b) Ni lini chanjo hiyo itakuwa tayari kutumika hapa nchini?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tafiti ya chanjo kwa ajili ya Malaria imekuwa ikifanyika hapa nchini pamoja na nchi mbalimbali za Afrika na matokeo yake yanaonesha kwamba chanjo hiyo iko katika kuweza kusaidia kupunguza au kuondoa maambukizi kwa awamu ya kwanza kwa zaidi ya asilimia 53 katika kipindi cha mwaka wa kwanza wa chanjo. Baada ya mwaka wa kwanza asilimia inaongezeka kufikia asilimia 61.6. Hivi sasa imo katika hatua ile ya tatu ya utafiti na itakapokuwa imekamilika basi tutakamilisha mapokezi yake baada ya kupata taratibu zote za kuidhinishiwa ili kuanza kutumika ikiwa imeshathibitika kutokuwa na matatizo yeyote kwa binadamu.

Na. 231

Barabara ya Singida –Ilongero-Ikhanoda

MHE. DIANA M. CHILOLO aliuliza:-

Wakati wa kampeni za Rais mwaka 2010 Rais aliahidi kutoa kipaumbele cha kujenga kwa kiwango cha lami barabara kuanzia Singida Mjini –Ilongero hadi Ikhanoda yenye urefu wa kilomita 38:-

Je, Serikali itakuwa tayari kutenga fedha za ujenzi kuanzia kwenye Bajeti ya mwaka 2012/2013?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Singida Mjini –Ilongero hadi Ikhanoda kilomita 38 ni barabara ya Mkoa na inahudumiwa na Wizara yangu kupitia wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatarajia kutenga fedha za kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara ya kutoka Singida Mjini –Ilongero hadi Ikhanoda kilomita 38 kwa kiwango cha lami mwaka 2013/2014.

Kutokana na ukosefu wa fedha hatukuweza kupanga mwaka 2012/2013. Hata hivyo, barabara hii imetengewa shilingi milioni 508.69 katika mwaka huu wa fedha 2012/2013 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ili ipitike mwaka mzima.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswlai mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, ahadi za Rais ni nyingi sana karibu Majimbo yote nchini, Je Serikali itakuwa tayari kutoa ratiba kwa Wabunge ili Wabunge wote wajue miradi iliyoahidiwa na Rais utekelezaji wake ni lini ili kuondokana na usumbufu wa kuwauliza Mwaziri kila siku?

(b) Kwa kuwa pia, ndani ya Mkoa wa Singida kuna barabara ya Sibiti-Katara inayounganisha Mikoa mitatu kwa maana ya Singida, Shinyanga na Arusha ilipandishwa daraja mwaka 2009 kuwa barabara ya Kitaifa.

Je Serikali itakuwa tayari kuiingiza barabara hii katika mpango wa kutengeneza kwa kiwango cha lami, kwa kuwa barabara hiyo imepita eneo lenye maji sana kiasi kwamba kwa utaratibu wa kutengenezwa kiwango cha changarawe itatumia gharama kubwa ya Serikali na ufumbuzi kamili utakuwa bado haujapatikana?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ahadi za Rais ni nyingi na pia katika Ilani ya Uchaguzi tumeorodhesha barabara nyingi ambazo tuliahidi wakati tunaomba kura. Suala la kutoa ratiba tunaliingiza kwenye mpango wa kila mwaka na ninaahidi kama Serikali kwamba ahadi za Rais na zile za Ilani ya Uchaguzi zote tunazitekeleza katika miaka mitano. Ahadi yangu ni kwamba tutazimaliza katika miaka mitano ambayo tupo madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara anayoizungumza kwamba imepandishwa daraja kuwa barabara ya Mkoa, kama tulivyosema kwenye sera ni kwamba kwanza nchi hii ni kubwa na barabara zipo nyingi, kuna barabara Kuu na barabara za Mikoa. Tunasema barabara za lami kwanza tumalize barabara kuu zinazounganisha mikoa ndiyo *priority* ya kwanza, baada ya pale tutaanza kuingia kwenye barabara za mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Chilolo avute subira tukimaliza barabara Kuu tutaanza barabara za Mikoa.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swlai dogo la nyongeza;

Kwa kuwa, barabara ya Mbande, Kongwa, Mpwapwa ipo kwenye ahadi ya Rais, na barabara hiyo inaunganisha Mkoa wa Dodoma na Iringa kwa upande wa kusini, ninaomba kujua ni lini sasa ahadi hiyo ambayo inaunganisha Wilaya mbili na Mkoa wa

Iringa itatimizwa maana ni ahadi ya Rais wakati wa kampeni?

NAIBU SPIKA: Majibu mengine Naibu Waziri unakuwa makini zaidi.(*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa makini kwa sababu najua Kongwa ndiyo anakotoka Naibu Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kabisa barabara hii tumeitolea ahadi kwamba tutaitengeneza kwa kiwango cha lami, na kwenye bajeti yetu tumeonesha mambo ya awali kama usanifu tutaanza kwenye Bajeti ya mwaka 2012/13 barabara ya Mbande, Kongwa hadi Mpwapwa.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, wananchi wa Kongwa mmesikia.

Na. 232

Serikali Kuanzisha Viwanda vipya vya Chakula

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU aliuliza:-

Je, ni hasara gani Serikali itapata kwa kuanzisha viwanda vipya hususan viwanda vya chakula baada ya sekta binafsi kuonyesha kushindwa?

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haitapata hasara kwa kuanzisha viwanda vipya kwa ajili ya uzalishaji wa chakula. Aidha, ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali ilijitoa katika uendeshaji wa moja kwa moja wa kufanya biashara na uanzishaji wa viwanda na badala yake jukumu hilo liliachiwa sekta binafsi ambayo ndiyo injini ya kukuza uchumi katika nchi yetu. Kazi ya Serikali ni kuhamasisha na kuweka mazingira mazuri ya kibiashara kwa ajili ya kuvutia wawekezaji katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta binafsi haijashindwa kuwekeza na kuanzisha viwanda vipya vya chakula hapa nchini. Hii inadhihirishwa na tathmini ya viwanda iliyofanyika mwaka 2009 ambayo ilionnyesha kuwa sekta ya usindikaji wa vyakula nchini imekuwa na idadi ya viwanda 189 kati ya viwanda 729 vilivyofanyiwa tathmini. Aidha, jumla ya miradi 495 imeshapewa leseni za kuanzisha viwanda na wakala wa usajili wa biashara na leseni (*BRELA)* kati ya mwaka 2005 na 2011.

Mhehsimiwa Spika, sera ya nchi kwa sasa ni kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda vya kusindika vyakula ili kuongeza thamani na kuondokana na uuzaji wa mazao yetu yakiwa ghafi.

Kwa kufanya hivyo, kutasaidia wakulima na wafanyabiashara wetu kuuza kwa faida na kujiongezea kipato na kukuza uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wote kushirikiana na Serikali katika kuhamasisha Halmashauri za Wilaya kutenga maeneo maalum kwa ajili ya viwanda vya chakula na kunadi fursa zilizopo katika maeneo yao kwa wawekezaji wa ndani na nje. Aidha, endapo katika Wilaya ya Kilwa Kaskazini kuna miradi ambayo sekta binafsi imeshindwa kuendeleza, namwomba Mheshimiwa Mbunge atutaarifu ili tuweze kunadi miradi hiyo kupitia vituo vyetu vya uwekezaji vya *TIC* na *EPZA*. *(Makofi)*

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru. Napenda kusema kwamba majibu ya Waziri hayawiani sana na swali ambalo nimeliuliza, ningependa nimwuulize maswali kadhaa ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri ya kusema kwamba sekta binafsi imeshindwa ni kwa maana kwamba sekta binafsi haimpi unafuu mwananchi na viwanda vingi ambavyo vimezungumziwa hata kwa takwimu ambazo Waziri ameitoa hapa kwamba vimebinafsishwa lakini vimeshindwa kufanyakazi. Mfumuko wa bei ni mkubwa na matatizo ya chakula ni makubwa sana. Mfano huu wa Serikali kutokushiriki kwenye biashara sijui umechukuliwa nchi gani duniani. Kwa sababu tunajua kabisa jambo muhimu kwa mwananchi ni chakula.

(a) Je, ni lini Serikali itafikiria kurejesha upya viwanda muhimu vya vyakula kwa mfano *NFRA* kwa nini wasipewe uwezo kwa kushirikiana na Bodi ya mazao mchanganyiko wakaanza uzalishaji wa chakula ili kumpa unafuu mwananchi?

(b) Tumesema kwamba Halmashauri zitenge maeneo, kutenga maeneo peke yake siyo tija, ni lini Serikali itawezesha Halmashauri zifanye *feasibility study* katika maeneo yao kutengeneza writeup na wao wawe wanauza miradi badala ya kutangaza tu maeneo, kwani kutangaza maeneo imeshaonesha haileti tija yeyote?

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, leo ni Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika mtachangia zaidi. Majibu Waziri.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa kwamba Serikali ijitoe katika uendeshaji wa viwanda na shughuli za biashara ulifanyika katika sheria ambayo tuliitunga hapa Bungeni mwaka 1992. Uamuzi huo kama tutatakiwa kuurudia tena maana yake ni kwamba sheria ile ni lazima iletwe hapa tuifanyie marekebisho.

Lakini jambo la msingi ni kwamba katika nchi nyingi, Serikali inajiondoa katika uzalishaji wa viwanda na kufanya biashara na badala yake inazingatia zaidi uboreshaji wa mazingira mazuri ya wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu ya Tanzania imekuwa ikiangalia karibu maeneo manne au matano katika kuweka mazingira mazuri ya biashara.

Kwanza ni kupunguza gharama za uzalishaji. Hili linaendelea na mkakati wa kuboresha miundombinu tumefanya taratibu za uandikishaji na uanzishaji wa viwanda kukua haraka. Tumeruhusu sekta binafsi kuwa na sauti kubwa kupitia *TCCIA, TSPF, CTI*. Lakini vile vile Serikali inajitahidi kuweka mawanda mazuri ya kodi na tozo ili kuzifanya kodi na tozo ziwe wezeshi badala ya kukwamisha uanzishwaji wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile Mbunge anafahamu kwamba tunayo sekta nzima ya uwezeshaji ukijumlisha *TIC* yenyewe na *EPZA*. Kwa hiyo jambo la msingi ni kwamba Serikali ni lazima iendelee na mazingira ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pili; Halmashauri za Wilaya tumeziagiza zitenge maeneo ili kuvutia wawekezaji na Wizara yangu kupitia *SIDO* na taasisi zingine tumekuwa tukishirikiana na Halmashauri hizi katika kuandika feasibility study hizo na hatimaye mfano mzuri ni Wilaya ya Himo tunashirikiana nao sasa ili kulifanya soko lile liwe la Kimataifa na kupata hadhi ya *EPZA*. Kwa hiyo, hayo ndiyo Serikali inafanya sasa hivi.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda tuendelee na swali linalofuata ambalo tutakubaliana ndiyo swali muhimu kweli kwa siku ya leo. *(Makofi)*

Na. 233

Kuzama kwa Meli ya Spice Islander

MHE. YAHYA KASSIM ISSA (K.n.y. MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR) aliuliza:-

Ajali ya Meli ya *Spice Islander* iliyotokea Nungwi imedhihisha kuwa Serikali haina vifaa na meli za kisasa kukabiliana na majanga yanayoweza kujitokeza Baharini, kwa mfano vifaa na zana zilizopelekwa kwa ajili ya kuokoa watu zilichukua muda mrefu sana kufika eneo la tukio.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na majanga ya baharini pindi yanavyotokea?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuunda kikosi maalum cha uokoaji Baharini?

NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla kujibu swali la Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mbunge wa Mfenesini, naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa Watanzania wote kwa msiba uliolikumba Taifa letu kwa ajali ya kupinduka na kuzama kwa meli ya *MV*

Skagit iliyotokea juzi tarehe 18 Julai, 2012 wakati inakaribia kufika katika bandari ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajali hii imeleta maafa na majonzi makubwa kwa Taifa na familia za Watanzania. Tunawapa pole wote ambao wamepoteza ndugu na rafiki zao na tunamwomba Mwenyezi Mungu awape nguvu na mioyo ya subira na uvumilivu katika kipindi hiki kigumu cha majonzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009, Serikali kupitia *SUMATRA* ilianzisha kituo cha utafutaji na uokoaji cha Dar es Salaam kwa ajili ya kuokoa maisha pindi ajali zinapotokea majini. Moja ya kazi kubwa za kituo hicho ni kupokea taarifa za ajali na kuratibu utafutaji na uokoaji wa watu waliopatwa na majanga ya ajali. Kituo hutoa taarifa muhimu za ajali kwa vyombo vya ulinzi na usalama au vyombo vingine vilivyoko karibu na eneo la tukio ili kutoa huduma ya uokozi wa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pindi vipokeapo taarifa hizo, vyombo hivyo ikiwemo Kamandi ya Jeshi la Wanamaji, Polisi Wanamaji, *KMKM*, Mamlaka ya usimamizi wa Bandari *TPA,* Shirika la Bandari Zanzibar (*ZPC*) na kadhalika, huchukua hatua za utafutaji na uokoaji.

Aidha, chini ya vipengele vya sheria ya Usafiri Majini ya mwaka 2003, meli yoyote ya Tanzania iwapo karibu na tukio la ajali hupaswa kufanya kazi ya utafutaji na uokoaji mara ipatapo taarifa za ajali. Kwa utaratibu huo huo, meli za nchi nyingine zilizo karibu na ajali huwajibika kutoa msaada. Katika ajali zilizotokea katika nchi yetu, vyombo vya ulinzi na usalama, meli na hata vyombo vya uvuvi vimehusika sana katika kazi ya kuokoa maisha ya watu. Kwa kutumia utaratibu huu, kwa mfano, jumla ya watu 4,207 waliookolewa katika kipindi cha kuanzia mwezi Machi, 2009 hadi Mei, 2012.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza utaratibu wa kuandaa sheria ya utafutaji na uokoaji *(Search and Rescue Bill*) na mpango wa Kitaifa wa utafutaji na uokoaji *(National Search and Rescue Plan).* Kupitia sheria na mpango huo, Serikali itazingatia hoja ya Mheshimiwa Mbunge ya kuunda kikosi maalum cha uokoaji baharini.

Hata hivyo, ni muhimu kukumbuka kuwa si rahisi kuwa na kikosi kimoja ambacho kitaweza kuwa maeneo yote ya nchi yetu kikitoa huduma ya uokozi. Hii ni kutokana na ukubwa wa nchi na hasa eneo la maji. Aidha, suala hili linahitaji kuangaliwa kwa umakini hasa ikizingatiwa kuwa litahusu mabadiliko ya kisheria na muundo wa ulinzi katika Bahari na Maziwa ya Tanzania.

NAIBU SPIKA: Sasa hili swali Bunge zima limesimama. (*Kicheko*)

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali ina watendaji wa kuangalia hali ya hewa, uangalizi wa idadi wa abiria na kadhalika.

(a) Je, Serikali haioni kutokuwajibika kwa wahusika dhamana zao ndio inasababisha ajali hizi?

(b) Je, kwa ajali ya meli ya *Spice Ilender* hatua gani za kisheria zimechukuliwa na kufikiwa kwa wahusika kutokana na uzembe uliofanyika na kusababisha vifo vya wananchi? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kila mtendaji anayo dhamana kwa kazi aliyopangiwa kufanya. Niombe tu kutumia nafasi hii kusema kwamba majanga haya ambayo yamekuwa yanatokea yanafuatiliwa kwa karibu na nilihakikishie Bunge lako tukufu kwamba kila mmoja atabeba mzigo wake na atawajibika ipasavyo kwa omission yoyote ukiachilia mbali *natural causes* ambazo zinaweza kuwa zimesababisha ajali hizi. Kwa hiyo, tutakapowasilisha rescue bill tutaweka humo vipengele vyote ambavyo vitakuwa vinawawajibisha ipasavyo watendaji wenye dhamana kuhusiana na mambo haya.

Kuhusu meli ya *Spice Islanders* uchunguzi ulifanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu chanzo cha ajali hiyo. Wale walionekana kuhusika kwa namna moja au nyingine kwa uzembe au kutotekeleza wajibu wao wote wamekwishafikishwa mahakamani na sheria inachukua mkondo wake. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa umuhimu wa swali hili nitaweka maswali matatu madogo ya nyongeza kama ifuatavyo. Ataanza Kiongozi wa Upinzani, atafuata Mheshimiwa Mbatia na swali la mwisho litakuwa la Mheshimiwa Nundu. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na matukio ya maafa yanayotokana na ajali baharini na hii ajali ambayo imetokea juzi imetokea ndani ya mwaka mmoja toka ajali ya mwanzo itokee na hatuoni uwajibikaji wa aina yoyote ile wa Serikali na siku zote kumekuwa na tume ambayo Serikali imeunda na hakuna kauli au mijadala ambayo inafanyika katika chombo cha uwakilishi wa wananchi kama Bunge.

Je, ni lini Serikali italeta mjadala kuhusiana na ajali ambazo zinatokea na kuchukua uhai wa wananchi wetu hapa Bungeni ili tujadili na kuisimamia Serikali na kuweza kuchukua hatua dhidi ya viongozi wote wanaohusika na sekta hizo? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, kama ifuatavyo:-

Matukio haya ya maafa kwa sheria tulizonazo yanao utaratibu wake wa kufuatiliwa. Kwa maana hiyo, ajali zote zilizotokea ziliundiwa Tume na mapendekezo ya Tume hizi yalifikishwa Serikalini na Serikali ikachukua hatua stahiki. Wanaokuwa

wamevunja sheria mahali pekee pa kuwapeleka ni mahakamani na jambo hilo limekuwa linafanyika.

Lakini kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi iko haja sasa ya kuleta sheria ambayo itaweka utaratibu sasa wa kisheria wa kutafuta na kuokoa watu wanaofikwa na ajali za majini, angani au nchi kavu. Hili tutawasilisha *bill* hiyo mwezi Februari mwaka kesho, 2013. (*Makofi*)

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa ni-*declare interest* kwamba nina taaluma kidogo katika masuala ya majanga. Kwa kuwa inaonyesha kwamba kuna udhaifu mkubwa sana katika kitengo hiki cha kupambana na majanga na kwa kuwa lengo la saba la *millennia* la *sustainability* na *environment protection Tanzania* ni nchi mojawapo tutajieleza mwaka 2015 kwamba tumelitekeleza kwa kiasi gani?

Kwa kuwa udhaifu huu upo na ni changamoto kubwa ukiangalia ajali iliyotokea tarehe 10 mwezi 9 mwaka jana na hii iliyotokea juzi tarehe 18 na uhai wa mwanadamu huwezi ukauweka kwenye thamani ya fedha.

Je, Serikali iko tayari kwa gharama yoyote ile hata kama ni kukopa kwenye taasisi za kifedha hata kama ni nje ya nchi yetu ili tuweze tukakamilisha kitengo hiki ili uhai wa Tanzania na siyo kwenye meli tu hata kwenye mabasi, kwenye ndege na vyombo vile ambavyo vinapoteza uhai wa mwanadamu ili tuweze

tukavipunguza kwa kiasi kikubwa ili tuweze tukafikia vizuri kwenye lengo la 7 la *millennia* ifikapo mwaka 2015? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika malengo ya millennia iko hiyo *component* ya uokoaji wa watu katika majanga mbalimbali. Niseme tu kwamba hadi sasa kituo cha uokoaji na utafutaji kilichopo Dar es Salaam (MRCC) kinafanya kazi ingawa siyo kwa kiwango ambacho tungetarajia kwa sababu baadhi ya vyombo ambavyo vinapaswa kuwepo katika kituo hicho bado havijapatikana.

Kituo kingine kilitarajiwa kujengwa huko Mwanza eneo limeshapatikana lakini ujenzi haujaanza kwa sababu wale wafadhili waliokuwa wameahidi kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho hawajatupatia fedha. Nikubaliane tu na Mheshimiwa Mbatia kwamba yako mapungufu katika kitengo hiki ambacho naamini Serikali inaendelea kuyafanyia kazi lakini dawa ipo kwanza katika kuwajibishana wale wenye dhamana sasa wafanye kazi yao vizuri yaani isiwe tu kisingizio kwamba hatuna vifaa kwa hiyo hata kazi ambayo ungeifanya kwa kutokuwa na vifaa uache kuifanya kwa sababu unasubiria vifaa. Hili tunalichukua na tunalifanyia kazi. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, nadhani Mheshimiwa Mbatia alitaka kujua jitihada za Serikali katika kuimarisha kitengo

kinachoratibu masuala ya maafa. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbatia kwamba tunayo sheria ya maafa ambayo imepitishwa na Bunge.

Lakini kwa upande wa Zanzibar vile vile wanayo sheria yao. Sheria ambayo imepitishwa na Bunge hili tumegundua kweli inayo mapungufu kwa sababu kitengo cha maafa hakiwezi kujitegemea chenyewe kwa maafa yote kwa sababu *players* ni wengi, lazima kuwe na zimamoto, *rescue* sijui marine. Kwa hiyo, hawa ni *coordinator*.

Lakini sheria hii haikuwapa nafasi na mamlaka ya kusimamia vyombo vingine wakati inapotokea maafa. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbatia hilo tumeliona kwamba hata sheria yenyewe inayosimamia kitengo hiki ni dhaifu. Hivi sasa tunakamilisha marekebisho ambayo tutayaleta hapa Bungeni ili Sheria hii na kitengo hiki kiwe na mamlaka kamili na uwezo wa ku-coordinate kazi mbalimbali ya vitengo na players mbalimbali ambao wanapaswa kusimamia masuala ya maafa. (*Makofi*)

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa ni dhahiri usimamizi na udhibiti wa usafiri wa majini ni suala la usalama na maisha ya wananchi hivyo basi linahitaji wadhibiti weledi na wa kutosha. Pia kuwe na mfumo ambao ni mtiririko unaohusisha nchi nzima. Je, kwa nini Serikali hizi mbili zisifikirie kuwa na mamlaka moja ya kushughulikia suala la usafiri wa

majini badala ya ilivyo sasa ambapo kuna mamlaka mbili tofauti. Moja ya Tanzania Bara na nyingine ya Zanzibar. Mfano kama huo upo tayari kwenye usafiri wa anga tuna mamlaka moja tu inayoshughulikia na haishii hapo katika kuangalia, tunajitayarishaje kabla hayajatokea lakini pia inatuhusisha kwenye uhusiano wetu wa shughuli hizi katika ngazi ya kimataifa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Nundu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi mwaka 2006 suala la usimamizi wa mambo ya marine lilikuwa moja kati ya pande mbili hizi za Muungano. Tulikuwa na sheria ya *Merchant Shipping Act* ya mwaka 2003 ambayo ilitengenezwa kwa ushiriki wa pande zote mbili za Muungano lakini baadaye Serikali ya Mapinduzi Zanzibar mwaka 2006 iliona iko haja ya kutekeleza baadhi ya masharti ya mikataba ambayo imeingiwa kati ya Tanzania na Mashirika ya Kimataifa na hivyo wakaanzisha sheria ya mambo ya Bahari ya Zanzibar ya mwaka 2006 *(The Maritime Transport Act)* ya Zanzibar ya mwaka 2006.

Niseme tu kwamba kati ya sheria hizi mbili tofauti kubwa sana iliyopo ni moja tu kwamba wao katika *Maritime Transport Act) Registry* yao ni *open* kwa maana kwamba hawajali umri wa meli, meli ya umri wowote inaweza kusajiliwa endapo tu itakaguliwa na kuonekana kwamba inafaa. Wakati huku *SUMATRA Registry* yao ni *closed* kwa maana kwamba meli

haiwezi kusajiliwa ikiwa ina umri wa zaidi ya miaka 20. Mengine yote ni mahitaji na matakwa ya kimataifa ambayo pande mbili zinazingatia.

NAIBU SPIKA: Sasa jinsia, tumalizie kwa *CUF.*

MHE. MAGDALENA HAMIS SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imekuwa inachukua mchakato mrefu kwenye masuala ya msingi kama yanayogusa maisha ya watu, kwa sababu tangia *MV. Bukoba* Serikali ilisema vikosi maalum vya kuokoa baharini na mpaka leo kwenye majibu ya Naibu Waziri wanasema wako kwenye mchakato.

Je, Serikali haioni inachangia kwa asilimia zote kusababisha maisha kupotea kwa sababu kwenye masuala ya msingi wanachukua muda mrefu? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba Serikali inachangia majanga haya kutokea. Tumesema kwamba yako majanga yanayotokana na sababu za kimaumbile kwamba huwezi kuyazuia.

Lakini yako majanga ambayo yanasababishwa na watu binafsi na vyombo vyao au utendaji wa watendaji wa Serikali. Nilichosema hapa ni kwamba pale ambako mtendaji wa Serikali atakuwa amebainika kufanya uzembe mwarobaini wake upo tutafanya kazi ya kumpata na kumwajibisha kwa mujibu wa kanuni, sheria na taratibu.

Lakini hili suala la vikosi kama alivyosema Mheshimiwa William Lukuvi, vikosi mbalimbali vipo ambavyo vina wajibu wa kufanya shughuli hizi za uokoaji, ajali zinapotokea. Suala hapa tulililoliona kama Serikali ni *coordination* ya hivi vikosi ndio maana sasa tunaleta bill ambayo itatengeneza chombo kimoja cha kitaifa cha kuratibu hivi vikosi mbalimbali vinavyohusiana na mambo ya uokoaji. Bill hii haiko mbali mwezi Februari tutaleta Wabunge mtajadili mtatoa maelezo kwa Serikali na sisi tutatekeleza. *(Makofi)*

Na. 234

Ratiba ya Ukarabati wa Reli Nchini

MHE. ISMAIL ADEN RAGE aliuliza:-

Je, kuna vipaumbele vyovyote vilivyopangwa kuhusu ratiba ya ukarabati na ujenzi wa reli nchini?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha kwanza na cha muda mfupi ni kukarabati mtandao wa reli uliopo ili kuweza kurudisha huduma ya usafiri wa treni katika hali yake ya kawaida. Kazi zinazofanyika sasa ni pamoja na kubadilisha km 89 za reli nyepesi na kuweka reli nzito za ratili 80 kwa yadi. Kazi hiyo inafanywa na kampuni ya *CCECC* ya *China* kati ya *Station* ya Kitaraka na Malongwe.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha pili ni ujenzi wa njia mpya ya reli ya upana wa kimataifa *(standard gauge* kutoka DSM mpaka Kigali (Rwanda) na Msongati (Burundi). Katika kufanikisha azma hii Serikali za nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi zinasimamia kwa pamoja mchakato wa mradi wa ujenzi wa reli hiyo. Kazi ya Upembezi wa kina *(detailed study)* ya mradi huu inafanywa na kampuni M/S CANARAIL ya nchini Canada. Kazi ilianza Februari, 2012 na inatarajiwa kukamilika Februari, 2013 chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukarabati huo, *RAHCO* wanaendelea na kazi za uimarishaji wa tuta la reli na madaraja mawili kati ya Kilosa na Gulwe na daraja moja hapa Kintinku. Aidha, kipande cha KM 210 cha reli kati ya Kaliua na Mpanda nacho kinawekewa reli zenye uzito wa ratili 56.6 kwa yadi na

kuondoa zile zenye uzito mdogo wa ratili 45 kwa yadi. Fedha kwa ajili ya mradi huu jumla ya shilingi bilioni 41.375 ipo.

MHE. ISMAIL ADEN RAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri.
(a) Nilitaka kujua iko haja gani ya kuendelea kuwa na mashirika mawili ya RAHCO na *TRL* wakati yote yanamilikiwa na Serikali hatuoni tunapoteza fedha za Serikali bila sababu yoyote? (*Makofi*)

(b) Je, ni lini Serikali italiagiza Shirika la Reli Tanzania kuongeza usafiri wa abiria kati ya Dar es Salaam, Tabora, Kigoma na kuanzisha usafiri wa kutoka Tabora kwenda Mwanza ambao mpaka hivi ninavyoongea leo haupo. Hamwoni wananchi wa kawaida ambao ndio wanaweza kusafiri kwa reli tunawanyanyasa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kabla ya kujibu maswali yake mawili ya nyongeza Mheshimiwa Ismail Aden Rage naomba nichukue fursa hii kumpongeza kwa jinsi alivyonifuatafuata sana kunisukuma niende Tabora kuangalia reli inafanyaje kazi pale na malalamiko ya watumishi wa reli na jambo hilo nililifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, *RAHCO* ilianzishwa makusudi wakati Serikali ikifikiria ubinafishaji wa lililokuwa Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* na madhumuni ya uanzishwaji wa *RAHCO* ilikuwa ni kulinda rasilimali ya nchi hii ambayo ilikuwa inaonekana haiwezi kuingizwa

katika ubia ambao ulikuwa unatarajiwa kuingiwa kati ya ubinafishaji na Shirika la Reli.

Kwa sasa kampuni zote hizi mbili *TRL* na *RAHCO* zinamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali. Niseme tu kwa kifupi kwamba Wizara imetengeneza kikosi kazi cha kuangalia sasa kama tunayo haja ya kuendelea kuwa na *RAHCO* kama *RAHCO* na kama *TRL* kama *TRL* lakini pia tumekwenda hatua moja zaidi katika hadidu za rejea kwamba waangalie sasa uwezekano wa kuunganisha. Kama itakuwa hivyo hilo Shirika la Reli na Bandari ili ziweze kuwa na *management* moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu *TRL* kuongeza treni za kwenda Tabora na Kigoma na Mwanza, niseme kwamba hali la Shirika lilivyo leo ni vigumu sana kuwa na uwezo huo wa kuongeza hizo treni za abiria kwenda Kigoma na Mwanza kwa sababu tu moja kubwa kwamba vichwa vilivyopo havitoshi kufanya hivyo, lakini pia hata na mabehewa ya abiria yamechakaa kwa kiasi kikubwa hayawezi kutumika na yakawa na sifa na hadhi ya kusafirisha Watanzania.

Tunachofanya, tushukuru kwamba Bajeti iliyotolewa mwaka huu kwa kiasi kikubwa imekidhi maombi ya kampuni hizi za *TRL* na *RAHCO* katika ku-*revamp* sasa shughuli za reli. Lakini niseme tu kwamba tumekwishatoa maelekezo kwa *TRL* na narudia hapa kwamba wajitahidi sana wahakikishe kufikia mwezi wa Septemba waanza safari za kwenda Mwanza hata kama itakuwa ni mara moja kwa wiki, lakini wafanye hivyo kwa ajili ya hawa watu ambao kwa kweli

hawana uwezo wa kutumia vyombo vingine na usafiri wa reli ndiyo rahisi kuliko usafiri mwingine. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Duniani kote, huwezi ukazungumza uchumi na kuondoa umasikini wa watu kama hauna reli imara. Leo Tanzania ni miongoni mwa nchi mbili ambazo zina reli duni duniani, Tanzania na Malawi. Majibu ambayo tunapewa na Serikali hapa ni kana kwamba tumepata uhuru jana sasa michakato inaanza leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kufahamu kutoka kwa Serikali ni lini itahakikisha reli ya Tanzania inakuwa sambamba katika viwango na reli za nchi zingine duniani kwa sababu mpaka sasa tunatumia reli ambayo ni ya karne ya kumi na nane kiasi kwamba leo tukitaka kutengeneza injini mpaka tutoe *special order* kwa sababu tu *fashion* tuliyonayo imekwisha kupitwa na wakati haipatikani kwingineko duniani. Kwa hiyo, mimi ningependa Serikali iseme kwamba ina mkakati gani na sio mkakati tu iseme kwamba imefikia wapi kuingiza Tanzania kwenye viwango vya dunia la leo katika suala zima la reli?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Davidi Kafulila, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Sera ya Serikali ni kwamba reli yote mpya, njia yote ya reli mpya itakayojengwa, itajengwa kwa *standard gauge* ndiyo maana design inayofanyika kutoka Isaka kwenda Msongati, Burundi na kule Kigali itajengwa kwa *standard gauge.* Tunae sasa hivi Mshauri Mwelekezi *Cana Rail* ya Canada kama nilivyosema, wanafanya upembuzi wa kina kwa ajili ya reli ya kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma, Mwanza na kuendelea mpaka Msongati na Kigali ambayo design ile watakayoifanya ni ya ku-*upgrade* kutoka hii *meter gauge* tuliyonayo kwenda kwenye *standard gauge.*

Lakini niseme tu hapa kwamba gharama inayokuwa *involved* katika kufanya hiyo *transfer* ya kutoka *meter gage* kwenda *standard gauge* ni kubwa sana na nina mashaka kwamba uwezo wa Serikali kwa utaratibu huu wa Bajeti itatuchukua miaka mingi kidogo.

Kwa hivyo, Wizara inaandaa mapendekezo ambayo itayafikisha Serikalini kuona ni namna gani tunaweza tukapata fedha nyingi kwa mara moja ili kuweza kufanya *investiment* hii kubwa tukiwa na uhakika kwamba tukiianza, tutafika nayo mwisho. Wasiwasi wetu ni kwamba tunaweza tukaanza kwa vipande vipande hivi, halafu tuka- *distort* kabisa mfumo mzima wa reli na tukashindwa kusafirisha mizigo. Kwa hivyo, lazima hapa utaratibu wa fedha nyingi kwa mara moja upatikane ili tuweze kuanza na kumaliza tukiwa na uhakika. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda naomba tuendelee, tumepitiliza kweli kweli. Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Uchukuzi kwa kweli leo imekuwa siku yako, tunakushukuru kwa majibu mazuri. (*Makofi*)

Wageni walioko katika Ukumbi wa Spika ni pamoja na mgeni wa Mheshimiwa Spika ambae ni Mchungaji David Fares Majanjala kutoka Philadelphia Ministries ya Dar es Salaam. Kama upo usimame, ahsante sana, karibu sana Mchungaji David Majanjala.

Wageni watano wa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika Mheshimiwa Christopher Chiza amba ni watoto wake pamoja na wanafamilia wengine, familia ya Mheshimiwa Waziri ahsante sana, karibuni sana, tuwahakikishie Mheshimiwa Waziri anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni na tunashukuru kuja kumpa moyo.

Wako wageni wa Mheshimiwa Rose Kamili, Waziri Kivuli wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirikaambao ni watoto wake wawili pamoja na wananchi wengine watano kutoka Hanang, watoto wawili wa Mheshimiwa Rose Kamili na wale wageni kutoka Hanang karibuni sana. *(Makofi)*

wageni wengine kutoka Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ni pamoja na Ndugu Mohamed Muya Katibu Mkuu wa Wizara karibu sana, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Sophia Kaduma, Naibu Katibu Mkuu wa pili *Engineer* Mbogo Mfutakamba, ahsante sana lakini pia wako Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara

pamoja na Wahisani kutoka Mashirika ya Maendeleo, Development Partners msimame kwa pamoja, karibu nanyi sana Dodoma, tunajisikia fahari kubwa sana kuwa naji katika Ukumbi wetu huu wa Bunge.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni pamoja na wageni watatu wa Mheshimiwa Lolensia Bukwimba kutoka Geita wakiongozwa na Mchungaji Obedi Mkulakula, wako pale na Mchungaji yuko wapi? Ahsante sana. waheshimiwa Wabunge tunafurahi sana mnapoalika Wachungaji na Ma-sheikh watusaidie kidogo kupunguza punguza kidogo hali ya hewa hii ambayo inakuwa nzito wakati mwingine.(*Kicheko/Makofi*)

Wageni 14 wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu ambao ni wanafunzi wa kidato cha pili waliofanya vizuri kwenye mitihani yao kutoka shule ya Balandalalu na walimu wao wanane karibu sana wanafunzi na walimu mliofanya vizuri kidato cha pili, hongereni sana kwanza kwa kufanya vizuri na karibuni sana Dodoma katika Ukumbi wenu, karibuni sana. wageni wanne wa Mheshimiwa John Cheyo kutoka Itimila Mkoa wa Simiyu, wako wapi wangeni wa Mheshimiwa Cheyo? *(Makofi)*

Karibuni sana. Lakini pia tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Tundu Lissu ambao ni Ndugu Alute Mughwai ambaye ni Kaka yake ambaye ameambatana na Mkewe Bi. Rose Mughwai na Dada yake? *(Makofi)*

Hapa wameandika vibaya, samahani sana, wameniandikia vibaya hapa na Dada yake wa Mheshimiwa anaitwa Rose Mughwai. Naomba radhi kwa makosa ya waandishi wangu. Tunao wageni wa Mheshimiwa Amos Makalla, Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ambao kwanza ni Wajumbe wa Sekretarieti ya CCM Wilaya ya Mvomero wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya, Ndugu Pororete Mgema. (*Makofi*)

Mwenyekiti, lakini pia amefuatana na Ndugu Kimati, Katibu wa CCM wa Wilaya, Ndugu Kidado Katibu wa Vijana wa Wilaya, Yusuf Kingu Katibu Mwenezi wa Wilaya, Bakari Bindo, Katibu Msaidizi, yuko Katibu wa wazazi wa Wilaya, lakini vile vile Katibu wa UWT Wilaya, hiyo ni timu kamili.(*Makofi*)

Lakini vile vile wako Makatibu wawili wa Mbunge ambao ni Jumanne Kombo nna Abdalah Mgaya, karibuni sana na mwisho yuko rafiki wa karibu Ndugu Francis Joseph ambae pia ni mshauri wake wa kisiasa. Karibuni sana Dodoma, niwahakikishie Ndugu zangu wa Mvomero kwamba Mheshimiwa Amos Makalla anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni, tunategemea mtaendelea kumwunga mkono na kumsaidia. Waheshimiwa Wabunge huo ndiyo mwisho wa matangazo yetu na ilikuwa nia yangu ifikapo wakati huu basi tuanze mambo yetu. Katibu?

KUHUSU UTARATIBU

NAIBU SPIKA: Wamesimama wangapi? Naona kuna wengine kule au? Mheshimiwa January umo? Ni wawili? Haya tuanze na Mheshimiwa Tundu Lissu, halafu Mheshimiwa Wenje.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nielekeze kiti chako kwenye Kanuni ya 47(1) ikismwa pamoja na Kanuni ya 47(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na niombe idhini yako kwamba Bunge hili Tukufu liahirishe shughuli kama zilivyoonyeshwa kwenye Orodha ya Shughuli za leo, ili kujadili jambo la dharula linalohusu ajali ya Meli ya *MV. SKAGIT* ambayo imesababisha vifo vya Watanzania wengi sana na wewe mwenyewe ni shahidi jinsi ambavyo swali la leo lililohusu ajali hizi za meli ambavyo limeibua hisia kubwa sana miongoni mwa Wabunge wa Bunge hili Tukufu Jambo hili halijawahi kujadiliwa ilipotokea ajali ya Mv. *Spice Islander* mwaka jana na leo imetokea tena, huu ni muda muafaka kwa Bunge lako Tukufu kujadili jambo hili kubwa badala ya kulipa Bunge likizo ajali inapotokea Bunge lijadili suala hili kama suala la dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba idhini yako kwa mujibu wa Kanuni hizi. Ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. EZEKIA D.WENJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuhusu utaratibu, lakini naombea utaratibu Kanuni ya 139 nilikuwa naangalia muda uliokuwa unatumia kutambulisha wageni imechukua *almost* dakika kumi mpaka kumi na tano ingawa hii

Kanuni ya 139 haijaweka *time limit* ya muda gani wa kutambulisha. Sasa Bunge hili mnatuharakisha kweli na hatupati hata muda wa kuuliza maswali ya nyongeza kwa manufaa ya Watanzania.

Je, *is it realistic* kutumia dakika kumi mpaka kumi na tano kutambulisha wageni huku Wabunge tunakosa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza kwa manufa ya Watanzania? Naomba nijue mwongozo wa kiti chako. *Is it rational* kwa Watanzania? *Does it add value* kwa Watanzania kutambulishwa wageni hapa kwa dakika kumi na tano huku tunanyimwa maswali ya nyongeza?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tulitoa taarifa ya awali, lakini baadaye nilisoma taarifa ya Mheshimiwa Rais ambaye alikuwa ameandika kuhusiana na ajali hii na kama tunavyojua meli ile ina usajili wa Zanzibar iliyopata ajali na Serikali imeshasema itafanya uchunguzi wa kina ili kujua chanzo kilichosababisha ajali ile na hivi sasa Serikali ime-*concentrate* katika kazi kubwa ya kuokoa miili na marehemu walioko kwenye kile chombo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilitaka tu nikupe taarifa kwamba Serikali yenyewe kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambako chombo kile ndiko kinakotoka na ndiko kilichosajiliwa iko katika hatua na itatoa taarifa kama ilivyotoa taarifa kwenye kile chombo cha mwisho na hatua zile zilichukuliwa kwa upande ule ambapo meli ile ilikuwa ya kwanza ilikuwa imesajiliwa na kwa upande huu hatua hizo hizo, Rais wa Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar ametoa taarifa na Rais wa Jamuhuri ya Muungano ametoa taarifa.

Mimi nilikuwa napendekeza Bunge lako Tukufu lisijadili sasa wakati wa maombolezo na majonzi wakati kazi ile ya msingi sasa inaendelea kufanywa. Tusibiri tumalize kazi ile ya msingi ya uwokozi na mazishi, tusubiri Tume itakayoundwa na Viongozi hawa wakuu ambao kwa mujibu wa Sheria inatakiwa ifanye hivyo badala ya kujadili hapa mjadala wetu ambao mimi nafikiri hautaweza kuwa na tija kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ombi langu nilikuwa naomba sisi Bunge tuache , Wabunge wenzetu tumeshawapeleka kule karibu 30 wawakilishi wa Bunge hivi sasa, tumeamua kwenye Kamati ya Uongozi na Bunge hili limeridhia, wanashiriki katika kazi ile kule Zanzibar kwa niaba yetu. Tuache kazi ile iishe kwanza.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi nakwenda kwenye Kanuni ya 68(7) kwenye jambo ambalo limejiri kabla wakati Bunge linaendelea kuhusu suala la meli ambayo ameuliza Mheshimiwa kule, meli ya *MV. Spice Islander*. Karibu nusu ya Wabunge walisimama wa Bunge hili kutaka kuuliza maswali ya nyongeza. Hili pekee yake lilipashwa kupeleka ujumbe kwamba hili ni jambo la muhimu.

Sasa tumefika mahala sasa hivi, Tanzania tunaunda Tume nyingi nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Waziri Lukuvi, Tume tunaunda, matokeo yake hatupewi taarifa na ukitazama wanaokufa wale ni Watanzania wenzetu bila kujali meli ni ya Zanzibar au meli ni ya Bara. Ukitazama meli ya *Mv. Bukoba* mpaka leo hatujapewa matokeo ya Tume yake. Meli ya *Mv. Spice Islander* na watu waliofariki meli hii ya jana kuna kitu kinajirudia na kuna kitu kinafanana mule ndani. (*Makofi*)

Tanzania sasa hivi hapa tumekuwa ni Taifa la kuomboleza, tunashusha bendera nusu mlingoti kila siku na mimi nataka niseme hata tungelishusha bendera mpaka chini kabisa bila kuchukua hatua stahiki Watanzania tunazidi kufa. Tunaomba mwongozo wako ili kuokoa maisha ya Watanzania tusife, suala hili lijadiliwe hapa Bungeni tusiliashe hivi hivi kwa sababu kama leo meli watu wanazama karibu kabisa na Ikulu pale na magogoni.

Je meli ikizama kule Ziwa Nyasa kule Ludewa, tutawaokoa? Kesho meli ikizama kule Tanganyika tutawaokoa? Kikosi cha maafa tunashindwa kuokoa karibu kabisa, jirani kabisa na Ikulu tunahangaika na watu wanakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako suala hili lijadiliwe na Wabunge pamoja na kwamba wenzetu wamekwenda kutuwakilisha kule Zanzibar. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mnipe nafasi nitoe mwongozo sasa. Kuna nini tena?

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nahitaji tu kuweza kutoa taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8) kwamba imekuwa ni kama sehemu ya kautamaduni au kautaratibu ambako sasa kanazidi kujengeka ndani ya Bunge letu.

Serikali imekuwa na kauli mbalimbali ambazo zimekuwa zikitupatia sisi Wabunge na wananchi wa Tanzania kwamba jambo fulani liko linashughulikiwa kuna watu wameagizwa huko. Wameenda kufanya na taarifa italetwa. Bunge hili haliwezi kuwa tu kwamba ni Bunge ambalo linapokea taarifa halafu kisha hatuzijadili ili kuweza pengine kuielekeza Serikali ifanye nini kwa masilahi yetu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba jambo hili tusichukue muda mrefu sana, tujadili.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Machali kwa Kanuni uliyoitumia yani uko nje kabisa. Sina nia ya kukukata lakini kwa Kanuni ambayo umeitumia, umetumia Kanuni ya kama kutoa taarifa hivi. Alipaswa awepo anaesema ili umpe taarifa sasa naangalia uliekuwa unampa taarifa sijui ni Filikunjombe au ni nani.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nilisimama mapema nilikuwa nampa taarifa Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu.

NAIBU SPIKA: Basi wakati ulishapita bahati mbaya. Ahsante sana. Mheshimiwa uwe wa mwisho basi ili tusonge mbele. Mmenitaka nitoe mwongozo.

MHE.RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi nataka kusimama katika Kanuni ya 68(8), nataka kumpa taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba anapenda..

NAIBU SPIKA: Pia hutaweza kwa Kanuni hiyo kwa sababu alishakaa zamani. Tumeshawahi kufafanua mara nyingi sana..

MHE.RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niliomba muda mwingi.

NAIBU SPIKA: Naomba ukae kidogo.

Ndugu zangu, tukizitumia hizi Kanuni vizuri mtaona kwamba, nitawapa tu nafasi ya kutosha. Ukishazitumia kwa kuzikosea, itakuwa ni vigumu. Taarifa, ni lazima umpe mtu wakati ule anapokuwa anazungumza. Lakini alishazungumza zamani, alishakaa kwa hiyo, kwa Kanuni ya Taarifa, itakuwa ni vigumu sana kuruhusu.

Sasa, ngoja kwanza ni-*klie (clear)* yaliyoko Mezani, maana vinginevyo yatakuwa mengi sana; kama yapo basi tutaendelea kuyazungumzia. Nianze na jepesi kabisa, lile la Mheshimiwa Wenje, anasema muda wa Maswali na Muda wa Matangazo.

Muda wa Maswali, Waheshimiwa Wabunge, ni saa 1 ninyi wote ni mashahidi. Tunaanza saa 3.00 kamili hadi saa 4.00. lakini leo nimevuta maswali hadi saa 4.20. Kwa hiyo, mtu akilalamika kwamba, muda wa Maswali hampati muda wa kutosha wakuweza kuuliza maswali ya nyongeza hata baada ya kuongeza dakika 20 za Maswali, atakuwa anaionea Meza. Kwa hiyo, katika hilo, naomba niseme nimejitahidi, nisilaumiwe katika hilo. *(Makofi)*

Kuhusu kutambulisha Wageni; huu ni utaratibu wetu jamani. Wageni hawa ni wetu sisi. *(Makofi)*

Kuhusu Hoja ambayo sasa imetuchukua muda hapa, ya Mheshimiwa Tundu Lissu, aliyoitoa kwa kutumia Kanuni ile ya 47 kwamba, Bunge sasa liahirishe shughuli, ili lijadili Jambo la Dharura; ni Hoja nzito, ameitoa vizuri, lakini ameokosea Kikanuni tu kwamba, hakutoa Hoja na kwa hiyo, haikuungwa Mkono kabisa.

Sasa mimi kama Mwendesha Kikao, *Rulling* yangu ni kwamba, Hoja hii haikuungwa Mkono na kwa hiyo, tunaendelea na shughuli zingine za Bunge. *(Makofi)*

Katibu tuendelee na *Order Paper.*

MUONGOZO WA SPIKA

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mwongozo wa Mheshimiwa Spika.

NAIBU SPIKA: Nitakuruhusu, lakini kwa jambo jingine; isije kuwa hili ambalo nimeshalitolea *Rulling. (Makofi)*

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tundu Lissu, kama ni hili, utakuwa unakosea kidogo, maana nimesha-*Rule* tayari.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, katika...

NAIBU SPIKA: Ninakuruhusu, kama ni jingine?

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nifafanue. Nilichoomba niliomba idhini yako, ili nitoe hoja; Kanuni ya 47 (3), inasema uombe idhini ya Spika, kutoa Hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nisingeweza kutoa Hoja, bila idhini yako; nilikuwa naomba idhini kwanza itolewe, halafu nitoe Hoja, ndio Hoja iungwe mkono, hiyo ndio Kanuni ya 47 (3). Nisingeweza kutoa Hoja, bila kwanza kupata idhini yako; naomba hili jambo ni kubwa sana, hatuwezi tukajifichaficha nyuma ya Kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetumia Kanuni sawasawa kabisa. Niliomba idhini, ili nipate idhini, nitoe Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, jambo tunalozungumzia liko kwenye Kanuni ya 47 (3). Hoja itatolewa na Mbunge, kwa kusimama mahali pake na kuomba idhini ya Spika, kutoa Hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge, kwa madhumuni ya kujadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma. Na Mheshimiwa Mbunge, alitoa Hoja, lakini Hoja hiyo, haikuungwa Mkono.

(Hapa, Waheshimiwa Wabunge walitoa sauti ya kuguna)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, hakuomba, mimi nafikiri kwamba, sisi binadamu tuna vichwa na tunatumia vichwa hivyo kufikiri na sio kufuga nywele. Utaratibu, ukisoma Ibara ya Kanuni ya 5, yako mambo 5 ambayo unatakiwa kuyatumia katika kuongoza Vikao vya Bunge, yako mambo 5 pale.

Kwanza kuna Katiba, pili kuna Sheria nyingine za Nchi, tatu kuna Kanuni nyinginezo, nne kuna Maamuzi ya Mabunge mengine, pamoja na Mila na Desturi za Mabunge. Sasa kuwa na nywele kichwani, hakumaanishi kwamba, unaweza kufikiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri labda hii Hoja, haikuungwa mkono...

KUHUSU UTARATIBU

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

NAIBU SPIKA: Kuhusu Utaratibu, Mheshimiwa Tundu Lissu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Utaratibu Kanuni ya 64 (1) (f). Mbunge, hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine yeyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, anasema kwamba, kuwa na nywele haina maana kwamba, una uwezo wa kufikiri. Ina maana kwamba, kuna Wabunge humu ndani ambao hawana uwezo wa kufikiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kama anatoa lugha ya namna hii...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tundu Lissu, Mwanasheria, hajasema hivyo.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, *that's exactly* ndicho alichosema.

NAIBU SPIKA: Kwamba, hebu rudia amesemaje?

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, amesema hivi, kuwa na kichwa haina maana una uwezo wa kufikiri. Ina maana kwamba...

(Hapa, Waheshimiwa Wabunge walitoa sauti ya kuguna)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, hapana...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, hakusikia huyo.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, kuwa na nywele kichwani, haina maana kwamba, una uwezo wa kufikiri.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, fuga nywele.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni matusi. Ni mbaya, matusi yanapotoka kwenye kinywa cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa Hoja halali ambayo imetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimeomba idhini, ili nitoe Hoja. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, anasema kwamba, nina nywele, lakini sina uwezo wa kufikiri.

(Hapa, Waheshimiwa Wabunge walitoa sauti kuguna)

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni matusi. Haya ni matusi. Afute hiyo kauli yake.

NAIBU SPIKA: Sasa naomba niendeshe Kikao na mnisikilize, ili tusoinge mbele.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, alichosema, kazi ya kichwa sio kufuga nywele peke yake, nimemsikiliza vizuri. na mtu akisema hivyo, kwa kweli, huwezi kumbana popote pale kwamba, kasema neno lolote ambalo linakwenda kinyume na chochote kwa sababu, ndio ukweli wenyewe.

(Hapa, Waheshimiwa Wabunge walitoa sauti ya kushangilia)

NAIBU SPIKA: Mimi narudi kwenye Kanuni, tusitoke kwenye reli ambayo ni ya mjadala, maana vinginevyo tutatoka nje kabisa ya mjadala. Kanuni aliyoisimamia Mheshimiwa Tundu Lissu, ni ya 47 (1) na 47 (3), kuhusu lile suala la msingi. Na hasa 47 (3), ambayo inasema hivi, *"Hoja itatolewa na Mbunge, kwa kusimama mahali pake."* Unaweza ukaendelea na mengine yote. *"Hoja itatolewa na Mbunge, na kuomba idhini ya Spika, kutoa Hoja ya kuahirisha*

shughuli za Bunge, kwa madhumuni ya kujadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma."

Unapoomba idhini kwangu, unakuwa unatoa Hoja ukiwa umesimama mahali pako; hukutoa Hoja na Hoja hiyo, haikuungwa Mkono. Maana ni utaratibu wa Bunge hapa, kwa Mbunge yeyote anayetoa Hoja, angalao iungwe Mkono na Wabunge wengine, ili Spika, aone uzito wa Hoja yenyewe. Ili katika kutoa uamuzi wake, azingatie uzito wa Hoja, kwa kuwa, inaungwa mkono kiasi gani na Wabunge wengine.

Kwa hiyo, kwa kuwa, maamuzi yangu hayatokani na kuona kwamba, jambo lile ni dogo au si dogo, hapana; ni jambo kubwa, ni jambo zito. Kilichokosewa hapa ni taratibu tu za Kikanuni. Sasa, kwa sababu, tumekosea kwenye Kanuni, tuendelee tu na utaratibu.

Naomba sasa tuendelee. Katibu, tuendelee. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani, naomba tuendelee.

Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwanza na mimi kutoa pole kwa wahanga wa ajali ya meli iliyotokea hivi majuzi. Lakini ninachoweza kusema tu, nawaombea wote waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki, wawe na subira katika muda huu wa majonzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwana alitoa, tena ametwaa. Jina lake, libarikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo Mifugo na Maji inayohusu Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, sasa lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa na afya njema ili tuweze kujadili bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania ambao wengi wao ni wakulima. Napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuniteua mimi, kuwa Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika. Uteuzi huu umeonesha imani yake kwangu.

Napenda kutumia fursa hii kumuahidi Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge, Wakulima na Watanzania wote kwamba nitatumia uwezo wangu

wote kwa uaminifu na uadilifu kuhakikisha kwamba rasilimali zinazotengwa kwa ajili ya Sekta hii zinawafikia wakulima wetu ili wazalishe mazao na kupata bei nzuri. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara mbalimbali. Kipekee nampongeza Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Mbunge wa Mkuranga, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, namuahidi ushirikiano katika kuendeleza kilimo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa msukumo wa pekee katika kuendeleza Sekta ya Kilimo. Msukumo huo umeoneshwa dhahiri katika shughuli zake mbalimbali mathalan, uzinduzi wa Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo *(Tanzania Agriculture and Food Security Investiment Plan – TAFSIP)* uliofanyika tarehe 8 Novemba, 2011 ambao unalenga kutekeleza Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Kilimo Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa kuzindua mkutano wa Mawaziri wa kilimo wa nchi saba za umoja wa *Grow Africa* uliofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 16 na 17 Februari 2012; kushiriki kwenye mkutano wa uwekezaji katika kilimo barani Afrika *(Grow Africa Investment Forum*) uliofanyika tarehe 8 na 9 Mei, 2012, Addis Ababa, Ethiopia; na kushiriki katika mikutano ya nchi tajiri duniani (G8) iliyofanyika tarehe 18 na 19 Mei 2012, huko Washington na Camp David, Marekani. Kutokana na jitihada zinazooneshwa na Mheshimiwa Rais na

mipango mizuri katika kuendeleza kilimo aliyoiwasilisha kwenye mikutano hiyo, Washirika wa Maendeleo walivutiwa na waliahidi kuipatia Tanzania Dola za Kimarekani milioni 897 kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2013.

Fedha hizo zitatumika katika kuendeleza miundombinu ya kusaidia kilimo hususan umwagiliaji, masoko, usindikaji na usafirishaji wa pembejeo na mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuelezea mipango ya uwekezaji katika kilimo iliyoeleweka vizuri na hivyo kuwezesha Washirika wa Maendeleo kutupatia kiasi hicho kikubwa cha fedha ambacho hatujawahi kupata katika miaka ya karibuni. Aidha, katika kuonesha umuhimu wa Ushirika nchini, Mheshimiwa Rais alizindua maadhimisho ya mwaka wa Kimataifa wa Ushirika na ujenzi wa jengo la Ushirika tarehe 20 Machi, 2012. Katika maadhimisho hayo, Mheshimiwa Rais alituasa tuimarishe uanzishwaji na uendelezwaji wa Vyama vya Ushirika vinavyoendeshwa kwa kutumia misingi ya uongozi bora, demokrasia, uwajibikaji, uwazi na usawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dokta Mohamed Gharib Bilal ambaye amekuwa akifanya ziara mikoani kuona shughuli za kilimo na maendeleo kwa ujumla na kutoa maelekezo mbalimbali ya namna ya kuendeleza kilimo. Katika ziara hizo, Mheshimiwa Makamu wa Rais amekuwa akisisitiza umuhimu wa kilimo endelevu na kinachozingatia hifadhi ya mazingira. Maelekezo hayo

yamezingatiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ili kuharakisha maendeleo ya kilimo nchini yanayolenga kuongeza usalama wa chakula na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda Mbunge *almaaruf Mtoto wa Mkulima* kwa kutumia muda wake mwingi kuhamasisha na kutoa maelekezo yenye lengo la kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo. Sisi wote ni mashahidi wa umahiri wa Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kufafanua na kujibu hoja za kilimo katika kipindi cha maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu ndani ya Bunge lako tukufu. Maelekezo yake yamezingatiwa katika utekelezaji wa mipango ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe mwenyewe, Naibu Naibu Spika na Wenyeviti kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge letu tukufu kwa umahiri mkubwa. Uongozi wenu ndio umetufikisha hapa ambapo hadi hivi sasa Bunge letu halina migogoro yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Janet Zebedayo Mbene Mbunge , James Francis Mbatia Mbunge , Saada Mkuya Salum Mbunge na Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo Mbunge kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Wabunge wa Bunge letu Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Alhaji Adam Omar Kimbisa Mbunge, Charles Makongoro Nyerere Mbunge, Shy-Rose Sadruddin Bhanji Mbunge, Anjela Charles Kizigha Mbunge, Abdallah Alli Hassan Mwinyi Mbunge, Maryam Yahaya Ussi Mbunge, Twaha Issa Taslima Mbunge, Nderakindo Perpetua Kessy Mbunge na Bernard Msomi Marunya, Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Ni matarajio yangu kuwa watatumia fursa hiyo kulinda maslahi ya kilimo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2011/2012 Bunge lako Tukufu lilipata misiba ya kuondokewa na Waheshimiwa Khamis Mussa Silima aliyekuwa Mbunge wa Uzini – Zanzibar (CCM), Jeremiah Solomon Sumari aliyekuwa Mbunge wa Arumeru Mashariki (CCM), Salum Amour Matondoo aliyekuwa Mbunge wa Bububu – Zanzibar (CCM) na Regia Estilatus Mtema aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA). Nawapa pole ndugu, jamaa na marafiki wa familia za marehemu hao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi kwa maoni, ushauri na ushirikiano mkubwa walioutoa na ambao wameendelea kuutoa wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2012/2013.

Naishukuru Kamati kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ya mwaka 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2012/2013 katika vikao vyake vilivyofanyika Dar es Salaam tarehe 07 na 08 Juni 2012 na Dodoma tarehe 13 Juni 2012. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa yamezingatiwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani na pongezi za pekee kwa wananchi wa Jimbo langu la Buyungu kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni.

Aidha, nawapongeza kwa juhudi wanazofanya katika kujiletea maendeleo. Napenda kwa niaba yao kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupatia eneo jipya la utawala kwa kuanzisha Wilaya mpya ya Kakonko. Nawaahidi kuwa tutashirikiana kuijenga Wilaya yetu mpya na kuondoa kero za Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa kwa mara nyingine tena kuwapongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Stephen Masato Wasira Mbunge na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Kalenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana kwa hotuba zao zilizotoa ufafanuzi Kuhusu Hali ya Uchumi kwa mwaka 2011, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2012/2013 ambazo zimeelezea kwa muhtasari Hali ya Kilimo chetu kilivyo hivi sasa na mwelekeo kwa mwaka ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hali ya Kilimo na Ushirika. Hali ya Kilimo; Sekta ya Kilimo ni moja ya Sekta muhimu katika uchumi na maendeleo ya nchi yetu kwa kuwa inatoa ajira kwa asilimia 75 ya Watanzania na inachangia wastani wa asilimia 95 ya chakula kinachopatikana nchini kwa miaka yenye mvua za kutosha. Katika mwaka 2011 Sekta ya Kilimo ilichangia asilimia 23.7 ya Pato la Taifa. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha ukuaji wa kilimo kimekuwa kikipanda na kushuka kulingana na hali ya hewa na matumizi ya pembejeo za kilimo. Katika mwaka 2011, Sekta ya Kilimo ilikua kwa asilimia 3.6 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2010. (*Makofi)*

Katika ukuaji huo mchango wa mazao ulikuwa asilimia 3.5 ikilinganishwa na asilimia 4.4 ya mwaka 2010. Mchango wa mifugo ulikuwa asilimia 3.9 ikilinganishwa na asilimia 3.4 ya mwaka 2010; ukuaji wa misitu na uwindaji ulikuwa asilimia 3.5 ikilinganishwa na asilimia 4.1 ya mwaka 2010. Sababu kubwa ya kushuka kwa ukuaji wa Sekta ndogo ya mazao ilikuwa ni ukame ulioikumba mikoa ya Tanga, Lindi, Mtwara, Pwani, Manyara, Singida, Dodoma, Tabora, Kigoma Kaskazini, Shinyanga na Kilimanjaro katika mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa Sekta ya Kilimo bado ni mdogo ikilinganishwa na lengo la ukuaji wa asilimia 6 ulioainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016).

Ukuaji huo mdogo, unachangiwa na uwekezaji mdogo. Kutokana na hali hiyo, Serikali ilianza kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Programme (ASDP)* kuanzia mwaka 2006 ambayo inalenga kuleta mageuzi katika Sekta hiyo.

Katika kutekeleza programu hiyo, mkazo umewekwa katika kuongeza upatikanaji na matumizi ya pembejeo kupitia mpango wa ruzuku; kuboresha utafiti wa mazao; kuboresha huduma za ugani kwa kuongeza idadi ya wagani na mashamba darasa; kuongeza matumizi ya zana bora za kilimo; kuendeleza kilimo cha umwagiliaji; na kudhibiti milipuko ya magonjwa na visumbufu vya mimea.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa *ASDP* katika ngazi ya Halmashauri unafanyika kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(District Agricultural Development Plans – DADPs)* na Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani *(District Agricultural Sector Investment Project – DASIP)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi nyingine ni pamoja na kuendeleza masoko ya mazao kupitia Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani Mazao na Huduma za Kifedha Vijijini *(Marketing Infrastructure Value Addition and Rural*

Finance Program – MIVARF) na uanzishwaji wa Stakabadhi za Maghala.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi hizo, ambazo kwa kiasi kikubwa zimekuwa zikigharamiwa na Serikali na wadau wa maendeleo, Serikali imedhamiria pia kuvutia uwekezaji wa Sekta Binafsi katika kilimo ili kiwe cha kibiashara kama ilivyoainishwa katika nguzo ya pili ya Kilimo Kwanza. Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi umeanza kutekelezwa kupitia Mpango wa Kukuza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania *(Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT)*. Mpango huo unalenga kuvutia uwekezaji katika kilimo kwa ushirikiano baina ya wakulima wakubwa na wadogo katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya Ushirika. Ushirika ni muhimu katika kuunganisha nguvu za wananchi ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia Vyama vya Ushirika vinavyomilikiwa na kusimamiwa kwa mujibu wa maadili na misingi ya Ushirika inayotambuliwa Kimataifa. Manufaa ya Ushirika ni pamoja na kuwezesha wanachama kununua pembejeo za kilimo na mifugo kwa gharama nafuu, kusindika mazao na kutafuta masoko yenye bei kubwa ndani na nje ya nchi. Ushirika unawezesha wanachama kupata huduma za kifedha kama vile uwekaji akiba, kupewa mikopo na ushauri pamoja na makazi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirika umeendelea kuimarika chini ya Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini (*Cooperative Reform and Modernization Program – CRMP*) ambapo idadi ya Vyama vya Ushirika imeongezeka kutoka 9,397 mwaka 2011 hadi 9,769 mwezi Juni 2012. Aidha, wanachama wa Vyama vya Ushirika waliongezeka kutoka 2,244,727 mwaka 2010/2011 hadi 2,396,001 mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya *SACCOS* pia iliongezeka kutoka 5,251 hadi 5,424 na wanachama wake waliongezeka kutoka 917,889 hadi 1,059,213; hisa, akiba na amana za wanachama ziliongezeka kutoka Shilingi bilioni 236.8 hadi bilioni 409.95 sawa na ongezeko la asilimia 73.1. Aidha, mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 703.3 ilitolewa kwa ajili ya shughuli za biashara na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Ushirika bado unakabiliwa na changamoto kubwa ya baadhi ya viongozi na watendaji wa Vyama vya Ushirika kukosa uaminifu, uwezo na kutowajibika katika kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Hali hii inasababisha Vyama kushindwa kukidhi mahitaji ya wanachama wake na jamii kwa ujumla. Changamoto nyingine ni idadi ndogo ya Maafisa Ushirika ikilinganishwa na idadi ya vyama na hivyo kusababisha kukosekana kwa usimamizi na utoaji wa huduma kama vile mafunzo na ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kukabiliana na changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi kwa kuongeza ukaguzi wa

Vyama, kuwajengea uwezo viongozi na kutoa mafunzo kwa wanachama kuhusu haki na wajibu wao na kuajiri Maafisa Ushirika katika Halmashauri na Wizara. Natoa wito kwa wananchi kujiunga na kuendeleza Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali za uchumi kwa manufaa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya chakula; uzalishaji na upatikanaji wa chakula. Katika mwaka 2011/2012, hali ya chakula nchini ilikuwa ya kuridhisha kutokana na uzalishaji mzuri wa mazao ya chakula katika msimu wa 2010/2011. Tathmini ya uvunaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2010/2011 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2011/2012, iliyofanywa mwezi Desemba 2011 ilionesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula kwa ujumla katika msimu huo ulifikia tani milioni 12.972 zikiwemo tani milioni 7.033 za nafaka na tani milioni 5.939 za mazao mengine. Uzalishaji huo ulitosheleza mahitaji ya chakula ya tani milioni 11.532 kwa mwaka 2011/2012 na kuwepo kwa ziada ya tani milioni 1.440.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hali hiyo nzuri, kulikuwepo na maeneo yenye upungufu. Tathmini za kina za hali ya chakula na lishe zilizofanyika mwezi Septemba 2011 na mwezi Machi 2012, zilibaini kuwa watu 1,062,516 katika Halmashauri 52 za Mikoa 15 ya Arusha, Kilimanjaro, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Kagera, Tanga, Pwani, Mtwara, Manyara, Iringa, Dodoma, Singida, Mara na Mbeya walikuwa na upungufu wa chakula na walihitaji tani 38,843 za chakula cha msaada kati ya mwezi Oktoba na Desemba 2011 na watu 1,231,436 katika Halmashauri

28 za Mikoa 11 ya Arusha, Kilimanjaro, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Kagera, Tanga, Pwani, Mtwara, Manyara na Iringa walihitaji tani 29,554 za chakula cha msaada kati ya mwezi Mei na Juni 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliidhinisha kutengwa na kutolewa chakula cha msaada tani 68,397 kwa wananchi hao ambapo hadi tarehe 27 Juni 2012, jumla ya tani 67,131.166 za mahindi zilikuwa zimechukuliwa na Halmashauri husika kutoka Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(National Food Reserve Agency – NFRA)* kwa ajili ya kusambazwa kwa walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam linalokadiriwa kuwa na wakazi takriban milioni nne (4) linahitaji wastani wa tani 250 za mahindi kwa siku. Kiasi hicho cha mahitaji ni kikubwa na kinaweza kutoa mchango mkubwa katika mfumuko wa bei iwapo kutatokea upungufu. Kutokana na upungufu wa mvua za vuli uliojitokeza katika robo ya nne ya mwaka 2010/2011, pamoja na upungufu wa chakula katika nchi za Somalia, Sudan ya Kusini na Kenya, upatikanaji wa mahindi katika Jiji la Dar es Salaam ulipungua na kusababisha bei za mahindi kupanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuona hilo, Serikali iliamua kuuza sehemu ya mahindi kutoka Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*National Food Reserve Agency – NFRA*) katika soko kwa lengo la kupunguza mfumuko wa bei, ambapo Jiji la Dar es Salaam liligawiwa tani 18,894.623. Hadi tarehe 30 Juni 2012, jumla ya tani 16,957.821 zilikuwa zimechukuliwa. Hali

hiyo ilisaidia kupunguza bei ya unga wa mahindi kutoka wastani wa Sh. 1,500 hadi Sh. 900 kwa kilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya tani 22,500 za mahindi zilitengwa kati ya mwezi Mei na Juni 2012 kwa masoko ya mijini katika Mikoa 14 ya Arusha (2,000), Kilimanjaro (900), Manyara (200), Shinyanga (5,000), Kagera (2,800), Tabora (3,000), Mwanza (3,000), Tanga (500), Pwani (2,500), Mtwara (500), Iringa (600), Dodoma (500), Singida (500) na Rukwa (1,000).

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 30 Juni 2012, Mikoa tisa ya Arusha, Kilimanjaro, Iringa, Shinyanga, Mtwara, Dodoma, Singida, Pwani na Tanga ilikuwa imechukua tani 8,325.40 kutoka maghala ya *NFRA* kwa ajili ya kusaga na kuuza unga kwa wananchi kwa bei elekezi zilizopangwa na mikoa husika. Kutokana na jitihada hizo bei ya unga ilishuka kutoka wastani wa Sh. 1,300 hadi 800 kwa kilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matarajio ya Hali ya Chakula Mwaka 2012/2013. Mwezi Juni 2012, Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya Tanzania Bara ilifanya Tathmini ya Awali ya hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula na utabiri wa hali ya chakula kwa mwaka 2012/2013. Matokeo ya tathmini hiyo yanaonesha kwamba uzalishaji wa mazao ya chakula utafikia tani 13,572,804 ikilinganishwa na mahitaji ya chakula yanayokadiriwa kuwa tani 11,990,115 kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa linatarajia kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 113 na hivyo

kuwa na ziada ya tani 1,582,690. Tathmini hiyo ilibaini kuwepo na ziada ya chakula katika mikoa nane (8) ya Iringa, Rukwa, Mbeya, Kagera, Mtwara, Kigoma, Ruvuma na Morogoro; utoshelevu katika mikoa saba (7) ya Pwani, Mara, Tanga, Lindi, Mwanza, Singida na Dodoma na uhaba katika Mikoa sita (6) ya Shinyanga, Tabora, Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa nafaka kwa msimu wa kilimo 2011/2012, unatarajiwa kufikia tani 7,558,342 wakati mahitaji ni tani 7,551,244 na hivyo kuwepo ziada ya tani 7,097 za nafaka. Aidha, uzalishaji wa mazao ya chakula yasiyo nafaka (viazi, muhogo, ndizi, maharagwe na kadhalika) unatarajiwa kuwa tani 6,014,463 wakati mahitaji ni tani 4,438,870, hivyo kuwepo ziada ya tani 1,575,592. Tathmini imebainisha pia kuwepo kwa upungufu wa chakula katika baadhi ya maeneo katika Wilaya 63.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya chakula duniani na nchi jirani. Taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(Food and Agriculture Organisation - FAO)* iliyotolewa mwezi Juni 2012, inaonesha kuwa katika mwaka 2011/2012, uzalishaji wa nafaka duniani unatazamiwa kuongezeka kwa asilimia 3.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya tani bilioni 2.42 za nafaka zitazalishwa ikilinganishwa na matumizi ya nafaka ya tani bilioni 2.38 kwa mwaka 2012/2013, matumizi ya nafaka kwa ajili ya chakula cha mifugo yataongezeka kwa asilimia 3.8 wakati matumizi ya chakula yanatazamiwa kuongezeka kwa asilimia moja

(1). Akiba ya nafaka duniani inatazamiwa kuongezeka kwa tani milioni 36 na kufikia tani milioni 548 sawa na ongezeko la asilimia saba (7) kutoka kiwango cha mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ongezeko la uzalishaji wa mazao ya chakula duniani, uzalishaji wa mazao ya chakula katika nchi 36 zenye kipato cha chini unatazamiwa kupungua na hivyo kusababisha upungufu wa chakula kwa viwango mbalimbali kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla nchi nyingi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika hususan, Burundi, Congo (*DRC*), Kenya, Sudan ya Kusini, Somalia, Madagascar, Malawi na Msumbiji zinatazamiwa kuwa na upungufu wa chakula kutokana na ukame, mafuriko na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Kutokana na upungufu huo, bei za vyakula katika nchi hizo zinatarajiwa kupanda. Hali hiyo inaweza kuathiri upatikanaji wa chakula nchini na hivyo kusababisha bei kupanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za kukabiliana na upungufu wa chakula nchini. Ili kukabiliana na upungufu wa chakula unaoweza kujitokeza kutokana na mahitaji ya chakula katika soko la ndani na nchi jirani, Serikali inachukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuiwezesha NFRA kununua tani 200,000 za nafaka katika msimu wa ununuzi wa 2012/2013, kutoka kwa wakulima wa Mikoa iliyozalisha ziada ya Rukwa, Iringa, Mbeya na Ruvuma;

(b) Kuhamisha tani 100,000 za akiba ya nafaka iliyopo kwenye maghala yenye ziada ya chakula kwenda kwenye maghala ya mikoa yenye upungufu wa chakula. Hatua hiyo itaiwezesha Serikali kukabiliana na upungufu wa chakula na mahitaji mengine ya soko kwa haraka zaidi na pia itatoa nafasi ya kuhifadhi nafaka zitakazonunuliwa msimu wa ununuzi wa 2012/2013; na

(c) Kuhimiza wakulima kujiwekea akiba ya chakula cha kutosha kwa ajili ya mahitaji ya kaya zao na kuuza ziada tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupata ufumbuzi wa muda mrefu wa tatizo la upungufu wa chakula hususan Mikoa ya Shinyanga, Arusha, Manyara, Tabora, Kilimanjaro, Dodoma na Singida ambayo huathirika na ukame wa mara kwa mara, Wizara yangu itaendelea kuwekeza katika miundombinu ya umwagiliaji pamoja na mabwawa ya kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji, mifugo na matumizi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia itahamasisha uwekezaji na matumizi ya teknolojia za umwagiliaji zinazotumia maji kwa ufanisi. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha wakulima kutumia mbegu bora za mazao yanayostahimili ukame kama vile mtama, uwele, ulezi, choroko na alizeti. Wizara pia itahamasisha matumizi ya matrekta katika maeneo yenye ardhi ngumu ili maandalizi ya mashamba yafanyike kwa wakati kuwahi msimu wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Mkoa wa Tanga kuonesha kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 114, baadhi ya maeneo katika mkoa huo yana upungufu wa chakula. Hali hiyo kwa kiasi kikubwa inasababishwa na kipato kidogo kwa baadhi ya wananchi waliokuwa wakitegemea ajira kutoka kwenye viwanda na mashamba ya mkonge ambayo sasa hayazalishi. Aidha, baadhi ya wakulima walipata fursa ya kupanda mazao ya chakula hususan mahindi na maharage kwenye mashamba ya mkonge fursa ambayo kwa sasa imepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliunda kikosi kazi cha kutathmini mashamba ya mkonge ambayo hayaendelezwi. Tayari kikosi kazi kimetathmini mashamba 32 kati ya 62. Katika mwaka 2012/2013, kazi hiyo itakamilishwa na wataobainika kukiuka masharti ya uwekezaji watachukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kupendekeza kwa Mamlaka husika kufuta hatimiliki za mashamba hayo ili kuwapa wawekezaji watakaoweza kuyaendeleza kwa ufanisi na kutoa ajira. Nawashauri wawekezaji waliopewa mashamba hayo kurejea makubaliano ya uwekezaji na kuyatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011, uzalishaji wa mchele nchini ulikuwa tani 1,461,408 ambapo mahitaji yalikuwa tani 816,648. Katika mazingira ya mtandao wa biashara uliopo, uzalishaji huo ni mdogo kukidhi mahitaji yetu ya mchele na mahitaji ya soko katika kanda ya Afrika Mashariki,

Kati na Kusini. Mahitaji hayo ya soko yalichangia kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo nchini kutoka wastani wa Sh. 1,229 kwa kilo mwezi Agosti 2011 hadi wastani wa Sh. 2,044 kwa kilo mwezi Aprili 2012 katika masoko ya jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, uzalishaji wa mchele ulikuwa tani 1,138,416 kiasi ambacho ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji ya soko la ndani na nchi zinazotuzunguka. Kutokana na hali hiyo, Wizara inaendelea kuhamasisha matumizi ya vyakula vingine badala ya mchele kama muhogo, viazi vitamu, viazi mviringo, ndizi, maboga, magimbi na vyakula vingine vinavyopatikana kwa wingi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia itaendelea kufuatilia mwenendo wa bei na kuchukua hatua za kuagiza mchele kutoka nje kama kutakuwa na upungufu. Vilevile, Serikali itaendelea kuwekeza katika kilimo cha mpunga katika miradi ya umwagiliaji na kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa mpunga katika mabonde makuu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa sukari katika mwaka 2011/2012, ulikuwa tani 260,055 ikilinganishwa na tani 263,461 za mwaka 2010/2011. Kushuka kwa uzalishaji kulitokana na mvua nyingi zilizonyesha mwezi Desemba 2011 na mwezi Mei 2012, kupungua kwa kiwango cha sukari (*sucrose content*) katika miwa, migomo ya wakata miwa na kuharibika kwa mitambo katika baadhi ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya sukari nchini kwa sasa ni tani 378,000 kwa mwaka. Kutokana na uzalishaji wa tani 260,055, nchi ilikuwa na upungufu wa tani 117,945. Upungufu huo ulisababisha bei ya bidhaa hiyo kupanda hadi kufikia wastani wa Sh. 2,500 kwa kilo. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Serikali iliruhusu wafanyabiashara kuagiza tani 200,000 bila kulipa kodi kwa lengo la kupunguza bei ya sukari kwa mlaji ifikie Sh. 1,700 kwa kilo. Hadi tarehe 31 Mei 2012, jumla ya tani 155,972 za sukari ziliingizwa nchini. Aidha, hadi tarehe 23 Juni 2012, tani 29,960 zilikuwa bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizo bei ya sukari imeendelea kuwa juu. Hadi tarehe 23 Juni 2012, bei ya rejareja ya sukari katika mikoa yote nchini ilikuwa ni kati ya Sh. 1,900 na 2,500 kwa kilo. Hali hiyo kwa kiasi kikubwa ilichangiwa na upungufu wa sukari katika nchi jirani; kukosekana kwa uaminifu wa wafanyabiashara na mfumo wa udhibiti na usambazaji. Kuanzia sasa Serikali itafuatilia mwenendo wa upatikanaji na usambazaji wa sukari yote inayozalishwa na inayoingizwa nchini mpaka kwa mlaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, uzalishaji wa sukari unatarajiwa kuwa tani 300,906. Kiasi hicho cha Sukari pamoja na albaki ya tani 82,911 zilizopo kwenye maghala ya wafanyabiashara na viwanda kinatarajiwa kukidhi mahitaji ya Sukari ambayo ni tani 378,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu inazungukwa na nchi zenye upungufu wa sukari, sukari inayotarajiwa kuwepo inaweza isitosheleze mahitaji.

Kutokana na hali hiyo, Wizara itaendelea kufuatilia kwa karibu upatikanaji wa sukari nchini na kama upungufu utajitokeza, Serikali itaruhusu uagizaji sukari kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo ni kuzalisha kwa wingi Sukari kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi hususan soko la Kanda ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini. Hivyo, Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji wa sukari. Pamoja na kuwa na mkakati wa uzalishaji katika viwanda vikubwa, suala la uanzishwaji wa viwanda vidogo na vya kati pia limepewa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari maeneo kadhaa yameainishwa kwa ajili ya mpango huo. Maeneo hayo ni Mfilisi, Ulaya, Kilosa, Mwaya na Kilombero (Morogoro); Bonde la Kiru na Babati (Manyara); Bonde la Lumuma (Dodoma); Peramiho, Liuli na Namtumbo (Ruvuma); Pangani (Tanga); Kihurio (Kilimanjaro); Kintinku (Singida); Mahurunga (Mtwara); Malagarasi, Kasulu na Kumsenga (Kigoma) pamoja na maeneo mengine yakiwemo yale yanayozunguka viwanda vilivyopo ambavyo uwezo wa kusindika miwa ni mdogo. Wizara yangu inafanya utafiti wa kina katika maeneo hayo. Uanzishwaji wa viwanda hivyo utasaidia kupunguza bei ya sukari, kupunguza tatizo la ajira kwa vijana na kuuza ziada nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa malengo na mipango mwaka 2011/2012; malengo na mipango ya 2011/2012. Mpango na Bajeti ya mwaka 2011/2012, ulilenga

kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wenye lengo la kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo *(Tanzania Development Vision 2025)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mpango huo uliendelea kutekeleza Malengo ya Milenia; MKUKUTA II; Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010; Azma ya Kilimo Kwanza; Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Program - ASDP*); na Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika *(Cooperative Reforms and Modernization Program – CRMP).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mpango wa Bajeti wa mwaka 2011/2012, Wizara ilitekeleza Malengo Mkakati kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo;

(ii) Kuwezesha upatikanaji wa Masoko ya Bidhaa za Kilimo;

(iii) Kuwezesha uongezaji wa Thamani ya Mazao ya Kilimo;

(iv) Kuwezesha na kuimarisha Ushirika na Asasi za Wananchi katika kilimo na Sekta nyingine za Kiuchumi;

(v) Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, uhifadhi, uchambuzi na usambazaji wa takwimu;

(vi) Kusimamia Sera, Sheria na Mikakati katika Sekta ya Kilimo;

(vii) Kuboresha uratibu katika Sekta ya Kilimo;

(viii) Kuboresha uwezo wa Wizara wa kutoa huduma; na

(ix) Kuzingatia Masuala Mtambuka katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza malengo mkakati hayo kumekuwa na ongezeko katika uzalishaji wa baadhi ya mazao ya kilimo kutokana na matumizi ya pembejeo na zana za kilimo; idadi ya Maafisa Ugani na idadi ya Vyama vya Ushirika, hisa, amana, akiba za wanachama na mikopo iliyotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji kumekuwepo na changamoto kubwa ya upatikanaji na mtiririko wa fedha hali ambayo imesababisha kutotekelezwa kikamilifu kwa baadhi ya malengo hayo. Aidha, uhaba wa mvua za vuli katika maeneo mengi ya nchi na kuchelewa kuanza mvua za masika kwa baadhi ya maeneo kumeathiri uzalishaji wa baadhi ya mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kupitia Fungu 43 ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 258.35. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 152.41 ni fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 105.94 ni fedha za maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, Shilingi bilioni 14.26 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 91.68 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara ilipokea nyongeza ya Shilingi bilioni 24.62 fedha za maendeleo kwa ajili ya Mradi wa Ukuzaji wa Usalama wa Chakula *(Accelerated Food Security Project - AFSP)* ili kulipa Mawakala wa Pembejeo na hivyo kusababisha fedha za maendeleo kuongezeka kutoka Shilingi bilioni 105.94 hadi Shilingi bilioni 130.56.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 30 Juni 2012, fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa ni Shilingi bilioni 116.53 sawa na asilimia 76.46 ya kiasi kilichoidhinishwa. Matumizi yalifikia Shilingi bilioni 113.14 sawa na asilimia 97.09 ya kiasi cha fedha kilichotolewa. Aidha, fedha za bajeti ya maendeleo zilizotolewa ni Shilingi bilioni 129.24 sawa na asilimia 98.99 ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na zilizotumika ni Shilingi bilioni 125.11 sawa na asilimia 96.81 ya fedha zilizotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Fungu 24 ilitengewa Shilingi bilioni 6.66 za matumizi ya kawaida. Hadi tarehe 30 Juni 2012, fedha zilizopokelewa ni Shilingi bilioni 5.32 sawa na asilimia 79.88 ya kiasi kilichoidhinishwa. Matumizi yalifikia Shilingi bilioni 5.29 sawa na asilimia 99.52 ya kiasi cha fedha kilichotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa malengo mkakati; kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo. Uzalishaji wa mazao makuu ya biashara ambayo pamba, korosho, pareto, mkonge na chai uliongezeka kwa kati ya asilimia tatu (3) na 38 katika mwaka 2011/2012 ikilinganishwa na mwaka 2010/2011. Aidha, uzalishaji wa mazao ya tumbaku na

kahawa ulishuka kwa asilimia tatu (3) na 45 mtawalia ikilinganishwa na mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa zao la kahawa umeshuka kutokana na ukosefu wa mvua za vuli katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Tanga; mabadiliko ya ratiba ya mvua katika mikoa ya Kagera na Mbeya yaliyosababisha kukauka kwa maua na msimu wa 2011/2012 kuangukia kwenye msimu mdogo wa uzalishaji *(low season cycle)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa tumbaku umeshuka kutokana na kushuka kwa bei katika mwaka 2010/2011 na kushuka kwa mahitaji kwenye soko la dunia na hivyo kusababisha wakulima kukosa motisha ya kuzalisha tumbaku zaidi.

Jedwali Na. 1 Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Biashara

Zao	**2010/2011 Uzalishaji (Tani)**	**2011/2012 Uzalishaji (Tani)**	**Matarajio Badiliko (%)**	**2012/2013 (Tani)**
Chai	32,000	33,000	3	7,000
Tumbaku	130,000	126,624	-3	120,000
Pamba	163,644	225,938	38	355,000

Pareto 6,060	5,000	5,700	14
Mkonge 40,000	24,828	28,650	15
Kahawa 55,000	60,575	33,219	-45
Korosho 165,000	121,070	160,000	32

Chanzo: Bodi za Mazao

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, kwa ujumla uzalishaji wa mazao ya bustani uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2010/2011. Uzalishaji wa matunda uliongezeka kutoka tani 3,751,174 hadi tani 3,938,730; mazao ya mboga mboga kutoka tani 858,740 hadi tani 901,680; maua kutoka tani 9,100 hadi tani 9,850 na vikolezo *(spices)* kutoka tani 7,150 hadi tani 7,370.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la uzalishaji wa mazao ya bustani ni fursa ya kuinua kipato cha mkulima na uchumi wa nchi kama ambavyo imedhihirika katika nchi mbalimbali. Kwa mfano, nchi jirani ya Kenya ambayo haina fursa nyingi kama Tanzania mwaka 2011 ilipata takriban Dola za Kimarekani bilioni 1.35 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 389 tu ambazo Tanzania ilipata kutokana na kuuza mazao ya bustani nje ya nchi. Aidha, Tasnia ya mazao ya bustani nchini Kenya mwaka 2011 iliajiri watu milioni 4.5 ikilinganishwa na

watu 450,000 walioajiriwa na tasnia hiyo nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kunufaika na fursa zilizopo, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa mazao ya bustani itaendelea kuboresha teknolojia na miundombinu ya kilimo inayolenga kuongeza uzalishaji na biashara ya ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara inalenga kutumia fursa ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe – Mbeya kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya bustani katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi Kilele ya Mazao ya Bustani (*Tanzania Horticultural Association - TAH*A) itajenga vituo vya kukusanya mazao hayo katika mikoa ya Njombe, Morogoro, Tanga na Arusha. Vituo hivyo vitawawezesha wakulima kukusanya, kupanga madaraja, kufungasha na kuhifadhi mazao kabla ya kuyauza katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Aidha, mashamba darasa yataanzishwa kwa ajili ya kilimo cha mazao hayo katika Mikoa ya Iringa, Morogoro, Pwani, Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta uliongezeka kutoka tani 1,812,461 mwaka 2010/2011 hadi tani 2,415,880.

Jedwali Na. 2: Uzalishaji wa Mbegu za Mafuta

Na.	Zao	2010/2011 Uzalishaji (Tani)	2011/2012 Uzalishaji (Tani)	Badiliko (%)
1	Alizeti	786,902	1,125,000	43
2	Karanga	651,397	810,000	24
3	Ufuta	357,162	456,000	28
4	Mawese	17,000	24,880	46
	Jumla	**1,812,461**	**2,415,880**	**33**

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa uzalishaji wa mbegu za mafuta unaongezeka, nchi yetu inaagiza takriban asilimia 60 ya mafuta ya kula kutoka nje kwa mwaka. Fursa ya kuongeza uzalishaji hapa nchini bado ipo, na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameahidi katika hotuba yake kwamba Serikali itapitia upya vivutio vya sekta ya viwanda vya ndani vinavyotumia malighafi za ndani vikiwemo viwanda vya mafuta ya kula, Wizara yangu katika mwaka 2012/2013, itaweka mkazo katika kuendeleza uzalishaji wa mbegu za mafuta kwa

kuimarisha utafiti, uzalishaji wa mbegu bora, kuimarisha huduma za ugani na kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika usindikaji wa mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na takwimu za mazao ya kilimo kuonesha ongezeko katika uzalishaji, tija kwa mazao hayo kwa wakulima bado ni ndogo ikilinganishwa na tija inayoweza kupatikana. Kwa mfano, tija anayopata mkulima katika zao la pamba ni wastani wa tani 0.4 kwa hekta ikilinganishwa na tija inayoweza kupatikana ya tani 2.0 kwa hekta na tija anayopata mkulima katika zao la mahindi chotara ni wastani wa tani 3.9 kwa hekta ikilinganishwa na tija inayowezekana ya tani 7.5 kwa hekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastani wa tija kwa mazao mengine ni kama inavyooneshwa katika Kiambatisho Namba sita. Tija hiyo ndogo inatokana na matumizi madogo ya pembejeo za kilimo zikiwemo mbolea, mbegu bora na zana bora za kilimo. Matumizi ya mbolea hapa nchini ni wastani wa kilo 10 kwa hekta ikilinganishwa na wastani wa kilo 50 kwa hekta nchini Afrika Kusini, kilo 285 kwa hekta Vietnam na kilo 114 kwa hekta Brazil. Aidha, kilimo chetu kimeendelea kutegemea mvua kwa kiasi kikubwa na hivyo kuathiriwa na ukame wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto ya kuinua tija na uzalishaji wa mazao, Wizara yangu iliendelea kuhimiza na kuongeza matumizi ya pembejeo na zana bora za kilimo; kuimarisha huduma za kitaalam (utafiti, ugani na mafunzo); kudhibiti visumbufu vya magonjwa na

mimea; kupanua eneo la umwagiliaji na kuendeleza hifadhi ya udongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa pembejeo. Katika mwaka 2011/2012, upatikanaji wa mbolea ulikuwa tani 302,453 ikilinganishwa na tani 275,684.8 mwaka 2010/2011, sawa na ongezeko la asilimia 9.7. Hata hivyo, ongezeko hilo bado ni dogo ikilinganishwa na mahitaji halisi ya tani 485,000 kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa iliyochangia kutofikiwa lengo la mahitaji ni kupanda kwa bei ya mbolea katika soko la dunia na gharama za usafirishaji ambazo zilisababisha wafanyabiashara kusita kuagiza kiasi kikubwa cha mbolea kwa kuhofia wakulima kushindwa kumudu bei ya mbolea hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua tatizo la ongezeko la mara kwa mara la bei za mbolea, Wizara itaendelea kuhamasisha matumizi ya mbolea ya Minjingu Mazao inayozalishwa hapa nchini ambayo bei yake ni nafuu ikilinganishwa na mbolea kutoka nje. Wizara pia itaendelea kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuanzisha viwanda vya mbolea kwa kutumia rock phosphate na gesi asili nchini. Mazungumzo kati ya Serikali na wawekezaji walioonesha nia ya kuwekeza katika eneo hili yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika jitihada za kukabiliana na tatizo la uhaba na bei, Wizara

ilikubaliana na kampuni ya *YARA* kuingiza mbolea kwa wingi *(bulk importation).* Tayari kampuni hiyo imeanza ujenzi wa ghala kubwa lenye ujazo wa tani 45,000 kwa ajili ya kazi hiyo. Uagizaji wa mbolea kwa wingi utapunguza makali ya bei. Katika mwaka 2012/2013, mahitaji ya mbolea yanakadiriwa kuwa tani 485,000. Wizara itaendelea kuwasiliana na kutoa ushauri kwa makampuni yanayotengeneza na yanayoagiza mbolea ili kuhakikisha upatikanaji kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na tatizo la kuwepo kwa mbolea isiyokidhi viwango vya ubora, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kutumia Sheria ya Mbolea Na. 9 ya mwaka 2009 ilianzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania *(Tanzania Fertilizer Regulatory Authority – TFRA)*. Tayari Mamlaka hiyo imekwishaanza kazi yake katika maeneo yanayolalamikiwa kuwepo kwa mbolea isiyokidhi viwango. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuijengea Mamlaka uwezo ili itekeleze jukumu lake la kusimamia ubora wa mbolea nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, upatikanaji wa mbegu bora ulikuwa tani 28,770.22 ikilinganishwa na tani 26,545 mwaka 2010/2011 sawa na ongezeko la asilimia 8.4. Hata hivyo, ongezeko hilo bado ni dogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya tani 60,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa ya kutofikia lengo ni uzalishaji mdogo nchini ambao ulikuwa tani 13,241.8 tu. Kati ya hizo tani 3,082 zilizalishwa na Wakala wa Mbegu za Kilimo *(Agricultural*

Seed Agency – ASA) katika mashamba yake na tani 2,080 katika mashamba ya Magereza na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ambapo Sekta Binafsi ilizalisha tani 8,079.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuongeza uzalishaji wa mbegu bora hapa nchini, Wizara iliendelea kuijengea uwezo *ASA* kwa kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, ambapo visima vitano (5) vyenye uwezo wa kumwagilia hekta 200 vimechimbwa katika mashamba ya Arusha na Msimba na ujenzi wa mfereji umefanyika katika shamba la Kilangali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile zana za kulima, kupanda na kuvuna zimenunuliwa kwa ajili ya mashamba hayo. Katika mwaka 2012/2013, visima vingine vinne (4) vyenye uwezo wa kumwagilia hekta 100 vitachimbwa katika shamba la Msimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia imeruhusu Sekta Binafsi kupata mbegu mama (*breeder seeds*) kutoka katika Vituo vya Utafiti kwa madhumuni ya kuzalisha mbegu za msingi (*foundation seeds*) zitakazotumika kuzalisha mbegu zilizothibitishwa (*certified seeds*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kudhibiti mbegu zisizokidhi viwango vya ubora, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilikagua hekta 9,800 za mashamba ya kuzalisha mbegu bora. Wizara pia ilipima ubora wa mbegu kwenye maduka ya pembejeo za Kilimo katika wilaya 38. Aidha, Wizara iliboresha maabara ya Taasisi

ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu *(Tanzania Official Seed Certification Institute – TOSCI*) ili itambulike kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa maabara hiyo kutahamasisha makampuni ya mbegu ya ndani na nje ya nchi kuzalisha mbegu kwa wingi na ziada kuuzwa nje ya nchi. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kukagua mashamba ya kuzalisha mbegu na mbegu zinazoingizwa nchini na zilizoko madukani kwa lengo la kudhibiti ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, jumla ya aina 85 za viuatilifu ziliidhinishwa kwa ajili ya kuagizwa, kusambazwa, kuuzwa na kutumika kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizopo nchini. Viuatilifu hivi vinaweza kutumika na wadau mbalimbali hususan wakulima wa aina zote, wafugaji na wadau wa afya ya binadamu ili kudhibiti visumbufu vya mazao, mifugo na afya ya binadamu hivyo kuongeza tija katika kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, zimejitokeza changamoto za kuuzwa viuatilifu bandia, kuuza viuatilifu visivyosajiliwa nchini, kusambaza viuatilifu vilivyokwisha muda wa kutumika, uhamishaji wa viuatilifu toka katika viwekeo vya asili (*repacking*), kuchanganya viuatilifu na chakula kwenye sehemu za biashara, kusambaza viuatilifu visivyo na viwekeo na vibandiko sahihi na baadhi ya wauzaji kutokuwa na elimu ya viuatilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto hizo, katika mwaka 2012/2013, Wizara imepanga kufanya yafuatayo:-

(i) Kukagua ubora wa viuatilifu katika mfumo mzima wa uzalishaji, uagizaji na usambazaji na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya makampuni au wafanyabiashara watakaobainika kukiuka sheria na taratibu zilizopo ikiwa ni pamoja na kuwafutia leseni zao;

(ii) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ili kuleta ushindani na kuondoa ukiritimba katika biashara ya viuatilifu;

(iii) Kuendelea kuimarisha ofisi ya Msajili wa viuatilifu kwa kuajiri wakaguzi wa viuatilifu. Aidha, Wataalam wa Taasisi ya Kudhibiti Viuatilifu vya Kitropiki *(Tropical Pesticides Research Institute – TPRI)* watashiriki katika kuhakiki ubora wa viuatilifu; na

(iv) Kutoa mafunzo kwa wataalam wa ugani na watendaji kata kuhusu matumizi sahihi ya viuatilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa ruzuku ya pembejeo. Serikali ilianza kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima kuanzia mwaka 1974 kupitia Mradi wa Mahindi wa Taifa. Hata hivyo, katika kutekeleza mageuzi ya kiuchumi, ruzuku ya mbolea iliondolewa katika mwaka 1994/1995. Kuondolewa kwa ruzuku ya mbolea kulisababisha wakulima wengi kushindwa kununua mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na hali hiyo, katika Kikao cha Nane cha Mkutano wa 13 wa Bunge kilichofanyika tarehe 13 Novemba, 2003, Serikali ilitoa Tamko la fidia ya sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini katika msimu wa kilimo wa mwaka 2003/2004. Madhumuni ya fidia hiyo ilikuwa ni kupunguza makali ya bei ya mbolea kwa mkulima na hivyo kuchangia katika kuongeza uzalishaji wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea, ulihusisha Serikali kuingia mikataba na makampuni yaliyotakiwa kuagiza na kuifikisha kwenye vituo vikuu vya kuuzia na kuziuza kwa bei iliyokubaliwa baina ya Serikali na Makampuni. Fidia ya gharama ya usafirishaji na sehemu ya bei ya mbolea katika soko ililipwa na Serikali kwa makampuni baada ya kuwauzia wakulima pembejeo. Utaratibu huo ulionekana kuwa na kasoro nyingi ikiwemo ya pembejeo kutowafikia wakulima walengwa kwa wakati kwa sababu zifuatazo:-

(i) Wasambazaji kutozingatia mikataba waliyosaini na Serikali;

- Maandalizi hafifu ya kuteua Mawakala wenye uwezo wa kusambaza mbolea na kupanga bei za kuuzia mbolea katika kila Wilaya;

- Wakulima wakubwa kuuziwa mbolea nyingi kwa wakati mmoja na kusababisha

wakulima wadogo kutopata mbolea ya kutosha; na

- Mbolea kuvushwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondokana na kasoro zilizojitokeza, Serikali ilianza kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa kutumia utaratibu wa vocha kuanzia mwaka 2008/2009. Malengo ya utaratibu huo ni pamoja na kuongeza upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima; kuongeza uelewa wa wakulima kuhusu matumizi ya mbegu bora na mbolea na kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya chakula hususan mahindi na mpunga. Kutokana na mpango huo, kaya zilizonufaika ni 737,000 mwaka 2008/2009; 1,500,000 mwaka 2009/2010 na 2,000,000 mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilitoa ruzuku ya pembejeo za kilimo ambapo wakulima 1,781,367 walinufaika. Jumla ya tani 178,136 za mbolea na tani 18,240.34 za mbegu bora za mahindi na mpunga zilitolewa. Changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza utaratibu huo ni pamoja na vocha kuchelewa kufika kwa walengwa; uteuzi wa Mawakala na wakulima usiozingatia vigezo na udanganyifu uliofanywa na Mawakala kwa kushirikiana na Kamati za Pembejeo katika ngazi mbalimbali za utekelezaji na baadhi ya watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia mapungufu hayo, katika mwaka 2012/2013, licha ya Wizara kuendelea kutoa ruzuku ya pembejeo kwa kutumia utaratibu wa vocha, Wizara itaboresha utaratibu huo

kwa kutumia makampuni ambayo yatawajibika kuteua Mawakala watakaosambaza pembejeo kwa wakulima. Maboresho hayo yanatarajiwa kuwa na matokeo chanya yafuatayo:-

(ii) Kudhibiti upotevu wa fedha za Serikali;

(iii) Kuwezesha upatikanaji wa pembejeo kwa wakati; na

(iv) Kuhakikisha ubora wa pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza idadi ya wanufaika wa mpango wa ruzuku na kuboresha mfumo wa ugharamiaji wa pembejeo za kilimo, Serikali kwa kushirikiana na wadau inaangalia utaratibu wa kutoa mikopo ya pembejeo kwa wakulima kupitia vikundi kuanzia mwaka 2013/2014. Vikundi hivyo ni Vyama vya Ushirika vya Msingi (*SACCOS, AMCOS*); Umoja wa Umwagiliaji katika skimu; Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) na wakulima walio kwenye kilimo cha mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utaratibu huo, wakulima watakaokopeshwa watatakiwa kuwa katika vikundi vilivyosajiliwa kisheria. Ili utaratibu huo unaopendekezwa uweze kutekelezwa kikamilifu, maandalizi yanahitajika kuvifanya vikundi hivyo kuwa na sifa za kukopesheka ambazo ni pamoja na vikundi kuwa na asilimia 20 ya thamani ya mkopo na hesabu zilizokaguliwa. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau katika maandalizi hayo, ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa

wakulima, kuhamasisha uanzishwaji na kusajili vikundi vya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo ulitengewa kiasi cha Shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya kutoa mikopo ya kununulia na kusambaza pembejeo na zana za kilimo. Hadi tarehe 20 Juni, 2012 Mfuko ulipata Shilingi bilioni 2.0 kutoka Serikalini na ulikusanya marejesho ya madeni ya miaka iliyopita ya Shilingi bilioni 3.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 20 Juni 2012, Mfuko wa Pembejeo ulitoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 4.4 kwa ajili ya kununua matrekta yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.942; pembejeo za kilimo na mifugo (mbolea, vifungashio, viuatilifu na madawa ya mimea na mifugo) zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.4; na zana za umwagiliaji na usindikaji zenye thamani ya Shilingi milioni 92. Utaratibu wa kutoa mikopo ya Shilingi bilioni 1.5 zilizopokelewa mwezi Mei unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo utatoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 6.54 ikiwemo mikopo ya matrekta makubwa, matrekta madogo ya mikono, pembejeo za kilimo na mifugo, vifaa vya umwagiliaji na vifaa vya usindikaji. Changamoto kubwa ni kwa baadhi ya wakopaji kutorejesha mikopo kwa wakati na uwezo mdogo kifedha ikilinganishwa na maombi yanayopokelewa. Hivyo, natoa rai kwa wote waliokopa kurejesha kulingana na mkataba wa mkopo ili kutoa fursa kwa waombaji wengine kuweza kupata mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kuhamasisha matumizi ya zana bora za kilimo ili kupunguza harubu ya kazi na kuongeza ufanisi katika shughuli za kilimo. Kutokana na juhudi hizo matumizi ya zana yameongezeka kutoka matrekta makubwa 7,823 na madogo 3,400 mwaka 2010 hadi matrekta makubwa 8,466 na madogo 4,571 mwaka 2011. Ongezeko hilo limefanya eneo linalolimwa kwa matrekta kuongezeka kutoka asilimia 12 mwaka 2010 hadi asilimia 14 mwaka 2011, eneo linalolimwa na maksai limebaki kuwa asilimia 24 na eneo linalolimwa kwa jembe la mkono limepungua kutoka asilimia 64 hadi 62.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, jumla ya matrekta makubwa 645, matrekta ya mkono (*powertiller*) 326 na majembe ya kukokotwa na wanyamakazi 49,794 yaliingizwa nchini na Sekta binafsi. Aidha, kati ya matrekta 1,860 yaliyoingizwa nchini na SUMA JKT mwaka 2010/2011, hadi kufikia tarehe 8 Julai 2012, matrekta 780 yamekwishauzwa. Ili kuwawezesha wakulima wengi kumudu kununua matrekta, Serikali imepunguza bei ya matrekta hayo kwa kati ya asilimia 15 hadi 36 kama inavyooneshwa kwenye.

Jedwali Na. 3: Punguzo la Bei ya Matrekta yanayouzwa na SUMA JKT

Na.	**Trekta**	**Bei ya Zamani**	**Bei Mpya**	**Punguzo**

		(Sh.)	(Sh.)	%
1.	*Farmtrac 60 (50 HP; 2wd)*	25,635,759	16,480,952	35.71
2.	*Farmtrac 60DT (50 HP; 4wd)*	32,751,160	23,267,522	28.96
3.	*Farmtrac 70 (60 HP; 2wd)*	34,737,675	23,155,067	33.34
4.	*Farmtrac 70DT (60 HP; 4wd)*	39,569,957	30,489,632	22.95
5.	*New Holland 75 HP; 2wd*	40,477,573	31,030,487	23.34
6.	*New Holland 75 HP; 4wd*	45,821,307	38,784,527	15.36

Chanzo: SUMA JKT

Mheshimiwa Naibu Spika, matrekta ya SUMA JKT yanauzwa kwa wakulima, vikundi na Vyama vya Ushirika kwa fedha taslimu au mkopo unaomtaka mnunuzi kutanguliza asilimia 30 ya bei ya trekta au kwa kuweka dhamana ya mali isiyohamishika. Aidha, muda wa kurejesha mkopo umeongezwa kutoka miaka miwili (2) hadi minne (4). Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Umma wanaweza kukopa kwa kudhaminiwa na waajiri wao. Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa Mikoa na Wilaya kukopa na kuhamasisha wananchi kutumia fursa hii kukopa matrekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha usimamizi wa ubora wa mashine za kilimo zinazoingizwa nchini, Wizara ilishiriki katika mikutano ya kitaalam chini ya usimamizi wa Shirika la Viwango Tanzania *(Tanzania*

Bureau of Standards – TBS) katika kuandaa viwango vya ubora wa matrekta (TZS 1415:2011), jembe la plau linalokokotwa na trekta (TZS 1416:2011) na trekta la mkono (TZS 1417:2011). Aidha, utaratibu wa kukagua ubora wa zana za kilimo yakiwemo matrekta kutoka nje ya nchi umeandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utafiti wa kilimo. Katika mwaka 2011/2012, Wizara ilitoa na kuidhinisha aina mpya 16 za mbegu za mazao kupitia Vituo na Taasisi za Utafiti. Mbegu hizo ni aina mbili (2) za ulezi, moja (1) ya maharagwe, nne (4) za muhogo, nne (4) za chai na tano (5) za kahawa. Aidha, Sekta Binafsi ilitoa aina 10 za mbegu mpya kupitia makampuni ya *Pioneer Overseas, Tanzania Breweries, Suba - Agro Trading and Engineering, Monsanto* na *Meru Agro - Tours and Consultants.*

Mheshimiwa Naibu Spika, aina na sifa za mbegu hizo ni kama zinavyoonyeshwa katika Kiambatisho Namba nane. Katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia vituo na taasisi za utafiti itaendelea kutafiti aina za mbegu mpya za mazao zinazotoa mavuno mengi, zinazokomaa mapema, zinazostahimili ukame, zenye ukinzani dhidi ya magonjwa na visumbufu vya mimea na zinazokidhi viwango vya ubora na matakwa ya wadau na soko kwa lengo la kupata mbegu bora. Aina 10 za mbegu bora za mazao zinatarajiwa kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imezalisha tani 29.2 za mbegu mama zikiwemo mpunga tani 0.4, mahindi tani 1.88, ngano tani 7.0, mtama tani 1.0,

uwele tani 0.3, maharagwe tani 8.0, mbaazi tani 5.5, kunde tani 1.5, choroko tani 0.84, karanga tani 0.823 na ufuta tani 0.959. Mbegu hizo zimezalishwa kwa ajili ya kuzalisha mbegu za msingi na hatimaye kupata mbegu zilizothibitishwa ambazo husambazwa kwa wakulima. Katika mwaka 2012/2013, Wizara inatarajia kuzalisha tani 16 za mbegu mama na pingili milioni 2.3 za muhogo, vipando 181,500 vya viazi vitamu na miche 200,000 ya mizabibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kufanya utafiti wa bayoteknolojia kwa njia ya tishu kwa lengo la kupata miche bora ya muhogo, zabibu na viazi vitamu inayostahimili magonjwa. Kwa kutumia utafiti huo, Wizara imebaini aina mbalimbali za virusi vya magonjwa ya batobato na michirizi ya kahawia na kuainisha maeneo yenye virusi hivyo. Katika utafiti huo aina tatu (3) ya nzi weupe wanaosambaza magonjwa ya muhogo na viazi vitamu waligunduliwa na pia uhusiano wao wa kijenetiki ulibainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo haya yatasaidia kubuni mbinu sahihi za kukabiliana na magonjwa hayo. Vilevile, utafiti umeboresha aina saba (7) za mbegu za muhogo wa kienyeji kwa kuziwekea jeni (*gene*) za ukinzani dhidi ya magonjwa ya batobato ya muhogo kwa njia ya Uhandisi Jeni *(Genetic Engineering)* na hivi sasa zipo katika hatua ya maabara. Utafiti huo utaendelea katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia ya uhandisi jeni ambayo huzalisha *Genetically Modified Organisms*

(GMO) katika kilimo inaweza kuongeza ubora na uzalishaji wa mazao ya kilimo; kupunguza gharama za uzalishaji; kuhifadhi mazingira kwa kupunguza matumizi ya madawa na mbolea; kusafisha mazingira na uzalishaji wa nishati mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, yapo madhara yanayoweza kutokea kama hakutakuwa na utafiti wa kutosha katika teknolojia ya Uhandisi Jeni. Madhara hayo ni pamoja na uharibifu wa bayoanuai na uoto wa asili na uchavushaji wa mazao na mimea mingine; utegemezi kwa kampuni chache; ongezeko la sumu na mzio (*allergy*); uharibifu kwa viumbe ambavyo havikukusudiwa; kuongezeka kwa magugu na kuibuka kwa visumbufu na magonjwa sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na faida za uhandisi jeni, na ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea kuna umuhimu wa kuendelea kufanya utafiti. Hivyo, Wizara yangu imeongeza uwezo wa Vituo vya Utafiti vya Mikocheni na Makutupora ili kuweza kufanya utafiti huo kwa kusomesha wataalam na kujenga maabara ya kisasa ya Uhandisi Jeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, utafiti huu umekwama kutokana na masharti magumu yaliyomo katika Kanuni za Kusimamia Matumizi Salama ya Bayoteknolojia (*Biosafety Regulations*, 2009). Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itashirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na wadau wengine kuangalia uwezekano wa kurekebisha Kanuni hizo ili kuwezesha utafiti huu muhimu uendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kuhakiki teknolojia za urutubishaji husishi wa udongo *(Integrated Soil Fertility Management Options)* kulingana na ikolojia za kilimo kwa lengo la kuwawezesha wakulima kutumia aina na viwango sahihi vya mbolea kulingana na aina ya udongo katika maeneo yao. Aidha, Wizara kwa kupitia maabara za udongo za Vituo vya Utafiti vya Mlingano, Uyole, Selian na Ukiriguru imechunguza sampuli 3,410 za udongo kutoka kwa wadau mbalimbali kwa lengo la kupima viwango vya virutubisho katika udongo ili kutoa ushauri wa matumizi bora ya mbolea.

Matokeo ya awali yanaonesha maeneo mengi yaliyochunguzwa yana upungufu wa virutubisho vya Naitrojeni, Fosforasi na Potasiamu. Pia maeneo muhimu yanayolima mpunga na mahindi yana upungufu wa virutubisho vya aina ya Salfa, Kalsiamu na Magneziamu. Wizara inahamasisha matumizi ya mbolea kulingana na mahitaji ya udongo katika maeneo husika na kilimo cha mzunguko wa mahindi na mazao ya jamii ya mikunde kama maharagwe na soya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Vituo vya Utafiti vya Mlingano, Uyole, Selian na Ukiriguru itakamilisha mradi wa kuhakiki na kupendekeza teknolojia tano za urutubishaji husishi wa udongo (*Integrated Soil Fertility Management Options*) kulingana na ikolojia za kilimo zilizoko katika Wilaya 53 ambazo zinapata ruzuku ya pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kufanya utafiti wa sayansi ya jamii na uchumi kuhusu matumizi ya teknolojia na mbinu bora za kilimo pamoja na kufanya uchambuzi wa matumizi ya pembejeo na mapato (*farm budgets*) kwa mazao mbalimbali. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwepo kwa tofauti kubwa ya mapato kwa wakulima wanaotumia pembejeo na kuzingatia kanuni bora za kilimo ikilinganishwa na wale wanaolima kwa mazoea kama inavyooneshwa katika Jedwali Namba nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo hayo yatatumika kuwashauri wakulima kuchagua mazao, kutumia pembejeo na mbinu bora za uzalishaji ili kuongeza tija. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kufanya utafiti katika Kanda zote, ili kubaini faida inayoweza kupatikana katika kilimo cha mazao mbalimbali nchini.

Jedwali Na. 4: Faida inayoweza kupatikana kwa kutumia mbegu bora na Kanuni Bora za Kilimo (Sh/Ha)

Zao	**Kilimo cha kanuni bora za Kilimo**	**Mbegu Mazoea**	**Mbegu Bora na Kufuata**
Karanga (Kanda ya Kusini)		538,000	706,500	1,010,000

Mpunga (Kanda ya Magharibi)	406,500	1,134,500	2,967,500
Mahindi (Kanda ya Ziwa)	667,000	1,151,500	1,956,500
Pamba (Kanda ya Ziwa)	828,300	-	1,279,300
Mpunga (Kanda ya Ziwa)	1,713,800	2,697,500	3,332,000
Mtama (Kanda ya Ziwa)	565,500	796,400	1,434,400

Chanzo: Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ya Kanda ya Ziwa yanayolima migomba yanakabiliwa na ugonjwa wa unyanjano ambao husababishwa na bakteria *(Bacterium Xanthomona campestres pv musacearum*). Ili kukabiliana na ugonjwa huo, Wizara kupitia Kituo cha Utafiti cha Maruku imetoa mafunzo ya jinsi ya kuutambua na mbinu sahihi za kuudhibiti kwa Maafisa Ugani na Wakulima wa maeneo yaliyoathiriwa na ugonjwa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, machapisho 4,000, vitini 100, majarida na vipeperushi 10,000 vyenye ujumbe wa jinsi ya kudhibiti ugonjwa huo vimesambazwa. Aidha, vitalu 133 vimeanzishwa na vimetoa miche ya migomba safi 2,037,220. Pia wakulima wamefundishwa njia rahisi na nyepesi ya kuzalisha miche safi ya migomba ili kuepuka ugonjwa huo. Katika kuendeleza jitihada za kukabiliana na ugonjwa wa unyanjano wa migomba, katika mwaka 2012/2013, Wizara itapeleka wakulima kutoka Mkoa wa Kagera kwenda nchini

Uganda kwa ziara ya mafunzo ambako kwa kiasi kikubwa wameweza kudhibiti ugonjwa huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, magonjwa ya batobato na michirizi ya kikahawia katika zao la muhogo yameenea katika mikoa ya Mwanza, Mara, Kagera, Mtwara na Mbeya. Utafiti unaonesha kwamba ugonjwa wa batobato hupunguza uzalishaji kwa takriban asilimia 95 wakati michirizi ya kikahawia hupunguza kwa asilimia 74. Katika kukabiliana na magonjwa hayo, Wizara imetoa vipando bora vya muhogo vinavyozaa sana na vyenye ukinzani wa magonjwa hayo. Baadhi ya vipando hivyo ni Pwani, Kiroba, Mkombozi, Mkumba, Dodoma, Makutupora, Mumba, Hombolo na Kyaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikisha vipando hivyo kwa wakulima, katika mwaka 2011/2012, Wakala wa Mbegu wa Taifa *(ASA)* kwa kushirikiana na Magereza umezalizasha vipando bora vya muhogo 20,101,866. Kati ya hivyo, vipando 13,553,466 vimezalishwa katika Magereza ya Kiabakari (8,855,000), Ilagala (350,000), Kibondo (180,000), Kilimo Urambo (15,000), Kanegele (2,639,520), Ushora (225,946), Kitengule (440,000), Butundwe (83,000), Kasungamile (765,000) kwa ajili ya Kanda Magharibi na Kanda ya Ziwa. Vipando 6,548,400 vimezalishwa katika magereza ya Kanda ya Mashariki kwa ajili ya maeneo mengine. Katika mwaka 2012/2013, *ASA* kwa kushirikiana na Magereza itazalisha vipando vya muhogo 15,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za ugani. Mojawapo ya changamoto katika kilimo ni wakulima wengi kutokuwa na uelewa wa kanuni za kilimo bora na za kisasa. Katika jitihada za kuhakikisha wakulima wanapata stadi za kilimo, Wizara imeendelea kuboresha huduma za ugani kwa lengo la kueneza teknolojia za kilimo kwa kutumia Mbinu Shirikishi Jamii, ikiwa ni pamoja na matumizi ya Shamba Darasa. Jumla ya Mashamba Darasa 7,515 yenye wakulima 148,460 (wanawake 74,270 na wanaume 74,170) yametumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kuimarisha mfumo wa kupeleka teknolojia kwa wakulima, Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata *(Ward Agricultural Resource Centers - WARCs)* 147 vimejengwa na 65 vimekarabatiwa katika Halmashauri 61 za mikoa 19 ya Tanzania Bara kwa lengo la kutoa mafunzo ya teknolojia mbalimbali kwa wakulima. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kueneza teknolojia kwa kutumia Mbinu Shirikishi Jamii katika kilimo kwa kuongeza matumizi ya Mashamba Darasa kufikia 10,000 yenye wakulima 250,000. Aidha, Wizara itatumia wataalam wa ugani 150 waliopatiwa mafunzo kuandaa na kusimamia Mashamba Darasa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Programu ya Kilimo Afrika Mashariki ya Kuongeza Tija na Uzalishaji *(Eastern Africa Agricultural Productivity Programme - EAAPP)* ilitoa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga, ngano na muhogo kwa Maafisa Ugani 149 na Wakulima Wawezeshaji 170 kutoka katika Halmashauri za Wilaya 26 katika mikoa ya Mbeya, Mwanza, Mara,

Morogoro, Shinyanga, Kagera, Kigoma, Manyara, Iringa, Rukwa na Kilimajaro. Wakulima wawezeshaji hao wataendelea kutoa mafunzo kwa wakulima (*Farmer-to-Farmer Extension*) katika skimu zao kupitia mbinu shirikishi ya Shamba Darasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha utoaji wa mafunzo, Kitabu cha Kilimo Bora cha Mpunga kimeandaliwa na miongozo ya kufundishia kilimo bora cha muhogo, ngano, mpunga na usindikaji wa mpunga (kwa ajili ya wataalam wa ugani) iliandaliwa na itasambazwa wakati wa maonesho ya Nane Nane 2012. Jumla ya vipindi 44 vya redio na runinga vinavyohusu ukulima wa kisasa vilirushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeratibu maonesho ya Sikukuu ya Wakulima (Nane Nane) yaliyofanyika Kitaifa Dodoma na kanda za kilimo za Mbeya, Morogoro na Arusha. Katika maadhimisho hayo, Wizara kwa kushirikiana na *YARA Tanzania Limited, Export Trading Company, ASA, TANSEED International, Agricultural Harvest, Aquasolar Ltd na Aquawell Drilling Company* ilitoa zawadi kwa wakulima bora tisa (9): Wakulima bora wa mazao watatu (3), Wamwagiliaji maji bora watatu (3) na Vyama vya Ushirika bora vitatu (3).

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, zawadi zilitolewa kwa wakulima bora wa mazao makuu ya biashara ya kahawa, chai na mkonge. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuratibu maonesho ya Sikukuu ya Wakulima (Nane Nane) yatakayofanyika

Kitaifa Dodoma na Kanda za Kilimo za Mbeya, Morogoro na Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya Maafisa Ugani na wakulima. Ili kufikia lengo la kuwa na Afisa Ugani mmoja kwa kila Kijiji na Kata tulilojiwekea mwaka 2007/2008, Maafisa Ugani 15,082 wanahitajika. Katika kuongeza idadi ya Maafisa Ugani, Wizara ilidahili na kufundisha wanachuo 3,485 mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI imeajiri vijana tarajali 2,948 waliohitimu mafunzo na kufanya idadi ya Maafisa Ugani kufikia 7,974. Vijana tarajali 1,514 wenye Astashahada ambao hawakupata ajira mwaka 2011/2012 na vijana tarajali 1,000 waliohitimu mwezi Juni 2012 wameombewa kibali na wataajiriwa katika mwaka 2012/2013. Wizara pia imekarabati Chuo cha Kilimo Mubondo - Kasulu kwa lengo la kupokea wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itagharamia mafunzo ya kilimo kwa vijana 3,500 wakiwemo wa Stashahada na Astashahada kwa ajili ya kuongeza idadi ya Maafisa Ugani. Aidha, Wizara itakarabati majengo katika Vyuo vya Kilimo vya *KATC* - Moshi na Tumbi - Tabora. Vile vile, Wizara itaboresha mtaala wa matumizi bora ya ardhi na kuchapisha vitabu vya kiada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao. Wizara iliendelea kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao

ambavyo husababisha upotevu wa mavuno wa kati ya asilimia 30 na 40 kwa mazao ya nafaka iwapo havitadhibitiwa. Visumbufu hivyo ni kwelea kwelea, nzige wekundu, viwavijeshi, panya na magonjwa ya mimea. Katika mwaka 2011/2012, udhibiti wa nzige wekundu ulifanyika kwenye mazalia ya asili katika mbuga za Iku-Katavi, Ziwa Rukwa na Wembere katika hekta 6,000 na kuokoa tani 150 za zao la mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa ndege aina ya kwelea kwelea ulifanyika katika hekta 2,134 katika mikoa ya Mwanza (Misungwi), Shinyanga (Shinyanga Vijijini, Maswa, Kishapu), Tabora (Igunga), Singida (Singida Mjini, Singida Vijijini), Dodoma (Dodoma Mjini, Chamwino, Bahi na Kondoa) na Mbeya (Mbarali) ambapo tani 734 za nafaka ziliokolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, udhibiti wa panya ulifanyika katika hekta 88,632 kwenye vijiji 322 vya mikoa ya Morogoro, Lindi na Pwani ambapo takriban tani 3,988 za nafaka na muhogo ziliokolewa. Wizara pia ilidhibiti viwavijeshi katika mikoa ya Singida, Dodoma, Morogoro, Mbeya, Mtwara na Lindi sambamba na huduma ya utabiri wa viwavijeshi katika maeneo yote ambayo huvamiwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliingiza nchini manyigu 14,481 kwa lengo la kudhibiti nzi wa matunda ajulikanae kama *Bactrocera invadens* na kuyasambaza kwenye wilaya za Kibaha na Mkuranga. Aidha, Wizara ilisambaza lita 150 za kivutia wadudu aina ya *Methyl eugenol* katika Wilaya 15 nchini kwa ajili ya kudhibiti nzi wa matunda. Vilevile, Wizara ilizalisha

na kusambaza mbawakavu milioni 15 katika Ziwa Viktoria pamoja na mabwawa 22 ili kudhibiti gugumaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kudhibiti uenezaji wa visumbufu vya mimea inayoingia nchini na inayosafirishwa nchi za nje, Wizara ilikagua jumla ya tani 791,493.57 za mazao mbalimbali yaliyosafirishwa nchi za nje na tani 445,383.34 za mazao yaliyoingizwa nchini. Vyeti 6,009 vya usafi wa mazao na vibali 517 vya kuingiza mazao nchini vilitolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujenga uwezo wa kudhibiti na kutoa huduma za afya ya mimea, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilitoa mafunzo kwa wakaguzi wa mazao 56 na kuajiri Wakaguzi 25. Ili kuweza kukabiliana na milipuko ya visumbufu vya mimea kwa wakati, katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu imetenga Shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kununua ndege ya kunyunyizia madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji unazingatia Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010 na Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002. Maeneo ya kipaumbele ni uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji; matumizi ya teknolojia za umwagiliaji zenye ufanisi katika matumizi ya maji na tija katika uzalishaji wa mazao na utoaji wa huduma za kitaalam kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilikusudia kuendeleza eneo la umwagiliaji lenye jumla ya hekta 40,000. Kati ya eneo

hilo, hekta 21,965 ni za skimu 24 ambazo zililengwa kuendelezwa kwa kutumia fedha kutoka Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Umwagiliaji (*National Irrigation Development Fund - NIDF*) na hekta 18,035 zinatokana na skimu 136 zilizolengwa kutumia fedha kutoka Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji Ngazi ya Wilaya (*District Irrigation Development Fund – DIDF*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, eneo lililoanza kuendelezwa ni hekta 17,824 sawa na asilimia 45 ya lengo. Kati ya hizo hekta 8,594 ni za skimu nane ambazo zinatekelezwa kwa kutumia fedha za *NIDF* na hekta 9,230 zimetokana na skimu 26 zinazoendelezwa kwa kutumia fedha za *DIDF*. Utekelezaji huo umekuwa chini ya lengo kutokana na fedha kidogo ambazo pia zilichelewa kupatikana. Kutokana na hali hiyo, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea na ujenzi wa skimu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara imeendelea kujenga mabwawa nane (8). Kati ya hayo, mabwawa ya Inala (Tabora–Manispaa), Mahiga (Kwimba), Lwanyo (Mbarali), Dongobesh (Mbulu) na Mesaga (Serengeti) yapo katika hatua za ujenzi. Mabwawa ya Idodi (Iringa Vijijini), Mang'onyi (Singida) na Masengwa (Shinyanga Vijijini) yapo katika hatua ya kuandaa zabuni. Ujenzi wa mabwawa hayo utakamilika katika mwaka 2012/2013. Mabwawa mengine tunayotarajia kujenga ni Kasuga (Kakonko), Ulindwanoni (Kaliua), Kalembela (Urambo), Gidahababieg (Hanang), Ngipa (Kiteto), Msange (Singida), Mongoroma - Serya (Kondoa) na Tlawi (Mbulu).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara pia kupitia mradi wa *DASIP* ilikamilisha usanifu wa skimu 27 za umwagiliaji zenye uwezo wa kuongeza eneo la umwagiliaji la hekta 2,546. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itakamilisha ujenzi wa skimu hizo. Skimu zilizo chini ya Mradi wa *DASIP* zinatarajiwa kuongeza eneo litakalomwagiliwa katika Mkoa wa Shinyanga kwa hekta 604 ili kupunguza tatizo la upungufu wa chakula linalotokana na ukame wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, skimu 34 za umwagiliaji zenye eneo la jumla ya hekta 23,510 zimefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu 24 zenye hekta 2,250 zitakazotumia teknolojia zenye ufanisi katika matumizi ya maji kwa njia ya matone na kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya mizabibu, migomba na pamba unaendelea. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutafuta fedha kutoka Serikalini na vyanzo vingine kwa ajili ya ujenzi wa skimu hizo. Aidha, skimu nyingine 20 zenye hekta 30,000 zitafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu katika mwaka 2012/2013, itasimamia uendelezaji wa skimu za umwagiliaji 21 zenye eneo la hekta 19,567 ambapo skimu 15 zitagharamiwa na Mfuko wa Pamoja wa Serikali ya Tanzania na Japan (*Food Aid Counterpart Fund – FACF)* na skimu sita zitagharamiwa na Shirika la Misaada la Marekani (*United States Agency for*

International Development – USAID) kupitia programu ya *Feed the Future*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta Binafsi pia imeonesha ushiriki wake katika kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji. Katika mwaka 2011/2012, baadhi ya wawekezaji na maeneo ambayo sekta hiyo imewekeza ni pamoja na *Aviv Tanzania Limited* na *Lipokela Southern Farm Limited* (Songea) hekta 470 za umwagiliaji kwa njia ya matone kwa zao la kahawa; *Kilombero Plantation Limited – KPL* (Kilombero) hekta 200 za umwagiliaji kwa njia ya kunyunyizia (*Center Pivot*) kwa zao la mpunga; Mlilingwa *Agro-Based International Limited* (Morogoro) hekta 12 za umwagiliaji kwa njia ya matone kwa mazao ya mbogamboga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia *Shiwanda Farm* (Mbozi) hekta 150 za umwagiliaji kwa kunyunyizia na njia ya matone kwa zao la kahawa; *Rubana Farm* (Bunda) hekta 50 kwa zao la mpunga; Mtitaa (Bahi) hekta 12 za umwagiliaji kwa njia ya matone kwa zao la zabibu na Mkiwa (Singida) hekta 20 za umwagiliaji kwa njia ya matone kwa zao la zabibu. Wizara yangu itaendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuongeza kasi ya kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza tatizo la uhaba wa wataalam wa umwagiliaji, mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliendelea kuwasiliana na Vyuo vya elimu ya juu ambavyo tulishirikiana navyo kuandaa mitaala ya fani ya Uhandisi Ujenzi na Umwagiliaji. Vyuo hivyo ni pamoja na Chuo cha Ufundi

cha Arusha na Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji. Katika Chuo cha Arusha, wanafunzi 51 wa Shahada ya Kwanza ya Uhandisi Ujenzi na Umwagiliaji na wanafunzi 41 katika ngazi ya Stashahada wanaendelea na masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji wanafunzi 12 wanaingia mwaka wa pili wa masomo katika ngazi ya Stashahada. Wanafunzi hao wamekuwa wakipangwa kufanya mafunzo kwa vitendo katika miradi ya kuendeleza skimu za umwagiliaji inayosimamiwa na Kanda za Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Chuo cha Ufundi cha Arusha kitadahili wanafunzi 30 katika ngazi ya Shahada na 50 katika ngazi ya Stashahada. Aidha, Wizara yangu itawasiliana na Vyuo vya Sayansi na Teknolojia, Mbeya; Chuo cha Uhandisi cha Mtakatifu Joseph, Dar es Salaam na Nelson Mandela cha Sayansi na Teknolojia Afrika, Arusha kwa madhumuni ya kuandaa kwa pamoja mitaala inayohusu mafunzo katika fani ya uhandisi wa umwagiliaji ili vyuo hivyo viweze kutoa mafunzo katika fani hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hifadhi ya udongo na matumizi ya ardhi. Wizara ina jukumu la kuhakikisha kuwepo kwa matumizi bora na endelevu ya ardhi ya kilimo. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na TAMISEMI iliendelea kupima maeneo kwa ajili ya matumizi

mbalimbali ya kilimo kwa lengo la kuondoa migogoro na kuainisha maeneo yanayofaa kwa uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kuainisha na kupima maeneo yanayofaa kwa uwekezaji kwa kilimo katika Vijiji vinane (8) vya Nyarutanga (hekta 141.1), Mbwade (hekta 1,905.47) na Bwila juu (hekta 1,533) katika Mkoa wa Morogoro na Vijiji vya Gwata (hekta 14,637.69), Sofu (hekta 14,172.02), Mafumbi (hekta 2,267.66), Pongwekiona (hekta 3,000) na Mkoko (hekta 1,500) katika Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeratibu uhakiki, uhuishaji na upimaji wa mipaka ya maeneo yanayomilikiwa na Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Selian; Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo vya Ukiriguru, Tumbi na Naliendele; *TPRI* Arusha pamoja na vituo vyake vya Mabogini, Magugu na Ngarenaro na shamba la mbegu la Dabaga (Kilolo) linalomilikiwa na *ASA*. Upimaji umekamilika na utaratibu wa kupata hatimiliki unaendelea. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kupima maeneo ya vituo vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Utalii na Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe imeandaa mpango wa kina wa matumizi bora ya ardhi katika Kijiji cha Gwata Wilayani Kisarawe ili kiwe kijiji cha mfano katika kutafsiri kwa vitendo utekelezaji wa mipango ya

matumizi bora ya ardhi ya vijiji inayoratibiwa na Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hiyo imetekelezwa kwa kuandaa ramani inayoainisha maeneo yaliyotengwa kwa matumizi mbalimbali kama vile makazi, kilimo, ufugaji, misitu na hifadhi. Pia sampuli za udongo kwenye mashamba ya wakulima zilikusanywa kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara ili kubaini aina za udongo na viwango vya rutuba na hivyo kushauri ipasavyo juu ya aina za mazao yanayofaa kupandwa na matumizi sahihi ya mbolea, ardhi na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kushirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula Duniani *(FAO)* na Halmashauri za Wilaya za Ngorongoro na Moshi Vijijini kutekeleza mradi wa *Globally Important Agricultural Heritage Systems* unaosaidia jamii za wafugaji wa kijiji cha Engaresero kwa kuboresha na kuhifadhi mifumo ya asili ya usimamizi na matumizi ya rasilimali za malisho na vyanzo vya maji na pia kilimo mseto (*Chagga home gardens*) katika Kijiji cha Shimbwe Juu, Kata ya Uru Wilaya ya Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wakulima 65 katika kijiji cha Shimbwe Juu wamewezeshwa kulima zao la *Vanilla* na pia kuboresha kilimo chao cha kahawa kwa njia ya kilimo hai ambapo wakulima 630 wamepewa mafunzo. Miche 12,000 ya kahawa bora imegawiwa kwa wakulima hao na kupandwa na mingine 18,000 itaongezwa. Kazi hiyo inafanywa kwa kushirikiana na Chama Kikuu cha Ushirika cha *KNCU*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwezesha upatikanaji wa masoko ya bidhaa za kilimo. Upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo ni kivutio kikubwa katika kuchochea uzalishaji. Kwa kiasi kikubwa masoko ya mazao makuu ya biashara yana mfumo wa soko unaosimamiwa na Bodi za Mazao husika. Hata hivyo, mfumo huo bado unategemea uuzaji wa mazao nje unoathiriwa na mabadiliko ya bei ya mara kwa mara katika soko la dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mazao ya chakula, bustani na mbegu za mafuta hayana mfumo rasmi wa soko unaowezesha ushindani. Kutokana na hali hiyo, wanunuzi hununua mazao kutoka kwa mkulima kupitia mfumo usio rasmi ikiwa ni pamoja na kununua mazao yakiwa shambani. Changamoto nyingine ni kukosekana kwa taarifa sahihi na miundombinu ya masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara inaendelea kuimarisha Bodi za Mazao ili zitekeleze majukumu yake ya usimamizi na ufuatiliaji wa masoko ya mazao husika kikamilifu; kurejea Sheria za Mazao na Kanuni zake kwa lengo la kuondoa mapungufu yaliyopo; kuhamasisha uongezaji thamani mazao; kuimarisha miundombinu ya masoko na kuanzisha soko la bidhaa za mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Masoko ya Mazao ya Kilimo. Wizara kupitia Bodi za Mazao iliendelea kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi kwa mazao makuu ya biashara ya kahawa, korosho, pamba, pareto, tumbaku na mkonge yaliyozalishwa

katika mwaka 2011/2012. Hadi kufikia mwezi Juni 2012, mazao yote yameuzwa isipokuwa tani 13,500 za korosho ambazo zipo kwenye maghala, zikisubiri kuchukuliwa na mnunuzi ambaye amekwishapatikana. Maandalizi ya masoko kwa ununuzi wa mazao ya msimu wa 2012/2013, yameanza ambapo majadiliano ya bei dira kwa mazao ya pamba, Pareto na Chai yamefanyika. Wizara pia itaendelea kusimamia kwa karibu na kuboresha utendaji wa Bodi za Mazao kwa lengo la kuhakikisha zinatoa huduma bora zaidi kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwenendo wa bei za mazao makuu; kati ya mwaka 2007/2008 na 2011/2012, bei za mazao makuu ya biashara ya mkonge, chai, pareto na kahawa (*Robusta*) katika soko la dunia ziliongezeka. Bei ya mazao ya pamba, kahawa (*arabica*), tumbaku na korosho yana mwenendo wa kupanda na kushuka). Mabadiliko hayo ya bei yanaathiri bei anayopata mkulima, hususan pale bei zinaposhuka sana. Kutokana na hali hiyo, katika mwaka 2012/2013, Wizara itashauriana na wadau wa mazao hayo kuangalia uwezekano wa kuanzisha mifuko maalum ya kufidia bei za mazao kwa wakulima pale inaposhuka *(Price Stabilization Funds).*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara itafanya mapitio ya mifumo ya masoko ya mazao kwa lengo la kuhakikisha mkulima anapata sehemu kubwa ya bei ya soko. Katika kuimarisha masoko ya mazao hayo, natoa wito kwa wadau wote wanaohusika na ununuzi wa mazao ya wakulima kuanza kutafuta masoko mengine nje ya yale ya asili ili kupanua wigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala kwa lengo la kuwawezesha wakulima kupata bei nzuri. Kupitia Vyama vya Ushirika, mazao ya kahawa, korosho na ufuta yanatumia mfumo huo. Katika mwaka 2011/2012, Vyama vya Ushirika vya Msingi 43 wilayani Mbinga viliweza kukusanya na kuuza tani 1,522.46 za kahawa kwa wastani wa bei ya Shilingi 9,000 kwa kilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Vyama wanachama wa Vyama Vikuu vya Ushirika vya *TAMCU Limited, ILULU Limited, MAMCU Limited, TANECU Limited, DARECU Ltd na CORECU Limited* vimekusanya tani 154,544 za korosho sawa na asilimia 115.7 ya lengo na kuuza tani 152,896.9 kwa wastani wa bei ya Sh. 1,614 kwa kilo. Uhamasishaji wa matumizi ya mfumo huo kwa mazao mengine umeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio ya mfumo huo, bado kuna changamoto ya wakulima kutoelewa vizuri utaratibu unavyotumika, ukosefu wa uwazi katika biashara inayofanyika, hivyo wanachama kutofahamu mapato na gharama zinazotumika na malipo ya mwisho wanayostahili kupata. Wizara itaendelea kuhimiza viongozi wa Vyama vya Ushirika kutoa elimu na taarifa kuhusu taratibu zinazotumika katika kuuza mazao na taarifa za mwenendo wa masoko ya mazao kwa wanachama wao. Aidha, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaeneza Mfumo wa Stakabadhi za Maghala katika Mikoa ya Mbeya na Mara (kahawa); Singida (alizeti) na Skimu za umwagiliaji 27 (mpunga).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara inaendelea kuimarisha Mfumo wa Stakabadhi za Maghala ili uweze kutumika kama msingi wa uanzishwaji wa Soko la Bidhaa na Mazao ya Kilimo *(Commodity Exchange)*. Maandalizi ya uanzishwaji wa soko hilo yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za Serikali za kuweka mfumo wa usimamizi wa mazao ambayo hayana bodi, Serikali ilianzisha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko mwaka 2010/2011, kwa lengo la kufanya biashara na kuendeleza mazao hayo. Aidha, Serikali iliendelea kujenga uwezo wa Bodi hiyo kwa kuteua Bodi ya Wakurugenzi, kuandaa Muundo wa Bodi, Miundo ya Watumishi, kukamilisha kanuni za Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko na kukabidhiwa mali zilizokuwa za Shirika la Usagishaji la Taifa *(National Milling Corporation - NMC)* zilizoko Iringa na Mwanza. Utaratibu wa kukabidhiwa mali nyingine unaendelea. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kujenga uwezo wa Bodi kwa kuajiri watumishi na kuiwezesha kuanza kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, *NFRA* ilinunua tani 125,000 za mahindi kutoka kwa wakulima. Katika kuwezesha upatikanaji wa masoko kwa wakulima, *NFRA* imeuza tani 80,000 za mahindi kwa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani *(World Food Programme - WFP)* kupitia mradi wa *Purchase for Progress (P4P)*. Katika mwaka 2012/2013, *NFRA* itanunua tani 200,000 za mahindi na kati ya hizo tani 100,000 zitauzwa kwa *WFP*. Zoezi hili likifanikiwa

litatoa mwanya kwa *NFRA* kununua mahindi zaidi kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NFRA* ilianza ununuzi wa mahindi tarehe 15 Julai 2012 katika Vituo vya Sumbawanga, Songea, Mbozi na Dodoma na ununuzi katika vituo vingine utaanza mwezi Agosti 2012 kutegemea kiwango cha ukavu wa mahindi. Aidha, katika kutumia fursa ya soko la nchi zinazotuzunguka ikiwa ni pamoja na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, *SADC* na Pembe ya Afrika wanunuzi wengine wataruhusiwa kununua na kuuza mazao ya chakula yanakohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Mradi wa *DASIP* ilijenga maghala 17, masoko 22, barabara za vijijini zenye jumla ya kilomita 126 na vituo vya ukusanyaji maziwa 36. Aidha, Wizara tayari imepata wataalamu elekezi wa kusanifu na kusimamia ujenzi wa masoko ya kimkakati *(strategic markets)* ya Nyamaraga (Tarime), Murongo na Nkwenda (Karagwe), Kabanga (Ngara) na Busoka (Kahama). Utaratibu wa kumpata msanifu mwelekezi wa kusanifu na kusimamia ujenzi wa masoko ya Mnanila (Kasulu) na Mutukula (Misenyi) unaendelea. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itakamilisha ujenzi wa masoko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwezesha uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo. Kwa kiasi kikubwa mazao yetu huuzwa yakiwa ghafi na hivyo kupoteza faida ambazo zinaambatana na kusindikwa kwa mazao hayo. Usindikaji mdogo wa mazao ya

kilimo unalikosesha Taifa mapato ya fedha za kigeni, kupunguza mapato ya mkulima na ajira, hivyo kupunguza mchango wa Sekta ya Kilimo katika Pato la Taifa na ukuaji wa uchumi na maendeleo kwa ujumla. Serikali katika kukabiliana na hilo iliendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuongeza thamani kwa mazao ya mkonge, korosho, tumbaku, pareto, pamba na kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa 2011/2012, jumla ya tani 10,247 za bidhaa mbalimbali za mkonge zilipatikana katika viwanda vya Amboni, *Tancord, 21st Century*, Ubena na Kiwanda cha Magunia cha *TPM* baada ya kuongezwa thamani. Pia, Serikali imeendelea kuhamasisha matumizi ya mkonge katika utengenezaji wa bidhaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na samani za majumbani, ufuaji umeme, gesi, mbolea na chakula cha mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuhamasisha usindikaji na matumizi ya bidhaa za mkonge, imedhihirika kuwa baadhi ya bidhaa bado hazijafikia viwango vya ubora unaokidhi matumizi yaliyokusudiwa. Ili kulinda viwanda vya ndani, Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara katika kuhakikisha kuwa viwango vya ubora wa bidhaa za mkonge vinazingatiwa ili kuongeza ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa zao la korosho, jumla ya tani 31,000 zilibanguliwa hapa nchini ikiwa ni asilimia 19 ya korosho zilizozalishwa. Maandalizi ya ujenzi wa viwanda viwili vya *TANECU Limited* na *Perfect*

Cashew Kernel vyenye uwezo wa kubangua tani 32,000 yanaendelea. Taarifa za ukaguzi wa viwanda vilivyobinafsishwa zinaonesha kuwa, baadhi ya viwanda hivyo haviendeshwi kulingana na masharti ya ubinafsishaji. Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na Shirika Hodhi la Mashirika ya Umma (*Consolidated Holdings Corporation - CHC*), kuhakikisha kwamba viwanda hivyo vinaendeshwa kulingana na masharti ya ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wa usindikaji wa tumbaku hapa nchini ni tani 120,000 kwa mwaka. Uwezo huo ni mdogo ikilinganishwa na uzalishaji, mathalan, katika mwaka 2011/2012, uzalishaji wa tumbaku ulikuwa tani 126,624. Ili kuongeza uwezo wa usindikaji wa tumbaku, Serikali inaendelea kuhamasisha wadau kufufua na kujenga viwanda vipya katika mikoa inayozalisha zao hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi zilizokwishaanza ni uandaaji wa andiko la biashara kwa Kiwanda cha *SONTOP* – Songea, ujenzi wa kiwanda kipya Mkoani Mbeya cha Kampuni ya *Premium Active Tanzania Limited* ambapo tayari wamepata eneo la ujenzi huko Chunya. Aidha, Vyama vya Ushirika wa Tumbaku nchini vimeazimia kujenga Kiwanda cha Usindikaji Mkoani Tabora ambako asilimia 60 ya tumbaku huzalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, usindikaji wa awali wa zao la pareto unafanyika kwa pareto yote inayozalishwa nchini ili kupata sumu ghafi na Gristi ya Pareto *(Pyrethrum Grist)*. Tasnia ya pareto inahitaji mitambo ya kuchuja sumu ghafi ili itumike katika

viwanda vya kutengeneza madawa ya kuua wadudu majumbani na mashambani. Serikali inaendelea kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kwenye viwanda vya kuchuja sumu ya pareto.

Mheshimiwa Naibu Spika, takriban asilimia 70 ya pamba yote inayozalishwa inauzwa nje ikiwa ghafi na kiasi kinachobaki kinatumiwa na viwanda hapa nchini. Kwa kutambua hilo, Wizara kupitia Bodi ya Pamba imeshirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuandaa mkakati wa kuongeza thamani ya pamba kwa kutengeneza nyuzi *(Cotton yarn)* na nguo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati huo uko tayari na utaanza kutekelezwa mwaka 2012/2013. Aidha, Wizara imefanya mazungumzo na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na Benki Kuu ambao wameonesha nia ya kuwawezesha wawekezaji wa ndani kuanzisha viwanda vya nyuzi na nguo. Napenda kutoa rai kwa wawekezaji wa ndani kujitokeza na kutumia fursa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika zao la kahawa, Wizara kupitia Bodi ya Kahawa imeendelea kuhamasisha vikundi vya wakulima, Vyama vya Ushirika na Sekta Binafsi kuwekeza katika viwanda vya usindikaji na ukaangaji wa kahawa nchini. Aidha, Bodi inatekeleza mkakati wa kutoa mafunzo na mashindano ya utayarishaji wa kinywaji cha kahawa. Wizara pia itahamasisha uanzishwaji wa migahawa ya kahawa ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuhamasisha wakulima kupukuchua (*pulping*) kahawa mbivu kabla ya kuiuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kuhamasisha usindikaji wa mazao ya chakula katika ngazi ya kaya kwa lengo la kupunguza upotevu wa mavuno na kuongeza kipato. Katika mwaka 2011/2012, wakulima viongozi 350 katika skimu saba za umwagiliaji walipewa mafunzo. Mafunzo hayo yalihusu usindikaji wa mazao, ubora na usalama wa mazao ya chakula, kupanga madaraja, ufungaji na ufungashaji, kuweka chapa bidhaa za kilimo, upatikanaji wa masoko na ujasiriamali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia kupitia Mradi wa *DASIP* ilinunua na kusambaza mashine za kukoboa na kusaga nafaka 145, mashine za kukamua mafuta 11, mashine za kuchakata muhogo 13 na mashine za kupukuchua kahawa 24 katika Wilaya 28 za Mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia mradi wa *Japan Policy and Human Resources Development – PHRD* itagharamia ujenzi wa maghala matatu (3) katika skimu za Uturo (Mbarali), Lekitatu (Meru) na Bagamoyo - *BIDP* (Bagamoyo) na kukarabati maghala matatu (3) ya Skimu za umwagiliaji za Mombo (Korogwe), Mkula (Kilombero) na Mkindo (Mvomero).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwezesha na kuimarisha Ushirika na Asasi za Wananchi katika Kilimo na Sekta nyingine za Kiuchumi. Kuhamasisha Uanzishwaji na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika. Wizara iliendelea kuhamasisha wananchi kuanzisha au

kujiunga na Vyama vya Ushirika kupitia kampeni zilizofanyika katika mikoa minane (8) na skimu za umwagiliaji saba (7) ili kuanzisha *SACCOS, AMCOS (Agricultural Marketing Cooperative Societies)* na Vyama vya Ushirika wa Umwagiliaji. Juhudi hizo zimewezesha kuundwa kwa vyama 408 zikiwemo *SACCOS* 173, *AMCOS* 87, Vyama vya Wafugaji 66 na vingine 82. Aidha, Vyama 36 vilifutwa baada ya kuviunganisha na Vyama vingine. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kusimamia na kuimarisha uendeshaji wa *SACCOS* na Benki za Ushirika kwa kusambaza miongozo ya uendeshaji, kutoa mafunzo kwa Maafisa Ushirika 300 kuhusu usimamizi wa kitaalam wa taasisi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Vyama Vikuu vya Ushirika vya mazao vimeimarika na kuhimili ushindani katika soko huru. Vyama hivyo vimeweza kutafuta masoko ya mazao ya wanachama wao na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii. Wanaushirika wa Kagera kupitia *KCU* (1990) *Limited* wameweza kuuza kahawa nje ya nchi tani 2,500 zenye thamani ya Dola za Kimarekani millioni 8.39 sawa na Shilingi bilioni 14.8. Aidha, wanachama hao walipewa *Social Premium* ya Dola za Kimarekani milioni 1.09 sawa na Shilingi milioni 500 ambazo zilitumika kwenye shughuli za kijamii ikiwemo kujenga na kuendesha shule, zahanati, kuongeza mtaji wa *SACCOS* na kujenga maghala.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni mbali na kusimamia kilimo cha kahawa hai kwa kutumia Maafisa Ugani 50. Aidha, Chama cha KANYOVU kiliweza

kumlipa mkulima Shilingi 5,000 hadi 6,000 kwa kilo kwa kahawa ya maganda na Shilingi 8,000 hadi 8,500 kwa kahawa safi. Vyama vingine vya *KNCU, KDCU, ACU, WETCU, LATCU, CHUTCU* na *SHIRECU* vinaonesha mafanikio kwa kuwaongezea kipato na huduma wanachama wao na jamii. Haya yanadhihirisha yale aliyoyasema Mheshimiwa Zitto Kabwe naendelea kuwapongeza wakulima wa kahawa kule Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuwawezesha Maafisa Ushirika katika Halmashauri ili watekeleze majukumu yao ya ukaguzi, usimamizi na ukusanyaji wa takwimu za Vyama ambapo vyama 2,577 vimekaguliwa. Ukaguzi maalum na uchunguzi ulifanyika kwa Vyama Vikuu sita (6), *AMCOS* 240, *SACCOS* 42, *Joint Enterprise* moja (1), mashamba ya Vyama vya Ushirika 41 na kiwanda kimoja (1).

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za uchunguzi na ukaguzi zimeonesha kasoro mbalimbali ikiwemo ubadhirifu kwa baadhi ya Vyama; kuajiri watumishi wasio na sifa na elimu ndogo ya Ushirika kwa wanachama, viongozi na watendaji wa Vyama. Taarifa hizo zimewasilishwa kwenye Mikutano Mikuu ya Vyama husika na hatua za kuboresha utendaji zimechukuliwa. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na watendaji wenye kasoro kuachishwa kazi, Bodi za Vyama kuondolewa madarakani na wabadhirifu kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara vile vile imeendelea kutoa ruzuku kwa Shirika la Ukaguzi na

Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) ili kuimarisha shughuli za ukaguzi wa Vyama ambapo jumla ya Vyama 1,931 vimekaguliwa vikiwemo Vyama Vikuu 15, *AMCOS* 553, *SACCOS* 1,181. Matokeo ya ukaguzi huo yalionesha kwamba vyama vyenye hati yenye mashaka vimepungua kutoka 941 mwaka 2010/2011 hadi 242 mwaka 2011/2012 na vyama vyenye hati chafu kutoka 236 hadi 36 katika kipindi hicho. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuiwezesha *COASCO* kukagua Vyama vya Ushirika kwa lengo la kuimarisha Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo kwa Wanachama, Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Ushirika. Wizara imetoa mafunzo ya utawala bora na ujasiriamali kwa wajumbe wa Bodi na wawakilishi 2,050 wa Vyama vya Ushirika na mafunzo ya utunzaji wa vitabu kwa watendaji 55. Mafunzo yaliyotolewa yalilenga kuwajasirisha wanachama ili kuongoza Vyama vyao kwa misingi ya Ushirika na kufanya maamuzi kwa manufaa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo kwa watendaji yalilenga katika kuwajengea stadi katika utekelezaji wa majukumu yao na kutoa taarifa kwa wanachama na sehemu ambazo wanawajibika kuzipeleka kwa Mamlaka ya Kodi, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na Benki Kuu. Wizara pia imetoa mafunzo kwa Wenyeviti na Mameneja wa *SACCOS* 50 zenye mitaji ya zaidi ya Shilingi milioni 500 nchini pamoja na Maafisa Ushirika 10 kuhusu usimamizi wa Vyama ili kuboresha utendaji na ujasiriamali wa ukuzaji wa mitaji na ujenzi wa akiba (*savings mobilization*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itatoa mafunzo ya usimamizi wa fedha kwa Vyama vya Mazao na *SACCOS* kwa lengo la kuviandaa vyama hivyo kushiriki katika utaratibu wa kusambaza ruzuku ya pembejeo katika msimu wa 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwezesha Asasi za Ushirika Kutekeleza Majukumu yake. Wizara imeendelea kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Ushirika (*TFC*) na Muungano wa Vyama vya Akiba na Mikopo (*SCCULT*) katika kuhamasisha uanzishwaji na uendelezaji wa ushirika nchini. Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara (*MUCCoBS*) imefanya tafiti 27 zilizohusu maendeleo ya ushirika na kusambaza matokeo ya tafiti hizo kwa walengwa. Aidha, chuo kimetoa mafunzo kwa watendaji wa Vyama vya Ushirika ikiwemo kuendesha mafunzo kazini kwa Maafisa Ushirika waliopo Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliratibu majadiliano kati ya benki na Vyama vya Ushirika vya Tumbaku ambayo yaliviwezesha kupata mikopo ya Dola za Kimarekani 96,838,334.48 sawa na Shilingi bilioni 151.6 kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo msimu wa 2011/2012. Pembejeo hizo zilipokelewa na kufikishwa kwa wakulima waliolengwa. Vilevile, Wizara ilihamasisha Vyama vya Ushirika Mkoani Kilimanjaro ambapo *SACCOS* 51 na *AMCOS* 102 zilichangia ujenzi wa mtaji wa Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro (*KCBL*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia ilishirikiana na Chama Kilele cha Tumbaku kuandaa utaratibu wa kusambaza pembejeo za tumbaku katika mwaka 2012/2013. Utaratibu uliokubalika ni kuwa Vyama vya Ushirika vya Msingi vitachukua mikopo kutoka benki kwa kusimamiwa na Vyama Vikuu baada ya kukusanya mahitaji na kuyawasilisha Chama Kilele cha Tumbaku ambacho kitaagiza pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, uhifadhi, uchambuzi na usambazaji wa takwimu. Ili kuwa na mipango endelevu katika kuendeleza Sekta ya Kilimo, upatikanaji wa takwimu sahihi na kwa wakati ni muhimu. Kutokana na umuhimu huo, Wizara kwa kushirikiana na wadau iliandaa mfumo wa kuboresha ukusanyaji wa takwimu za kilimo kwa kutumia mtandao wa TEHAMA wa *Local Government Monitoring Database System – LGMD2*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, mfumo huo ulianza kutumika katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Mara, Mwanza, Shinyanga, Kagera na Kigoma. Katika mwaka 2012/2013, mfumo huo utaendelezwa katika Mkoa ya Mbeya, Ruvuma, Iringa, Rukwa, Katavi, Njombe, Mtwara, Lindi, Pwani, Dar es Salaam, Tabora na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha upatikanaji wa takwimu sahihi za Ushirika, Wizara imeendelea kuboresha mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu za ushirika kwa kutumia mfumo wa TEHAMA wa *Cooperative Data Analysis System - CODAS*. Aidha, takwimu

zimekusanywa kutoka Wilaya za Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara na Kagera na kuingizwa kwenye mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikoa ya Singida, Mara, Kagera na Manyara imepewa kompyuta moja kila mkoa kwa ajili ya matumizi ya mfumo huo. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa Ushirika 50 kutoka Mikoa ya Mbeya, Iringa, Rukwa na Ruvuma kuhusu ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu za ushirika na kila mkoa utapewa kompyuta moja kwa ajili ya kutumia mfumo wa *CODAS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusimamia Sera, Sheria na Mikakati katika Sekta ya Kilimo. Mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kimuundo yaliyotokea katika miaka ya hivi karibuni yamesababisha Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997 kupitwa na wakati. Tangu mwaka 1997 yametokea mabadiliko mengi katika ngazi ya Kimataifa, Kitaifa na katika Sekta ya Kilimo ambayo hayakuzingatiwa katika Sera hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko hayo ni pamoja na kupitishwa kwa malengo ya Milenia, MKUKUTA, Sera ya Kilimo na Maendeleo Vijijini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, maazimio ya Maputo (2003) na Abuja (2006). Aidha, kutungwa kwa Sera ya Ushirika ya mwaka 2002; Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002; Sera ya Mifugo ya mwaka 2006; Sera ya Masoko ya Mazao ya mwaka 2008 na Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010 kumefanya Sera hiyo kutokuwa na sifa ya kuwa Sera ya Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imeandaa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Kilimo ambayo iko katika hatua za kuidhinishwa. Aidha, Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010 imetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na iko kwenye hatua za uchapishaji. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itakamilisha uandaaji wa Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilikamilisha na kuchapisha kwenye Gazeti la Serikali Kanuni za Sheria ya Sekta ya Kahawa, Mkonge, Pamba, Tumbaku na Kanuni za Sheria ya Mbolea ya mwaka 2009. Wizara pia iliandaa mapendekezo ya kurekekebisha Sheria ya Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (*Plant Breeders Rights*) ya mwaka 2002 ambayo yalisomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Saba wa Bunge la mwezi Aprili 2012. Aidha, Wizara imekamilisha Mapendekezo ya Muswada wa kurekebisha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 20 ya mwaka 2003 ili iwezeshe kuundwa kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itakamilisha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Mimea; Sheria ya Taasisi ya Viuatilifu vya Ukanda wa Kitropiki (*Tropical Pesticides Research Institute-TPRI*) ya mwaka 1979; Sheria ya Mbegu ya mwaka 2003; Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Pembejeo Na. 9 ya Mwaka 1994 na Sheria ya Mamlaka ya Kuendeleza Bonde la Rufiji (*RUBADA*) ya mwaka 1975.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia itakamilisha mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria ya Ardhi ya Kilimo; Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo; Sheria ya kusimamia umwagiliaji ambayo itawezesha kuundwa kwa Tume ya Umwagiliaji; Sheria ya Kilimo cha Mikataba na Sheria ya Kulinda Nasaba za Mimea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itazirejea kanuni za Sheria ya Kahawa Na. 23 ya mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2009 ili kuondoa migongano iliyojitokeza katika soko la kahawa na uendeshaji wa Bodi ya Kahawa. Aidha, Wizara itazirejea kanuni nyingine ambazo zitaonekana kuwa na upungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji wa Sekta Binafsi katika Kilimo. Pamoja na kutambua nafasi na umuhimu wa wakulima wadogo, kilimo chao bado ni cha kujikimu. Ili kukibadilisha kilimo hicho kuwa cha kisasa na cha kibiashara ushiriki wa wakulima wakubwa na wa kati wenye mitaji, teknolojia na ubunifu ni muhimu ili wakulima wadogo waweze kunufaika na ubia utakaotokana na ushirikiano huo. Hivyo ushiriki wa wakulima wakubwa na wa kati hauna lengo la kuwafanya wakulima wakubwa kuwa mbadala wa wakulima wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kujenga uhusiano kati ya wakulima wakubwa, wa kati na wadogo katika kutumia fursa zilizopo ili kuongeza ufanisi katika uzalishaji wa mazao na upatikanaji wa masoko. Katika ubia huo, wakulima wadogo

hawatanyang'anywa mashamba yao ili kuwapa wakulima wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi malengo hayo, Serikali imeendelea kuweka mazingira yanayovutia uwekezaji katika Sekta ya Kilimo, kwa mfano, kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vipuri vya zana za Kilimo. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itashirikiana na Wizara ya Fedha kutafuta utaratibu mzuri wa kubainisha vipuri vya mashine na mitambo iliyosamehewa kodi ili kuondoa usumbufu wanaoupata waagizaji na watumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali imeendelea kushirikisha Sekta Binafsi kuwekeza katika kilimo kupitia Mpango wa Kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania *(Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT*) ambapo Kituo cha Kuratibu Utekelezaji wa Mpango huo *(SAGCOT Centre*) kimeanzishwa. Aidha, Mfuko Kichocheo *(Catalytic Fund*) kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa miundombinu na uwekezaji uko katika hatua za mwisho za uanzishwaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, katika Wilaya ya Kilombero mwekezaji wa kampuni ya Kilombero *Plantation Limited (KPL)* ameanza uzalishaji wa mpunga katika shamba la Mngeta kwa kushirikisha wakulima wadogo wa Vijiji vya Mkangawalo, Mchombe, Lukolongo, Ikule, Njagi, Merera, Chita na Udagaji vinavyozunguka shamba hilo ambapo wakulima 1,350 walipata mafunzo ya *System of Rice Intensification - SRI* na kuwawezesha kuvuna mpunga

kutoka tani mbili (2) hadi tani nane (8) kwa hekta. Lengo ni kufikia wakulima 5,000 wanaozunguka shamba hilo ifikapo mwaka 2015.

Wizara kupitia Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Rufiji *(Rufiji Basin Development Authority - RUBADA)* imeendelea kupima na kuainisha maeneo kwa ajili ya uwekezaji katika shamba la Ngalimila lenye ukubwa wa hekta 5,128. Utaratibu wa kupata hatimiliki unakamilishwa. Aidha, hekta 105,000 zitapimwa na kufanyiwa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, TAMISEMI na Sekta binafsi kupitia *SAGCOT* itaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi na kuainisha ardhi inayofaa kwa uwekezaji kwa kuanzia na Wilaya za Kilombero na Ulanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara itafanya upembuzi yakinifu na usanifu katika maeneo ya uwekezaji ya shamba la Kihansi (hekta 5,200) na Ngalimila (hekta 5,128) kwa ajili ya kuvutia wawekezaji. Wizara pia itaweka kipaumbele katika kuongeza uzalishaji wa mpunga na sukari.

Wizara itafanya upembuzi yakinifu wa mashamba ya wakulima wadogo yanayozunguka mashamba makubwa kwa ajili ya kuweka miundombinu ya umwagiliaji. Mashamba hayo yako katika vijiji vya Sonjo

na Mpanga-Ngalimila (Kilombero) na Lupiro (Ulanga) na kuanza ujenzi katika skimu ya Itete (Ulanga). Wizara pia kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta itafanya tathmini ya maghala na masoko katika Kongani ya Kilombero kwa nia ya kuboresha miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inafahamu kwamba vijana wengi wanakimbilia mijini kuepuka kilimo cha kujikimu ambacho hakina tija. Kutokana na hali hiyo, Wizara inaendelea na juhudi za kukifanya kilimo kiwe cha kibiashara ambacho kitavutia vijana na kitazalisha mazao kwa wingi yatakayokidhi kuwepo viwanda vya usindikaji katika maeneo ya uzalishaji na hivyo kutoa ajira kwa vijana wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri katika kuhamasisha vijana kujiunga katika vikundi na kuainisha maeneo ya ardhi kwa ajili ya kuwapatia vijana ili wajiajiri katika kilimo. Aidha, Wizara itaendelea kutoa utaalam wa kuunda na kuimarisha vikundi na stadi za kilimo bora cha kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia azma hiyo, Wizara yangu itashirikiana na Wizara za Kazi, Ajira na Vijana na Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine; vyuo vingine na wadau mbalimbali kuandaa programu ya kuwawezesha vijana wanaohitimu katika fani ya kilimo kupata mitaji na ardhi ili waweze kujiajiri katika kilimo cha kisasa na cha kibiashara. Utaratibu kama huo

umeonesha mafanikio ya kuongeza ajira kwa vijana nchini Misri.

Mheshimiwa Spika, kuboresha uratibu katika Sekta ya Kilimo; utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP I)* ambao ulianza mwaka 2006 utakamilika mwezi Juni 2013. Wizara za Sekta ya Kilimo kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo zimeanza mchakato wa kuandaa *ASDP II* ambao unashirikisha wadau wengi ili kupanua wigo wa uwekezaji katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugharamiaji wa *ASDP II* utafanywa na Serikali kwa kushirikiana na wadau wa Maendeleo kupitia Mfuko wa pamoja na kupitia miradi mingine mipya inayotekelezwa katika Sekta ya Kilimo kama vile *Feed the Future*, *Marketing Infrastructures Value Addition and Rural Financing Support Programme (MIVARF)*, *Bread Basket* na *SAGCOT.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kuwepo kwa wadau wengi zaidi katika utekelezaji wa ASDP II ni dhahiri kuwa kutakuwa na changamoto katika uratibu wa *ASDP II*. Kutokana na hali hiyo, Wizara za Sekta ya Kilimo zimeandaa uratibu wenye lengo la kuhuisha utekelezaji wa mipango ambao utahusisha uandaaji wa pamoja wa bajeti na mipango kazi, utoaji wa taarifa na ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo itasaidia kupunguza mwingiliano wa utekelezaji pale ambapo kuna utekelezaji wa mradi zaidi ya mmoja katika eneo moja na hivyo kutumia rasilimali kwa ufanisi zaidi. Aidha,

uratibu huo utahakikisha kuwa mipango na programu zote zinaandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vya sekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutekeleza Programu Kabambe ya Kuendeleza Kilimo Afrika (*Comprehensive Africa Agriculture Development Programme-CAADP*) kwa kuandaa Mpango wa Uwekezaji Katika Sekta ya Kilimo *(Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan- TAFSIP)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huo ni wa miaka 10 na una lengo la kukifanya kilimo kiweze kuchangia kwa asilimia angalau sita kwa mwaka katika ukuaji wa uchumi; kuongeza pato la mkulima na Taifa kwa ujumla na kuhakikisha Taifa linajitosheleza kwa chakula na lishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huo umeandaliwa ili kuiwezesha Sekta Binafsi pia kuchangia katika uwekezaji kwenye Sekta ya Kilimo tofauti na ilivyo hivi sasa ambapo sekta hiyo inategemea kupata fedha kutoka kwenye bajeti ya Serikali, michango ya wadau wa mazao, wafadhili, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (*NGOs*) na Benki za Ushirika na za Jumuiya *(Cooperative and Community Banks)* ambazo bado hazijaimarika. Mpango huo utaanza kutekelezwa kupitia *ASDP* katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeshiriki kuandaa Itifaki ya Afya ya Mimea na Wanyama *(SPS Protocol)* na Mpango Kazi wa Usalama wa Chakula na Sera ya Tabianchi *(EAC Food Security Action Plan and*

Climate Change) katika Sekta ya Kilimo kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wizara pia imeshiriki katika mikutano ya kujadili utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki *(EAC Common Market Protocol Monitoring Framework).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Katika kuongeza ujuzi na ufanisi wa watumishi, Wizara ilitoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Jumla ya wataalam 21 waliendelea kupata mafunzo ya Shahada za Uzamivu *(PhD)*, 65 katika Shahada ya Uzamili *(MSc)* na 74 Shahada ya Kwanza *(BSc)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 238. Mafunzo hayo yalihusu uchambuzi wa sera; usimamizi wa fedha; utafiti, matumizi ya zana za kilimo; usindikaji wa mazao; uchumi; matumizi bora ya maji; utawala; utunzaji kumbukumbu; usanifu na usimamizi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, watumishi wapatao 145 wamepandishwa cheo katika madaraja mbalimbali na watumishi 371 wameajiriwa. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itapandisha cheo watumishi 584 katika madaraja mbalimbali na kuajiri watumishi 615 ikiwa ni pamoja na kuendelea kushirikiana na Sekretarieti ya Ajira kupeleka wataalam wa kilimo kwenye Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha utawala bora na kupambana na rushwa Wizara iliendelea kusimamia Mfumo wa Wazi wa Tathmini ya Utendaji Kazi (*Open Performance and Review Appraisal System - OPRAS)* ambapo zaidi ya asilimia 80 ya watumishi wa Wizara wamefanyiwa tathmini kupitia mfumo huo. Watumishi wengine wameendelea kupatiwa mafunzo ya *OPRAS*. Aidha, mafunzo ya maadili, utawala bora na uwajibikaji yalitolewa kwa watumishi wa Wizara na viongozi 201 wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (*Tanzania Federation Cooperatives - TFC*) kwa lengo la kuzuia na kupambana na rushwa na kuimarisha Utawala Bora.

Mafunzo ya Utawala Bora pia yametolewa kwa wajumbe wa Bodi za Uongozi za Vyama Vikuu vya Ushirika vya *ACU* (1984) *Limited*, *KNCU* (1984) *Limited*, *VUASU Limited* na Bodi ya Uongozi wa Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro (*KCBL*) kwa lengo la kuviimarisha. Aidha, yametolewa mafunzo ya ukaguzi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika kwa Maafisa Ushirika wa wilaya zote za mikoa ya Dar es salaam, Morogoro, Mwanza, Mara, Shinyanga na Kagera ili kuwajengea uwezo wa kusimamia na kukagua vyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeandaa Mpango Mkakati unaolenga kuinua matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Sekta ya Kilimo kwa nia ya kuongeza ufanisi. Mpango Mkakati huo umezingatia sera ya matumizi ya TEHAMA katika kilimo na usalama katika matumizi ya TEHAMA Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara imeendelea kuboresha tovuti yake ya *www.kilimo.go.tz* au *www.agriculture.go.tz* kwa kuweka taarifa zinazohusu kilimo zikiwemo za uzalishaji wa mazao ya kilimo. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa TEHAMA ambapo itaandaa Mfumo wa Takwimu za skimu 27 za umwagiliaji na kuboresha Tovuti ya Wizara kwa kuweka taarifa zaidi za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuimarisha mawasiliano na wadau wa Sekta ya Kilimo ili kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu Sera, Mikakati, Programu, huduma na majukumu yanayotekelezwa katika kuendeleza kilimo nchini. Taarifa hizo zimekuwa zikitolewa kupitia njia mbalimbali za mawasiliano ikiwemo matangazo na makala kwenye vyombo vya habari vya runinga, magazeti na redio.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyingine ni kutayarisha na kusambaza kalenda, vipeperushi, majarida, mabango na kuandaa maonesho mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa ambayo yanahusu Sekta ya Kilimo. Wizara pia imekamilisha maandalizi ya rasimu ya Mkakati wa Mawasiliano wa Sekta ya Kilimo na kuisambaza kwa wadau kwa lengo la kuiboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea kujenga uwezo wa watumishi kwa lengo la kuwezesha uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika maandalizi ya bajeti. Katika mwaka 2011/2012, wataalam sita (6) wa bajeti walipatiwa mafunzo ya kuandaa bajeti zenye mtazamo wa kijinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imefanya tathmini ya awali *(baseline survey)* katika skimu za umwagiliaji 27 ili kupata taarifa za msingi za hifadhi ya mazingira na kutoa mafunzo kwa wakulima 178 kuhusu hifadhi ya mazingira na kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Mazingira. Wizara pia imeendelea kuwapatia vyakula vyenye virutubisho pamoja na matibabu watumishi 17 wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Aidha, Wizara imetoa elimu kwa watumishi kuhusu kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI na imewahamasisha kupima kwa hiari.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani, naomba nitumie nafasi hii kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia sana Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo. Kwanza napenda kuzishukuru nchi za Japan, Ireland, China, India, Israel, Indonesia, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Ubelgiji na Uholanzi. Nayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo:-

Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *AU, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID*, *KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, CFC, AVRDC, AGRA, WARDA*, *Bill and Melinda Gates Foundation, Gatsby Trust*, *Rockfeller Foundation* na *Unilever*. Ushirikiano na misaada ya nchi na mashirika hayo bado tunauhitaji ili tuweze kuendeleza kilimo nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa

wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Mbunge wa Mkuranga; Katibu Mkuu Bwana Mohamed Said Muya; Naibu Katibu Mkuu Bibi Sophia Elias Kaduma; Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Mbogo Futakamba; Wakurugenzi wa Idara; Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara; watumishi wote wa Wizara na wadau mbalimbali wa Sekta ya Kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2011/2012 kama nilivyofafanua katika hotuba hii. Ni matarajio yangu kwamba, Wizara itaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2012/2013. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa hotuba hii. Lakini kipekee basi niishukuru familia yangu mke wangu Elisafina, watoto na wajukuu kwa sala zao ambazo zimenipa mafanikio katika kutekeleza majukumu yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni biashara inayoweza kuleta utajiri na maendeleo kama zilivyo biashara nyingine. Kwa kuwa kilimo kinaajiri asilimia 75 ya Watanzania, kina nafasi kubwa ya kupunguza umaskini katika nchi yetu. Aidha, nchi yetu ina uwezo mkubwa wa kupanua kilimo chake kutokana na rasilimali zilizopo. Ni lengo la Serikali kuondokana na kilimo cha kujikimu chenye tija ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, natoa wito kwa Watanzania wote ikiwemo Sekta Binafsi na vijana

kuwekeza katika kilimo cha kibiashara. Wizara itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha uwekezaji katika sekta hii muhimu. Kipekee naomba Waheshimiwa Wabunge niungane nao mkono katika azma ya makusudi ya kuwawezesha vijana kujiajiri kupitia Sekta hii ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe Sh. 237,624,575,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, Fungu 43 kwa mwaka 2012/2013. Kati ya fedha hizo, Sh. 170,364,421,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na sh. 67,260,154,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha za bajeti ya maendeleo, sh. 14,937,000,000 ni fedha za ndani na sh. 52,323,154,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 24 fungu hili linahusu Ushirika. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu kupitia Fungu 24 inaomba sh. 6,104,209,000 kwa ajili ya shughuli za kuendeleza Ushirika nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa hotuba yako nzuri, tumeisikiliza kwa umakini. Sasa nimwite Mwenyekiti wa

Kamati Mheshimiwa Profesa Mwakyusa. Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu!

MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo ni kubwa ni nyeti na ina majukumu mengi. Kwa hiyo, ripoti yetu ni ndefu, ninachoomba kwamba *Hansard* iichukue yote kama ilivyo kwa sababu kwa muda ulionipa siwezi kugusia mambo yote ambayo tulibaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 7 na 8 Juni, 2012 Kamati ilikutana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika katika Ofisi Ndogo ya Bunge ya Dar es Salaam ili kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara, maoni na ushauri wa Kamati kuhusu makisio ya mwaka wa fedha 2011/2012, pamoja na malengo na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013, ambayo yaliambatana na maelezo ya maeneo ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ikiwa msimamizi wa Wizara hii, ilitoa maoni na ushauri wa kuzingatiwa wakati ilipojadili na kuchambua bajeti ya Wizara kwa

mwaka wa fedha 2011/2012, kwa lengo la kuboresha sekta hii muhimu. Wizara imejitahidi kuyafanyia kazi maoni na ushauri wa Kamati. Baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa kazi ni pamoja na haya yafuatayo:-

(a) Kamati iliishauri Serikali kuanzisha Mfuko wa Maafa katika Halmashauri badala ya kusubiri Mfuko wa Maafa wa Taifa. Wizara ilieleza kuwa, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Maafa iko katika mchakato wa kutunga sheria mpya ya maafa ambayo itapendekeza kuanzishwa kwa Mifuko hiyo katika ngazi ya Wilaya. Kamati inaendelea kuhimiza uharakishwaji wa uanzishwaji wa Mifuko hiyo ya Wilaya;

(b) Kamati ilishauri kwamba ushuru wa mazao uondolewe ili kupunguza bei kubwa sokoni ambayo inamuumiza mlaji. Wizara ilitoa taarifa kwamba, Serikali inafanya uchambuzi ikishirikisha na wadau mbalimbali kuhusu ushuru wa mazao kuondolewa. Kamati inasisitiza mchakato huo uharakishwe;

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzalishaji wa mbegu. Kamati ilielezwa ya kwamba asilimia 70 ya mbegu zinazotumika nchini zinaagizwa kutoka nje. Kamati iliiagiza Wizara ianze kuzalisha mbegu bora nchini ili kuondoa utegemezi na vile vile kupunguza gharama ya kuagiza mbegu kutoka nje ya nchi. Wizara iliiarifu Kamati kuwa inaimarisha Vituo vyake vya Utafiti ili kuzalisha mbegu bora nchini. Aidha makampuni binafsi yamehamasishwa kuzalisha mbegu za kutosha hapa nchini. Serikali pia inatekeleza mkakati wa kuimarisha uwezo wa wakulima wadogo vijijini kuzalisha mbegu za daraja la kuazimiwa (*QDS*); na

(d) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha Wizara inawawezesha vijana kushiriki katika Kilimo, Wizara ilieleza kuwa imeanza hatua ya awali *(pilot phase)* ambapo kwa kushirikiana na Mikoa ya Lindi na Mtwara imevipatia vikundi vya vijana mafunzo ya kilimo na seti 20 za mashine za kusindika mhogo. Jukumu hili la kuwapatia vijana ajira ni kubwa lakini ni la muhimu sana. Kamati inaona kwamba hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa kuwawezesha vijana kujiajiri katika Kilimo. Kamati inasisitiza kwamba, iandaliwe programu maalum ya kuwawezesha vijana kujiajiri katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ilikumbana na changamoto zifuatazo:-

(a) Mtiririko usioridhisha wa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya kutekeleza kazi zilizopangwa;

(b) Ukosefu wa Mawakala wa kutosha na wenye uwezo wa kufikisha pembejeo za kilimo katika maeneo ya vijijini;

(c) Mahitaji makubwa ya wakulima ya Mfuko wa Pembejeo wakati bajeti ya Mfuko huo ni ndogo; na

(d) Idadi ndogo ya Maafisa Ushirika ikilinganishwa na idadi ya Vyama vya Ushirika, hivyo kusababisha kukosekana kwa usimamizi madhubuti wa vyama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu yake, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, chini ya Fungu 43, inaomba jumla ya sh. 237,624,575,000/=. Kati ya fedha hizo, sh. 170,364,421,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na sh. 67,624,575,000/= ni kwa miradi ya maendeleo. Aidha, kati ya fedha za maendeleo shilingi 14.9 bilioni ni fedha za ndani na shilingi 52.3/= bilioni ni fedha za kutoka nje. Wizara chini ya Fungu 24, inaomba jumla ya sh. 6,104,209,363/=. Kati ya fedha hizo shilingi 897,781,000 ni mishahara na shilingi 5,206,428,363/= ni matumizi mengineyo**.**

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazoombwa na Wizara zinakusudia kutekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(a) Kuongeza uzalishaji na tija katika sekta ya kilimo. Wizara:-

- Itakamilisha ujenzi, ukarabati na uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu 24 na mabwawa nane ya kumwagilia eneo la hekta 40,000 katika kanda saba za umwagiliaji;

- upatikanaji wa pembejeo za mbolea na mbegu bora;

- Usambazaji wa pembejeo kwa mfumo mpya wa kutumia kadi za Kielektoniki (*e-Voucher*);

- Ruzuku ya kuzalisha miche bora ya chai, kahawa na vipando bora vya mhogo;

- Mfuko wa Taifa wa Pembejeo utatoa mikopo ya matrekta makubwa na madogo, pembejeo za kilimo na mifugo (mbolea, vifungashio, sumu na madawa ya mimea na mifugo; na

- Uhifadhi wa udongo na matumizi ya ardhi na uendelezaji wa mazao.

(b) Kwa kushirikiana na sekta binafsi katika kilimo, Wizara itaendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji kupitia mradi wa *SAGCOT*, mpango huu utakwenda sambamba na kuandaa matumizi bora ya ardhi na kuainisha ardhi inayofaa kwa uwekezaji.

(c) Kubuni mipango ya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo kwa Wizara kutoa mafunzo ya matumizi ya mashine za usindikaji mazao ya kilimo katika skimu za umwagiliaji 12 na maandalizi ya kuweka mtambo wa kuchanganya *(blending)* muhogo na mtama.

(d) Kuwezesha upatikanaji wa masoko ya bidhaa za kilimo, Wizara kupitia *NFRA* imekusudia kununua tani 200,000 za mahindi na kati ya hizo tani 100,000 zitauziwa *WFP*, fedha itakayopatikana itatumika kununulia mahindi kutoka kwa wakulima. Wizara pia itashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na wadau wengine wa sekta binafsi wakiwemo *Farm Radio* kutoa mafunzo kwa vikundi 15 vya wakulima

wasindikaji kuhusu upatikanaji wa taarifa za masoko kupitia huduma za TEHAMA kwa kutumia simu za mikononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza utekelezaji wa maoni ya Kamati, changamoto na maeneo ya utekelezaji kwa mwaka 2011/2012, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni Bajeti. Bajeti ya Wizara hii bado ni ndogo na hii ni sababu kubwa ya sekta ya kilimo kushindwa kuchangia kwa kiasi cha kutosha katika ukuaji wa uchumi. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Sekta ya Kilimo ilichangia asilimia 26 tu ya pato la Taifa licha ya ukweli kwamba Watanzania wanaokadiriwa kufikia asilimia 80 wanajishughulisha na kilimo. Ukuaji wa Kilimo unashuka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2008/2009, Kilimo kilikua kwa asilimia 4.6, mwaka 2010 kilikua kwa asilimia 4.2 na mwaka 2011 kilikua kwa asilimia 3.6 tu, wakati huo huo idadi ya watu inakua kwa asilimia 2.9**.** (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Bajeti inayotengwa kwa kilimo imekuwa ikiongezeka kwa kiasi kidogo sana. Mwaka 2008/2009 ilikuwa ni shilingi bilioni 440 sawa na asilimia 6.4 ya bajeti ya Taifa, mwaka 2009/2010 shilingi bilioni 666.9 sawa na asilimia 7, mwaka 2010/2011 shilingi bilioni 903 sawa na asilimia 7.7, mwaka 2011/2012 shilingi bilioni 926, sawa na asilimia 6.7 na mwaka 2012/2013 shilingi bilioni 792, asilimia 5.3 tu ya Bajeti yote ya Serikali. Kamati

inaishauri Serikali ifanye uamuzi wa makusudi, bajeti ya Sekta ya Kilimo iweze kufikia angalau kiwango kilichokubaliwa na nchi za *SADC* cha asilimia 10 ya Bajeti ya Serikali ili sekta ya kilimo iweze kuchangia kikamilifu katika uchumi wa Taifa na wa mkulima mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na bajeti kupungua kila mwaka, bado bajeti hiyo inaelekezwa mijini na kusahau kabisa kutenga fedha kwa ajili ya shughuli za kilimo vijijini. Kamati inatoa rai kwa serikali kutenga bajeti kwa ajili ya kilimo vijijini ili kuinua uchumi wa wakulima wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inaishauri Serikali kuwa fedha za wafadhili zinazopatikana nje ya bajeti, Bunge lifahamishwe kupitia Kamati zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu kilimo kwanza; Kamati inaamini kuwa dhana ya Kilimo Kwanza ilibuniwa kwa nia ya kuleta mapinduzi ya kijani na kukifanya kilimo chetu kuwa cha kisasa ili nchi iweze kujitosheleza kwa chakula na kupata mazao mengi ya biashara na ya chakula kwa ajili ya soko la ndani na la nje. Kwa kufanya hivyo, uchumi wa mkulima mmoja mmoja na wa Taifa utaimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara, Kamati imetambua kwamba hakuna mikakati ya dhati ya kutekeleza dhana hiyo. Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Wizara zote zinazohusika na Sekta ya Kilimo zipewe fungu la kutosha kutekeleza azma ya Kilimo Kwanza ili utekelezaji wake uanze mapema na Wizara ziwajibike ipasavyo kwa matumizi bora ya fungu hilo;

(ii) Serikali itoe elimu kwa wakulima na wananchi kwa ujumla kuhusu maana halisi ya Kilimo Kwanza ili dhana hii ieleweke kwa mapana zaidi; na

(iii) Serikali iendelee kuhusisha Sekta Binafsi katika utekelezaji wa Kilimo Kwanza kwa kuhakikisha inawawekea vivutio mahsusi ikizingatiwa kwamba sekta binafsi inachangia kwa asilimia kubwa katika kukua kwa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni suala la utafiti; ili nchi iweze kuendelea katika sekta ya kilimo ni lazima iwekeze katika utafiti. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Mfuko wa Utafiti unaoratibiwa na *COSTECH*. Kamati inaishauri Serikali iendelee kuongeza fedha katika Mfuko huu ili hatimaye ufikie angalau asilimia moja ya pato la Taifa (1% *GDP*). Kwa upande wa taasisi mbalimbali za utafiti nchini kiasi cha fedha zinazotengwa katika bajeti ni ndogo na mtiririko wake hauridhishi. Kamati inasisitiza yafuatayo:-

(i) Fedha zinazotengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu katika taasisi za utafiti zinachelewa sana kuzifikia taasisi hizo. Kamati inashauri kwamba fedha hizo zigawiwe mapema ili taasisi zianze utekelezaji wake bila kuchelewa;

(ii) Matumizi ya teknolojia ya GMO (Genetically Modified Organisms) bado hayajatiliwa mkazo. Kuna taarifa nyingi kuhusu matumizi ya teknolojia hii zisizo sahihi ambazo zinawatia hofu wananchi; Serikali itoe elimu kwa umma kuhusu teknolojia hii ya *GMO* ili utekelezaji wake uende kwa haraka kwa kuwa una manufaa makubwa. Kamati inashauri Serikali kuangalia upya kanuni ambayo iko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ambayo imekuwa kikwazo kwa matumizi ya *GMO* ili ziweze kutumika;

(iii) Utafiti wa matumizi ya bioteknolojia ufanyike ili kutengeneza mbegu bora zenye vinasaba vyenye uwezo wa kustahimili ukame kwa kuzingatia kwamba bioteknolojia imeendelea kukua kwa kasi kubwa ulimwenguni na kuwa nyenzo kubwa katika kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo;

(iv) Vituo vya utafiti vitengewe fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha vinapatiwa vitendea kazi bora na vya kisasa; na

(v) Serikali ihakikishe matokeo ya utafiti yanawafikia wakulima kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne ni suala la pembejeo; tukianzia na mbolea. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza wigo wa ruzuku ya pembejeo; pamoja na pongezi hizo Kamati bado inasisitiza yafuatayo:-

- Serikali iendelee kuongeza idadi ya wakulima wanaopata ruzuku kwani itasaidia katika kuongeza tija. Aidha, Serikali ihakikishe inafanya utafiti ili kutambua jinsi misimu inavyotofautiana katika kila Kanda au Mikoa. Hii itahakikisha mbolea inawafikia wakulima wa kila eneo kwa wakati muafaka;

- Serikali ijenge Viwanda vya Mbolea nchini ikizingatiwa kuwa nchi yetu imebarikiwa kwa kuwa na gesi asilia na madini ya *phosphate* ambayo ni malighafi muhimu;

- Gharama ya kuleta mbolea ambayo tayari imefungwa katika mifuko kutoka nje ya nchi ni kubwa mno. Kamati inashauri mbolea hiyo iingizwe nchini in *bulk* ili ifungwe hapa hapa nchini. Hii itapunguza kwa kiasi kikubwa gharama ya bei kwa wakulima;

- Ili wakulima wenye mahitaji ya viwango tofauti waweze kupata mbolea kulingana na uwezo na mahitaji yao, ni vyema mbolea zikafungwa katika mifuko yenye ujazo tofauti, mfano kilo tano (5), 10, 25 na 50. Hii itasaidia wakulima kujitokeza kununua kulingana na mahitaji na uwezo wao kifedha; na

- Pamoja na kwamba Serikali imekuja na mfumo mpya wa usambazaji pembejeo, utaratibu huo ufanyike kwa makini, vinginevyo bado hautakidhi mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia Kiwanda cha Mbolea cha Minjingu kusitisha uzalishaji wa mbolea ya Minjingu, (Minjingu Mazao) ambayo utafiti umeonesha

ina ubora kama mbolea inayoagizwa kutoka nje ya nchi *(DAP)*, Kamati inashauri yafuatayo:-

- Kwa kuwa kulikuwa na makubaliano kati ya Kiwanda cha Minjingu na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kufuatia agizo la Waziri Mkuu, ni vyema Serikali ikatekeleza makubaliano hayo kwa kuagiza mbolea moja kwa moja kutoka kiwandani;

- Serikali ithamini viwanda vya ndani ambavyo vinakuza ajira kwa vijana wetu na kukuza uchumi wa nchi; na

- Ni vyema ruzuku inayotolewa na Serikali inufaishe viwanda vya ndani kuliko ilivyo sasa ambapo kiwango kikubwa cha ruzuku ya mbolea inakwenda kwa viwanda vya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbegu bora ni moja ya misingi ya kuleta tija katika kilimo ili kuwawezesha wakulima kuzalisha chakula cha kutosha na kuhakikisha kunakuwepo na usalama wa chakula. Kamati inasisitiza yafuatayo:-

- Serikali ihakikishe usimamizi na uratibu wa ubora wa mbegu unafanywa kwa umakini. Aidha, wakulima wapelekewe mbegu kwa wakati ili kuwadhibiti wafanyabiashara wanaowahadaa kwa kufunga mbegu zisizo na ubora unaostahili kwenye vifungashio vinavyotumika kwa mbegu bora; na

- Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka jukumu la kuzalisha mbegu bora na za kutosha kwa

Jeshi la Magereza na Jeshi la Kujenga Taifa badala ya kutegemea mbegu za nje ambazo hazina uhakika na ubora wake. Hii itapunguza gharama za ununuzi wa mbegu kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pembejeo ya tatu ni madawa. Kutokana na mazao mengi yakiwemo ya chakula na ya biashara kushambuliwa na wadudu waharibifu, Kamati inashauri Serikali iongeze bajeti ya madawa ya mazao haya ili kuongeza uzalishaji. Aidha, utafiti wa kutumia viuatilifu vya kimaumbile uendelee ili wakulima wavipate kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano ni kuhusu uwekezaji; ili kilimo kikue kwa kasi inayotakiwa na kuwavutia wawekezaji ni vyema nchi iweke mazingira mazuri katika kilimo. Kamati inashauri kwamba:-

(i) Serikali iongeze bajeti ya Sekta ya kilimo kwa kadri itakavyowezekana;

(ii) Serikali iweke vivutio kwa wawekezaji ili washawishike kuja kuwekeza katika kilimo cha mashamba makubwa;

(iii) Serikali ipunguze urasimu ili kuondoa usumbufu kwa wawekezaji;

(iv) Serikali iwahimize wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kujenga Viwanda vya Kusindika Mazao ili kuongeza thamani yake;

(v) Serikali iishirikishe Sekta binafsi katika suala zima la uwekezaji kwani inachangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa sekta hii;

(vi) Serikali iangalie mikataba inayoingia na wawekezaji ili kuepuka kuingia mikataba ya muda mrefu yaani ya miaka mingi na hatimaye kupoteza eneo kubwa la ardhi bila tija. Aidha, ushirikishwaji wa wanachi katika kutoa maeneo ya uwekezaji uzingatiwe ili kuhakikisha uhusiano mzuri unakuwapo na kuepusha migogoro isiyo ya lazima;

(vii) Serikali izingatie matumizi sahihi ya ardhi yanayoendana na mkataba unavyotaka ili kuepuka matumizi mengine yanayowanufaisha wawekezaji na kudhoofisha maendeleo ya wananchi;

(viii) Serikali inashauriwa kwa mara nyingine kutenga maeneo kwa ajili ya Benki ya Ardhi ili yawe tayari kuwapatia wawekezaji mara tu wanapojitokeza kuendesha shughuli za kilimo; na

(ix) Zoezi la upimaji wa ardhi ya vijiji linakwenda taratibu sana. Kamati inashauri zoezi hili liwezeshwe ili liende kwa kasi zaidi ikiwa ni pamoja na ushirikishwaji wa wanakijiji katika zoezi la uainishaji wa maeneo ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita ni suala la uzalishaji wa Mazao; mosi ni mazao ya chakula; Kamati inasisitiza kwamba uzalishaji wa mazao ya chakula upewe kipaumbele kwa kuongeza ruzuku ya pembejeo katika maeneo yanayolima mazao hayo. Aidha, kwa

maeneo yenye ukame Serikali isimamie ulimaji wa mazao yanayostahimili ukame kama vile mtama, uwele na muhogo ili kuondokana na baa la njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni mazao ya biashara, mazao haya ni muhimu kwa uchumi wa watu wetu na Taifa kwa ujumla. Hata hivyo, kumekuwa na matatizo katika hatua za uzalishaji, usindikaji na hata soko, kiasi cha kuwakatisha tamaa wakulima wa mazao husika mfano:-

(a) Pamba; takribani watu milioni 16 nchini wanategemea kilimo cha pamba kwa maisha yao. Kilimo hicho ni cha mkataba kati ya mkulima na mnunuzi, mnunuzi anamkopesha mkulima bila kujua bei ya pamba mwisho wa msimu. Mathalani katika msimu huu, gharama ya uzalishaji kilo moja ya pamba ni shilingi 800 wakati bei ya soko ni shilingi 660 jambo ambalo limekuwa ni kero kubwa kwa wakulima na kushindwa kumudu maisha yao. Aidha, asilimia 70 ya pamba ghafi inauzwa soko la nje na asilimia 30 tu ya pamba hiyo ndiyo inatumika katika viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo pia na tatizo la mbegu ambazo hazioti na madawa ambayo hayauwi wadudu; yote haya yakiongeza hasara kubwa kwa mkulima. Kamati inashauri Serikali kufanya jitihada kuhakikisha kwamba, viwanda vingi vya kutengeneza nguo vinafufuliwa nchini ili wakulima wengi wapate masoko na kuongeza ajira kwa wananchi.

(b) Korosho; Tanzania ni moja ya nchi ambazo zinazalisha korosho kwa wingi lakini tatizo lake kubwa ni ukosefu wa viwanda na soko na hivyo kulazimika kuuza zaidi ya asilimia 75 ya korosho ghafi nje ya nchi. Aidha, kumekuwepo na tatizo la kupata pembejeo kwa wakati. Kamati inashauri kwamba Viwanda vya Korosho vilivyopo nchini vifufuliwe na vile ambavyo vimebinafsishwa lakini havifanyi kazi virejeshwe Serikalini.

(c) Kahawa; kwa sasa bei ya kahawa katika soko la dunia ni nzuri. Kamati inasikitishwa na utaratibu mpya wa kununua kahawa mbichi (*cherry coffee*) na kuwakosesha wakulima mapato yao. Kamati inaitaka Serikali kuangalia upya kanuni inayoruhusu kununua kahawa mbichi toka kwa mkulima.

(d) Tumbaku; hili ni zao la kwanza kuliingizia Taifa fedha za kigeni, lakini tatizo kubwa la zao hili ni ukosefu wa soko la kuaminika na upungufu wa wateuzi (*tobacco classifiers*). Kamati inashauri Serikali ikishirikiana na Bodi ya Tumbaku kutafuta soko la uhakika.

(e) Chai; wakulima wadogo wadogo wa chai wamekuwa wakiuza chai yao (*green leaf*) kwa wakulima wakubwa na wenye viwanda kwa bei ya chini na hivyo kutonufaika. Kamati inashauri kwamba, Wizara iendeleze zao la chai (*tea development*) na kuanzisha vikundi vya ushirika kwa kilimo cha chai, ili wazalishe kwa tija, wasindike na hatimaye kuuza katika soko (*value chain*). Kama ilivyo katika nchi jirani ya

Kenya yenye viwanda vya wakulima wadogo wadogo zaidi ya 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kilimo cha mazao ya biashara kiwe endelevu, Kamati inashauri yafuatayo:-

- Serikali ione uwezekano wa kuweka kinga katika mazao iwapo bei itashuka chini ya gharama za uzalishaji;

- Serikali ikishirikiana na Bodi za mazao, ihakikishe kwamba Ushirika katika mazao ya biashara unaimarika; na

- Serikali ishirikiane na Bodi za Mazao ya Biashara kutafuta masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni mazao mengine; Kamati inasisitiza Serikali ijikite katika kuhimiza uzalishaji wa mazao mengine mapya kama viungo, matunda, mbogamboga na maua; mazao haya yatasaidia kuliongezea Taifa pato na kukuza uchumi wa nchi. Serikali ihakikishe inawapatia mitaji na utaalam wakulima. Aidha, Serikali itumie Chuo cha Utafiti cha *KATRIN* katika kupeleka utaalam wa mazao ya viungo kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba ni kuhusu Benki ya Kilimo; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutenga fungu maalum kwa ajili ya Benki ya Kilimo. Kamati inasisitiza mchakato wa kuanzisha Benki ya Kilimo uharakishwe na kukamilishwa ili wakulima waweze kufaidika na mikopo ya riba ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa kipindi hiki ambacho benki haijaanza kufanya kazi, Serikali ione umuhimu wa kuweka dirisha dogo katika benki zinazowafikia wakulima kwa urahisi vjijini na mijini. Utaratibu huu upo katika Benki ya Rasilimali Tanzania *(TIB)* lakini wakulima wa vijijini hawanufaiki nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane ni kuhusu huduma za Ugani; Kamati inatambua umuhimu wa huduma za ugani katika kuhakikisha kilimo kinakuwa na tija. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Vyuo vya Ugani toka vyuo nane (8) hadi vyuo kumi na nne (14). Hata hivyo, Kamati inasisitiza huduma za ugani ziboreshwe kwa kuhakikisha yafuatayo yanatekelezwa:-

- Wagani wapatiwe motisha kwa kujengewa makazi hasa maeneo ya vijijini na kuhakikishiwa usafiri ili iwe rahisi kutoa huduma kwa wakulima wa maeneo ya mbali;

- Idadi ya Wagani iliyopo haikidhi mahitaji, hivyo, Serikali izalishe Wagani wengi zaidi katika vyuo vyake;

- Wagani waliopo wapewe waraka unaoelekeza majukumu yao *(job Description)* na usimamizi (*supervision)* ili uwajibikaji uwepo;

- Wataalam wa ugani wanaopangwa sehemu zinazolima mazao maalum wapewe elimu ya ziada ya mazao hayo ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi; na

- Vyuo vya Ugani vilivyopo viboreshwe kimiundombinu ili kuleta ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa ni kuhusu Mfuko wa Taifa wa Pembejeo; Mfuko huu ni muhimu sana hasa katika kipindi hiki ambacho Benki ya Kilimo bado haijaanza kufanya kazi kwani inasaidia kutoa mikopo kwa wakulima. Mfuko huu umekuwa ukipokea maombi mengi kuliko uwezo wake kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko huu ndio unaotoa mkopo kwa riba ndogo sana, lakini inasikitisha kwamba bajeti yake haikidhi mahitaji makubwa yaliyopo. Bajeti ya Mfuko imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka wakati mahitaji yanaongezeka kila siku. Kwa mwaka huu 2012/2013 ni shilingi bilioni 3.4 tu zilizotengwa ambazo ni pungufu ya bajeti ya mwaka 2011/2012 ya shilingi bilioni 3.8; Kamati inaishauri Serikali iongeze bajeti ya Mfuko huu ili iweze kuwahudumia wakulima wengi zaidi, kwani maombi ya mikopo ya pembejeo ni mengi zaidi ikilinganishwa na fedha inayotengwa kwa ajili ya Mfuko huu muhimu. Maombi ni wastani wa shilingi bilioni nane kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi ni suala la Vyama vya Ushirika; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kulipa madeni ya Vyama vya Ushirika. Hatua hii itaweza kuvipunguzia mzigo wa madeni Vyama hivyo na kufufua vilivyokuwa vimekufa. Pamoja na hatua hiyo, Kamati inashauri yafuatayo:-

- Serikali iharakishe mchakato wa kuanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika ikiwa ni sehemu ya

mkakati wa kuongeza wanachama wa Ushirika kwa njia ya uhamasishaji;

- Watendaji wa sekta ya Ushirika ni wachache ikilinganishwa na mahitaji. Maafisa Ushirika waliopo katika Mikoa na Wilaya za Tanzania Bara ni 547, wakati mahitaji halisi ni 950. Hivyo, Serikali iweke mikakati ya kuongeza maafisa hao pamoja na kuwawezesha kwa vitendea kazi; na

- Ili kukomesha ubadhirifu unaofanywa na baadhi ya Viongozi wa Vyama vya Ushirika, Wizara iongeze Maafisa Wakaguzi wa Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na moja ni kuhusu Bodi za Mazao; Bodi hizi ni muhimu sana katika kusimamia mazao yetu na kuhakikisha yanazalishwa kwa kiwango kikubwa. Ili Bodi hizi ziweze kusimamia mazao husika vizuri, ni lazima ziwezeshwe vya kutosha kifedha. Bodi nyingi bado hazitengewi fedha za kutosha, hivyo, kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kamati inashauri:-

- Serikali iendelee kuziongezea fungu Bodi hizi kulingana na mahitaji yao;

- Serikali ihakikishe kuwa Bodi hizi zinaendeshwa kwa mujibu wa sheria ili kuondoa urasimu wa kutoa leseni za biashara za mazao ambao unaathiri ushindani kwa kiwango kikubwa; na

- Bodi za mazao zihimize umuhimu wa kuongeza thamani ya mazao kabla ya kuuza ndani na

nje ya nchi ili kuongeza kipato cha mkulima na pato la Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na mbili ni Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA);* Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kuendelea kusaidia Wakala wa Hifadhi ya Chakula nchini. Pamoja na pongezi hizi, Kamati ina ushauri ufuatao:-

(i) Maghala ya kuhifadhia chakula ni machache nchini ikilinganishwa na mahitaji halisi. Serikali iongeze maghala haya Ili uhifadhi wa chakula uweze kufikia lengo la kuhifadhi na kusambaza chakula cha njaa cha kutosha;

(ii) Maghala yaliyopo yamechakaa na mengine yanavuja wakati wa mvua. Serikali itenge fedha za kukarabati maghala haya ili chakula kinachohifadhiwa kisiharibike;

(iii) Wakala wa chakula upewe uwezo zaidi wa fedha wa kununua mazao ya chakula ili kiwepo chakula cha kutosha ghalani wakati wote. Aidha, Vyama vya Ushirika vishirikishwe katika kununua mazao na kuhifadhi; na

(iv) Vitendea kazi duni vilivyopo kwenye maghala vinadhoofisha utendaji kazi wa Wakala. Serikali iangalie upatikanaji wa magunia ya kuhifadhia chakula kwani yaliyopo hayatoshi na viwango vyake vya ubora haviridhishi. Aidha, viwanda vinavyotengeneza magunia vipewe msukumo ili kuhakikisha yanapatikana kwa wingi na kwa ubora wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na tatu ni kuhusu kilimo cha umwagiliaji; kutokana na ukame unaojitokeza mara kwa mara pamoja na mabadiliko ya tabianchi, kilimo cha umwagiliaji ndiyo mkombozi wa uhakika kwa upatikanaji wa mazao ya chakula na biashara nchini. Ukuaji huo wa kilimo cha umwagiliaji unakwenda taratibu mno ukilinganisha na mahitaji makubwa ya kilimo hicho. Hivyo Kamati inaishauri Serikali:-

- Kuongeza bajeti kwa ajili ya kuanzisha skimu ndogo, za kati na kubwa katika maeneo mbalimbali nchini;

- Kuainisha na kuyatumia mabonde mengi ya Maziwa na Mito Kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji;

- Kuviongezea uwezo wa kiutendaji Vituo vya Kanda vya Umwagiliaji ikiwa ni pamoja na kuboresha na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za wakulima wadogo na kujenga skimu mpya katika maeneo yanayofaa kuendelezwa ili kuweza kuwahudumia wananchi na Halmashauri za Wilaya kwa wingi; na

- Kuongeza idadi ya wataalam wa umwagiliaji na kuwaajiri katika Halmashauri za Wilaya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika,kumi na nne ni suala la ushuru wa mazao; kwa muda mrefu sasa wakulima wamekuwa wakitozwa ushuru wa mazao yao wanapoyatoa shambani kuyapeleka nyumbani.

Ushuru huu kwa kiasi kikubwa ndio sababu ya kupanda kwa bei ya chakula. Kamati inaishauri Serikali:-

- Iangalie taratibu za kutoza ushuru wa mazao ili kuepuka kuwatoza wakulima wanaotoa mazao yao shambani na kuyapeleka nyumbani; na

- Ushuru wa asilimia mbili wa zao la tumbaku ambao Serikali iliahidi ni vyema ukazingatiwa kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mjumbe; Mheshimiwa Abdusalaam S. Ameir, Mjumbe; Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mjumbe; Mheshimiwa Namelok E. M. Sokoine, Mjumbe; Mheshimiwa Daktari Christine G. Ishengoma, Mjumbe; Mheshimiwa Seleman Said Jafo, Mjumbe; Mheshimiwa Moshi S. Kakoso, Mjumbe; Mheshimiwa Sylevester M. Kasulumbayi, Mjumbe; Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mjumbe; Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mjumbe na Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mjumbe. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mjumbe; Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran, Mjumbe; Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mjumbe; Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mjumbe; Mheshimiwa Rose Kamil Sukum, Mjumbe; Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mjumbe; Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mjumbe; Mheshimiwa Seleman Said Bungara, Mjumbe; Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mjumbe; Mheshimiwa Daktari Titus Mlengeya Kamani, Mjumbe; Mheshimiwa Daktari Lucy Sawere Nkya, Mjumbe na mwisho ni mimi mwenyewe Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika, Mheshimiwa *Engineer* Christopher Chiza na Naibu Waziri Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, kwa ushirikiano wao mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni na kisheria ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Ndugu Mohamed Muya na Manaibu Katibu Wakuu, Ndugu Sophia Kaduma na *Engineer* Mbogo Futakamba, pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Daktari Thomas Kashililah na Katibu wa Kamati hii Ndugu Elieka Saanya kwa kuihudumia vizuri Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru vile vile wapiga kura wangu wa Rungwe Magharibi kwa heshima waliyonipa na kunirudisha katika mjengo huu bila kupingwa. Lakini mwisho kwa shukrani, namshukuru mke wangu Margareth ambaye najua yupo pale *Area D* ananiangalia kwenye luninga kwa nguvu anayonipa na ushauri, nasema ahsante sana Margareth. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika Fungu 43, kwa mwaka 2012/2013 jumla ya sh. 237, 624, 575,000/= na Fungu 24, jumla ya sh. 6,104,209,363/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati na kwa heshima kubwa kabisa, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Mwakyusa Mwenyekiti wa Kamati inayosimamia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Waheshimiwa Wabunge wakati natangaza wageni wetu, kuna wageni waliokuwa wamechelewa kidogo ambao ni wanafunzi na walimu 26 wa Shule ya Msingi ya Kinondoni, wageni wa Mheshimiwa Idd Azzan wanaongozwa na Mwalimu Mkuu Msaidizi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani aje kutoa maoni ya Kambi hiyo. Mheshimiwa Sukum!

MHE. ROSE K. SUKUM – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii na kwa niaba ya Wabunge wenzangu wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani kutoa rambirambi kwa ndugu, jamaa na marafiki kwa msiba mkubwa uliolikumba Taifa wa kuzama meli ya abiria iliyokuwa inatoka Zanzibar kuja Dar es Salaam. Mwenyezi Mungu atupe wote roho ya subira na ustahimilivu. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(7), Toleo la 2007 kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa moyo wa dhati napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema na fadhila kwa kunijalia uhai, afya njema na kwa upendo wake anaotujalia kila mmoja wetu kwa nafasi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee napenda kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Mwenyekiti wa Chama makini cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Makamanda wenzangu wa chama hiki makini cha watu. Aidha, napenda kuwashukuru Watanzania wote wenye mapenzi mema na nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya kilimo na chakula nchini. Hali ya kilimo nchini si nzuri, kwani, sekta ya kilimo nchini kwa mwaka 2011 imezorota kwa asilimia 0.6% ikilinganishwa na mwaka 2010. Aidha, mchango wa sekta ya kilimo kwenye pato la Taifa *(GDP)* umeshuka kwa asilimia 0.4% kwa mwaka 2011/2012, ukilinganishwa na mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya chakula nchini hairidhishi, kwani uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa 2010/2011 umepungua ukilinganishwa na mahitaji ya chakula kwa mwaka 2011/2012. Kwa mujibu wa Taarifa ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwenye Kamati ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo ya tarehe 8 Juni, 2012 ni kwamba kuna upungufu wa jumla ya tani 204,821 kwa mazao ya nafaka . Kati ya upungufu huo mahindi yakiwa ni tani 160,917 na ngano upungufu wa tani 111,717.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kueleza mbele ya Bunge hili kuwa imechukua hatua gani hadi sasa katika kukabiliana na upungufu wa chakula nchini, hasa ikizingatiwa kuwa nchi hii ina mabonde mengi yanayofaa kwa kilimo na maji ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya kilimo na hatma yake katika uchumi. Kilimo ni sekta ambayo ni tegemeo na ni kimbilio la Watanzania wengi katika kuendeleza maisha yao. Kwa mujibu wa Taarifa Fupi ya Benki ya Dunia (2011) kuhusu uchumi wa Tanzania, ni kwamba takriban asilimia 80 ya kaya za Kitanzania hutegemea kilimo kama shughuli zao za msingi za

kiuchumi. Taarifa hiyo inaeleza kwamba, kitendo cha Watanzania wengi kiasi hiki kutegemea kilimo, kinauweka uchumi wa Tanzania katika hali ya hatari kutokana na kilimo kuwa na tabia ya kuathiriwa sana na mabadiliko ya hali ya hewa pamoja na kupanda na kushuka kwa bei za mazao katika masoko ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ya hatari tayari imeanza kutokea kwani kwa muda wa miaka kumi iliyopita kilimo kimekuwa kinashuka nafasi katika uchangiaji wa uchumi wa Taifa. Kwa mujibu wa taarifa fupi ya Benki ya Dunia (2011) kuhusu uchumi wa Tanzania ni kwamba, sekta zinazoongoza kwa kuchangia uchumi wa Taifa katika miaka kumi iliyopita ni madini, ujenzi, mawasiliano, huduma na sekta ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, si jambo baya kupata mapato kutoka katika Sekta nilizozitaja, ila ni hatari sana uchumi kutegemea rasilimali zinazokwisha *(non-renewable resources)* kwa mfano madini. Ni hatari vile vile uchumi kutegemea sekta ndogo kama ujenzi, mawasiliano, huduma na fedha kwa kuwa hazina wigo mpana wa ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kama hii husababisha uchumi kuwa ni wa kitendawili kwa maana kwamba; wakati hali ya uchumi wa Taifa inaonekana kwenda vizuri, idadi ya watu wasio na ajira inaongezeka na umaskini wa mtu mmoja mmoja unaongezeka pia. Hii ina maana kwamba sekta zinazoongoza katika kuchangia uchumi wa Taifa kwa

sasa hazina mchango wa moja kwa moja kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja. Hivyo, kuna umuhimu mkubwa sana wa kuwekeza katika kilimo kwani kinaajiri watu wengi zaidi hapa nchini (80% kwa sasa) na msingi wake ni rasilimali ardhi ambayo ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa Bajeti iliyopita 2011/2012. Taarifa ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Kamati ya Bunge (ukurasa wa 26) ni kwamba, fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya Wizara hii Fungu 43 mwaka 2011/2012 ni shilingi bilioni 258.35; Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 152.41 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 105.94 zikiwa ni fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 31 Mei, 2012 fedha za matumizi zilizopelekwa Wizarani kutoka Hazina ni shilingi bilioni 103.06 sawa na asimia 67.62 ya kiasi kilichoidhinishwa. Kwa upande wa fedha za maendeleo hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2012 fedha zilizokuwa zimepelekwa Wizarani kutoka Hazina ni shilingi bilioni 72.63 sawa na asilimia 68.56 ya fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika muktadha huo huo, fedha zilizoidhinishwa kwa Wizara hii, Fungu 24 kwa mwaka 2011/2012 zilikuwa ni shilingi bilioni 6.612 kwa matumizi ya kawaida. Hata hivyo, fedha iliyokuwa imetolewa na Hazina hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2012 ni shilingi bilioni 4.63 sawa na asilimia 70 ya kiasi kilichoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi, ni kwamba, bajeti ya Wizara hii katika Fungu 43 haikutekelezwa kwa zaidi ya theluthi moja. Huu ni uthibisho kamili kwamba malengo yaliyopangwa kufikiwa katika mwaka wa fedha 2011/2012 hayakufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo mbele ya Bunge hili Tukufu kwa nini tuipatie fedha inazoomba kwa Wizara hii, wakati mwaka jana haikutekeleza bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na hivyo kuzorotesha malengo ya Wizara hii. Aidha, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza itatekeleza vipi viporo vya malengo ambayo hayakutekelezwa kwa mwaka uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka 2012. Kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji ya Wizara hii (ukurasa wa 62), (Fungu 43) bajeti imepungua kutoka shilingi bilioni 258.35 mwaka 2011/2012 hadi shilingi bilioni 237.624 sawa na punguzo la asimia 8.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupungua kwa jumla kwa bajeti, matumizi ya kawaida yameongezeka kutoka shilingi bilioni 152.41 mwaka 2011/2012 hadi kufikia shilingi bilioni 170.364, sawa na ongezeko la asilimia 11.78.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati matumizi ya kawaida yameongezeka kwa takriban asilimia 12, bajeti ya maendeleo katika Wizara hii imepungua kutoka shilingi bilioni 105.94 mwaka 2011/2012 hadi

kufikia shilingi bilioni 67.260, ikiwa ni anguko la asilimia 57.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza, Hivi kitendo cha kupunguza fedha za maendeleo kwa asilimia 57.5 katika Wizara ya Kilimo ndio mkakati wa kutekeleza kauli mbiu ya Kilimo Kwanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na fedha hizi za maendeleo kupungua kiasi hiki, bado bajeti ya maendeleo imeendelea kuwa tegemezi kwa fedha za nje kwa asilimia 77.7. Tafsiri ya utegemezi huu ni kwamba sasa Serikali imeamua kukiweka kilimo chetu rehani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa makini Jedwali namba saba (7) lenye mchanganuo wa bajeti ya matumizi ya maendeleo katika taarifa ya utekelezaji ya Wizara hii ukurasa wa 65, utagundua kuwa miradi ambayo inaweza kuendeleza kilimo chetu kwa mfano utafiti na maendeleo, umwagiliaji, mpango wa matumizi ya ardhi, kilimo cha kisasa imetengewa fedha ndogo sana za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoshangaza kabisa ni kwamba kasma 5001 inayohusu Usalama wa Chakula wa Taifa, hakuna hata senti moja kutoka ndani. Hii ina maana usalama wa chakula wa Taifa uko mikononi mwa wahisani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali isifanye mzaha kabisa na masuala ya

usalama wa chakula nchini kwa kuwa usalama wa chakula ndio uhai wenyewe wa wananchi. Kutotenga fedha za ndani kwa ajili ya usalama wa chakula ni kuweka rehani maisha ya Watanzania na huku ni kuudhalilisha utu na uhuru wa Mtanzania na kamwe hatutakubaliana na hali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani kwa mara nyingine inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ina mpango gani wa kuwahakikishia Watanzania usalama wa chakula ikiwa fedha zote za usalama wa chakula zinatoka nje? Pili, Serikali ieleze njia nyingine mbadala za kuendeleza kilimo iwapo wahisani au wafadhili watakoma kutoa misaada katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema: “Tunakipuuza kilimo; kama tungekuwa hatukipuuzi, basi Wizara zote, mashirika ya umma yote na mikutano yote ya chama ingekuwa inafanya kazi kushughulikia mahitaji ya wakulima. Ni lazima sasa tuache kukipuuza kilimo. Ni lazima tukifanye kilimo kiwe ndio shina na mwanzo wa mipango yetu yote ya maendeleo. Kwani kwa hakika, Kilimo ndio msingi wa maendeleo yetu” (Nyerere, 1982).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupunguza bajeti hii ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ni dhahiri kwamba, Serikali hii ya CCM inapuuza kilimo. Hivyo, Kambi ya Upinzani inaiasa Serikali ya CCM kuzingatia wosia wa Baba wa Taifa ambaye tangu mwaka 1982 alishagundua kuwa CCM inapuuza kilimo ambacho ndio tegemeo la Watanzania wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwiano wa mgawanyo wa bajeti na usalama wa chakula nchini; mojawapo ya malengo ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ni kuhakikisha usambazaji na uwepo endelevu wa chakula katika kila kaya. Kwa maneno mengine lengo hili likifikiwa, kutakuwepo na usalama wa chakula katika kila kaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa utafiti wa Gabagambi (2011), Tanzania haizingatii hali ya usalama wa chakula katika mgawanyo wa bajeti ya kilimo. Katika utafiti huu ilibainika kwamba Mikoa 10 ya Tanzania Bara ambayo ni Arusha, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mara, Mwanza, Mtwara, Shinyanga, Singida, na Tabora haina usalama madhubuti wa chakula. Utafiti uliofanywa, unaonesha kuwa mikoa hii haipatiwi kipaumbele maalum cha kibajeti ili kuhakikisha kuwa kuna usalama wa chakula katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya utafiti wa Gabagambi (2011), unaonesha kwamba mikoa kumi iliyotajwa ambayo ni karibu asilimia 50 ya mikoa yote ambayo ni asilimia 46.2% ya idadi ya watu wote nchini, ilipewa asilimia 30.2 tu ya bajeti ya Kitaifa ya *District Agricultural Development Plans (DADPs)* kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ni vigezo gani vinatumiwa katika kugawa fedha za *DADPs*. Pili, Serikali ina mkakati gani maalum wa kuhakikisha kuwa kuna usalama wa chakula hasa katika mikoa yenye upungufu mkubwa wa chakula nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pembejeo na zana za kilimo. Katika kufanikisha lengo la kukuza kilimo nchini, Serikali imepunguza bei ya trekta za SUMAJKT ili kuwawezesha wakulima kumudu bei, mfano *Farmtrac* 60 (yenye *horse power* 50, *2 wheel drive*) iliyokuwa inauzwa shilingi milioni 25.64 na baada ya punguzo sasa inauzwa shilingi milioni 16.5 kiwa ni punguzo la asilimia 35.71%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka wazi ni kwa nini punguzo hili halikufanywa mapema ili kuwawezesha wananchi kufaidi punguzo hili mapema? Pia vifaa kwa ajili ya matrekta haya kama *harrow*, majembe, *planters*, na kadhalika kwa nini havikupunguzwa bei ili wananchi waweze kunufaika na punguzo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa mkulima inalenga kupunguza gharama za kuendesha kilimo kwa wakulima wadogo. Hata hivyo, mfumo wa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima umekuwa na matatizo mengi. Moja ya matatizo yaliyojitokeza katika mfumo wa vocha za ruzuku ya pembejeo kwa wakulima ni pamoja na baadhi Viongozi wa Serikali kula njama na Mawakala kuiba vocha kwa kutumia majina hewa na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu huku wananchi wakibaki bila pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Gazeti la Mwananchi la Machi 6, 2011, shilingi 5,004,169,500/= zilikuwa zimeibwa na wajanja kutoka katika Mfuko wa Pembejeo. Upotevu huo unawahusisha baadhi ya

watendaji wa Serikali na baadhi ya Wakuu wa Wilaya ambao ndio wasimamizi wakuu wa Mfuko wa Pembejeo. Aidha, Gazeti la Habari Leo la Juni 21, 2012, lilimnukuu Mkuu wa Mkoa wa Arusha akiamuru Wkala wa pembejeo Ndugu Selestine Magati kupelekwa Mahakamani kwa kuwaibia wakulima mbolea ya ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mfumo huu wa kusambaza pembejeo za kilimo kwa njia ya vocha umegubikwa na wingu la rushwa, wizi, ulanguzi na hata uchakachuaji wa pembejeo (kwa mfano mbolea kuchanganywa na saruji), Serikali imebuni njia gani mbadala ambayo itasaidia wakulima kupata pembejeo bila usumbufu wanaoupata sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sera ya Kilimo ya mwaka 1997 inasema kilimo kiwe cha kisasa na endelevu, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuacha mtindo wa kuzifanya pembejeo kama mbolea na mbegu kuwa bidhaa za msimu na badala yake bidhaa hizo ziwe kwenye soko muda wote wa mwaka. Hii ndiyo njia pekee itakayoondoa rushwa na ulanguzi katika usambazaji wa pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo Mfuko wa pembejeo wa Taifa ambao hutoa mikopo ya vifaa vya kilimo kama trekta, *power tiller*, mikopo ya kukarabati trekta, mashine za umwagiliaji na usindikaji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo hii huwa ni mikubwa kiasi kwamba wanaoweza kumudu

marejesho ni wakulima wakubwa ambao ni wachache. Hii ina maana kwamba wakulima wadogo wadogo ambao ndio wengi hapa nchini hawanufaiki na Mfuko huu na hivyo kilimo chao kinazidi kuzorota.

Mheshimiwa Naibu Spika, masharti ya Mfuko huu yarekebishwe ili na wakulima wadogo wadogo waweze kunufaika na Mfuko huu ambao kwa sasa si rafiki wa wakulima wadogo. Aidha, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwe na Mfuko mmoja wa Pembejeo ili kutowachanganya wakulima wakati wa ufuatiliaji wa pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo kwa wakulima. Katika utoaji wa mikopo kwa wakulima hapa nchini kumekuwa na matatizo kama:-

- Mikopo kufika bila kuzingatia misimu ya kilimo;

- Urasimu na mlolongo mrefu katika kuchukua mikopo;

- Urejeshaji wa mikopo mara kwa mara bila kuzingatia msimu wa mavuno;

- Taasisi chache za mikopo na zisizokuwa na matawi mengi nchini, hivyo kusababisha wakulima kusafiri umbali mrefu katika kufuatilia mikopo; na

- Upendeleo katika utoaji wa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kutoa mapendekezo yafuatayo ili

kuondokana na matatizo yatokanayo na mikopo kwa wakulima:-

- Mfuko wa Pembejeo wa Taifa na zana za kilimo ufungue ofisi katika kila Wilaya na kutoa mikopo moja kwa moja kwa wakulima bila kupitia katika uongozi wa Mikoa au Wilaya, hili litasaidia kupunguza urasimu mrefu wanaokutana nao wakulima wakati wa kuchukua mikopo;

- Taasisi za fedha zipunguze masharti ya upatikanaji wa mikopo kwa wakulima hasa wadogo ikiwemo kupunguza riba zinazotozwa wakati wa urejeshaji wa mikopo, tunapendekeza kupunguza kiwango cha malipo ya mwanzo kutoka asilimia 50 ya sasa hadi asilimia 25 ili kuwawezesha wakulima wadogo kumudu kupata mikopo hiyo; na

- Muda wa marejesho ya mkopo uongezwe na uzingatie msimu wa mavuno tofauti na sasa ambapo msimu wa mavuno hauzingatiwi na mkopaji hutakiwa kurejesha mkopo muda mfupi tu baada ya kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi mabaya ya mashamba ya *NAFCO*. Mashamba hayo yaliyo chini ya mwekezaji *NGANO Limited* yanatumika chini ya kiwango na hivyo kwenda kinyume na sera ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ekari 30,000 za mashamba ya Murjanda, Gidamowd na Setchet, ni ekari 9,000 tu zinazolimwa. Kutokana na hali hii,

takriban watu 600 wamekosa ajira kutokana na matumizi ya mashamba haya chini ya kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha shamba la *Bassotu Plantation* halijapata mwekezaji. Shamba hili lina vifaa kama Matrekta, *Combine Harvesters*, *Boom Sprayers* na vifaa vingine ambavyo vinaharibika kwa kutu, kuungua, na vingine kuibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasemaje kuhusu hasara inayotokana na uharibifu wa vifaa inayoendelea kutokea katika Shamba la *Bassotu Plantation*? Aidha, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kurudisha mashamba haya kwa wanachi kwa kuwa kwa sasa yanatumika chini ya kiwango na hivyo kutowanufaisha wananchi kwa maana ya ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji, uagizaji na usambazaji wa mbegu bora. Serikali ilitunga sheria inayoitwa *Protection of New Plant Varieties* (*Plant Breeders Rights) Act, 2002,* inayotambua haki miliki za wazalishaji wa mbegu na mimea mipya na itakayokidhi mabadiliko ya kijamii na kiuchumi kulingana na soko huria la uzalishaji na usambazaji wa mbegu nchini. Haki hizo zinawawezesha wazalishaji wa mimea na mbegu mpya kunufaika na utafiti wao kutokana na malipo watakayopata kwa kutoa leseni au kuruhusu mbegu zao zitumiwe na wazalishaji wengine kwa ajili ya biashara (*seed multiplication*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi mwaka 2011 kuna jumla ya makampuni 53 ambayo yamesajiliwa kisheria nchini. Aidha, mwaka 2006, Serikali ilianzisha Wakala

wa Mbegu za Kilimo (*Agricultural Seed Agency*) kwa lengo la kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbegu zilizozalishwa na taasisi za Serikali za utafiti zitalindwa chini ya Sheria hii na kuiwezesha Serikali kupata mapato kutoka kwa wazalishaji wa kibiashara watakaoomba na kupewa leseni za kuzalisha au kuuza mbegu na mimea mipya iliyogunduliwa na watafiti wa Serikali. Aidha, kwa kutumia njia ya kuwasajili wazalishaji wa mbegu na mimea mipya, Serikali itaweza kudhibiti ubora wa mbegu mpya, ikiwa ni pamoja na kuwadhibiti wazalishaji holela.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya mbegu bora yamefikia tani 120,000 kwa mwaka iwapo kila mkulima atatumia mbegu bora. Hata hivyo, upatikanaji umeongezeka kutoka tani 6,781 mwaka 1980 hadi tani 17,000 mwaka 2011. Lengo la Serikali ni kuongeza upatikanaji pamoja na matumizi ya mbegu bora ili yafikie tani 60,000 za mazao ya nafaka, mikunde na mbegu za mafuta ifikapo mwaka 2015. Miaka ya 2000 hadi 2003 Mashamba ya mbegu ya Serikali yalichangia tani 594, sawa na asilimia nne, zikiwa ni mbegu za msingi. Chini ya utaratibu wa uzalishaji wa mbegu kwa kutumia wakulima wadogo, tani 553 zilizalishwa. Makampuni ya mbegu yaliingiza nchini tani 10,878 za mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa katika Maonyesho ya Kilimo Nane Nane 2010 hapa Dodoma alisema:

“Tumekuwa tukiagiza mbegu kwa asilimia 75 kutoka nchi za nje, lakini hazitufai kutokana na aina ya mbegu hizo na mazingira yetu, mbegu inatakiwa ifanyiwe utafiti katika eneo husika inapopandwa.”

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na takwimu tajwa hapo juu za mahitaji ya mbegu na asilimia ya mchango wa makampuni ya nje, ni dhahiri kuwa kama nchi kilimo chetu kiko mashakani, haiwezekani kwa nchi ambayo zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wake wanapata riziki zao kutokana na sekta hiyo na pale pale aslimia 75 ya mbegu zinazotegemewa kwa mazao ya chakula zinatoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ubinafsishaji na ufilisikaji kwa Kampuni ya Mbegu Tanzania *(TANSEED)*, mfumo wa uzalishaji na usambazaji wa mbegu nchini, nao ulisambaratika sambamba na kampuni hiyo ya Mbegu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili ni mkakati gani mahususi wa kuyafufua mashamba yote yaliyokuwa yanazalisha mbegu hapa nchini. Kwani kama hatutaweza kuwa na uwezo wa kutosheleza mahitaji ya mbegu bora kwa wakulima wetu ni dhahiri. Kauli mbiu ya Kilimo Kwanza haitakuwa na maana kwa maendeleo ya wakulima wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi za Mazao ya Biashara na maendeleo ya kilimo. Kilimo cha mazao ya biashara hapa nchini kwa sasa kina changamoto nyingi. Changamoto hizo ni pamoja na kukosa soko na bei za uhakika za mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya kuwa na Bodi hizi za Mazao ilikuwa ni kuwasaidia wakulima kupata masoko na bei nzuri kwa mazao yao. lla cha kusikitisha Bodi hizi badala ya kupigania haki za wakulima, zimekuwa zikijali maslahi ya wajumbe wake huku wakulima wakiachwa bila msaada wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuonesha jinsi Bodi za Mazao haziwatendei haki wakulima wa nchi hii, naomba kunukuu sehemu ya hotuba ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni aliyoitoa hapa Bungeni mapema tarehe 25/06/2012. Nanukuuu:

"Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa tuliyonayo ni kwamba, mfumo wetu wa kilimo cha mazao ya biashara kimehodhiwa na Bodi za Mazao ambazo kazi yake kubwa ni kunyonya *(extractive behaviour)* wakulima badala ya kuwaendeleza. Bodi za Mazao yote hapa nchini kama zilivyoundwa baada ya kuvunja Mamlaka za Mazao zimeonesha kushindwa kabisa kusimamia mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima ndio anaathirika na Bodi za Mazao kutokana na maamuzi yao ambayo hayazingatii haki za wakulima na bodi hizi kuongozwa kisiasa zaidi na makada wa CCM wakiwemo Wabunge kuliko utaalam. Ni hakika basi kuwa Chama cha Mapinduzi hakiwezi kukwepa lawama ya kilio cha wakulima, nchi hii kwa kushindwa kuongoza Bodi hizi na kuzigeuza vitega uchumi". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Korosho na matumizi mabaya ya fedha za wakulima. Kwa kukazia hoja ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba nitoe mfano wa Bodi ya Korosho jinsi inavyowanyonya wakulima wa korosho katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani na Ruvuma kwa kujilipa posho nyingi na marupurupu mengine huku wakiwaacha wakulima wa korosho wakiteseka na kuhangaika huku na huko kama kondoo wasio na mchungaji bila kutatua matatizo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ilipokea kiasi cha shilingi bilioni mbili kati ya mwezi Oktoba, 2011 na Januari, 2012 kutokana na ushuru wa mazao ya nje *(Export levy*) ya korosho kwa msimu wa 2010/2011. Kiasi hicho kilikuwa ni kwa ajili ya shughuli za kuendeleza tasnia ya korosho nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa fedha hizo hazikutumika kufanya shughuli kama ilivyotarajiwa na badala yake zilitumika kugharamia vikao vya Bodi ya Wakurugenzi na safari za viongozi (*management* ya bodi) ambazo hazijaleta tija kwa tasnia nzima kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yanapata ushahidi kutokana na matumizi ya kulipa posho kwa wajumbe wa Bodi wanaounda Kamati ya Ajira na uwekezaji ambayo wajumbe wake ni wanne, lakini aliwekwa na mke wa mjumbe katika malipo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kikao cha siku moja kilichofanyika tarehe 29/11/2011 wajumbe wa Bodi hiyo walilipwa posho kama ifuatavyo:-

(1) Mheshimiwa J. Bwanausi, Mjumbe wa Bodi, huyu alilipwa jumla ya sh. 1,550,000/=, ikiwa sh. 750,000/= ni posho ya kawaida *(per diem)* na sh. 800,000 ni *working session* kama ilivyoandikwa kwenye fomu ya malipo.

(2) Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, huyu alilipwa jumla ya sh. 1,800,000/= kwa mchanganuo ufuatao: Posho ya kikao sh. 500,000/=, usafiri sh. 300,000/=, posho ya kawaida *(per diem)* sh. 900,000/= na usafiri Dar es Salaam sh. 100,000/=.

(3) Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, huyu alilipwa kwa mara nyingine tena kwenye kikao hicho hicho, jumla ya sh. 1,550,000/= ikiwa posho ya kikao ni sh. 400,000/=, Usafiri wa Ndege sh. 300,000/=, posho ya kawaida *(per diem)* sh. 750,000/= na usafiri Dar es Salaam sh. 100,000/=.

(4) Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi, huyu alilipwa jumla ya sh. 1,550,000/=, ikiwa posho ya kikao ni sh. 400,000/=, usafiri wa ndege sh. 300,000/=, posho ya kawaida *(per diem)* sh. 750,000/=, usafiri wa kuja Dar es Salaam sh. 100,000/=.

(5) Mrs. Mudhihir M. Mudhihir, mke wa Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, huyu alilipwa jumla

ya sh. 875,000/= kwa mchanganuo ufuatao: Posho ya kikao sh. 200,000/=, usafiri sh. 300,000/=, posho ya kawaida *(per diem)* sh. 375,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya fedha zote zilizolipwa (kwa watu watano) katika kikao hiki cha Wakurugenzi wa Bodi ya Korosho cha tarehe 29/11/2011 ni sh. 7,325,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya matumizi ya fedha hizi kuwa hayana tija kwa kuwa matatizo ya wakulima wa korosho hayajapatiwa ufumbuzi hadi sasa, utaratibu walioutumia wajumbe hawa kujipatia fedha hizi una dalili za kifisadi ndani yake. Hii ni kwa sababu mke wa Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir ambaye si mjumbe wa kikao aliingia kwenye kikao na kulipwa posho. Utaratibu uliotumika kumlipa mke wa Mudhihir haueleweki na hata viwango vilivyotumika kukokotoa malipo yake pia havifahamiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, dalili ya ufisadi mwingine katika Bodi hii, ni kwa Mjumbe wa Bodi Mheshimiwa Jerome Bwanausi kulipwa posho hiyo mara mbili. Katika fomu za malipo kwa Mheshimiwa Bwanausi, fomu moja ameandika jina lake kwa kifupi yaani J. Bwanausi na tarehe ya kuchukua fedha ameandika ni tarehe 28/11/2011, wakati katika fomu ya pili ya malipo ameandika jina kamili yaani Jerome Bwanausi na tarehe ya kuchukua fedha kaandika 29/11/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira kama hayo, yanaibua hisia kuwa Mheshimiwa Bwanausi alijipatia fedha hizo kwa njia ya udanganyifu na hivyo

kuwaaminisha watu kuwa alitumia nafasi yake kama mjumbe wa Bodi ya Korosho kuchukua fedha za wakulima wanyonge wa korosho. Kambi ya Upinzani, tunaitaka Serikali kutoa majibu juu ya Bodi hizi za mazao na utaratibu wa kulipana posho ukoje? Aidha, tunamtaka Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali kufanya ukaguzi maalum *(special audit)* kwenye matumizi ya Bodi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bodi ya Pamba na mgogoro wa kilimo cha mkataba na bei ya pamba nchini. kwa mujibu wa Sheria ya Pamba namba mbili (2) ya mwaka 2001, majukumu ya Bodi ya Pamba ni pamoja na kukuza na kuendeleza sekta ya pamba kwa kujenga mazingira ya ushindani wa haki, kuongeza uzalishaji na uchambuaji wa pamba pamoja na kuboresha masoko ya pamba na kusimamia na kudhibiti ununuzi wa pamba, mbegu na nyuzi kuanzia ngazi ya gulio, kiwandani na masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali mbaya inayokikumba kilimo cha pamba na biashara ya pamba kwa sasa, ni dhahiri kwamba Bodi ya Pamba imeshindwa kutekeleza majukumu yake ya kisheria kama nilivyoyataja hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa hivi kuna mgogoro mkubwa na malalamiko makubwa miongoni mwa wakulima wa pamba kutokana na bei ya pamba kushuka sana, lakini pia kuna hali ya sintofahamu juu ya kilimo cha pamba kwa mkataba kwa wakulima wa pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni kulikuwa na hisia kuwa kilimo cha pamba cha mkataba kingekuwa mkombozi kwa mkulima wa pamba. Lakini kwa hali inayoendelea ni kwamba kilimo cha mkataba sasa kimekuwa mwiba na kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya kilimo cha pamba nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa nadharia ya kilimo cha mkataba ni kwamba, mkataba unafanyika baina ya mkulima na mnunuzi na kwamba bei hupangwa kwa makubaliano kabla ya uzalishaji kufanyika. Tofauti na mwongozo huu wa kinadharia ni kwamba kinachofanyika sasa hivi kwenye kilimo cha pamba ni kwamba makampuni ya kibiashara ndiyo yanapanga bei tena baada ya pamba kuvunwa na bila makubaliano na mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wakulima wa pamba wana chombo cha uwakilishi yaani Bodi ya Pamba ilitakiwa mkataba ufanyike baina ya makampuni hayo na bodi kwa niaba ya wakulima. Tofauti na hivyo Makampuni hayo yanaingia mkataba na wakulima moja kwa moja na wakulima ambao hawana uelewa wa sheria za mikataba na hivyo kuwalaghai na kuwanyonya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni kwamba, wakulima hawa wanasainishwa fomu kuwa tayari, wamepokea pembejeo ambapo wakati mwingine pembejeo hizo haziletwi kwa idadi ambayo imesainiwa kwenye fomu. Vile vile mkulima hajui gharama ya pembejeo na hivyo kutojua kama anapata faida au anapunjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine pembejeo nyingine kama dawa na mbolea huwa zimechakachuliwa na hivyo kutofanya kazi. Pia mkulima analazimishwa kumuuzia mnunuzi kwa mkataba, hata kama kuna makampuni mengine au viwanda vyenye bei nzuri. Mkulima pia hana hiari ya kutouza pamba yake kusubiri bei nzuri ingawa mnunuzi anaweza kuwasubirisha wakulima bila kununua pamba yao akisubiri bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna malalamiko pia kwamba Bodi ya Pamba ambayo ina mamlaka kisheria kusimamia kilimo na biashara ya pamba inafanya biashara kwa kuwauzia wakulima mbegu kupitia makampuni ya biashara. Bodi hii inalalamikiwa pia kuwa imeyaacha huru makampuni haya kwenda kuwalaghai wakulima juu ya kilimo cha mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili limejidhihirisha pale ambapo makampuni haya ya biashara yalipowauzia wakulima mbegu zilizoharibika ambazo hazikuota, madawa na mbolea zilizochakachuliwa na Bodi kukaa kimya bila kuyachukulia makampuni haya hatua yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yote haya yenye utata yanatoa picha kwamba Bodi ya Pamba inahusika kwa kiwango kikubwa na mgogoro wa biashara ya pamba kwa sasa. Kwa sababu hiyo, Kambi ya Upinzani inataka kujua Serikali inachukua hatua gani dhidi ya Bodi ya Pamba ambayo imewageuka wakulima wa pamba kwa maslahi yake binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka Serikali ya CCM ielewe kwamba kuongoza dola ni pamoja na kuwa na uwezo kuingilia kati migogoro ya kiuchumi kama huu unaowakabili wakulima wa pamba sasa hivi na kuupatia ufumbuzi. Kitendo cha Serikali kukaa kimya na kuwaacha wakulima hawa wakiteseka na kutojua cha kufanya ni udhalimu mkubwa dhidi ya juhudi za wakulima katika kuujenga uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kushindwa kusimamia kilimo ambacho kinaajiri asilimia 80% ya Watanzania wakiwemo wakulima wa pamba, ni kukosa sifa kabisa ya kuongoza dola. Hii ni kwa sababu msingi wa dola ni watu na kama watu hawa wanapuuzwa na Serikali basi moja kwa moja Serikali inakosa sifa ya kuwaongoza watu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo ya utata wa kilimo cha pamba cha mkataba na imechukua hatua gani hadi sasa kutatua mgogoro wa bei ya pamba ambayo ni kikwazo kikubwa kwa wakulima wa pamba kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tunataka kujua zimechukuliwa hatua gani kuhusiana na kupatikana kwa wanunuzi wa pamba ambao pamoja na bei kuwa ndogo baadhi ya maeneo hakuna wanunuzi mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bodi ya Kahawa na kuzorota kwa kilimo cha kahawa nchini; kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka

2011 ni kwamba uzalishaji wa zao la kahawa ulipungua kutoka tani 60,575 mwaka 2010 hadi tani 32,304 mwaka 2011, sawa na upungufu wa asilimia 88. Sababu zilizotolewa kwa kushuka kwa uzalishaji ni pamoja na kupungua kwa mvua za vuli katika Mikoa ya Kagera na Mbeya na matumizi duni ya pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika kama Tume ya Mipango hutembelea mikoa husika na kubaini sababu mahsusi za kushuka kwa uzalishaji wa zao la kahawa. Hii ni kwa sababu, inatoa sababu za jumla mno kiasi cha kushindwa kujua kiini cha tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sababu za Tume ya Mipango, ni kwamba uzalishaji wa kahawa umepungua kwa sababu baadhi ya wakulima wamejitoa kwenye kilimo cha kahawa. Ukweli ni kwamba wakulima wengi wa kahawa katika Jimbo la Vunjo na hasa katika eneo la Kilema, Mkoani Kilimanjaro ambapo ndipo kilimo cha kahawa nchini kilipoanza, wamekatishwa tamaa ya kuendelea na uzalishaji baada ya Vyama vya Ushirika na vya Msingi kufilisiwa na hivyo kushindwa kuwapatia pembejeo na pia kushindwa kununua kahawa ya wakulima kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hii wakulima hasa katika vijiji vya Kilema Pofo na Masaera katika jimbo la vunjo wameng'oa miti ya kahawa na badala yake wameanza kilimo cha nyanya, kabichi, hoho na matango ambapo kwa maoni yao kina tija zaidi kuliko kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wananchi wengi wa Mkoa wa Kilimanjaro wamejikita zaidi kwenye kilimo cha ndizi na hivyo kupunguza kasi ya kilimo cha kahawa. Tatizo hili linaweza kuwa ni kubwa kwa maeneo mengine yanayolima kahawa nchini kama Mkoa wa Kagera. Kama Serikali itaendelea kutokuwa makini na zao la kahawa kama ilivyo sasa, kuna hatari kubwa ya zao la kahawa kuondoka kwenye safu ya mazao ya biashara yanayoliingizia Taifa hili fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inataka Serikali kutoa maelezo katika Bunge hili, kuwa Bodi ya Kahawa imechukua hatua gani katika kuhakikisha kilimo cha kahawa kinafufuliwa hapa nchini ambacho kwa sasa kimezorota?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa tamko sasa kama kuna haja ya kuendelea kuwa na Bodi hizi za Mazao wakati zimeshindwa kutatua matatizo ya wakulima. Pili, Serikali inatoa kauli gani kuhusu matumizi ya kifujaji yanayofanyika katika Bodi hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Utafiti vya Kilimo; utafiti wa kilimo ndio msingi wa mapinduzi ya kilimo endelevu chenye tija kwa mkulima na kwa Taifa. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuviendeleza Vituo vya Utafiti wa Kilimo kwa kuvipatia fedha na vifaa ili viweze kukamilisha tafiti za kilimo kwa maendeleo ya kilimo chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema hivi kwa sababu baadhi ya Vituo vya Utafiti viko katika hali mbaya kwa sababu ya kukosa fedha za kuendeshea tafiti na kuwalipa watumishi. Kwa mfano, Kituo cha Utafiti cha Mikocheni, Dar es Salaam hakikupatiwa fedha kilizoomba katika bajeti ya 2011/2012 kwa ajili ya utafiti wa minazi, huku wafanyakazi wakilalamikia maslahi duni na magari chakavu. Aidha, kituo hiki kimekuwa hakifanyi kazi *(dormant)* kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashangazwa na uwepo wa kituo hiki na Serikali inaendelea kuwalipa watumishi wakati haipeleki fedha za maendeleo na hivyo kufanya kituo hiki kushindwa kufanya kazi. Hali kama hii imesababisha kilimo cha minazi kufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza Bunge hili, inawalipa watumishi wa kituo hiki kwa kazi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza hali ya maendeleo ya Vituo vingine vya Utafiti wa Kilimo nchini na mikakati ya kuviboresha ili kuleta mapinduzi ya kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo cha umwagiliaji; mwaka 2010 Serikali ilijiwekea lengo la kufikia hekta milioni moja za eneo la umwagiliaji kufikia mwaka 2015, mpaka kufikia Julai mwaka 2011, jumla ya hekta 345,690 zilikuwa zimekamilika na Serikali ikajiwekea lengo la kuongeza hekta 40,000 ili kufikia hekta 385,690 kufikia mwaka 2012. Mpaka sasa jumla

ya hekta 17,824 zinatarajiwa kukamilika ikiwa ni tofauti ya hekta 22,176 ya lengo la Serikali lililoombewa fedha mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kasi ndogo ya ukamilishaji wa skimu mbalimbali za umwagiliaji ni dhahiri kuwa lengo la Serikali la kufikia hekta milioni 1,000 ,000 ifikapo mwaka 2015 ni ndoto. Aidha, Kambi ya Upinzani inapenda kuishauri Serikali yafuatayo:-

(1) Juhudi kubwa za Serikali sasa zihamishiwe kwenye kilimo cha umwagiliaji, kwani pamoja na kutolewa kwa pembejeo na zana ni dhahiri kuwa bila juhudi hizo kuhamishwa katika kilimo cha umwagiliaji mapinduzi ya kijani hayataweza kutokea;

(2) Serikali itoe mikopo kwa sekta (wakulima) binafsi kwa ajili ya kutafuta vyanzo vya maji, kuchimba visima, kuvuna maji ya mvua na kujenga mabwawa na malambo; na

(3) Juhudi kubwa ziongezwe katika kutafuta vyanzo vipya vya maji ili kufanikisha kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa Miradi ya *DASIP*; bado miradi kadhaa inayotekelezwa chini ya *District Agricultural Sector Investment Program (DASIP)* haijatekelezwa wakati Programu hii inatarajia kumaliza muda wake mwaka huu 2012. Hii ina maana kwamba, kuna uwezekano mkubwa kabisa wa fedha za mradi kurudishwa na hivyo kutowanufaisha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa zilizopo ni kwamba, kukwama kwa utekelezaji huu wa mradi kunatokana na kiburi cha Afisa wa Kitengo cha Manunuzi katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Ndugu Burhani Shabani. Afisa huyu ni mng'ang'anizi wa madaraka na hivyo akitoka ofisini anafunga shughuli zote za kimaamuzi hadi yeye mwenyewe awepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukiritimba kiutendaji, kati ya miradi 20 ya umwagiliaji ya *DASIP* Kanda ya Ziwa ni miradi mitatu tu iliyotekelezwa hadi sasa. Miradi ya Masoko Mkakati yaliyokuwa yajengwe katika Wilaya za Tarime, Karagwe na Kasulu hayajajengwa hadi sasa. Pikipiki za mradi zilizokuwa zigawiwe kwa wadau wa kilimo Kanda ya Ziwa hazijagawiwa hadi sasa. *Power Tillers* za mradi Mwanza hazijigawiwa hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge kwa nini miradi hiyo imeshindwa kutekelezwa hadi programu hii inakaribia kumalizika?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu migogoro katika Sekta ya Kilimo; tumeshuhudia migogoro mingi katika maeneo mengi nchini baina ya makundi mbalimbali inayohusiana moja kwa moja na shughuli za kilimo. Migogoro hiyo ni kama ifuatavyo:-

Migogoro kati ya wakulima na wafugaji; migogoro ya aina hii imetokea katika maeneo kama Kilosa, Kilombero, Ikwiriri, Kiteto, Kagera na migogoro hii

pamoja na sababu nyingine nyingi kwa kiasi kikubwa inasababishwa na sababu hizi:-

(a) Serikali kushindwa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya kilimo na ufugaji;

(b) Serikali kutokufanya maandalizi ya kutosha kabla ya kuwahamisha wafugaji kwenda katika maeneo yaliyotengwa ikiwemo miundombinu kwa ajili ya ufugaji kama vile majosho na malambo; na

(c) Utendaji mbovu wa watendaji wa Serikali wakiwemo Watendaji wa Vijiji na Kata na Polisi kwa upande mwingine. Watendaji hawa wamekuwa wakipokea rushwa na hivyo kupendelea upande mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na migogoro iliyokithiri kati ya wakulima na wafugaji, Kambi ya Upinzani inajiuliza, hivi mbona tumeweza kutenga maeneo kwa ajili ya wanyamapori, tunashindwa nini kuwatengea maeneo wakulima na wafugaji wetu? Tunapenda kutoa ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

(a) Kutengwa maeneo maalum kwa ajili ya wakulima na wafugaji yanayokidhi mahitaji ya makundi hayo. Aidha, maeneo ya wafugaji yawe na miundombinu muhimu kama majosho, malambo ya maji, maeneo yenye malisho na yasiyo kuwa na wadudu au wanyama hatari kwa mifugo; na

(b) Serikali iwawajibishe viongozi wabovu na wakulima au wafugaji wanaokiuka sheria baada ya kutengewa maeneo.

Migogoro baina ya wawekezaji na wananchi; mgogoro huu kati ya wananchi na wawekezaji katika masuala ya ardhi na kilimo umetokea mara kwa mara tangu nchi yetu ilipopata uhuru. Migogoro hii ni kama ile iliyotokea Kiru, Mbarali, Arumeru na kadhalika. Pamoja na sababu nyingine zinazosababisha migogoro hii ni pamoja na:-

(a) Mikataba mibovu kati ya Wawekezaji na Serikali bila ya kuwashirikisha wananchi wanaoendesha shughuli zao katika maeneo wanayopewa wawekezaji;

(b) Wawekezaji kuhodhi ardhi bila kuiendeleza na hivyo kuwashawishi wananchi kuvamia kwa nia ya kutaka kufanya shughuli zao ili kukidhi mahitaji yao;

(c) Uwekezaji katika kilimo kutowanufaisha wananchi wanaozunguka eneo husika kama kuwapatia huduma za kijamii kama vile maji, shule, zahanati, barabara na ajira kwa wazawa; na

(d) Sera au mkataba isiyo wazi kwa pande zote juu ya umiliki wa maeneo husika. Hivyo, kila upande kudai na kuamini kuwa eneo linalobishaniwa ni la kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na migogoro hii ya wakulima na wawekezaji kambi ya upinzani inapendekeza yafuatayo:-

(a) Kuwepo na ushirikishwaji mkubwa wa wananchi katika makubaliano na mikataba inayofanywa kati ya wawekezaji na Serikali;

(b) Serikali itoe fidia ya ardhi yenye thamani sawa na ardhi anayohamishwa mwananchi, fidia ya mali inayopotea na usumbufu unaotokea kutokana na uwekezaji utakaofanywa;

(c) Uwekezaji uwe ni wa kuwanufaisha wananchi kwa kutoa huduma kwa wananchi kama vile kujenga shule, barabara, zahanati, maji na kutoa ajira kwa wananchi;

(d) Misamaha ya kodi kwa wawekezaji iondolewe ili kuongeza pato la Taifa na Halmashauri husika; na

(e) Wawekezaji wanaoshindwa kuendeleza ardhi wanyang'anywe na kurudishiwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya Msingi na Ushirika viliwasaidia sana wakulima hasa wa mazao ya biashara katika kuwapatia wakulima pembejeo na masoko kwa mazao yao. Hata hivyo, Vyama vya Msingi na Uushirika kwa ajili ya biashara ya mazao ya kilimo umedhoofika sana hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa utafiti wa Profesa Sam Maghimbi (kwa sasa ni Mkuu wa Kitivo cha Humania na Sayansi za Jamii katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam *(DUCE)* wa mwaka

2010, juu ya Vyama vya Ushirika, ni kwamba Vyama vya Ushirika vimefilisika kutokana na madeni mengi na kwamba ni vyama viwili tu vya Kagera *Cooperative Union (KCU)* na Karagwe *District Cooperative Union (KDC)* vyenye afadhali kwa kuwa na fedha kidogo za kununua mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyama hivi vimefilisika na vingine vimeanza mchakato wa kuuza majengo yake ili kulipa madeni. Kwa mfano, Kilimanjaro *National Cooperative Union (KNCU)* kimeanza mchakato wa kuuza majengo yake ili kukinusuru Kiwanda cha Kukoboa Kahawa *(TCCCO)* kinachodaiwa zaidi ya shilingi milioni 757 (hii ni kwa mujibu wa gazeti la Mwananchi la 8/7/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani haioni kama kuuza majengo ya chama hicho ni suluhisho la kudumu la madeni ya chama hicho na badala yake ni hatua ya kukiua kabisa chama hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa tamko katika Bunge hili kuwa ina mkakati gani juu ya kuvifufua Vyama vya Ushirika vya Msingi vya mazao ya biashara ambapo miaka ya nyuma ndivyo vilivyokuwa mtetezi na msaidizi wa haraka kutatua matatizo ya wakulima?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua, ni nini mchango wa taaluma ya Ushirika inayotolewa na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara *(MUCCOBS)* hapa nchini ikiwa ushirika hasa katika mazao ya biashara unazidi kudimia?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenendo wa Kibajeti Katika Wizara; kwa mujibu wa utafiti wa Daktari Damian M. Gabagambi (2011) ambaye ni Mtafiti na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Morogoro, kuhusu Mgawanyo wa Kibajeti katika Sekta ya Kilimo nchini ni kwamba kwa ujumla bajeti ya matumizi ya kawaida katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imekuwa inaongezeka wakati bajeti ya maendeleo katika Wizara hii imekuwa ikipungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa utafiti huu, mwenendo huo sio mzuri kwa kuwa unakwenda kinyume na ari ya kuendeleza kilimo. Hata hivyo, pamoja na fedha za maendeleo kupungua, asilimia 90 ya bajeti ya maendeleo ni fedha za nje kwa maana ya mikopo na misaada. Hii ina maana kwamba Serikali hutumia fedha kidogo sana kutoka mapato yake ya ndani katika sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwenendo huu, ni dhahiri kwamba ni vigumu kufanya maboresho endelevu katika Sekta ya Kilimo. Vile vile ni ishara ya wazi kuwa Serikali haijaweka kipaumbele katika Sekta ya Kilimo ambacho zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania wanakitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa taarifa katika Bunge hili kwamba ina mpango gani na Kilimo cha Tanzania? Pili, endapo fedha za wahisani hazitakuwepo, Serikali ina mikakati gani ya kuendeleza Kilimo nchini kwa kutumia fedha zake za ndani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kuwa nchi yetu haiwezi kupata maendeleo endelevu bila ya kilimo. Kuna umuhimu sasa kilimo kupewa kipaumbele si tu kwa nadharia, kama ilivyo sasa bali kwa vitendo na uwajibikaji. Pamoja na umuhimu wa zana na pembejeo za kilimo katika maendeleo ya kilimo, nguvu zaidi inatakiwa ielekezwe kwenye upatikanaji wa maji ya kutosha ili kuongeza kasi ya kilimo cha umwagiliaji ambacho hakiathiriwi sana na msimu au mabadiliko ya hali ya hewa. Kwa kufanya hivyo, Taifa litajihakikishia usalama wa chakula na pia litajipatia fedha za kigeni kwa kuuza ziada ya mavuno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana na naomba nikushukuru sana Mheshimiwa Rose Kamili Sukum, tunakushukuru sana kwa hotuba yako. Kwa dakika chache zilizobaki Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani kama unaweza kuzitumia, Mheshimiwa Kabwe Zitto.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika Wizara ya Kilimo, sikuwa nimepanga kuchangia Wizara hii, lakini kuna baadhi ya vitu vimenisukuma kidogo kuomba kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni suala la ubinafshaji. Katika ukurasa wa 72 na 73 wa hotuba Waziri wa Kilimo amezungumzia viwanda vilivyobinafsishwa na kushindwa kufanya kazi, Viwanda

vya Korosho anasema: “Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na *CHC* kuhakikisha kwamba viwanda hivyo vilivyobinafsishwa na kushindwa kazi vinaendeshwa kulingana na masharti ya ubinafsishaji” na kabla ya hapo anasema kwamba ‘’taarifa ya tathimini hiyo inaonesha kuwa baadhi ya viwanda hivyo haviendeshwi kulingana na masharti ya ubinafsishaji.”

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ambavyo haviendeshwi kulingana na masharti ya ubinafsishaji, vimevunja mikataba havipaswi kubembelezwa, vinapaswa kurejeshwa. Jambo hili siyo jipya kwa sababu tayari Kamati ya Mashirika ya Umma katika taarifa yake ya mwaka huu, ilileta mapendekezo na yakapitishwa Bungeni, Viwanda 10 vya Korosho vilivyobinafsishwa na havifanyi kazi hivi sasa, Serikali ivifanyie *repossession* na tuangalie utaratibu upya wa kuweza kuwasaidia wakulima wa korosho kuongeza thamani kwenye mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapeleka nje zaidi ya 80%, Kamati ya Bunge imesema 75%, zaidi ya 80% ya korosho yetu kama ghafi. Maana yake ni kwamba, tunapeleka ajira za watu wetu India badala ya kusaidia wakulima wetu wa korosho wakaongeza thamani ya mazao yao na kuhakikisha kwamba tunabakiza ajira hapa nchini. Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hilo kwamba tayari Bunge limeshaelekeza viwanda hivi kuwa walioshindwa wanyag’anywe, hatutaki kuona tunabembeleza watu ambao wamepewa mali ya umma na kushindwa kuiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Waziri amezungumzia kupewa kwa kinu cha NMC cha Iringa na Mwanza kwa Bodi ya Mazao Mchanganyiko, Waziri hajazungumzia kabisa kinu cha Arusha na baadhi ya mali ambazo zipo hapa Dodoma zilizokuwa za *NMC* na tunafahamu kwamba kwa muda mrefu sana *NMC* imekuwa ikiendeshwa na mtu mmoja haina Bodi, haina utaratibu wala haina mahesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo hayo yamegundulika baada ya suala la kiwanja namba 10 pale *Pugu Road* kugundulika, kwa hiyo, naomba Waziri na Wizara waliangalie jambo hili kwa umakini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine linalonifanya nichangie ni kwamba, nimeshtushwa sana kuona namna ambavyo sasa hivi tunapigia debe *GMO* na Serikali kwa kuzungumza bila uwoga, nchi hii sasa bila aibu tunapigia debe *GMO*. *GMO* zinaturudisha kwenye ukoloni, *GMO* zitafanya nchi yetu iwe tegemezi, hatupingi maendeleo ya sayansi, hatupingi maendeleo ya utafiti, tunapinga kuifanya nchi yetu na wakulima wetu kila mwaka kutegemea mbegu kutoka kwenye makampuni ya mbegu ya Marekani na Ulaya (*Monsanto*). Nimeona hapa namna ambavyo *Monsanto* inashiriki katika kila hatua ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu kama tumefikia hatua ya kukubali *GMO* tunakwenda na kutengeneza *dependency,* hatuna uwezo wa kuzalisha mbegu kama ambavyo makampuni makubwa ya Kimataifa yanazalisha mbegu, maana yake ni kwamba mkulima wetu badala ya kumjengea uwezo na

kuimarisha mbegu zetu za asili, kumfanya akilima aweke kwenye kichanja na mwakani aweze kupanda tena, hivi sasa tunafanya kwamba mbegu ziwe zinanunuliwa dukani na hawa watu wakishindwa ku-*supply* mbegu ipasavyo nchi yetu itaingia kwenye matatizo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutangaza binafsi kuwa siungi mkono *GMO*, napinga *GMO*. *GMO* ni *Neo Colonialism* (Ukoloni mambo leo) *GMO* ni kuirudisha nchi yetu kwenye makucha ya mabeberu na ningependa Mtanzania yeyote aliyesomeshwa na fedha za nchi, aliyefaidika na Ujamaa na Azimio la Arusha apinge *GMO* na naomba kurasa zote katika hotuba ya Waziri zinazohusiana na *GMO* ziondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, naomba tuangalie namna ya kufanya kutokana na matatizo yanayotokea kwenye pamba, korosho na kahawa kuhusiana na bei tuanzishe *stabilization fund* ambayo itakuwa ina-*regulate* bei hizi. Lakini katika hili naomba nisisitize sana, Waziri amezungumzia suala la *commodity exchange*. Napenda kuipongeza Wizara na Serikali, *commodity exchange* ndiyo *solution* ya masuala yote ya bei na wenzetu Ethiopia wamepiga hatua kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichonisikitisha katika hotuba ya Waziri ni pale ambapo anasema, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara bado inaendelea kujadiliana ili kuweza kuona namna ya kuanzisha *Commodity Exchange*. *Commodity Exchange* inatakiwa kuanzishwa sasa. Njia pekee ya

kwanza ni kuhakikisha tunaunda kama Dar es salaam *Stock Exchange (DSE)* tuwe na *CEO*, tuwe na Bodi, tukishapata Bodi na mtu ambaye kazi yake ni kusimamia hili suala hili litaweza kufanikiwa bila tatizo lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusirudi nyuma, wenzetu Ethiopia nchi ambayo ilikuwa inalia njaa miaka michache iliyopita, sasa hivi ndiyo imekuwa nchi ya mfano kwenye *Commodity Exchange.* Naomba jambo hili Serikali ilipe kipaumbele cha pekee katika ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliacha suala la Kapunga, tulitoa taarifa hapa Bungeni mwaka 2009 kwamba, Serikali iliuza shamba, ikauza na kijiji na wananchi wake wakati inauza shamba la mpunga la Kapunga. Tukatoa maelekezo kuwa zile hekari ambazo ziliuzwa na hazikupaswa kuuzwa wananchi warejeshewe, sijaona katika hotuba hii sehemu yoyote ambayo Waziri anazungumzia jambo hili. Pia liliulizwa swali Bungeni hapa na Mbunge wa Mbarali, Waziri akasema kwamba, atalifuatilia, hatujaona taarifa yoyote. Tunataka kufahamu wananchi wa Kapunga wataondokana na adha hii lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuzungumzia vitu viwili vya mwisho; kwanza, tumeambiwa hapa kwenye bajeti na kwenye Mpango wa Maendeleo na bahati nzuri Waziri wa Mipango na Uchumi Mheshimiwa Wasira yupo hapa, kwamba kuna miradi maalum ya kilimo cha mchele kwa maana ya

mpunga na miwa katika mabonde ya Kilombero na Malagarasi.

Nimesoma hii hotuba mwanzo mpaka mwisho, hakuna eneo hata moja linalotaja miradi hii maalum kwa ajili ya kutatua tatizo la sukari nchini na kwa ajili ya kutatua tatizo la mchele hapa nchini. Jamani, Mbunge aliyesoma na kuona hilo eneo anionyeshe. Hakuna hata eneo moja! Sasa hii miradi iko chini ya Wizara ya Mheshimiwa Wasira, iko chini ya Waziri wa Fedha au iko chini ya Wizara ya Kilimo, kwa sababu hakuna kwenye bajeti tulipoambiwa, kwenye Mpango wa Maendeleo hakuna tulipoambiwa, kwenye Wizara ya Kilimo miradi hiyo mikubwa haipo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni maombi; moja Bonde la Mto Riche, tunaomba mtusaidie bonde la Mto Riche liingie katika mpango maalum wa kuzalisha mpunga kwa ajili ya kutengeneza ajira kwa vijana wa Mji wa Kigoma. Juzi nilikwenda na vijana wasanii wa kizazi kipya Kigoma, tukawapeleka kule Kalinzi na Makyazo waweze kuona namna ambavyo kahawa inalimwa, kuvunwa na mpaka, kuandaliwa lakini tuna matatizo makubwa sana ya *CPU's*. Naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie *CPU* kama nne hivi kwa ajili ya kusaidia kuongeza ubora pale Kalinzi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi nikuombe suala letu tulifanye jioni, kwa sababu ya muda.

Naomba nitambue uwepo wa Walimu wa Kinondoni kama wamerudi mpo eh! Karibuni sana wallimu kutoka Kinondoni ambao ni wageni wa

Mheshimiwa Iddi Azzan. Nawahakikishia Mbunge wenu anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni na ni golikipa wetu katika *Bunge sports club* karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kipindi cha maswali nitumie kama nusu dakika kwa kifupi sana nifafanue kwa sababu sote tunajifunza ili tuweze kuelewana kidogo. Mheshimiwa Tundu Lissu alisimama kwa Kanuni ya 47 kwa kutaka Bunge liahirishe shughuli ili tujadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma. Ukifungua ile Kanuni ya 47 utaona ndiyo kanuni inayohusika, alipatia kwa kuipata Kanuni, lakini nasema hivi, baada ya muda wa maswali kwisha kitu ambacho baada ya maswali kwisha Mbunge yoyote anaweza kutoa hoja na hii siyo mara ya kwanza ndugu zangu tunafanya jambo hili.

Kama mtakumbuka wakati fulani Kanuni hii iliwahi kutumiwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe kwenye suala la Nishati na Madini na ikafanya kazi. Kwa sababu Mbunge akitaka kutumia Kanuni hii ni lazima asimame atoe hoja na akitoa hoja Kanuni hii inasema mimi nitaangalia, je inaungwa mkono na watu wanaozidi 10? Kwa hiyo, lazima uwe umefanya kazi yako ya *lobbying* kwanza kwa Wabunge wenzako ili utakapotoa hoja yako iungwe mkono, ukikaa uniachie mimi niweze kuwa na nafasi ya kuona tunafanyaje...

Inayofuata ni ile ya tatu ambayo aliishikilia sana, inaanza na neno hoja itatolewa ndiyo sentensi ya kwanza Hoja itatolewa na Mbunge kwa kusimama mahali pake inaendelea kusisitiza ile ya kwanza

kwamba utatoa hoja kwa kusimama mahali pako na kuomba idhini ya Spika kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge. Sasa yeye alishikilia idhini ya Spika ambayo ufafanuzi wa idhini ya Spika ipo ile ya nne hii inayofuata.

Iwapo Spika ataridhika kwamba jambo hilo ni la dharura halisi na lina maslahi kwa umma, basi ataruhusu hoja hiyo itolewe kwa muda usiozidi dakika tano na mjadala juu ya hoja hiyo utaendelea. Baada ya kuwa umetoa hoja na imeungwa mkono na Spika karidhika kuwa jambo hili kweli lina dharura, sasa anakuruhusu uitoe hoja yako kwa mapana kwa dakika tano. Baada ya hapo hoja ile inaendelea kuchangiwa na Wabunge kwa dakika ambazo zitakuwa zimewekwa kwa kadri atakavyokuwa ameona kuwa inafaa.

Huo ndio utaratibu wenyewe ndugu zangu, kwa hiyo, kukasirika na kuzira siyo mambo mazuri sana, kinachosaidia ni kuzielewa tu vizuri Kanuni na ukishazielewa vizuri jipange vizuri mapema. Wajulishe Wabunge wenzako mapema nia yako ni nini kwa sababu Bungeni hapa tunafanya kazi kwa *lobbying* wakiku-*support* wenzio hapa mimi siwezi kuzuia jambo ambalo nyie Wabunge mnataka kufanya. Waheshimiwa Wabunge, mkiazimia kufanya jambo fulani, kwangu ni vigumu kulizuia, siyo rahisi hata kidogo.

Baada ya maelezo hayo, niseme tu kuwa, jioni wachangiaji wetu wa mwanzo watakuwa ni

Mheshimiwa Lembeli, Mheshimiwa Kafulila na Mheshimiwa Chibulunje na wengine watafuata.

Baada ya kusema hayo, naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja leo jioni na hapa mezani atakuwepo Mheshimiwa Zungu.

(Saa 7.06 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa Zungu Azzan) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae. Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU-SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya Kifungu cha 150(1) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kutoa hoja ya kutengua Kanuni za Bunge kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, Mkutano wa Nane wa Bunge wa kushughulikia Bajeti ya Serikali pamoja na shughuli zingine za Bunge zilizopangwa, umepangwa kumalizika tarehe 18 Agosti,2012;

Na kwa kuwa, ratiba ya shughuli zote zilizopangwa kufanyika katika Mkutano huu wa Nane zimepangwa kwa kuzingatia Kanuni ya 99(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007;

Na kwa kuwa, tarehe 18 Julai, 2012 Taifa letu lilipata msiba mzito uliotokana na kupinduka na kuzama kwa meli ya *abiria* ya *MV. Skagit* katika eneo la Chumbe Zanzibar, hivyo Bunge kulazimika kusitisha shughuli zake tarehe 19 Julai, 2012.

Katika kikao cha Kamati ya Uongozi ya Bunge kilichofanyika katika Ukumbi wa Spika, tarehe 19 Mwezi Julai, Wajumbe wote wa Kamati hiyo waliohudhuria waliazimia kuliomba Bunge likubali kufanya kazi siku za Jumamosi za tarehe 21 Mwezi wa Saba, tarehe 28 Mwezi wa Saba na tarehe 18 Mwezi wa Nane, ili kuwezesha Bunge kufanya kazi zake zilizopangwa kwa ufanisi na kumalizika katika muda uliopangwa ikiwa ni pamoja na kupitisha bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya mwaka 2012/2013, iliyoondolewa siku ya tarehe 18 Mwezi wa Saba kufuatia msiba huo uliotokea Zanzibar;

Na kwa kuwa, kwa mujibu wa Kanuni ya 28 (15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 Bunge haliwezi kukutana na kufanya kazi siku ya Jumamosi, Jumapili au siku za mapumziko na kwa kuwa ili kuliwezesha Bunge kuweza kukutana siku za Jumamosi tarehe 21 Julai, tarehe 28 Julai na tarehe 18 Agosti, ni lazima Bunge litengue Kanuni ya 28(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 kwa mujibu wa Kanuni ya 150(1);

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Nane, Kanuni ya 28(15) itenguliwe kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 28(15) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Bunge halitakutana siku ya Jumamosi na Jumapili na siku za mapumziko itenguliwe na badala yake likutane siku za Jumamosi tarehe 21 Julai, tarehe 28 Julai na tarehe 18 Agosti, kuanzia saa tatu asubuhi hadi hapo shughuli zilizopangwa kwa siku hiyo zitakapomalizika, isipokuwa tu kwamba siku hiyo hakutakuwa na kipindi cha maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Bunge liliafiki Kutengua Kanuni za Bunge zilizotajwa)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU-SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya Kifungu cha 150 (1) Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007, naomba kutoa maelezo ya kutengua Kanuni za Bunge.

Kwa kuwa Mkutano wa Nane wa Bunge unaoendelea umepangwa kumalizika tarehe 18 Mwezi wa Nane;

Na kwa kuwa, kwa mujibu wa Kanuni ya 28 (2) Bunge linakutana hadi saa Saba Mchana na kuahirishwa mpaka saa kumi na moja jioni;

Na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 28 (4) Bunge huendelea kukaa mpaka saa 1.45 usiku ambapo Spika husitisha shughuli za Bunge na kuliahirisha hadi siku nyingine;

Na kwa kuwa kwa mujibu wa Kifungu cha 104(1) wakati wa Kamati ya Matumizi Mwenyekiti ana mamlaka ya kuongeza dakika zisizozidi thelathini iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuahirisha kikao cha Bunge na Kamati ya Matumizi bado haijamaliza kupitisha mafungu;

Na kwa kuwa ndani ya kipindi cha Mkutano wa Nane, waumini wa dini ya Kiislam watatumikia Mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambao utaanza hivi karibuni, naambiwa utaanza kesho, kwa kipindi cha mwezi mmoja;

Na kwa kuwa waumini wote wa dini ya Kiislamu watakaofunga hutakiwa kuswali na kufuturu kila siku ifikapo saa kumi na mbili na dakika arobaini na tano;

Ili kuliwezesha Bunge kutekeleza shughuli zake zilizopangwa kikamilifu na wakati huo huo kuwawezesha Wabunge ambao ni waumini wa dini ya Kiislamu waweze kuswali na kufuturu kwa wakati muafaka kwa mujibu wa taratibu za dini yao, inabidi Bunge litengue Kanuni kadhaa za Bunge zinazotumika kwa sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 150(1).;

Na kwa kuwa katika Kikao cha Kamati ya Uongozi kilichofanyika katika Ukumbi wa Spika jana tarehe 19 Julai, Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge waliohudhuria walikubaliana na umuhimu wa kutengua Kanuni husika;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Nane, Kanuni ya 28 (2), Kanuni ya 28 (4) na Kanuni 104 (1) kitenguliwe kama ifuatavyo:-

Kwanza, Kanuni ya 28 (2) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Bunge litakutana hadi saa Saba Mchana ambapo Spika ataahirisha shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika hadi saa kumi na moja jioni, itenguliwe na badala yake Bunge likutane hadi saa saba na robo mchana ambapo Spika ataahirisha shughuli za Bunge hadi saa kumi jioni.

Pili, Kanuni ya 28(4) ambayo kwa ujumla wake inaeleza kwamba Bunge litaendelea kukaa hadi saa moja na dakika arobaini na tano usiku ambapo Spika atasitisha shughuli na kuliahirisha hadi kesho yake itenguliwe na badala yake Bunge liendelee kukaa hadi saa kumi na mbili jioni.

Tatu, Kanuni ya 104(1) ambayo kwa ujumla wake inampa mamlaka Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Matumizi kuongeza dakika zisizozidi thelathini iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuahirisha kikao cha Bunge na Kamati ya Matumizi bado haijamaliza kupitisha mafungu, itenguliwe na

badala yake Mwenyekiti asiongeze muda wowote katika hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti Naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Bunge liliafiki Kutengua Kanuni za Bunge zilizotajwa)

TAARIFA

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 55 (3) (b) na Kanuni ya 69 (1)-(3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 55(3) inasema: “Hoja zifuatazo zinaweza kutolewa bila taarifa” na (b) inasema: “Kuahirisha Bunge au kuahirisha mjadala”. Kanuni ya 69 inasema:

“(1) Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uahirishwe hadi wakati wa baadaye anaweza kutoa hoja “kwamba, mjadala sasa uahirishwe” na atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani na pia atalazimika kutoa sababu kwa nini anataka mjadala uahirishwe.

(2) Kama Spika, atakuwa na maoni kwamba kuwasilishwa kwa hoja hiyo ni kinyume cha uendeshaji

bora wa shughuli za Bunge atakataa kuitoa ili iamuliwe, vinginevyo papo hapo atawahoji Wabunge juu ya hiyo kadri atakavyoona inafaa.

(3) Endapo hoja iliyowasilishwa haitapata kibali cha Bunge mjadala kuhusu hoja iliyopo mbele ya Bunge utaendelea.

(4) Mbunge yeyote hataruhusiwa kutoa hoja kwa kufanya mabadiliko katika hoja iliyotolewa kwa mujibu wa Kanuni hii".

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nisome vifungu vyote hivi ili kuweka bayana juu ya dhamira yangu ya kuondoa hoja iliyopo mezani kwetu. Hoja yenyewe ni hoja ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza aliyeiwasilisha ambapo katika bajeti yake hii, imebainika kwamba kwa upande wa miradi ya maendeleo, wakulima wote na sekta ya maendeleo kwa ujumla imetengewa bilioni 67.2 na kwamba kati ya hizo shilingi bilioni 14.9 tu ndizo fedha za ndani na bilioni 52 zinategemea fedha kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, wakulima wa Tanzania wapo zaidi ya asilimia 75 au zaidi ya asilimia 80 ya watu bilioni 40 wa Tanzania. Kwa kutengewa bilioni 14 kutoka katika bajeti ya nchi huku tunazungumza habari ya mapinduzi ya kilimo na huku tunataka mabonde ya umwagiliaji yaweze kuboreshwa ili tuweze kufanya mapinduzi ya kilimo na kumwezesha mkulima wa pamba na wakulima wote wa nchi hii ni kuwadhihaki Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, rai yangu hapa ni kupendekeza kutoa hoja kwamba hoja hii sasa iahirishwe ili Serikali ikakae na kuongeza fedha kwa ajili ya maendeleo ya kilimo nchini. Ili dhamira ya kweli ya kuleta mapinduzi ya kilimo kwa Watanzania iwe ni ya kweli na isibaki kama ilivyo, maana kwa sasa bilioni kumi na nne ni hela ndogo tu ambayo inategemewa kuwapa Watanzania zaidi ya milioni thelathini na tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, naomba kutoa hoja na naomba Wabunge wenzangu waniunge mkono.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole-Sendeka, utaratibu wa taarifa, unatoa taarifa pale ambapo kuna msemaji anazungumza, ndiyo unamtolea taarifa, sasa taarifa umenitolea mimi. Kwa hiyo tunaendelea, Katibu!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa James Lembeli.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kwanza jioni hii kuchangia hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, naomba ku-*declare interest* kwamba, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Kahama, Mkoa wa Shinyanga, Mkoa ambao unalima pamba kwa

wingi kuliko mikoa yote hapa nchini. Nimezaliwa na kukua katika mazingira ya kulima pamba, lakini pia sasa hivi nina majukumu mengine, nipo hapa Bungeni kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Kahama ikiwa ni pamoja na wakulima wa zao la pamba, tumbaku na mazao mengine yanayolimwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, napenda niseme kabla sijasahau kwamba, sitaunga mkono hoja hii na sitaiunga mkono hata kesho kwa sababu zifuatazo:-

Moja, ninavyozungumza hivi sasa wakulima wa pamba wa Jimbo la Kahama, wakulima wa pamba wa Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara na kwingineko ambako pamba inalimwa wamekaa mkao wa msiba. Wanamachungu ya tatizo la zao lao la pamba, wana huzuni na wanajuta ni kwa nini wao ni sehemu ya wakulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la bei ya pamba mwaka huu si geni, limezungumzwa katika maeneo mengi na katika maeneo yanayozalisha zao la pamba sasa hivi tatizo la pamba linahatarisha amani katika maeneo hayo. Kwa nini siungi mkono hoja hii? Katika hotuba ya Waziri kwa bahati mbaya sana ni rafiki yangu tunapita njia moja, hajazungumza wala kuelezea lolote kuhusu matatizo yanayowakabili wakulima wa pamba nchini hivi sasa. Kwa maana hiyo ni kwa nini mimi kama mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kahama ambako pamba inalimwa nisimame hapa niunge mkono hoja hii, nitakuwa mjinga mimi

mwenyewe, lakini nitakuwa siwatendei haki wakulima wa zao la pamba nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusema kwamba siungi mkono hoja hii kwa namna yoyote ile, itapitishwa lakini ninachotaka kusajili ni kwamba, wananchi wanaolima zao la pamba wamenyimwa haki yao na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina tofauti ya kiitikadi na Mzee wangu Mzee Cheyo, lakini namuunga mkono kwa kauli yake aliyoitoa ndani ya Bunge hili kwamba, bila shilingi elfu moja hakuna kuchukua pamba ya mkulima. Ni afadhali wakulima wa zao la pamba waifungie pamba yao au watengeneze magodoro angalau wafarijike kwa kulala sehemu nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui wakulima wa pamba wameikosea nini Serikali, mwaka uliopita kulikuwa na *crisis* ya zao la korosho, nilishuhudia kwa macho yangu, nilisikia kwa masikio yangu viongozi wa ngazi za juu Serikalini wakielekea Mtwara. Lakini mwaka huu wakati tuna tatizo kubwa la zao la pamba Serikali iko kimya na ndiyo maana hata katika hotuba ya Waziri hapa hajazungumza. Au kwa sababu wananchi na hususan Wasukuma wamezoea kusema *ndoho tabhu,* haiwezekani! Nami nitaungana nao mkono ili kuhakikisha kwamba bila shilingi elfu moja hakuna kuchukua pamba ya mkulima. Hiyo ni sababu ya kwanza kwa nini siungi mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mbaya sana Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba ambaye ndiye chimbuko la matatizo yote haya mwezi mmoja uliopita ilitangazwa kwamba amesimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi wa kina na kukidhi matakwa ya wadau wa pamba na wakulima wa pamba. Waziri katika mkutano wa wadau kule Mwanza alithibitisha kwamba uamuzi umeshafikiwa na ndugu huyu amesimamishwa kazi, mpaka juzi tarehe 16 Mkurugenzi huyu wa Bodi ya Pamba alikuwa ofisini. Hii ni dharau, hii ni kejeli, kwa wakulima wa zao la pamba nchini. Serikali imefikia mahali pa kumlinda mtu mmoja na kudharau malalamiko ya wananchi wake ambao wameiweka Serikali madarakani! Siungi mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili ni kwamba, Wilaya yangu tunalima tumbaku, wakulima wa tumbaku katika Wilaya ya Kahama wamekuwa wakidhulumiwa kila kunapokucha, mathalani mwaka huu bei ya mfuko mmoja wa mbelea aina ya *NPK* ni dola 54.61, lakini bei halisi ya mbolea hii kwa mfuko ni dola 38.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana nyingine dola 16.61 ambayo inasemekana ni gharama ya usambazaji na mchanganuo wa Vyama vya Msingi kwa Chama cha Ushirika inanyang'anywa kutoka mkononi mwa mkulima. Kumlipisha mkulima ziada ya dola 16.61 ni kumuibia, lakini Serikali imekaa kimya ina-*enjoy,* haioni kwamba wakulima hawa wa tumbaku wanapata shida sana katika kilimo cha tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu kwa hakika unapaswa kupingwa kwa nguvu zote ikiwezekana hata kwa nguvu za sungusungu. Nitatoa mfano, Chama kimoja cha msingi kule Uloa mwaka huu kimenunua mifuko 6,000 ya mbolea, ukizidisha mara dola 16 unapata karibu dola 100,000, milioni 160,000 Chama kimoja cha Msingi. Katika Jimbo la Kahama kuna zaidi ya Vyama 20 vya Msingi. Maana yake wananchi hapa wanaliwa dola milioni mbili takribani bilioni nne. Halafu Serikali inanitaka nisimame hapa niunge mkono hoja, siungi mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwenye bei ya tumbaku, bei ya wastani Kitaifa ni dola 1.82, cha ajabu Kahama wakulima, tumbaku yao inanunuliwa kwa wastani wa dola 1.73, senti tisa kwa kila kilo anayouza mkulima wa tumbaku Kahama inaliwa na wajanja. Ukizidisha na kilo milioni 2,800,000 ambazo wakulima wa Jimbo la Kahama walikuwa wameuza kwa Vyama vya Msingi unazungumzia zaidi ya dola milioni 2,500,000. Wakulima maskini wako kule wanahangaika, Serikali inafanya nini? Serikali wajibu wake ni kuwatetea wakulima, lakini haifanyi jambo lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kutamka kwamba siungi mkono hoja. Nakushukuru. *(Makofi)*

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuweza kuchangia Hotuba ya Wizara ya Kilimo jioni hii ya leo. Kwanza kabla sijachangia, ningependa nitoe salama za shukrani kwa wasanii wote wa Mkoa wa Kigoma

ambao juzi walikusanyika wote Mkoani Kigoma na kufanya tamasha kubwa kuonesha mshikamano wa Mkoa wa Kigoma na nafasi ya Mkoa wa Kigoma katika Historia ya Tanzania na mageuzi ya kisiasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana Waziri wa Kilimo na Chakula sina shida naye, ni mzee wangu na namheshimu sana. Lakini inapokuja hoja ya maisha ya binadamu, maisha ya watu ni wazi hakuna namna nyingine ya kufanya isipokuwa ni kutokubaliana na hoja ambayo imetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni Taifa ambalo kwa namna yoyote ile lina nafasi kubwa sana ya kukifanya kilimo kiweze kuondoa umaskini wa Mtanzania. Nimepata kuzungumza mara kadhaa kwamba hii njaa ambayo ipo kwenye pembe ya Afrika, hii njaa ambayo inayakabili Mataifa ambayo ni majirani zetu kwa nafasi yetu ambayo Mwenyezi Mungu alitujalia ingetosha kabisa mtaji kwetu, kuwa mauzo kwetu, kuwa moja ya nyenzo ya kuondoa umaskini wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ambayo ina mabonde ya kutosha kwa ajili ya kilimo, Tanzania ni nchi ambayo ni ya 11 kwa mito mingi duniani. Kwa taarifa tu ni kwamba Tanzania ina takribani hekta milioni 29,400,000 ambazo zinazotosha kwa kilimo cha umwagiliaji. Mazingira ya sasa ambayo Mataifa mengine yanashindwa kilimo hawana mabonde sisi kwetu ingekuwa faraja, sisi kwetu ingekuwa ni namna sasa ya kufaidika na njaa yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini inaelekea kwamba tunazungumza hapa lakini hatusikilizwi. Kuna usemi unasema kwamba akufukuzaye hakwambii toka, kwamba kila siku tunazungumza tuongeze kasi ya ukuaji wa sekta ya kilimo, lakini Serikali ambayo inajiita sikivu, sijui labda ina ugonjwa wa masikio, huwezi ukatenga bilioni 14 kama mapato ya ndani uwekeze kwenye kilimo, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu hakiwezekani! Ndio maana naungana na Mzee wa TANU Mzee Christopher Ole–Sendeka kwamba kama hiki chama kingekuwa kinaheshimu misingi yake, hii hoja isingeletwa hapa. Mngekaa kwanza huko mkajadiliana mkaleta kitu ambacho kimekamilika. Lakini kwa kuwa mmeshaacha misingi yenu, ndio maana mmeanza kuleta hoja ambazo hazijadiliki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kuna miradi ya umwagiliaji ambayo tangu mwaka 2006 iko nusu ya Konkwa, Mgambazi, Kalilya; ukienda Kasulu kuna miradi ambayo iko nusu. Rungo Mpya kule ukiangalia kwenye bajeti, hakuna hata chembe ya shilingi ambayo Serikali inaonesha kwamba inatekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo kwa kweli katika hali ya kawaida haiwezekani mtu mzima ukapitisha bajeti ya namna hii. Kwa hiyo, bado nasisitiza kuna umuhimu mkubwa wa bajeti hii kurejeshwa ilikotoka mwende mkapange upya. Hakuna cha kujadili hapa, msitufanye Wabunge wapiga kelele, mmeleta vitu ambavyo havina msingi,

tupigiane kelele humu, tupandishiane hasira mwishoni tushikane mashati. Haiwezekani hakuna kitu, nendeni mkaleta bajeti ambayo ni bajeti, hii siyo bajeti. Tunahitaji kuona kilimo kinakua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kinategemewa na asilimia 75 ya Watanzania. Tunazungumza hapa kwamba uchumi vijijini haukui kwa sababu kilimo hakikui. Utafiti unaonesha kwamba kilimo kikikuzwa kwa asilimia 10 miaka mitatu tu mfululizo mnaweza mkakata umaskini kwa asilimia 50. Huu ni utafiti umefanywa na *REPOA,* tangu mwaka 2006 mpaka leo bado mnaleta bajeti za kizee ambazo hata hazina msingi wowote. Kilimo kinakuzwa kwa asilimia tatu au nne haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo nitaomba radhi kama nitakosea kwenye kauli. Lakini kimsingi naumia sana. Naombeni ndugu zangu katembeleeni vijijini muone kiwango cha umaskini kwenye kilimo kilivyo. Watu wanaumia, mnafanya matumizi ambayo hayana ulazima wa kufanywa mnaainisha matumizi ambayo si ya lazima kufanya.

TAARIFA

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye kifungu cha 68(8): “Mbunge yeyote anaweza kusimama mahali pake na kusema taarifa na kwa ruhusa ya Spika, atatoa taarifa ya ufafanuzi kwa Mbunge anayesema”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Mbunge anayeendelea kuzungumza hapa kwenye kifungu cha 64(g) katika maelezo yake Mheshimiwa Mbunge amesema bajeti hii ni ya kizee. Maneno bajeti hii ni ya kizee ni ya kuwadhalilisha wazee wote nchini, ambao wamelitumikia Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa lugha nyepesi kwa sababu najua na yeye ana wazee ndio wamemlea na wamemfikisha katika hatua hiyo, atumie busara vile vile kufuta maelezo yake hayo kutokana na kifungu hicho cha 64 (g), kwamba hatatumia lugha ya kuudhi au inayowadhalilisha watu wengine. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kafulila nafikiri ulianza kufuta hiyo kauli kabla, naomba ufute tena rasmi ili uendelee.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema tu kwamba hii bajeti ni bajeti ambayo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kafulila nimekuomba, ulishaanza kufuta hiyo kauli siyo rasmi, nakuomba ufute rasmi uendelee.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, leo tuna miaka 50.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kafulila, futa hilo neno la wazee endelea ndugu yangu, kuna shida Kigoma watu wanahitaji maji, mbolea.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepewa taarifa naweza nikaipokea au nisipokee. Nimepewa taarifa, *otherwise* kama kuna kanuni zingine. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tuendelee.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hatuwezi kukuza kilimo kama hatuwezi kwenye miundombinu ya kilimo. Kwa hiyo, naishauri Serikali pamoja na kuleta bajeti ambayo kimsingi haijadiliki, bado tunaendelea kuisisitiza kwamba kuna kila sababu ya Serikali kuanza kutenga fedha za kutosha kuwekeza kwenye kilimo. Tukiwekeza kwenye kilimo tutaondoa umaskini wa wapiga kura wetu. Tutaondoa umaskini wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tukiwa na miaka 50 tangu uhuru bado tunaagiza mbegu kutoka Malawi, yaani Malawi nchi ambayo uchumi wake ni duni kabisa, tunaagiza mbegu kutoka Malawi, Uganda na Kenya; ina maana kwamba, Tanzania bado kwa miaka 50 tunashindwa kujitegemea kwenye kuzalisha mbegu, siyo mazao, kuzalisha mbegu, hii ni aibu, tunaagiza asilimia 75 ya mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashindikana nini kama Serikali ina dhamira ya kuweka mkakati kuhakikisha kwamba ndani ya mwaka huu wa fedha tuwe na miundombinu ambayo itatuwezesha tuzalishe mbegu zetu sisi wenyewe? Mataifa mbalimbali wanazalisha mbegu wao wenyewe. Hii ni aibu. Kwa hiyo, naiomba

Serikali baadhi ya mambo ambayo kwa kweli ni ya aibu, tuyaepuke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu kuna shamba kubwa la mchikichi. Mkoa wa Kigoma, ni Mkoa ambao leo ni *supplier* mkubwa wa *product* za mafuta ya kula, wa product za michikichi duniani. Nchi ya Malaysia walikuja Kigoma kujifunza kuhusu michikichi mwaka 1990, mpaka sasa Serikali ya Tanzania haina mkakati wowote wa kulifanya zao hili liwe zao ambalo linaweza likatoa mchango mkubwa kwenye uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Malaysia, hii michikichi yale maganda yale wanayatumia kutengeneza vigae ambavyo vinatumika kujenga nyumba za thamani kubwa sana duniani. Kule kwetu sisi tunakoka kupikia maharage. Wenzetu haya mawese, yale mabaki yake yanatengenezewa mafuta ambayo yanatumika kulainishia mitambo, sisi kwetu ni takataka. Itatuchukua miaka mingapi kuweza kuufanya utajiri ambao tumepewa wa michikichi kutafsiri maisha ya watu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Serikali ianze kutafakari namna ya kufanya zao la michikichi liingie kwenye mipango ya Serikali kwa sababu lina nafasi kubwa ya kukuza uchumi wa Kigoma lakini lina nafasi kubwa ya kuchangia sehemu kubwa sana ya maisha ya wakazi wa Tanzania na wakazi wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Kigoma bado tuna ardhi kubwa ya kilimo, lakini kuna tatizo kubwa moja, utaratibu mzima wa upatikanaji wa pembejeo umejaa rushwa. Nimepata kuwaambia Mheshimiwa Waziri na Mkuu wa Wilaya, ukienda pale Nyanganga ni mfano mmoja tu, watu wameandika majina ya marehemu, wamegawa *voucher* kwa majina ya marehemu, wamechukua fedha. Nikamwambia Mkuu wa Wilaya, *PCCB* watakwenda, mpaka kesho haijulikani kesi iko wapi. Kesi haifunguliwi, taratibu hazijulikani zinakwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtakaa hapa na bado mnatenga fedha kidogo na bado hizo kidogo mifumo yake ya kiusimamizi inajaa uchakachuaji, leo watu wa Burundi wanafaidi mbolea ya ruzuku ya Tanzania, ni aibu. Mbolea ya ruzuku inakwenda Kigoma, viongozi wa Serikali wanafanya wizi na ufisadi, wanafanya ujambazi kabisa watu wa Burundi wanafaidika na mbolea ambayo tayari imekuwa *subsidize* kutoka Tanzania. Hii Serikali ni lini itapata uwezo wa kusimamia mali zake? Ni lini mtamhakikishia kwamba mkulima sasa mnaweza mkamsimamia aweze kupata haki yake hata hiyo kidogo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwangu kule kuna zao la tumbaku pia. Lakini bado kuna changamoto kubwa sana ya namna gani ya kupata bei na namna ya kupata zile *grade* za tumbaku. Anakuja mtu ambaye kama hujamhonga anatoa *grade* ya chini kwa tumbaku yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wakulima wetu tumbaku ya kwao, lakini bado watoe rushwa ili kupewa *grade* sahihi ya tumbaku yao. Sijui nisemeje! Sijui itatuchukua miaka mingapi kuweza kutoa huduma ambayo kimsingi ni haki yao kabisa, lakini wanalazimika kutoa rushwa ili wapate *grade* yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukitoa taarifa Serikalini hakuna hatua inayochukuliwa. Inafika mahali wakulima wanaanza kutafakari hivi hawa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Kilimo aliyoiwasilisha leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nataka kwa niaba ya Wanachilonwa wote ambao nawawakilisha hapa Bungeni, nitoe rambirambi na pole nyingi kwa msiba mkubwa uliolipata Taifa kutokana na kuzama kwa meli kule Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nichukue fursa hii fupi kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri *Engineer* Christopher Chiza pamoja na Naibu wake kwa kupewa fursa ya kuongoza Wizara hii, Wizara ambayo Mheshimiwa Chiza ameitumikia kwa muda mrefu, nampongeza sana na namtakia kila la heri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inaitwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Mimi nikiwa mmoja wa wadau wakuu wa shughuli za Ushirika nchini, ningependa nianze kwa kujielekeza kwenye shughuli ya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi Mheshimiwa Waziri, alipokuwa anawasilisha hoja hapa alitaja changamoto kadhaa ambazo zinasababisha kuzorota kwa shughuli za ushirika hapa nchini. Nakubaliana naye, lakini nataka tu nimkumbushe tatizo moja la msingi ambalo linatakiwa litiliwe mkazo, ambalo ni kukosekana kwa ukaguzi wa mara kwa mara kwenye Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata tukianzisha Vyama Vingi kwa kadri itakavyowezekana lakini kama hakuna hii shughuli ya ukaguzi wa mara kwa mara ni kazi bure kwa sababu ushirika utaendelea kuzorota kwa sababu hakuna mwangalizi mahususi. Kazi hii inatakiwa ifanywe na Idara ya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu kubwa ya Idara hii ya Ushirika ni kuhamasisha uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika, kuviandikisha, lakini pamoja na kuvikagua. Mimi sina tatizo na suala la uhamasishaji na uandikishaji wa vyama linafanyika vizuri sana na idadi tuliyopewa hapa inaonesha jinsi ambavyo shughuli hii inavyofanyika. Lakini sioni kabisa shughuli ya (*inspectorate*), ukaguzi wa Vyama vya Ushirika kazi ambayo huko nyuma nataka niseme kwamba, nilishaifanya kwa zaidi ya milioni 30 hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule tukifanya habari ya ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, vyama vingi vilikuwa viko macho, kila mara na kwa hiyo, ubadhirifu unaotokea sasa hivi ulikuwa hautokei kama ambavyo unatokea sasa. Lakini kwa bahati mbaya sana sioni kabisa shughuli za ukaguzi kama zinaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe tu kwa sababu sasa hivi Serikali ina mchakato wa kuanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika, hii kada ya ukaguzi wa Ushirika ambayo *inspectorate* irejeshwe rasmi. Kwa sasa hivi haipo na irejeshwe, ifanye kazi kwa uhuru kwa kujitegemea na isimamiwe na Mrajisi moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mtindo wa sasa ambao idara ama kada hii ya ukaguzi inasimamiwa na Ukurugenzi wa Halmashauri za Wilaya haufai kabisa kwa sababu watumishi hawa hawafanyi kazi kwa uhuru na wakati mwingine wanatumwa kazi zingine ambazo hazihusiani na ukaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi ukaguzi unaofanywa na Vyama vya Ushirika ni sawasawa na ukaguzi wa aina nyingine. Kwa hiyo, wanatakiwa wajitegemee. Kwa hiyo, niombe tu Tume itakapokuwa imeanzishwa, suala hili liangaliwe na kitengo hiki kipatiwe watumishi wa kutosha wa kuweza kusimamia Vyama vya Ushirika na kama nilivyosema waweze kufanya kazi kwa uhuru unaotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika ni tofauti na Wasajili wa mambo mengine. Unajua Mrajisi na Msajili ni vitu viwili tofauti pamoja na kwamba wote wanaitwa *registrar* kwa sababu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika ana jukumu la ziada la kuhakikisha kwamba anakagua na kusimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ana jukumu lile la udhibiti tofauti na usajili wa aina nyingine. Kwa hiyo, hili lingeangaliwa nadhani hata katika kuiunda Tume, kitengo hiki kinaweza kikapewa nafasi yake stahiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo ningependa nichangie ni suala zima la shughuli za umwagiliaji. Kwanza nataka niipongeze Serikali, kusema kweli kwa kusimamia shughuli za umwagiliaji hasa katika maeneo kame ukiwemo na Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu la Chilonwa kwa mfano, kumekuwa na shughuli za umwagiliaji zinazoendelea pamoja na mradi mkubwa wa umwagiliaji kwa njia ya matone pale Chinangali, kilimo cha zabibu. Jambo kama hili wakulima wa Chinangali pamoja na wana Chilonwa kwa ujumla wamesema nilete salaam za kuishukuru Serikali. Kwa hiyo, kwa kipengele hiki nataka niseme kwamba, naunga mkono hoja hii kwa sababu wananchi wangu wamenituma niseme hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa nilete maombi. Shughuli za umwagiliaji zinazoendelea katika sehemu mbalimbali katikaWilaya yetu zikiwepo kule Bwigiri, Chalinze na huu mradi wa umwagiliaji kwa matone, zimeanza kunufaisha baadhi ya wakulima wetu kule Vijijini. Lakini nilete ombi kwako Mheshimiwa Waziri, kuna ile skimu ya umwagiliaji ya Chalinze ya Bwawa la Ikoa ambalo Mheshimiwa Waziri unalifahamu siku nyingi. Mradi huu ulianza siku nyingi sana kutoka mwaka 1957. Miundombinu yake bado ni imara, isipokuwa bwawa lenyewe sasa hivi linahitaji ukarabati mkubwa ili liendelee kunufaisha wakulima wa Kijiji cha Chalinze ambao sasa hivi wananufaika kidogo kwa kumwagilia zile heka 240 ambazo ziko katika mradi huu.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano wa kutenga fedha zaidi kwa ajili ya kusaidia mradi huu wa *scheme* ya umwagiliaji Chalinze katika Bwawa la Ikoa na wananchi watanufaika sana na niseme kwamba, pamoja na kwamba humu umeeleza kwamba mnachimba mabwawa mengine mapya na *scheme* nyingine mpya, lakini hizi *scheme* za zamani ambazo bado ziko imara, nadhani mkiziimarisha litakuwa ni jambo bora zaidi na ndiyo jambo ninalosisitiza sana kuiangalia hiyo *scheme* ya Bwawa la Ikowa pale Chalinze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisemee habari ya zao la zabibu. Zao la zabibu hapa Dodoma lilishamiri sana katika miaka ya nyuma wakati kukiwa na kiwanda cha *DOWICO* ambacho kilikuwa ndiyo soko. Kiwanda kile ilikuwa ni kampuni tanzu ya Shirika la Serikali la *NMC*, lakini *DOWICO* ilipofilisika na kuacha kufanya shughuli,

kilimo cha zabibu kilififia sana. Lakini kwa bahati nzuri kwa msimamo wa Serikali, na kusema kweli hapa tumshukuru sana aliyekuwa Mkuu wetu wa Mkoa wa zamani, Mheshimiwa Lukuvi, alisimamia sana suala la kufufua kiwanda kipya cha kutuwezesha kupata soko la zabibu.

Kiwanda kile kipo Hombolo cha *Central Tanzania Winery Company* ama *CETAWICO*. Kilipoanzishwa, wakulima wameitikia sana katika kilimo cha zabibu, lakini kwa bahati mbaya sana wakulima hawa ambao wanalima zabibu katika Wilaya za Bahi, Chamwino, pamoja na Dodoma Mjini, wameanza kupata tatizo kubwa la mnunuzi huyu pekee *CETAWICO,* kwa kutoa bei ndogo. Kwa hiyo, wakulima sasa hawana namna. Kwa hiyo, zao hili liko katika hatari ya kufa, tena kama Serikali haitaingilia kati. Maana mwekezaji huyu bado anapata nafuu ya kodi kwa msisitizo ule wa kuhakikisha kwamba anainua kilimo cha zao la zabibu. Lakini vile vile anavyo vibali vya kuagiza malighafi kutoka nje ambayo anaitumia kwa jina la *wine* ya Dodoma, lakini kwa bahati mbaya, zabibu zetu za Dodoma hazinunuliwi kwa bei stahiki na wakati mwingine nyingine zinakosa soko kabisa*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu kwa taarifa, kukuza eka moja ya zabibu inamgharimu mkulima karibu Shilingi milioni sita. Sasa mnunuzi huyu haangalii gharama zote hizi ambazo mkulima anagharamia. Mimi ombi langu ni kwamba, Serikali iingilie kati, ifuatilie mwenendo wa mwekezaji huyu kama kweli anachokifanya kinalingana na yale yaliyokuwa yamekusudiwa. Lakini tuombe tu kwamba pengine

tuanzishiwe kiwanda chetu pale Chinangali ili kuhakikisha kwamba...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)

MHE. SULEMAN M. N. SULEIMAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Lakini naomba nianze kwa kuwashukuru wafuato:-

Namshukuru sana *DC* wangu mgeni kwa namna ambavyo halali, anawahi kuingia ofisini na anachelewa kutoka kwa ajili ya wakulima na wananchi wa Jimbo la Kishapu. Namshukuru sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyaga kwa kazi tunayoifanya; na habari njema tu kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, tuna kituo kikubwa cha matrekta takribani 5,000 yatakuja kwa jitihada katika awamu yake. Wanakishapu watapata matrekta zaidi ya 150 kwa jitihada za Mkuu wa Mkoa, *DC* na Mbunge wao. Lakini niwashukuru pia wafuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilikuwa Wizara ya Kilimo, nilipata nafasi ya kukaa na Katibu Mkuu, Katibu Mkuu Msaidizi, Wahandisi kwa ajili ya kukitazama kilimo cha umwagiliaji. Nawashukuru sana kwa kweli walikuwa wema, tulijadili mambo mengi na niwashauri Wabunge wenzangu wakipata nafasi wakawaone pia Watendaji, wapate mawazo mazuri waliyonayo, tuweze kuwa na sifa ya uongozi wa pamoja badala ya kulaumu hapa; twende katika ofisi zao na wao wako tayari kututembelea, watakuja Kichapu wameniahidi timu nzima, na nimeamini kweli kuna Watendaji hasa

Katibu Mkuu na timu yake, ni wasikivu wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nianze na pamba. Suala la pamba, niliongea sana kwenye hotuba ya Wizara ya Fedha. Kanuni ya vita, Askari wakishindwa vita anayetakiwa kuondoka ni Mkuu wa Majeshi. Bodi ya Pamba ndiyo msimamizi wa zao la pamba na kwa sababu tangu uhuru mpaka leo hii tatizo la pamba limeendelea kuwepo. Mimi niliishauri, Serikali kwa nini isivunje Bodi ambayo ndiyo imeshindwa kusaidia zao la pamba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakaa kwa ajili ya kupanga bei ya pamba, hawakai kwa ajili ya mikakati ya kusaidia wakulima wa pamba *for the next hundred years.* Marekani wanakaa kwa ajili ya kuona wanafanya nini miaka 50 na 100 ijayo, sisi kila siku tunalia. Mheshimiwa Waziri unapojibu, tafadhali asiogope ana mamlaka kamili. Avunje Bodi kwa sababu matatizo yameendelea kuwepo. Sisi tutamsaidia, hatuko hapa kum-*attack*, hatumvamii, tunamsaidia avunje Bodi kwa sababu wameshindwa kufanya kazi yao. Wameshindwa kuhudumia Watanzania milioni 16 wanalia, Bodi ya Pamba, watu wachache! Leo mimi nilikuwa kwenye Kikao cha Bodi ya Pamba, wanakwenda kununua masuzuki kwa ajili ya kuwahudumia wakulima wa pamba. Mimi nimekuwa Kishapu, Padri aliyekuwa pale Wela Okenyenge alikuwa anatoka na pikipiki *one ten* kwenda kusalisha Misa Musoma na kurudi, leo wanashindwa, wanataka kununua ma-*Hard Top*, ma-

VX, wananunua Suzuki wakati mkulima anatumia jembe la mkono na ng'ombe? Vunja Bodi ya Pamba tafadhali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utapeli kwenye mbegu, lazima tukusaidie Mheshimiwa Waziri, tuko hapa kwa ajili ya kukusaidia, wewe ni Baba Mkwe wangu, mimi nimeoa Kigoma na wewe ni Baba Mkwe wangu na mimi ni Mkwe wako. Kwa hiyo, lazima nikusaidie, ninakuheshimu sana. *(Kicheko)*

Watu wamekuja, wameanzisha vitaasisi, mbegu zinauzwa dola moja, Sh. 1,600/= na hakuna kinachofanyika, ananunua mbegu za wakulima hao hao, zinakwenda zinanyolewa manyoya, zinauzwa kwa dola moja. Hii biashara ni ya aina gani? Huu ni wizi! Tafadhali liangalie. Bei ya pamba, Ndugu zangu milioni 16 wanalia. Serikali ya CCM ni sikivu, wasikilizeni Watanzania milioni 16. Mimi ni mkulima, ninalima pamba, mtama, matunda, ninajua uchungu tunaoupata. Mmeanzisha na mliahidi Bima ya Mazao itaanza mwaka huu. Kwa nini isianzie kwenye pamba? Ninyi wenyewe mlituahidi, ianzie kwenye pamba, wakulima hawa wanufaike. Nilisema suala la viwanda, kwa muda mrefu tuongelee miaka 10 mpaka 100, mashirika yetu ya Serikali *NSSF, PPF* na wengineo wasijenge maghorofa makubwa Dar es Salaam, wawekeze kwenye viwanda vinavyoweza kutoa ajira kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie hili, Watanzania milioni 16 wanalia na Mbunge wa Kishapu nikiwa ndani

ya hao Watanzania milioni 16, watoe *guarantee* kwenye viwanda vya nyuzi, viwanda vya nguo, lakini Serikali nayo iangalie inafidia kiasi gani. Wapiga kura wetu wanalia. Nimekwenda kufanya Mkutano Bubiki, nimewaambia umeme unakuja, maji yanakuja, wananiuliza Wasukuma, *alo bholobha wakinehe,* kwamba pamba ni vipi? Tunakosa raha Majimboni, naomba mtusaidie sana kwa zao la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeliongea vizuri sana suala la matrekta, Wanakishapu, mimi nasema Mbunge wenu yuko makini, yanakuja matrekta 150, wajiandae na vikundi na mambo yatakuwa safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye zao la sukari, miwa. Historia ndiyo inayotuelekeza, kwamba Tanzania tulikuwa tunazalisha sukari tani 98,000 kwa mwaka mmoja, leo hii tunazalisha 325,000. Viwanda kama Kilombero, wakulima wadogo wa nje walikuwa wananunuliwa mazao yao kwa Shilingi bilioni saba kwa mwaka. Leo hii Kilombero inanunua miwa ya nje zaidi ya Shilingi bilioni 30. Mtibwa Sugar walikuwa wananunua Shilingi milioni 800 kwa mwaka, leo hii wananunua zaidi ya Shilingi bilioni 7.5. Mheshimiwa Rais ana nia njema, amekwenda Brazil na sehemu mbalimbali kwenda kuangalia namna gani wenzetu wanalima miwa. Amekwenda na wataalamu, nawashauri Waheshimiwa Mawaziri na Baba Mkwe wangu akiwemo, Mheshimiwa Rais ana nia njema, mpeni *support,* wasikilizeni pia Watendaji, saidieni ni kwa nini tuendelee kuingiza sukari nchini? Wako wakulima wadogo wadogo wanalima, wameonyesha

nia, kwa nini tusiwasaidie tujitosheleze sisi na sukari itoke Tanzania iende nje tupate pia *foreign currency?* Kwa nini twende kwenye vibali? Nakuomba Mheshimwa Waziri pia Bodi ya Sukari uiangalie. *(Makofi)*

Uingereza nilisema, watu wakichaguliwa kuwa Wajumbe wa Bodi, wanakwenda kusomea ufanisi na kazi za Bodi. Sisi isiwe ni ajira, ruzuku ama takrima. Tunafanya kazi za kuwakomboa Watanzania. Mashirika pia yatoe *guarantee* kwa hawa wakulima wadogo na wakubwa wanaoonyesha nia yao kutokana tani 98,000, leo 325,000 mwaka 1998 mpaka 2012 wakati Brazil na maeneo mengine wana zaidi ya miaka 200. Msiende kuuliza mnazalisha hekta 25,000 tani 150,000, ulizeni mlianzaje mpaka mmefika hapa mlipofika leo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba sana, historia ndiyo inayotueleza, kuna Uturuki leo wanaongoza duniani kwa mazao matano makubwa. Nyanya zikiwemo, *cucumber*, waulizeni kwa nini na mimi nimekwenda Wizarani, nimewauliza wataalamu wana *documents* zote. Mheshimiwa Waziri kaa na watu wako, waite Wabunge wenye maeneo mbalimbali ya kilimo, shauriana nao, nchi hizo zilivyofika hapo zilipofika, ziliamua, zilifanya jitihada, zilijifunga mkanda, sisi tunaogopa nini? Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, Bodi ya Pamba vunja, unda Bodi mpya. Bodi ya Sukari vunja, wao mawazo yao ni kuingiza tu sukari kutoka nje; korosho vunja; kahawa vunja; wameshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja kwa sababu Kishapu wanapata materkta na nina imani bei ya pamba mtaongeza ruzuku.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ili na mimi nichangie katika hotuba hii ya Waziri wa Kilimo. Lakini nianze kwa utangulizi na niwakumbushe wenzangu kwamba bajeti kuu ya Serikali tuliipitisha sisi wenyewe humu ndani na tukisema kwamba tuanze kunyofoa huku na huku, kwa njia moja au nyingine tutakuwa hatumtendei haki Waziri mhusika. Lakini mimi namshauri Waziri wa Fedha kwamba sisi wadau, baada ya hapa tutafute namna nyingine ya kupata vyanzo vya mapato yetu ya ndani na nje ili haya tuliyoyasema yaweze kutekelezeka kwa sababu ni kweli pesa inayotengwa kwenye kilimo ni kidogo sana. Huo ndiyo ushauri wangu wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mtoto wa mkulima, lakini sana natetea wakulima wa zao la pamba. Mkulima wa zao la pamba anaibiwa kwenye mbegu, viuwa wadudu, pembejeo, bei, mzani na anakopwa. Kwa nini? Juzi juzi tu nilikuwa Jimboni kwangu, iko mizani aina tatu ambayo kwa masikitiko makubwa sana, kwa kweli Serikali yangu sijui inafanya makusudi au namna gani! Katika hotuba ya Waziri, Mheshimiwa Mary Nagu, aliyekuwa Waziri wa Viwanda na biashara wakati huo, katika hotuba yake alisema naomba kunukuu: “Kupitia GN. Na. 233 ya tarehe 3 Julai, 2009 nimepiga marufuku matumizi ya mizani aina ya *steel yard* baada ya kubainika (siyo maneno yangu

haya) kuwa mizani hiyo ya *steel yard* ya Mizani ya Rula ni rahisi kuchezewa na hivyo kuwaibia wakulima hasa wakati wa ununuzi wa zao la pamba.

Mheshimiwa Waziri juzi tena kaja na samahani. Hapa, naomba sana, tunaposema humu Ndugu zangu, Waheshimiwa Mawaziri, mtusikilize. Ukitaka kujua kwamba wakulima wanaibiwa, uliza mizani leo. Nimeshuhudia mwenyewe mzani *steel yard*, wanamwibia mkulima zaidi ya kilo 12 kwa mzigo mmoja. Mmeruhusu mizani mitatu ya *ruler*, kuna sijui *spring balance, digital* na yote hii ni kutaka kumwibia mkulima. Kwa nini tusiende na mzani mmoja? Hii ni janja tu, hawa wanunuzi wa pamba, oh! Hii haiwezekani! Miaka mitatu, mzani mmoja! Haiwezekani!

Mheshimiwa Waziri, nakuheshimu sana na wewe unaheshimika sana, hebu jaribu kubadilika kidogo kama ulipokuwa Naibu Waziri, hukuwa hivyo, tunakujua. Hebu chapa kazi yako ili uwasaidie wakulima hawa, vinginevyo Mheshimiwa Waziri kwa kweli tutakuwa hatukuelewi tena kwa sababu wanaoumia ni wakulima wa zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taarifa kwenye nchi ya India ambaye ni mkulima mkubwa wa zao la pamba, kuna upungufu mkubwa sana kwenye zao la pamba. Pamba ni ndogo India wanatumiaji wakubwa wa pamba. Watakapoingia sokoni kutafuta pamba, nina uhakika pamba yetu bei itapanda. Ombi langu na ninaomba wakati utakapofanya majumuisho, utamke wala usimung'unye maneno; narudia, utamke,

Serikali isimung'unye maneno itamke kwamba kuanzia sasa soko la ununuzi wa pamba liwe huria ili kutoa nafasi kwa wale wengine ambao wamefungwa mikono. Lakini unaweza kujua kwamba kwa sababu bei ya pamba itakapopanda na nina uhakika itapanda tu, na niliwaambia wakulima wangu wa Mwanza kwa maana ya Sumve, Kwimba na Kishapu na sehemu nyingine zote Sengerema, Geita kwamba bei ya pamba lazima itapanda tu kwa sababu India wana upungufu mkubwa wa pamba. Waziri, chonde chonde. *(Makofi)*

Halafu Mheshimiwa Waziri naomba, Waheshimiwa Wabunge humu tangu wakati wa bajeti ya Waziri wa Fedha, Waziri Mkuu na bajeti nyingine, Wabunge tumesema kweli kweli kuhusu pamba, lakini nashangaa na kusikitika kwamba Serikali imekaa kimya tu. Hata kutoa tamko tu, inafikia kipindi maeneo ya wanaolima pamba watu wanaanza kupigana, maghala yanachomwa moto, watu wanapigwa, wanapeana faini, Serikali imekaa kimya kama vile haisikii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, tunaposikia kilio sehemu fulani na hawa Wabunge, siyo kama wanasema ili kujifurahisha, hapana. Yanayotokea kule, sisi tunayajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo huyu mkulima wa pamba ana pamba nyumbani kwake, hajauza mpaka leo kwa sababu, ya bei ambayo inamnyonya mkulima huyu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri na Serikali, nilishasema mwanzo, kwamba, tusiwapuuze wananchi hawa, tuwaheshimu kwa sababu wao ndio

wanaotupigia kura, lakini na wao ni Watanzania na walipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, ni kuhusu hali ya chakula. Niliuliza swali humu ndani, na wewe bahati nzuri ukiwa Naibu Waziri, ulilijibu mwenyewe, kuhusu kusogeza ghala la chakula pale Bukwimba Stesheni. Chakula cha njaa unapokishushia Shinyanga, wananchi wa Mara, Kagera na Mwanza kwa ujumla, wanapata taabu sana kukifuata chakula. Lakini kwa sababu, miundombinu ya Bukwimba Stesheni inajitosheleza, tuamue ili tuwapunguzie gharama ya kwenda kukifuata chakula Shinyanga, Kituo kiwe Stesheni ya Bukwimba. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumewapunguzia gharama, na gharama ya chakula kile itapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni sukari. Sukari kwa sasa, imekuwa kama vile ni anasa.

(Hapa, kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kengele ya pili au ya kwanza?

MWENYEKITI: Ya kwanza.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sukari imekuwa ni anasa. Naomba sana Mheshimiwa, ule utaratibu unaofanyika, inawezekana kwa njia moja au nyingine unawanufaisha hawa wanunuzi au waagizaji wa sukari ambao ni wachache.

Leo kilo moja ya sukari ni Sh. 2,500/=, ni nani atakayemudu wakati bei ya pamba ya huyu mkulima, kilo moja ya pamba ni Sh. 660/=? Hivi huyu Msukuma, huyu mtu wa Kibondo atamudu kweli kwenda kununua sukari ya Sh. 2,500/= wakati yeye bei yake ya pamba ni Sh. 660/=? Naomba sana Mheshimiwa Waziri na Serikali, hili litazamwe vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nasisitiza sana suala la mizani. Kuna wizi mkubwa! Naomba Mheshimiwa Waziri awasiliane kama anaweza, najua ataweza tu; awasialiana na Waziri wa Viwanda na Biashara, Kitengo cha Mizani, kitakwambia ni kiasi gani cha mizani iliyokamatwa tangu mauzo mpaka leo, ni mizani mingi mno kwa ajili ya kuwaibia wakulima wa zao la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nitaunga mkono hoja baadaye. Ahsante. *(Makofi)*

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi nichangie Hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Nianze kwanza na mambo matatu ya msingi, yanayolihusu Jimbo la Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha ambao sasa unakwisha, ama mwaka wa kilimo, mwaka 2011, hali ya chakula katika Jimbo la Mbozi Magharibi, hususan Tarafa ya Kamsamba na Msangani, ni mbaya sana kuliko maelezo. Tarafa ya Kamsamba, ina Kata tano na Tarafa ya Msangano ina Kata mbili. Kwa hiyo, kuna jumla ya Kata saba ambazo

zina hali mbaya sana ya chakula katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ilitokana na nini? Ni kwamba, mwaka 2011 wananchi wa Mbozi Magharibi, ama Wilaya Mpya ya Momba, walipanda vizuri sana mazao yao, yakaota vizuri kabisa, lakini baadaye baada ya ule msimu wa kilimo, lilikuja jua la ajabu, yaani ukame ambao hatujawahi kuuona tangu miaka 50 tupate uhuru. Sasa ukame ule ulisababisha mazao yote yakauke. Katika Jimbo la Mbozi Magharibi, hususan katika maeneo hayo ya Tarafa ya Kamsamba na Msangano, kipindi kama hiki debe la mahindi huwa linanunuliwa kwa takribani Sh. 3,000/= ya Kitanzania, lakini sasa hivi bei inakwenda kuanzia Sh. 11,000/= mpaka Sh. 15,000/= kwa debe moja la mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya sana, wananchi wa Momba, hususan katika hayo maeneo na Wizara kwa ujumla, tunaomba angalau kwa wakati huu, mpeleke chakula cha msaada kwa wananchi wale ambao wanateseka na ni wananchi wa Tanzania hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hili, ningependa nizungumzie na nitaendelea kulirudia. Kazi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini ni nini? Kwa sababu, kama wangeweza kutabiri vizuri, wananchi wangepanda mazao yanayolingana na hali ya ukame, na hii hali ya njaa isingekuwepo kwa kiwango hiki kinachojitokeza. Ndiyo maana mimi mara zote nimekuwa nikisema sina imani kabisa na Kitengo cha

Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini. Ni waongo wa hali ya juu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema waongo kwa sababu, wanashindwa kuwa na tafsiri za uhakika za hali ya hewa. Ndiyo maana hata yaliyotokea haya ya meli ya *MV Skagit,* ni kwamba, moja ya utaratibu kabla ya meli kuanza kusafiri, huwa wanapata taarifa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa, kwamba: Je, hali ya bahari ni safi ama salama? Watu wa *MV Skagit,* wakaambiwa hali ya hewa ilikuwa ni safi na salama, wakaingia majini. Matokeo yake ndiyo haya yaliyotokea kwa wananchi. Kwa hiyo, wanapokwenda kuulizwa wanasema mkondo wa bahari wa nchi yetu ni *spontenious,* yaani unaweza tu ukabadilika wakati wowote. Sasa kama tunaweza tukawa na Mamlaka ya namna hii, maana yake tunakuwa hatuna Mamlaka ya msingi ambayo inaweza kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hali hii ndiyo ambayo ilisababisha wananchi wa Mbozi, hususan Mbozi Magharibi, Tarafa ya Kamsamba pamoja na Msamlam, ambao siku zote tumekuwa tukifuata utaratibu wa mvua za kila mwaka; hali hii matokeo yake yakawa ni hili lililojitokeza, kwamba umetokea ukame wa hali ya juu. Sasa leo Viongozi tunaanza kulalamikiwa kwamba, ni miongoni mwa watu ambao tumesababisha. Lakini yote ni kwa sababu taarifa zilizo sahihi hazitolewi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mamlaka ya Hali ya Hewa, ukiacha tu kubadilisha mfumo, lakini kuna haja sasa kwenye upande wa kilimo

ikawa inahusika kwa asilimia mia moja. Mifano mingine ni ile ya mwaka 2011, baada ya matukio. Maana ni kitu cha ajabu sana, hii Mamlaka yenyewe imekuwa ikitoa taarifa baada ya matukio. Mwaka 2011 baada ya mafuriko ya Kigogo pale Dar es Salaam, wakatoa taarifa kwamba, itakuja mvua ya hali ya juu, lakini mpaka leo, hata tone la mvua halikutokea ambalo lingeweza kuleta maafa. Ndiyo walichokifanya hata juzi na ndicho ambacho wataendelea kukifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunaendelea kulea mambo ambayo siku zote yataendelea kusababisha maafa kwa wananchi, mimi siwezi kuungana mkono hii hoja, kwa mantiki hiyo tu kwamba, kuna haja sasa tukapewa mfumo mzima wa Mamlaka ya Hali ya Hewa, inahusika wapi zaidi na jukumu lake ni lipi? Kama hawana vitendea kazi, basi, tuelezwe. Hakuna haja ya kuwa na Kitengo hicho nchini kwa sababu, matukio yamekuwa yakijitokeza na maafa, yataendelea kujitokeza na tutaendelea kutafuta mchawi ni nani, wakati mchawi wa kwanza anakuwa ana uwezo wa kufahamika kiurahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo nafikiri lieleweke wazi. Naiomba Wizara kwamba ipeleke chakula katika hizo Tarafa nilizozitaja na maeneo mengine ya Jimbo la Mbozi Magharibi. Wananchi watawashukuru sana na wamekuwa wakilia, machozi yao naomba sasa yawafikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hiyo hiyo, katika Jimbo la Mbozi Magharibi, kuna miradi miwili ya umwagiliaji. Kuna Mradi wa Yendwe pamoja na

Ming'ong'o Chitete na lyendwe ipo katika Kata ya Kapere. Sasa ni karibu miaka mitano miradi hii haikamiliki. Lakini ukisoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwanza haipo na inaonekana ni miradi ambayo imekamilika. Lakini ni hovyo haijawahi kutokea. Kwa hiyo, ningeiomba Wizara iende katika Jimbo la Mbozi Magharibi, Wilaya Mpya ya Momba, ikaipitie hii miradi ione uovu ambao umewahi kutokea, yaani ni mfumo hovyo kabisa na wala siyo kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokwenda kwenye mradi, unakutana na kibao kimeandikwa "Kilimo Kwanza", kuwezesha sijui Kilimo Kwanza, lakini ukienda kwenye mradi wenyewe hauendani na Kilimo Kwanza, unaendana na Kilimo mwisho kabisa. Kwa hiyo, ningependa mwende mkafanye tathmini. Msiwe ni watu wa kupokea tu taarifa kutoka kwa Viongozi wa Halmashauri za Wilaya na Mikoa, lakini mnashindwa kuzifanyia kazi. Nendeni mkajionee, mwone miradi ya maendeleo hususan ya umwagiliaji, kama imetekelezeka kwa kiwango ambacho kilikuwa kimepangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kulimaliza hilo, sasa niende katika suala la tatu ambalo sisi katika Mkoa mzima wa Mbeya, hususan katika masuala ya Vocha za Pembejeo, maana sisi ndio kitu ambacho tunakitegemea. Hili linasikitisha sana. Mwaka wa 2011 mbolea katika Mkoa wa Mbeya na Jimbo la Mbozi kwa ujumla, zilifika mwezi wa Pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunasema Kilimo Kwanza, halafu unaleta mbolea mwezi wa Pili, maana yake ni kwamba, unakubali tunaua kilimo, ila kwa upande wa pili, tunawadanganya wananchi kwamba tunawatetea kwenye Kilimo Kwanza, lakini huu ni uwongo wa hali ya juu. Msimu wa Kilimo katika Mkoa wa Mbeya, ukichelewa kulima kufikia tarehe 15 mwezi Desemba, maana yake ndiyo msimu wa kilimo unakuwa umekwisha. Mkulima yeyote anayelima baada ya terehe 15 Desemba, maana yake huyo sio Mkulima. Sasa unapoleta Vocha za Pembejeo baada ya terehe 15 Desemba, maana yake huwatakii mema wananchi wa Mkoa wa Mbeya na maeneo yote yanayohusika na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa kwanza, hizi Vocha zisiendelee kuwa sanaa ambayo imeendelea kutokea. Lakini jambo la pili, hususan kwenye suala la mbolea, bei ni kubwa ukilinganisha na nchi nyingine za jirani, hususan kama Malawi. Malawi, wanauza kama mwaka 2010, ilikuwa ni Kwacha 500 ambayo ni sawasawa na Sh. 4,000/= ya Kitanzania. Malawi, wanachukua kiwanda kimoja tunakochukua sisi kama Taifa, Japan, pamoja na Zambia. Sasa unajiuliza, nchi ndogo kama hizi zinaweza ku-*accomodate* bei ya mbolea kwa wananchi wake na watu wakafaidika na kilimo kikawa kikubwa. Ndio maana nchi ya Malawi mpaka mwaka 2010, ilikuwa ni miongoni mwa nchi za Afrika zenye uzalishaji mkubwa wa mahindi. Hiyo kila mtu anafahamu. Lakini sisi ni nchi yenye ardhi kubwa, wenye hali ya hewa inayoruhusu, hili suala tunashindwa kulifanikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya mambo yaeleweke. Mengine yaliyozungumzwa masuala ya rushwa, masuala ya wananchi kupewa fedha badala ya vocha za mbolea, yapo na yataendelea kuwepo. Kwa hiyo, yote yafanyiwe kazi ili wananchi waweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni hoja ya Bajeti kwa ujumla. Fedha zilizotengwa ni ndogo, tuwe wakweli. Shilingi bilioni 14 fedha za ndani, Shilingi bilioni 52 fedha za nje, kama alivyozungumza Mheshimiwa Ole-Sendeka, siyo suala la kulidharau kama watu ambao hatuwezi kukaa na kufikiri mambo ya msingi. Ni suala la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo maana siku zote tumekuwa tukiwalaumu; jamani, mnaua chama chenu wenyewe! Mwaka 2015 sijui mtajibu kwa nani kwamba, ni nani alikuwa mchawi wa kuua Chama Cha Mapinduzi, wakati ninyi wenyewe ndio mnaoua. Kwa sababu mambo mengine yanaonekana! Ni sawasawa na kusema, mtu unaendesha gari, kama hujawahi kufanya *service,* mtu akikwambia bwana fanya *service,* gari lako litapata ajali, utamwambia wewe mpuuzi bwana, miaka yote nimeendesha gari sijawahi kufanya *service.* Ni sawasawa na ninyi na ndiyo maana tukiwaambia mnaelekea kushindwa chaguzi zinazokuja, hamwamini kwa sababu, hamjawahi kushindwa. Lakini sisi tunaona mnakwenda kushindwa. Mambo haya hatuwezi kuendelea kuwalea! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo. Ni tatizo kwa uongozi mzima wa Serikali pamoja na Watendaji wake. Hawana mpango kazi, hawana malengo, hawana mikakati, hawana takwimu, na hawajui matatizo kwa undani ya Watanzania yanawakabili vipi. Sasa hili ndio jukumu ambalo limekuwa likiwakabili. Lakini tunapowaambia kwa nia njema, hamtaki kulifuata na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, aliyetujaalia tuko humu ndani. Pia, namshukuru Mwenyezi Mungu, pamoja na malumbano yote, lakini hatujashikana mkononi, na anafahamu kinachofanyika ni nini na tunaendeleza nini katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba nichukue nafasi hii kuwatakia kila la kheri Waislamu wote ambao wanaanza Mfungo wa Ramadhan. Inshallah, Mwenyezi Mungu, ajaalie Ramadhan iwe njema na atujalie neema na amani nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, naomba pia nichukue nafasi hii kuiomba Serikali, iweze kuzungumza na wafanyabiashara wakubwa wanaouza bidhaa za sukari, mchele, unga, na nyinginezo, waweze kupunguza angalau kwa kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, wananchi

wapate nafuu ya bei, ili waweze kufunga bila kuwa na mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba niingie kwenye kuchangia hoja ya Wizara hii, na ninaomba nizungumzie zaidi katika Mkoa wangu wa Pwani. Nitakuwa mchache wa fadhila kama sijamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa rehema alizotupa watu wa Mkoa wa Pwani, kwa maana ya ardhi nzuri, yenye rutuba, tuna mito mikubwa yenye majina na inayoweza kunywesha maji hata watu wa nje ya Mkoa wake, japokuwa kwenye Mkoa wenyewe wengine hawayapati hayo maji. Lakini vilevile kuna bonde au mabonde mengi yenye rutuba, kungeweza kufanyika kilimo cha umwagiliaji. Ama kwa kutumia vijana wetu, ama kwa kutumia vikundi vya akina mama waliokuwepo katika Mkoa huo. Tuna mabonde mazuri sana Wilaya ya Bagamoyo. Tuna mabonde mazuri sana Wilaya ya Kisarawe, tuna mabonde mazuri sana Wilaya ya Kibaha Mjini na Vijijini, halikadhalika, Mkuranga na Mafia pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza, bajeti yake ya mwaka 2011, Serikali, hata mstari mmoja, haikugusia suala la umwagiliaji katika Mkoa huu wa Pwani, iwe Rufiji, iwe Kisarawe kwenye Bonde la Mto Ruvu, iwe Kibaha Vijijini kwenye Bonde la Mto Ruvu kule Mongomole na Kwala, iwe Mafia: Je, kweli, tunazungumzia Kilimo Kwanza? Je, kweli, tunataka kuinua kipato cha mwananchi wa Mkoa wa Pwani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Pwani, wengi wao tunatumia Kilimo cha Jembe la Mkono. Lakini ninaiomba Serikali ituambie imeweka mkakati gani katika kuwasaidia vijana ambao hawana kazi, hawana ajira, hawana Hati ya Kimila wala ile ya Serikali, ya Kumiliki Ardhi? Halikadhalika na wanawake hivyo hivyo. Je, Mheshimiwa Waziri, atakaposimama aniambie niwaletee vikundi vingapi kutoka katika Wilaya zilizoko Mkoa wa Pwani, ambao watapewa matrekta kwa mkopo, wakishalima walete fedha kidogo kidogo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo kwa sababu Mkuu wetu wa Mkoa Mheshimiwa Mwamtumu Mahiza, kwa kushirikiana na Wakuu wa Wilaya wa Mkoa wa Pwani, pamoja na Wakurugenzi, waliendesha mafunzo ya vijana katika fani mbalimbali ikiwemo ya kilimo. Tena, ningewashauri Waheshimiwa Wabunge humu ndani, wajitokeze waje wajifunze kwa kupitia kwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, kazi imefanyika nzuri. Lakini tumewapa mafunzo. Je, tutawawezesha ili waweze kulima? Naomba kilio hiki nikilete kwenye Wizara, kwenye Serikali, ili tuone itatusaidiaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu tunajivuna, tuna mazao mengi tunayolima kule Pwani; kuna korosho, kuna mpunga, halikadhalika tunalima na kilimo cha minazi. Lakini korosho hizo ninazosema, inatia uchungu, mpaka leo hii ziko kwenye maghala, na hizo ni za mwaka uliokwisha. Hazijanunuliwa, ziko pale, tumeletewa mnunuzi, lakini huyo mnunuzi mpaka leo hayupo. Watoto wa mjini wanasema kaingia mitini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pembejeo zimeanza kutoka, sisi hazijatufikia. Zao ulilovuna mwaka uliopita liko kwenye maghala halijauzwa, mkulima hajapata pesa zake zote, pembejeo haijafika, mikorosho imeshaanza kutoa maua; mkulima huyu tunamtakia nini? Kweli anaweza akapata pesa kutokana na kilimo? Naomba nipatiwe majibu, kasoro zile mnatusaidiaje kama Serikali ili ziuzwe? Halikadhalika, pembejeo ya salfa, itatufikia lini wakulima wa korosho wa Mkoa wa Pwani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la mihogo. Hakuna asiyejua kwamba, zao la muhogo linatoka Mkoa wa Pwani na bahati nzuri mbegu bora inatoka Wilaya ya Mkuranga. Lakini mpaka leo hii, sijui wakulima wangapi ambao wameweza kufaidika na sifa tunazopewa kwamba, zao la muhogo linauzwa mpaka nje ya nchi. Wakulima, wamejitahidi kwenye vikundi vyao, wanalima, wanavuna, wanasaga wenyewe unga na kujitafutia masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, kwa kuwa mpaka sasa haijaweza kuweka kiwanda cha kuzalisha unga wa muhogo kwa Mkoa wa Pwani, basi iwafikirie wale wakulima wadogo wadogo, waweke kwenye vikundi vijana, wanawake au wowote wale wanaoweza kusema kwamba, sisi tumeunda kikundi chetu; wawasaidie mashine za kuweza kuzalisha unga, halafu soko siyo tatizo. Hakuna asiyekula ugali wa muhogo humu ndani? Wote tunajua faida za muhogo, kuanzia mzizi mpaka jani lake. Naomba Serikali, itusaidie kutuambia ni vipi imejipanga kusaidia kuweza

kupata kiwanda au hao wakulima wadogo wadogo wa mazao ya muhogo, waweze kusaidiwa hivyo viwanda vidogo vidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nije kwenye zao la mnazi. Nina masikitiko makubwa sana kwa sababu, kwenye bajeti ya mwaka 2011 nilizungumzia zao la mnazi na nikaeleza faida za mnazi. Tunasikia tunavyohangaika kutokana na hali ya hewa ya nchi yetu, lakini mnazi ukishaanza kuzaa unavuna mara nne; inyeshe, isinyeshe, na jangusho moja unapata pesa kibao kwa sababu kila mnazi mmoja kama una mingi, unaangusha nazi nne nne na kama una minazi mia maana yake una nazi 400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa zao lile kwa bahati mbaya sana, leo narudia tena na ninarudia kwa uchungu kwa sababu mimi nimezaliwa kijijini na nimekuzwa na zao la nazi. Jangusho la nazi ndiyo lililonisomesha mimi. Kwa hiyo, naomba Serikali iniambie, kuna Kituo cha Utafiti, nimesoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, sikuona hata sehemu moja ambayo imetengewa fedha Kituo cha Utafiti wa Mnazi Mikocheni. Minazi imepata athari, wote tunaona tukipita barabarani, imekufa. Mheshimiwa Waziri ambaye sasa ni Waziri, katika bajeti iliyopita alikuwa Naibu Waziri, aliniahidi kwamba ataongea au atafuatilia suala hili ili tuweze kuona utafiti umegundua nini. Nakubaliana naye kwamba ile minazi ya muda mfupi ambayo ilikuwa imeletwa haikuwa na maana kwetu, kwani imeleta madhara makubwa sana, haikuweza kuendelea, lakini kuna ile minazi inayoitwa *East African Tall* inakaa zaidi ya miaka mia na ndiyo

iliyotusomesha baadhi yetu sisi humu ndani. Sasa utafiti ule umefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali imeamua kuliondoa hili zao la mnazi katika mazao ya biashara, basi ituambie inatuletea zao gani mbadala kwa Mkoa wa Pwani? Kwa sababu kwenye maeneo mengine huwezi kulima mchungwa wala huwezi kulima mihogo. Kwa mfano, katika Wilaya ya Mkuranga Kata ya Shungubweni huwezi kulima zao lingine lolote zaidi ya mnazi. Sasa naomba Serikali iniambie: Je watu wale watafaidika vipi na zao mbadala litakaloletwa kama mmeamua kulitoa zao la Mnazi? Kwa sababu miaka ya nyuma, zao la mnazi kulikuwa na viwanda vinakamua na yale mafuta ni mazuri hayana *cholesterol*. Sasa wote tulime alizeti, inawezekana? Mpaka tujifunze faida ya zao la alizeti siyo leo. Sisi tumeshazoea zao la mnazi, kwa hiyo, naomba Serikali inipatie majibu katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Pwani kwa asili hatuna migogoro ya ardhi, hatugombanii ardhi, Mkoa wa Pwani mwanamke anahodhi eneo lake na mwanaume anahodhi eneo lake. Watu wanakwenda kulima, leo wanavuna kwa baba, kesho kwa mama, keshokutwa kwa dada na kwa shangazi, lakini utamaduni huo kwa sasa hivi kwa Mkoa wetu wa Pwani haupo tena, na hapo kwa sababu gani? Wameletwa wafugaji. Jamani Mwenyezi Mungu hakufanya makosa kuwaweka wafugaji kwao na wakulima kwao. Tusichanganye mambo!

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Vullu, ahsante.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo ya kwanza hiyo?

MWENYEKITI: Ni ya pili, umezungumzia sana mihogo, hiyo ni kengele ya pili. *(Kicheko)*

Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Mrema, na Mheshimiwa Cheyo ajiandae.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. AGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Chiza kwamba alipokuwa Naibu Waziri kwenye Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, nimeshirikiana naye vizuri na amenisaidia mambo mengi katika Jimbo langu. Nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitayasema haya. Kuna mfereji wa Mchomba nilimwendea na kumwomba kuwa wananchi wangu wanahitaji maji kwa ajili ya umwagiliaji, nilikuwa nahitaji karibu Shilingi milioni 300, anilinifanyia mpango akaandika andiko kwenda

Japan na ule mfereji upate msaada. Sasa mtu wa namna hiyo mimi namwona ni mtu mzuri. *(Makofi)*

Pili, alinisaidia barabara ya Mawala ikatengenezwa vizuri ili wakulima waweze kuchukua mpunga wao shambani na kuufikisha sokoni. Lingine pia ambalo amenifanyia wakati huo akiwa Naibu Waziri ni Mfuko wa *DIDF* wa karibu Shilingi milioni 140. Huu Mfuko ulikuja na hizi fedha kwa ajili ya *scheme* ya umwagiliaji maji Kahe. Kwa hiyo, nilimjua Chiza kwa hayo mazuri na makubwa aliyonifanyia katika Jimbo langu. *(Makofi)*

La tatu, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete na nimpongeze Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo wamenisaidia kujenga miundombinu ya kuwasaidia wakulima wa Jimbo la Vunjo. Jambo ambalo limefanyika kubwa na ambalo nimemshirikisha Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, ni hili soko la Kimataifa ambalo wanaanzisha Njiapanda. Wakulima wangu wa ndizi na mboga walikuwa hawajui wauze wapi mazao yao, walikuwa wanapata shida, lakini Mheshimiwa Rais alikuja Njiapanda alitembelea na akaona soko lile ni zuri, lijengwe na liwe kubwa na liwe ni Soko la Ndizi na Mboga. Kwa hiyo, wananchi wote wa Vunjo, Kilimanjaro na Moshi Vijijini na watu wa Kenya, Uganda, Somalia au Sudani wanaotaka ndizi waje Njiapanda Himo.

La nne, soko la Lokolova, Waziri Mkuu alikuwa afike pale wakati wa ziara yake ya Angola, ikafa! Lakini juzi

nimeuliza swali katika Bunge na Serikali imeonyesha nia kwamba soko lile la kimataifa litakuwa linachukua mahindi kutoka Mbeya, Iringa, Rukwa na Songea na watu wanaotaka mahindi na wanaotaka kuuza nchi za nje na wale wa nchi za nje wanaotaka mahidi au nafaka watakuja pale.

Kwa hiyo, huko nyuma tulikuwa tunahangaika, wakulima wanalima mazao, lakini hayana soko. Kwa hiyo, ilikuwa tunapita kwenye vichochoro kwenda Kenya ili kutafuta masoko. Lakini hilo la kwanza ambalo nimefanikiwa, na wananchi wa Vunjo wamefanikiwa sasa nisipowashukuru nitakuwa sina shukrani na sina heshima na siku nyingine wataniangalia kwa jicho la husuda. *(Makofi)*

La tano, hata kutengeneza barabara za Vunjo wananchi wanajua Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete aliahidi barabara ya Marangu Mtoni kwenda Kilema Kaskazini, kwenda Kirua Vunjo Magharibi mpaka Kawawa anapotoka Mheshimiwa Mbatia, huko ni vijijini lakini aliahidi barabara ya lami na sasa hivi ukienda Marangu Mtoni *caterpillar* ipo inafanya kazi nzuri, tunawekewa lami vijijini kwa ajili ya kuweza kusafirisha zao la kahawa kwenda sokoni. Siyo barabara moja tu, hata barabara ya Kilema, Pofu kwenda Kilema Hospitali inajengwa na inawekwa changarawe ili kusafirisha mazao, kwani watu walikuwa wanahangaika, barabara ilikuwa haipitiki. Hata barabara nyingine ya Uchira kwenda Kisomachi mpaka kwa Laria ilikuwa haipitiki, lakini sasa hivi magreda yapo pale ili kurahisisha uzalishaji wa kahawa na ili kahawa iweze kwenda sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu, Mheshimiwa Rais alipokuja Himo alijua watu wakinywa maji yasiyokuwa salama hawawezi kuzalisha kahawa wala hawawezi kulima, lakini aliahidi Shilingi milioni 150 katika Jimbo langu, nikapata *advance* ya shilingi milioni 50. Siku moja Mheshimiwa Rais alitembelea Himo akaangalia lile soko, nikamwuliza ile fedha iliyobaki, Shilingi milioni 100 vipi? Jana nilikuwa naambiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji kwamba ile Shilingi milioni 100 imeshapatikana na wananchi wa Himo watasambaziwa maji. Mungu anipe nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Himo kuna Hospitali ya Wilaya. Zamani Vunjo ilikuwa tukiugua ni mpaka twende Mawenzi, lakini sasa naweza kusema Mawenzi *bye bye,* kwani hospitali yetu ni Himo. Sasa utaona hiyo ni miundombinu inayotengenezwa ili kumwinua mkulima.

Sasa Mheshimiwa Waziri ninakuomba uangalie sana zao la kahawa, kwani bei yake imefika Sh. 10,200/= kwenye Soko la Dunia kutokana na kwamba watu wengi wamejitokeza duniani wanakunywa Kahawa na wale waliokuwa na mashamba yao, wakulima wa Kahawa katika maeneo mengine imeharibika na tunaambiwa kwamba bei ya kahawa itaendelea kupanda Shilingi 10,200/= kwa miaka 20 ijayo. Sasa tunachotaka kuomba ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mkulima aweze kupata hiyo bei, kwanza tunaomba lile deni Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais mngewasaidia marafiki zangu Wamasai kwenye mdororo wa uchumi.

Ng'ombe zimekufa wakati wa kiangazi, wamepata fidia na wamefurahi sana. Marafiki zangu, wakulima wa pamba wakati wa mdororo wa uchumi mwaka 2008/2009 mliwafidia. Sasa sisi watu wa Kilimanjaro, kwenye *KNCU* tulikuwa tumekopa Shilingi bilioni 1.3 kutoka *CRDB*, sasa lile deni tunatakiwa tulilipe, lakini tulipata hasara katika kuuza kahawa. Kwa hiyo, ni zamu yetu na sisi mtusaidie jamani, msiseme Kilimanjaro tumeendelea, siyo kweli! Tuna matatizo makubwa kama waliyonayo watu wengine wa nchi hii.

La pili, tuliomba mwangalie bei ya kahawa. Nimeona hii Bodi ya Kahawa mliyoiteua juzi imeweka kwenye makisio yake kwamba itapata Sh. 9/= kwa kila kilo ya mkulima, wakati huo huo *KNCU* ilikuwa inakata Sh. 40/= mpaka Sh. 50/= kwa kilo. Sasa tuangalie makato haya, pengine ndiyo hayo hayo yanayonung'unikiwa na marafiki zangu wa pamba. Tuangalie hizi fedha zote zinazokatwa zinakwenda kumsaidia mkulima? Maana wangekuwa hata wanapekeleka *TAKRI* na *TAKRI* ndiyo wanazalisha kahawa, tena kahawa bora na ya kisasa inayozaa kwa miaka miwili unaweza ukavuna, tena wanazalisha kahawa ambayo yale magonjwa sugu yaliyokuwa yanatusumbua sisi mpaka tukakata tamaa na zao la kahawa. Kahawa hii mpya haina magonjwa sugu, lakini wananchi wa Vunjo wanataka kahawa na wameandaa mashamba. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)

MHE. DKT. AGUSTINE L. MREMA: Ni kengele ya pili?

MWENYEKITI: Ndiyo! Nakushukuru sana Dkt. Mrema.

MHE. DKT. AGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mchango huo nilioutoa, naomba uzingatiwe. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunashukuru. Mheshimiwa Cheyo!

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Baada ya kumsikia Mheshimiwa Mrema kwa mazuri yote aliyofanyiwa, nashangaa kwa nini Mheshimiwa Waziri hata kwa mara yake ya kwanza kuweka hotuba yake katika Bunge hili ameshindwa hata kuwakumbuka wakulima wa pamba milioni 16, *I don't understand!*

Nimesoma hapa kuna *paragraph* moja tu, Shilingi milioni 16 ndiyo wanaleta katika nchi hii. Watu milioni 16 ndiyo ng'ombe zao na pamba yao iliyosaidia kuleta uhuru wa nchi hii, lakini kwa kitabu hiki hawana thamani. Nimeshangaa sana na kwa mara ya kwanza nitaanza kwa kusema Mheshimiwa nakuheshimu sana, lakini kwa yale nitakayosema siungi mkono hotuba hii. *(Makofi)*

Kwanza niseme neno la utangulizi kwamba Soko la Pamba limechezewa miaka yote. Hata ukisoma hapa tunaanza na takwimu ambayo siyo sawa. Tunasema asilimia 70 ya zao la pamba inategemea soko la nje, siyo kweli! Asilimia 66 ya zao la pamba ni mbegu ambayo inaliwa hapa hapa nchini na kama ikiweza kupata *support* ya Serikali itaweza ku-*support* bei ambayo tunaitegemea kutoka nje. Ni asilimia 33 tu

ambayo ndiyo nyuzi inayokwenda nje na katika hiyo umesema asilimia 30 ndiyo tunaitumia hapa nchini. Kwa hiyo, tunaanzia *right from the beginning* tupo *wrong*!

Nimefurahishwa na kitu kimoja tu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Alipokuwa anamalizia anasema kilimo ni biashara. Kilimo ni biashara na ninakubaliana naye na kilimo cha pamba ni biashara kweli kweli! Kwa misingi hiyo hiyo Serikali imeshindwa kuwaambia wanunuzi wa pamba wanunue kwa buku moja au Sh. 1,000/= kwa sababu wataingia hasara. Lakini leo mkulima pia anatumia Sh. 800/= kwa kilo moja na leo anaambiwa auze kwa Sh. 660/= apoteze Sh. 120/= lakini mwenye pesa asipoteze hata senti moja, angalau atengeneze faida ya 7%. Ukweli upo wapi na haki iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchawi ni Bodi. Mambo yote hayo, na mimi nimesikitika sana, kwani tumefanya vikao na Wizara hii zaidi ya mara tano na tukisisitiza kuwa mchawi ni Bodi na kwenye Bodi kuna *Director* na *Director* yule Mheshimiwa Waziri ameniambia zaidi ya mara tano kwamba nimemsimamisha, kumbe hajamsimamisha!

Nataka leo uweke mbele ya Meza ya Mheshimiwa Spika barua ya kumsimamisha huyo mtu. Tumekutana tarehe 5 Mei, Mwanza akajifanya yeye sio *Director* ni mwezeshaji, lakini leo nina barua ya tarehe 16 Julai ameandika *Director* wa Bodi ya Pamba na sisi tumesema kwamba ni vizuri huyu *Director* akaachwa ili aweze kuchunguzwa kwa mambo mbalimbali pamoja

na kuleta ubaguzi katika zao au biashara ya pamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumegundua kwamba yeye anataka watu 10 ndiyo wawe *ginners* na anawajua yeye mwenyewe, na ndiyo maana tangu mwezi Januari ameweka *list* na *list* hiyo nimeambiwa eti hao Wanyantuzu, yaani watu wa Bariadi wanaingia mno kwenye biashara ya pamba. Tumefika huko? Nchi ya Nyerere tunaulizana wewe ni kabila gani? Nchi ya Nyerere tunaambiana wewe ni msukuma wa Mweri au Kusini au Msukuma wa Ntuzu? Tukasema achunguzwe kwa hili na hapa nina barua ambayo umeandikiwa wewe, baadhi ya Makampuni ambayo ni ya watu wanatoka Bariadi ambao wananyimwa leseni kwa kisingizio eti *they are black listed* na *Internationa Cotton Association,* yaani kwamba *International Cotton* haitawaruhusu kupeleka pamba yao Ulaya. Lakini hawa ni *ginners* biashara yao ni pamoja na kupata mbegu, pia wanaweza wakapata *lint* wakaiuza kwa Makampuni ya hapa hapa ndani na hakuna hata sababu yoyote kwamba hatujaweka katika sheria kwamba ukipata matatizo nje, basi nchini hutaweza kufanya biashara ya *ginners*, ubaguzi huo! Yapo hapa na umeandikiwa.

Pia ninaweza nikasema machache kwamba *KBL Enterprises, Chisano Cotton Ginners, Jambo Oil Meal, Vitrus Oil Limited, Badugu Gining Company etc.* Wote hawa ni wa Bariadi na sisi tunasema hawa wakiwekeza Bariadi *ginneries* zao ndiyo watoto wetu watapata kazi na bei ndiyo itakuwa nzuri kwa sababu siyo lazima uitoe pamba uipeleke Mwanza kwa kilomita 200 na

ushee. Ukiwekeza pale ndiyo kusema watu watafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa watu wanakwenda Mahakamani kuipeleka Bodi na huyu mtu ambaye sijui anakingwa na nani mwenye kinga kubwa, Mheshimiwa Waziri tuambie ni nani anayemkinga huyu? Ni bwana mkubwa gani huyo? Mimi siamini kwamba ni Mheshimiwa Rais wa Taifa hili; ni nani? Tuambie! Mimi nilikuwa nafikiri hawezi kuwa Katibu Mkuu, maana yake Katibu Mkuu ni mtu anayependa sana dini. Ni nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema siungi mkono. Ninaitaka hiyo barua. Mheshimiwa Waziri ameeleza kila mahali kwamba, kilimo cha mkataba ndiyo kinaleta matatizo katika Taifa hili, na mimi leo nasema kwamba, wale wote waliosaini mikataba walifanya hivyo wakati bei ikiwa Sh.1,000/=. Huwezi leo tena mkataba umesainiwa, eti ni wa upande mmoja tu, na mambo yenyewe ni Sh. 4,500/= kwa hekta moja ndiyo wanakupa ambayo ni pembejeo, na unafungwa kwa mwaka mzima kwamba, ni lazima umuuzie mtu mmoja kwa bei anayotaka yeye. Wakati walipokuwa wanasaini mikataba ile, bei ya pamba ilikuwa Sh. 1,000/=. Mimi niko tayari kujitolea fedha wakulima twende Mahakamani tuwashitaki mliosaini nao mikataba hii ili wawalipe Sh. 1,000/= kwa sababu mkataba hauwezi kuwa wa mkono mmoja (upande mmoja). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimemwambia Mheshimiwa Waziri aache haya mawazo ya kutoka nje,

kuna nyingine ameishukuru hapa sijui *Gatsby Trust*, hawa ndiyo wanaoleta matatizo katika zao la pamba. Mtu ana mawazo kutoka *London* anataka kuja kututengeneza au kutu-*organise* anavyotaka yeye. Haya mawazo na sisi hapa ni watu ambao tumesoma, mimi *I declare my interest, I'm textile technologist,* nimesoma *Leeds University, I know cotton*. Kuletewa mawazo ovyo ovyo tu kutoka nje na bila kujua kwamba pamba ndiyo msingi wa maisha wa watu milioni 16, unasema ni lazima kila mmoja asaini mkataba. Mkataba wenyewe ni wa mkono mmoja. Mheshimiwa Waziri angalia hili jambo, unatumaliza sisi Wasukuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei inaharibika kwa kuletewa mambo ya makato kila upande, *CDTF*. Serikali imesema itatoa pembejeo kwa nusu bei.

(Hapa kengele ya kwanza ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji unakaribia kwisha)

MHE. JOHN M. CHEYO: Hiyo ni kengele ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu pamoja na bei kuwa mbaya tulikwenda mpaka kwa Mheshimiwa Rais, Wabunge wa Kanda inayolima pamba, tukamwomba Mheshimiwa Rais angalau hebu tupunguze hizi *CDTF,* imeletwa Sh. 40/=, Sh. 20/= wanasema eti mkulima atatoa. Eti Sh. 20/= atatoa mtu anayenunua, ni uongo! Sh. 20/= hii bado inaangaliwa katika bei inayotolewa kwa mkulima. Sh. 40/= kwa zao ambalo mmetwambia mwaka huu litakuwa karibu kilo milioni 355, nikifanya hesabu za haraka haraka ni sawa

sawa na Shilingi bilioni 14 na ushee. Hizo Shilingi bilioni 14 unamwondoshea mkulima ambaye huwezi kumpa bei ya Sh. 1000/=. Bado unatumia sheria kumwondolea Shilingi bilioni 14. Jamani, hatuna huruma! Halafu unapeleka kwenye Mfuko ambao wala hakuna mtu anayeuangalia? Mfuko huo tangu uanzishwe haujaweza kukaguliwa na mtu, na hizi ni *public finance*. Hii ni fedha ya umma, inapelekwa tu inawekwa ndani ya chungu, watu wanagawana, wanapata magari, wanapeana posho, watu wakitaka kusafiri wanakwenda wanachota. Serikali gani hii inaangalia wanyonge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CDTF* hii tunashauri mwaka huu Sh. 40/= irudishwe kwa wakulima. Tunashauri hizi *CDTF* na kwa mazao mengine, hiyo sheria tuliyotunga iangaliwe upya. Kumbe tumetengeneza jalala la kutupa fedha ya wanyonge! Mheshimiwa angalia hilo. Mimi bado nawaunga mkono wakulima wote ambao wamesema, *no book, no cotton*. Kweli kama hakuna Sh. 1,000/= hakuna pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichonisikitisha ni kwamba, jana nilizungumza na Mheshimiwa Waziri akasema atatangaza soko huria, mbona hajatangaza? *(Makofi)*

(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cheyo, nakushukuru. Sasa mchangiaji wetu ni Mheshimiwa Ismail Aden Rage, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephati Kandege na Mheshimiwa Maria Hewa ajiandae.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha leo kuwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo na kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ila nimesikitika sana na hotuba yake. Mkoa wangu wa Tabora ameusahau kabisa. Nasikitika sana kwa sababu Kaka yangu Mheshimiwa Waziri anaujua vizuri Mkoa wa Tabora. Tabora ni *semi arid* na katika taarifa ambayo aliandika mwenyewe akiwa anafanya kazi Tabora akiwa *engineer* alisema kwamba, uwezekano wa kupata maji kutoka chini ni mgumu, kwa hiyo, mnahitaji kuwa na mabwawa mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na bwawa limetengwa pale Inara kwa Sh. 1,000/=, Sh. 700,000/=, lakini katika bajeti ya mwaka 2011/2012 ikatengwa Shilingi milioni 686, lakini jambo la kushangaza zilipelekwa Shilingi milioni 280 tu. Hivi sasa huo mradi umesimama. Jamani hizi ni fedha za Serikali, hamwezi kuwa mnatenga fedha halafu hazipelekwi! Tabora huwezi kulima mazao ya chakula kwa kutegemea mvua peke yake, haiwezekani. Lakini ardhi yake ni *so fertile* na sehemu kubwa ni *virgin*. Tunahitaji kuwa na mabwawa, lakini jambo la kusikitisha, Serikali bado

inaelekeza nguvu zake nyingi kwenye Mikoa ambayo ina mvua nyingi. Tabora inasahauliwa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Tabora wana masikitiko makubwa sana jinsi Serikali inavyodharau na kutokujali maendeleo ya Tabora. Tangu tupate uhuru mpaka leo maendeleo yake yanasuasua, hakuna kitu chochote! *(Makofi)*

Tulikuwa na kiwanda cha kutengeneza juisi na *slice* za embe pale Urambo, lakini nashangaa kile kiwanda kilikufa kikafungwa. Sasa ukifika, kuna majani tu pale. Mkoa wa Tabora tulikuwa tunaongoza kwa kuuza karanga, lakini wapi sasa hivi? Hakuna anayejali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri nitakuomba sana ujaribu, ikiwezekana uangalie jinsi ya kuongeza fedha katika mabwawa. Nitakupa mifano michache tu ya mabwawa katika Mkoa wangu wa Tabora. Kuna bwawa la Usoke pale mlimani ambalo lina hekta karibuni 214, tuta limekamilika lakini fedha hakuna. Kuna bwawa lingine la Kahama Haranga – Nzega, Uliyanyama – Sikonge na Mwamapuli. Kuna bwawa lingine Chuma cha Nkola – Igunga huko, kuna lingine la Igurubi mahali ambapo Mbunge wa Igunga alipata kura nyingi sana pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora tuna matatizo mengi sana, lakini nina imani kabisa *engineer* huyu ni mmoja kati ya watu waungwana sana. Halafu nina bahati, mimi ni *chairman* wake, huyu ni mwanachama wa klabu ya Simba hawezi kuniangusha hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tabora ndiyo unaoongoza katika uzalishaji wa asali na nta hapa nchini. Uzalishaji huo sasa umefikia takribani tani 13,500. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, zao hili analipigia debe sana. Kilio cha watu wa Tabora, hawana kiwanda sasa hivi. Zamani pale Wamishionari wa Kipalapala walikuwa wanatengeneza asali nzuri, ilikuwa inaitwa *queen honey* ambayo ilikuwa safi sana. Lakini kiwanda kile kilikufa. Kwa hiyo, nina imani kabisa Mheshimiwa Waziri anaweza akaangalia na kuona atatusaidia vipi Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliongea awali, tulikuwa na kiwanda cha embe pale Urambo. Mkoa wa Tabora una takribani miembe isiyopungua Sh. 150,000/=, inatosheleza kujenga kiwanda cha embe pale, lakini mpaka leo ukiendesha gari kutoka Bukene mpaka Mwambali unakata kushoto kuelekea Tabora Mjini kuna miembe, ukienda kwa wenye nyumba ukaomba embe moja wanakwambia, baba, chukua lote hilo limti kama unaweza kwa sababu yanaanguka chini inakuwa kero kwa wanachi kwa sababu hawajui mahali pa kupeleka hizo embe. Iko haja ya kufikiria kusaidia Mkoa wetu, maana yake umepata matatizo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuongea juu ya suala la tumbaku. Tabora tunazalisha tumbaku ukichanganya na Mikoa ya Katavi na Kigoma ni asilimia 85. Lakini jambo la kushangaza mpaka leo tumeshindwa kuwekewa kiwanda cha kusindika tumbaku. Wakati ukisoma Tovuti ya *Bank of Tanzania (BOT)* inaonesha kwamba, mpaka jana zao

linaloongoza kwa kuingiza fedha za kigeni nchini Tanzania ni tumbaku, lakini wakulima hawasaidiwi. Kaka yangu Mheshimiwa Lembeli alitoa hesabu ya mfuko wa mbolea, mimi nilikuwa nashauri njia rahisi ya kumsaidia mkulima ni Serikali ku-*subsidise transportation cost* ili bei ya mfuko wa tumbaku ishuke chini. Ikishuka chini mkulima atapata bei nzuri. Ni kweli sasa hivi tunapata bei ya kati ya *US$ 1.8 per kilogram*, lakini wengi haifiki hiyo. Tuna soko ambalo liko China kubwa sana. Uchumi wa Zimbabwe uliyumba kwa kipindi kirefu, lakini sasa hivi umeanza kuwa mzuri kwa sababu ya tumbaku, wanauza kati ya dola 3.8 mpaka dola tano kwa kilo. Tazama tofauti ni mara tatu ya bei ya Tanzania, na tumbaku inayopatikana Zimbabwe haina tofauti na ile inayopatikana Tabora na Malawi ambao sasa hivi wameanza kutushinda, nchi ndogo ile inauza China. Tatizo la China ni moja kwamba, hawaruhusu watu binafsi kufanya biashara ya tumbaku, wanataka makubaliano yafanywe baina ya Serikali mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimejitihidi, nilikwenda kumwona Balozi. Namshukuru Waziri wa Biashara aliyepita, alinisaidia sana kunifanyia *appointment* nikamwona Balozi nikaongea naye, akaniambia tatizo lililopo, Serikali yenu haijachangamka. Ikichangamka, tutanunua tumbaku yenu hapa. Kinachotakiwa ni mkataba kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la wale wanunuzi wanaitwa *classifiers* ambao wanachambua ile tumbaku. Zamani pale Tabora tuna Chuo cha Tumbaku.

(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti ya Mheshimiwa Waziri.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kupata nafasi jioni hii ili kuchangia hoja iliyoletwa mezani kwetu. Awali ya yote na mimi naomba niungane na Watanzania wenzangu ili kufikisha majonzi yetu kwa msiba mkubwa uliolikumba Taifa letu. Naomba Mungu atupe roho ya subira ili tuweze kuyakabili na kuyashinda magumu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nitajikita katika mambo tisa, kama muda utaruhusu. Jambo la kwanza, naomba nijikite katika suala la kusambaza pembejeo kwa wakati, jambo ambalo hata mwaka 2011 katika bajeti nilipopata nafasi ya kuchangia nililiongelea kwa nguvu zangu zote, lakini cha kushanganza naona kama Wizara haijifunzi. Yale yaliyotokea mwaka 2011 na mwaka huu 2012 yatatokea, na wala sioni kama kuna habari ya kimkakati ambayo inafanywa na Wizara kuhakikisha yale makosa yaliyofanyika mwaka 2011 hatuyarudii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tuko mwezi wa Saba, ambacho ndiyo kipindi wananchi wanauza mazao yao na wanakuwa na fedha. Maana yake ni nini? Ni kwamba katika kipindi hiki, ukimpelekea mkulima pembejeo atakuwa na uwezo wa kununua

kwa sababu ana fedha mfukoni mwake. Lakini hili halitokei, tunaambiwa Serikali inajipanga, inahangaikia vocha mpaka kufika mwezi wa Pili ndipo ambapo pembejeo zinapelekwa. Hii maana yake nini? Ni kwamba unawalazimisha wakulima waingie katika kuchakachua pamoja na wale wachache wasiowatakia mema wananchi. Kwa hiyo, ninaisihi Serikali, hiki ndiyo kipindi muafaka kuhakikisha pembejeo zinapelekwa kwa wananchi, maana kipindi hiki wana visenti (fedha kiduchu) na wanaweza kununua. Tusije tukasubiri mpaka kipindi ambacho tuna uhakika mwananchi hana fedha ndiyo unampelekea pembejeo, atanunua kwa kutumia fedha ya wapi? Wizara bado haijachelewa, kama walikuwa wanasubiri habari ya bajeti, mimi naunga mkono bajeti ipite ili pembejeo ziwafikie wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba nichangie kuhusu suala la ushirika. Naona suala la ushirika Wizara inaliona kama ni *appendage*, hailipi nguvu na msukumo unaotakiwa. Ukienda kwenye Majimbo yetu, elimu ya ushirika haijafika. Kwa hiyo, siyo rahisi utarajie mwananchi ambaye hana elimu ya ushirika kuhusu faida na hasara zake, eti umwambie ajiunge kwenye vikundi. Anajiunga kwenye vikundi kwa dhana ipi? Ameota kutoka wapi? Naiomba Wizara ihakikishe kwamba elimu hii inawafikia wananchi ili wajue faida ya kujiunga na vikundi pamoja na *SACCOS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, naomba kwa uchungu kabisa niongelee hali ambayo Wizara imekuwa ikikatisha tamaa wananchi kupitia *SCCULT*. Hii

ikiwa Taasisi ya Serikali, imefanya mambo ambayo hatutarajii yafanywe na Taasisi ya Serikali. *SCCULT* imefika Jimboni kwangu ikiwa kama mdhamini, ikadhamini *SACCOS* ya Kata ya Ulumi kwa kukopa Shilingi milioni 30 na wakaambiwa kwamba lazima watoe amana ya Shilingi milioni 10. Wakatimiza masharti hayo, wamelipa deni lile pamoja na riba baada ya kuchelewesha, lakini cha ajabu mpaka ninavyoongea leo hii Shilingi milioni 10 ambayo *SACCOS* ilitoa kama dhamana, haijalipwa na ninaambiwa *SCCULT* haina fedha, haina fedha imepeleka wapi? Naomba wakati Mheshimiwa Waziri anakuja kuhitimisha atuambie sisi wananchi kwa *SACCOS* ya Ulumi ambao tuliishalipa deni na mimi siku zote huwa naongea kwamba cha mtu tunakiogopa na hivyo huwa tunalipa kwa wakati. Sasa tumeshalipa, ni wajibu wao waturudishie fedha yetu Shilingi milioni 10 ambayo naamini kwa njia njema kabisa itakuwa ni rahisi sisi kuweza kununua matrekta na kufanya shughuli nyingine za kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo naomba niliongelee ni kuhusiana na uzalishaji wa mbegu za mafuta. Ukienda kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, anakiri kiasi kingi cha fedha ambazo tunatumia kuagiza mafuta kutoka nje. Lakini pia na yeye mwenyewe anakiri kwamba tuna uwezo wa kuzalisha mbegu kwa maana ya alizeti na michikichi. Ukienda ukanda wa Ziwa Tanganyika, ukienda mpaka kwa watani zangu wa Kigoma, kule tuna migazi ya kutosha, lakini migazi ile ni ya kizamani na alikuwa anasema mmoja kwamba Malaysia wamekuja kuiga kwetu, lakini wao wamekwenda

kuifanyia kazi. Lakini sisi bado kilimo chetu cha migazi ni kile kilichopitwa na wakati na sioni hatua za makusudi ambazo zinachukuliwa na Wizara kuhakikisha kwamba zao hili linaendelezwa ili tuondokane na hii tabia ya kuagiza mafuta ambayo tunaweza tukazalisha ndani kwetu hapa na bila kuyachakachua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina uhakika na mafuta yanayoagizwa, yanaingizwa kama mali ghafi wanachakachua, hayafai na ndiyo maana Watanzania wanapatwa na magonjwa ya ajabu. Naomba Mheshimiwa Waziri, na juzi nilimsikia akisema kwamba ametambua kwamba kuna uzalishaji mkubwa sana ambayo unaweza ukaendelezwa wa mazao ya alizeti akiitaja Mikoa wa Singida, Katavi, Dodoma akasahau kwamba hata Rukwa ndiyo imemzaa Katavi. Kwa hiyo, kimazingira, hakuna tofauti. Naomba nayo aingize kwamba ni pamoja na wananchi wa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, naomba niongelee kuhusiana na uhakika wa soko la mazao. Mwaka 2011 tulisimama hapa tukapiga kelele sana kwamba mwananchi huyu ambaye tunamtelekeza, pembejeo hazipelekwi kwa wakati, lakini inafikia kipindi ambacho chakula kiko tayari, tunaanza kumwekea mipaka kwamba asitoe hiki, mara nchi sijui ina shida; naomba Serikali ijipange ili kipindi ambacho kunakuwa na bei nzuri, turuhusiwe kuuza na wao ni wajibu wao kuhakikisha kwamba wanatafuta chakula kwa ajili ya kuwalisha Watanzania. Siyo wajibu wa watu wa Rukwa kuhakikisha eti wao ndiyo wanailisha nchi. Ni ni wajibu

wa kuhakikisha kwamba wanapata soko zuri wauze ili waweze kusomesha watoto wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ameongelea juu ya upungufu wa sukari na ameainisha kwamba kuna utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunalima miwa kwa wingi na tunazalisha sukari ya kuwatosheleza Watanzania, ni jambo jema hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kule Jimboni kwangu ipo miwa mingi sana na nikitembelea kule huwa nauliza, sasa hii miwa wataendelea kuitafuna mpaka lini? Kumbe Wizara inakuja na tiba kwamba wataanzisha viwanda vidogo vidogo, na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda amesema kwamba wanapaswa kuanzisha viwanda vidogo vidogo. Tunachohitaji sisi watu wa Rukwa, tuletewe mbegu ambazo zinafaa kwa ajili ya kuzalisha sukari na tusiishe kutafuna miwa. Ukienda Tanga kwa watani zetu wanatengeneza pombe ya boha. Sisi hatutaki kutengeneza pombe, tunataka tuzalishe sukari ili tusaidie Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika kwa juhudi zinazofanywa na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa pamoja na uongozi mzima wa Mkoa wa Rukwa na Katavi, na nimesikia kwamba tuna ahadi ya kupata matrekta. Kwa hiyo, nasihi Halmashauri wahakikishie kwamba wanaweka utaratibu mzuri ili wananchi waweze kukopeshwa matrekta na sisi tuondokane na kilimo cha wanyama kazi, wameshachoka wanyama kazi, tunataka tutumie matrekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, nikiwa na matumaini makubwa sana na Waziri pamoja na Naibu Waziri kwamba tunakwenda kufanya mapinduzi ya kilimo. Nashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge. Sasa mchangiaji wetu ni Mheshimiwa Maria Hewa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mponda na atafuatiwa Mheshimiwa Said Nkumba.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda tu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba hadi tarehe ya leo anaendelea kunipa pumzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nami ningelipenda kutoa salamu za rambirambi kwa Watanzania wenzetu waliopata maafa ya kuzama kwa meli iliyokuwa ikitoka Dar es Salaam kwenda Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mmoja wa Wahanga wa tukio hilo ambalo lilinipata katika Ziwa Victoria. Kwa hiyo, ninayajua machungu ya kukaa majini na kuja kuokolewa kwa wale wanaopata bahati ya kuokolewa, na kwa wale basi wanaokosa nafasi hiyo ndiyo hivyo, tutasema Mwenyezi Mungu ilikuwa ni siku yake. Lakini ushauri wangu katika hili, basi wote tunaosafiri kwenye maji tujali kabisa kuwa na boya karibu au ikibidi ulivae saa zote ukiwa katika usafiri huo. Hilo ndilo lililoniponyesha mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusema yafuatayo kuhusu Wizara iliyowasilishwa leo. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kumteua Mheshimiwa Waziri aliyepo katika Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa sababu hata kipindi kilichopita alikuwa Naibu wa Wizara hii. Sasa katika hili, nadhani alionyesha ukomavu, uzoefu na akaaminika mpaka mwisho, amekabidhiwa Wizara, tunakupa hongera Mheshimiwa Waziri na tunampongeza Rais wetu. Ninaamini ulipokuwa kule mwanzoni uliweza na naamini sasa utaweza na mbele ya safari nadhani utaendelea kuweza. Tunakutakia kheri katika kazi hii ngumu. Ni Wizara kubwa na ninaamini itahitaji nguvu ya ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa narudi nyumbani, pamba. Mimi najiuliza, hivi wakulima tunataka kuwaona kama yatima vile ndani ya nchi hii? Tunataka kuwaona kama vile ni wakimbizi na wenyewe waishi kama wakimbizi katika nchi hii! Hivi kwa nini sasa hivi mkulima hana kabisa ile thamani ya kuthaminiwa kwamba ni mkulima na ndiyo tegemeo la nchi hii na ndiyo tumejaza misemo, “Kilimo ni Uti wa Mgongo”, “Siasa ni Kilimo”, leo tuna “Kilimo Kwanza”. Lakini wapi thamani ya wakulima inapoonekana kama mazao yake hayanunuliwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi katika Kanda ya Ziwa pamba ndiyo zao la biashara. Unamwambia mkulima huyu auze kilo Sh. 600/=, yeye ametumia zaidi ya Sh. 800/= na zaidi kwa eka moja, hivi anapolima kwa hasara unamtakia nini huyu mkulima? Hivi sasa pamba

wanayo humo majumbani. Hivi ni nini jamani? Kwa nini kuna kigugumizi katika Serikali hii? Kuna kigugumuzi gani kutuambia tuuze kwa bei ambayo; Serikali ingelikuwa inaona mbali ingekuwa imekwishaweka kinga tayari! Hivi hatujui tunapozungumza mambo ya mfumuko wa bei, Serikali haijui hili kwamba lolote linaweza likatokea, tukawa na kinga kwa wakulima hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani tunawakatisha tamaa, hela hiyo wanayoitafuta ndiyo waweze kula, ndiyo waweze kuvaa, ndiyo waweze kusomesha watoto, matokeo yake na bahati nzuri, *anyway,* mkulima huyu wa Kanda ya Ziwa anafuga, nako hawatengenezewi malambo, hana huduma ya maji, anaondoka kwenda kutafuta malisho mahali pengine na huko wanafukuzwa. Hivi jamani hebu tufike mahali kweli Serikali sasa iwaonee uchungu wakulima hawa. Anamwacha mwanamke huko na hiyo pamba huko anaiuza namna gani? Akiiuza kwa bei ya hasara, ili iweje? Anauza kwa hasara! Hebu tufike mahali tuthamini wakulima hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamesema mtutamkie kwa kweli, hebu leo najua Serikali ikiwepo na nyie mna vikao vyetu vya Baraza la Mawaziri, Waziri Mkuu yupo, wote mna vichwa vinavyotosha. Sasa Mheshimiwa Waziri wakati uki-*wind up* ulifikirie suala la pamba, ututamkie kitu ambacho wakulima wa pamba watasikia na kufarijika. Lakini nasema kweli tukubaliane, Mheshimiwa Waziri atutamkie Kanda ya Ziwa na kote wanakolima pamba, anatuambia nini? Tuendelee kukaa na pamba majumbani mpaka lini? Tufe na njaa,

tuanze kuomba kumbe tuna mamilioni ndani ya majumba? Tuwe ombaomba wakati tuna mamilioni ndani ya nyumba? Hapana. Kesho, Mheshimiwa Waziri ajiandae kutuambia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la mbolea. Mimi nashangaa nchi hii! Mnajua nchi nzima haina kiwanda cha kutengeneza mbolea kinachofanya kazi! Unachoka kabisa! Nchi hii haina viwanda vya kutengeneza mbolea, hata kile ambacho kinajitokeza, nasikia kiwanda cha mbolea cha Mijingu na chenyewe kinapigwa vita. Hivi vipi sisi? Tumerogwa? Kwa nini hakuna kabisa hata kiwanda kile ambacho kinajitokeza cha Minjingu cha Mbolea, nakuomba Mheshimiwa Waziri, hebu tembelea kiwanda hicho kama hujawahi kwenda kukitembelea, ukaone hiyo mbolea inafaa au haifai? Lakini hiyo mbolea mimi kwa kupata taarifa mbalimbali wamesema inafaa na ina uwezo wa kukaa ardhini mfululizo kwa miaka mitatu. Naomba hebu Mheshimiwa Waziri nenda uje utuambie katika kikao kijacho au uone na kuidhinisha kwamba hiyo mbolea inatosha. Kuna siri gani kwenye mbolea ya Minjingu? Haitakiwi kutumika hapa nchini? Mnataka kuagiza mbolea kutoka nje, ndiyo maana mbolea inakuja muda umekwishapita kwa sababu mpaka ikatoke nje ni *process* ndefu na *bureaucracy* ya nchi hii ilivyo kali kama nini? Naomba kupata jibu la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Maria Hewa. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mheshimiwa

Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda na Mheshimiwa Said Nkumba ajiandae, na Mheshimiwa Profesa Kahigi pia ajiandae.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Lakini kama kawaida, naomba na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu uzima wa afya na mimi angalau nitoe mchango wangu kwa Taifa na Jimbo langu kwa wale wapiga kura wangu wa Ulanga Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa matayarisho na mawasilisho ya bajeti yao ambayo imekuwa *so realistic* kutegemea na pato la Serikali. Wameeleza mwisho kwamba wameomba Shilingi bilioni 237.6 na katika hizo, Shilingi bilioni 67 ndizo zimetengwa katika mambo ya maendeleo. Lakini jema limejitokeza kwamba kuna wadau. Tanzania hatuishi kama Kisiwa, wadau wapo tayari kutoka Shilingi bilioni 52. Jamani tusiache, na wametoa katika mazingira ambayo wameridhia Uongozi wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na vilevile utawala uliokuwa bora. Nchi nyingine hawapati nafasi kama hizi. Kwa hiyo, hatuwezi tukasema kwa sababu hatutaki bajeti yetu itegemee watu wa nje, hiyo siyo busara. Kwa hiyo, kwa misingi hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri na mimi namuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita hasa kwa tatizo ambalo wengi wamelitamka, na sisi Mkoa wa Morogoro tunayo majibu. Wametamka hapa kwamba kila anayeongea mnazungumzia mfumuko wa bei na hasa wengi wamegusia bei ya vyakula na Watanzania wengi nawaona sasa hivi wamebadili sana *style* ya vyakula, wengi sana sasa hivi wanakula wali, wanakula ubwabwa, wanakula pilau, wanakula biriani, hata ndugu zangu akina Mheshimiwa Charles Mwijage, ndugu zangu wa Ziwa kule akina Mheshimiwa Batenga sasa hivi ndizi wameshaanza kuziacha. Wanakula wali. Wajukuu zangu wa Kusini kule walikuwa wanakula ugali wa mhogo, Mheshimiwa Anna Abdallah na mjukuu wangu Mheshimiwa George Mkuchika sasa hivi wameacha, wanakula ubwabwa. Kwa hiyo, jamani, wala siyo mzaha, hilo ndilo hitaji kubwa la chakula kwa Watanzania. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama nilivyosema, tayari majibu yapo. Morogoro tumejaliwa na Mwenyezi Mungu, tuna mito zaidi ya 55, mito mikubwa na mito midogo yote inatiririka, inaelekea baharini. Sasa maji yale ni vyema tuyakusanye ili tuyatumie. Kwa hiyo, angalizo langu kwa Serikali, nimeona bajeti hii, kweli nakuomba tukimaliza Bunge hili, hapa tuongazane na Mheshimiwa Waziri, twende Morogoro tuanze pale Ofisi ya Mkoa. Mkuu wa Mkoa ninampongeza sana ndugu yangu Joel Bendera alikwishaliona hili na tayari amekwishakaa na watendaji wake, wameweka mikakati. Kwa hiyo, tunahitaji Serikali iwaunge mkono hawa Watendaji wa Mkoa wa Morogoro ili waweze

kulisha Taifa hili ambapo chakula kikuu sasa hivi ni wali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye Jimbo. Sisi mmetutengea miaka mingi, tunaona mnazungumzia skimu kama nne hivi, lakini naona zimekuwa hadithi hadi leo, hakuna skimu ambayo imekamilika. Sana sana naona kuna skimu pale ya Lupilo, lakini sana sana, ipo tu imeishia kwenye uchambuzi yakinifu sijui mpaka lini, huo uchambuzi yakinifu utaendelea? Bado kuna skimu ya Minepa, ya Itete, na Misegeze. Lakini skimu hizi kama zikikamilika na ikitengenezwa mifereji, hakika ninawahakikisheni Watanzania suala la punje itakuwa siyo tatizo. Pamoja na Serikali imetuahidi inaweka mikakati, lakini ni ya muda tu kwamba wataagiza mchele wa kutosha lakini sijui kama kweli inaweza ikatoa suluhisho la hili tatizo la chakula katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hapo hapo kwenye mpunga, tuna tatizo ambalo kilimo chetu bado mbegu tunazotumia za mpunga tunabahatisha. Mheshimiwa Waziri ukiangalia kitabu chako cha hotuba kiambatanisho Na. 8 umeeleza mbegu lakini hujaeleza mbegu ambazo ni za msingi zaidi za chakula kwa Watanzania, mbegu ya mpunga hakuna. Miaka mingi nimeshuhudia mimi mwenyewe, tafiti mbalimbali zimefanywa na Vyuo pamoja na *SUA* toka ile miaka 1970, miaka ya 1980 hizo tafiti naona zimeishia tu. Aidha, kwenye *publications,* kwenye *international journals,* aidha, zimeishia watu wapate udaktari na uprofesa.

Sasa nauliza Serikali, jamani hawa wataalamu wetu wa utafiti wa kilimo watatusaidiaje sisi wakulima wa Ulanga kupata mbegu zilizokuwa bora? Maana tunabahatisha kila mwaka na bahati mbaya kila mwaka tunapopanda zao lile linazidi kuwa finyu zaidi. Kwa hiyo, baadaye tutaishia na tutapata punje ambayo badala ya kupika kilo moja kwa kaya, utabidi upike mpaka kilo tatu na uzalishaji wenyewe umezidi kuwa duni. Huko nyuma miaka ile ya 1970, 1980 kwenye bonde la Mto Kilombero tulikuwa na mbegu saba. Tulikuwa na mbegu za mpunga kama zifuatazo: Kula Bibi na Bwana, Kaniki na nyinginezo, lakini hizi zote zimepotea na ambazo zilikuwa zinatusaidia kipindi cha uhaba wa mvua angalau mbegu nyingine kama dunduli, zilikuwa zinachukua miezi miwili tu unakuja kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la Kilimo Kwanza, mimi huwa najiuliza na nawauliza hata Wabunge wenzangu, mnaelewa? Kwa hiyo, bado changamoto kubwa iliyoko kwenye hiyo, aidha, mpango, maana wengine wanaita sera, wengine wanaita mpango, wengine mkakati, yaani kuna majina mengi sana kiashiria tosha kwamba watu hatujafahamu nini Kilimo Kwanza. Lakini kila Mkoa kuna magari ambayo yanawezesha kuelimisha watu, yale magari ambayo yana mitambo ya kuonyesha *video* yako wapi? Yatumike hayo! Maana miaka ya zamani tulikuwa tunaonyesha sinema hizi za *factual film* kila mwezi wanakuja kila kijiji. Naishauri Serikali watumie nafasi hiyo, waelimishe wananchi kuhusu hicho Kilimo Kwanza. Maana watu kwanza lazima waelewe ni nini hicho kitu? Yeye kama yeye ana mchango gani katika

Kilimo Kwanza? Maana ukimwuliza mwananchi mwingine, Kilimo Kwanza yeye anawaza ni trekta tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie, tuna tatizo katika Wilaya ya Ulanga na Wilaya ya Kilombero katika zao letu la mpunga, tunashambuliwa mara kwa mara na sasa hivi tuna mwaka wa kumi, tunashambuliwa, kule wenyeji tunaita “Kimnyanga”, lakini huu ugonjwa kwa kitaalamu unaitwa *Rice Yellow Motto* ni ugonjwa wa virusi. Lakini sasa nauliza watafiti, hadi lini? Ni mwaka wa kumi na kadri mwaka unavyokwenda, mazao yanazidi kupungua. Sasa hivi yanaathiri kiasi mpaka theluthi moja ya mazao katika shamba yanashambuliwa na hivi virusi. Sasa Serikali na uhaba wa huo mpunga unaendelea, na bado hatuna majibu, mwaka wa kumi huo ugonjwa wa virusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la pembejeo. Wenzangu wamechangia na haitofautiani kwenye Jimbo langu na hususan Mkoa mzima wa Morogoro. Tuna uhaba mkubwa sana wa pembejeo, na bahati mbaya pembejeo hizi zinakuja wakati hazihitajiki. Unatuletea mbolea mwezi Aprili!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa kutetea watu wa Kilombero kwa mpunga. Sasa namwita Mheshimiwa Saidi Nkumba na kama muda utaruhusu, Profesa Kahigi jiandae.

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru wote kuanzia Mheshimiwa Waziri, Mwenyekiti wa Kamati, lakini vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Msemaji wa Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo yote yanayosemwa na Wapinzani ni mabaya. Napenda nichukue fursa hii kwa kweli kumshukuru sana Mama Sukum kwa namna alivyowasilisha, lakini namna alivyoitambulisha familia yake ingawa ilikuwa familia nusu, namshukuru sana na namwomba wakati mwingine anapokuja, basi pamoja na watoto, na baba naye awepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na lile alilomalizia Mama Hewa, suala la mbolea ya Minjingu. Nilikuwa naomba sana Serikali iangalie uwezekano wa kusaidia kiwanda kile. *DAP* tunayoagiza nje inauzwa kwa wakulima Sh. 80,000/=, lakini mbolea hiyo hiyo ya Minjingu ambayo wataalam wetu wanatuambia kwamba inafanana kabisa na *DAP*, inauzwa mifuko miwili Sh. 64,000/=. Mimi nasema ni busara gani zinazotumika za kuendelea kuleta mbolea kutoka nje wakati kuna viwanda vyetu nchini vinaweza vikazalisha vikaweza kusambaza mbolea kwa wakulima wetu? Naiomba sana Serikali iangalie jambo hili kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni suala la mtikisiko wa mazao makuu ya biashara pamoja na mazao ya chakula. Hapa yamezungumzwa mambo ya pamba, mwaka 2011 tulikuwa na tatizo kubwa sana la tumbaku, kuna korosho ziko kule Kusini mpaka sasa hazijauzwa kwa sababu ya mtikisiko wa bei. Naishauri

Serikali kwamba mazao haya kwa sababu ndiyo nguzo kubwa ya uchumi, ni vizuri Serikali ikaamua makusudi kuwa na mifuko ya kuhakikisha kwamba panapotokea mitikisiko, basi mifuko hii isaidie kuwaweka vizuri wakulima, wasikate tamaa ya kuendelea kulima mazao hayo. Lakini tukiendelea na utaratibu huu, tutakata tamaa. Yako mengi yanayojitokeza huko, wenzangu wamezungumza masuala ya Bima ya Mazao, sijui kama Serikali inaona jambo hili ni muhimu. Lakini nasema mambo haya ni muhimu kwa sababu matatizo ya wakulima yako mengi, yako matatizo ya kutokuwa na mvua wakati mwingine, yako matatizo ya mvua za mawe, wakulima wanakuwa wamekwishakopa, hawawezi kurejesha. Serikali lazima ichukue hatua za kuwasaidia wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la ubora wa mbolea zinazoagizwa kutoka nje. Yamekuwepo malalamiko mengi ya wakulima kwamba baadhi ya mbolea zinazoagizwa kutoka nje hazina viwango bora. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba *TBS* wamekwenda baadhi ya maeneo, wamethibitisha na tumeanzisha chombo kinaitwa *TFRA*, chombo cha kudhibiti ubora wa mbolea. Lakini cha ajabu, badala ya kukiwezesha chombo hiki kiweze kufanya kazi zake vizuri, Serikali imewatengea fedha Sh. 122,000,000/= huu ni mchezo, tujitahidi sana tuwezeshe ili tuweze kuwa na ubora wa mbolea ambazo zinaweza zikawasaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la uanzishwaji wa viwanda vya kusindika tumbaku. Viko viwanda viwili vya kusindika tumbaku pale Morogoro. Mimi sina ugomvi navyo. Lakini nilikuwa naomba hii

mipango ambayo imeelezwa kwenye kitabu chenu hapa ikamilike. Suala la ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea kule Mbeya na suala la ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea kule Tabora, viwanda hivi vitasaidia kukuza uchumi wa wananchi katika maeneo hayo. Lakini zitapunguzwa vile vile gharama ambazo wakulima wa tumbaku nchini wanazipata kusafirisha mbolea, kusafirisha tumbaku yao kutoka katika maeneo ya Mikoani kupeleka tumbaku yao kule Morogoro. Gharama hizi wanabeba wakulima, jambo hili siyo haki. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba sana Serikali iongeze kasi katika kuendelea kulitafutia ufumbuzi jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la kilimo cha alizeti. Nawapongeza sana wakulima wa alizeti Tanzania katika Mikoa yote hapa nchini. Lakini vilevile alizeti hii tunapoizalisha, tunapokamua mafuta, wataalamu wetu walituambia haya ndiyo mafuta peke yake ambayo kwa kweli ni mafuta ambayo hayana hitilafu yoyote katika mwili wa binadamu.

Kwa hiyo, nilikuwa naiomba sana Serikali, pamoja na mambo yote, tumeweka utaratibu mzuri wa kuendelea kuhakikisha kwamba zao hili linakuzwa. Lakini naiomba na natoa ushauri kwamba ipo minong'ono inayosema kwamba ipo *crude oil* ya alizeti ambayo inaingizwa nchini kinyemela. Ikishaingizwa nchini inaleta kushusha soko kwa wakulima wale ambao wamezalisha vizuri alizeti hapa nchini, halafu wanashindwa kuwa na bei nzuri na mafuta ya humu nchini yanashindwa kupata bei nzuri. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, lakini vilevile Wizara ya Fedha na Uchumi na

Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika washirikiane kuhakikisha kwamba jambo hili wanalipa umuhimu wa kuendelea kulitatua hili wakulima wetu wa alizeti waweze kupata mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie na mambo mawili ya mwisho. La kwanza la wakulima wa tumbaku. Ndugu zangu mwaka huu hali ya tumbaku siyo mbaya sana kama mwaka wa 2011. Lakini nilikuwa naiomba sana Serikali, katika jambo hili, tumesema utaratibu wa sasa tunayapa mabenki yafanye biashara ya kukopesha, lakini na ushirika vilevile unaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umekuwepo utaratibu wa mabenki wakishirikiana na baadhi ya viongozi wa ushirika kuwabebesha mzigo mkubwa sana wa madeni wakulima kwa kuwakopesha vitu mbalimbali kama pikipiki, magari na kadhalika, halafu baada ya hapo, mkulima anashindwa kupata fedha zake na baadaye sasa matumizi yote yanakuwa yameishia kwenye madeni haya. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ijitahidi sana kuhakikisha wakulima wanawekwa vizuri ili kuhakikisha kwamba wanaendelea na jitihada za kutumia hizo fedha wanazozipata katika misingi ile ambayo tumeikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, wateuzi wa tumbaku. Naiomba sana Serikali, Chuo kile cha Tumbi kitumike katika kuhakikisha kwamba kinaandaa wataalamu wa kutosha. Sasa hivi hatuna tena wataalamu wengi, na hatuwezi kuajiri tena kwa sababu kila tukiamua kuajiri Bodi ya Tumbaku

tunaambiwa kwamba idadi tunayopewa haikidhi viwango hivyo ambavyo tunavikusudia. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba sana Serikali tujitahidi sana kule kwenye Chuo cha Tumbi tujitahidi kuhakikisha kwamba tunawapeleka vijana wetu, wapate mafunzo waweze kusambazwa ili waweze kusaidia katika kuhakikisha kwamba tunalinda zao hili la tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na unyenyekevu mkubwa naomba tena kile Kiwanda cha Songea ambacho kimekwama kwa muda mrefu kihakikishe kwamba kinafika mahali kinapata fedha ili kiweze kufanya kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Moja kwa moja, naomba nianze kwa kuungana na wenzangu wanaotoka Kanda ya Ziwa kwa kuiomba Serikali ifikirie sana suala hili la pamba. Kwa sababu kama mliweza kuyasaidia haya Makampuni, mliyoyapatia fedha nyingi sana kwa kipindi kilichopita walipokuwa wamepata hasara, kigugumizi kiko wapi? Kwa nini mnashindwa kuwasaidia wakulima? Kwa nini msitoe angalau ruzuku kidogo bei ikapanda badala ya hii Sh. 660/= kwa kilo?

Kwa hiyo naungana nao. Siwezi kuzungumza zaidi kuhusu hilo, isipokuwa tu labda nitazungumzia jambo moja ambalo linahusu kilimo cha mkataba ambalo, nakumbuka wakati ule tukiwa Ukumbi wa Msekwa

tulikubaliana kwamba kilimo cha mkataba kwanza kiandikiwe sheria, na sheria iletwe Bungeni. Waheshimiwa Wabunge waijadili, halafu ndipo kilimo hicho kianze na kiendelee. Sasa hiyo sheria haijaletwa, na mimi nashangaa hiyo sheria inayohusu kilimo cha mkataba italetwa lini hapa Bungeni? Kwa sababu hiyo sheria ndiyo ingeweza kuhakikisha kwamba, inamlinda huyo mkulima na bila ya kuwepo sheria, mkulima daima ataendelea kuumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nijielekeze kwenye Jimbo langu la Bukombe. Wananchi wa Bukombe wamenituma niongelee mambo matatu ambayo yanawatatiza sana hasa kuhusiana na azma ya Serikali kuendeleza Kilimo Kwanza. La kwanza kabisa ni pembejeo na jinsi ilivyogawiwa mwaka 2011/2012. Tukianza na mbegu ya mahindi, nina takwimu hapa. Mbegu za mahindi kilo zilizohitajika zilikuwa 7,200 kwa Kata moja tu ya Igulwa. Halmashauri ya Bukombe ina Kata 29. Kwa Kata moja ya Igulwa kilo zilizohitajika ni 7,200, lakini kilo ambazo ziligawiwa na Wakala ni 700 tu. Pungufu ya kilo ni 6,500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbolea ya kupandia. Kata moja hiyo ya Igulwa ilipangiwa kupata mifuko 1,440, lakini Wakala aliyekuwa amepangiwa kwenye Kata hiyo alileta mifuko 10 tu. Mifuko iliyopungua ni 1,430. Mbolea ya kukuzia, Kata hiyo moja tu ilikuwa imepangiwa kupata mifuko 1,440, lakini mifuko iliyoletwa kwa Kata nzima ni sita (6) tu. Mifuko ambayo haikufika pale kwenye Kata ni 1,434. Cha ajabu na cha kushangaza na inawezekana kabisa mastaajabu kama haya yanatokea tu hapa Tanzania,

kwa sababu vocha zote kwa pembejeo zote zilizopangwa zilisainiwa na Watendaji wa Vijiji kwa kulazimishwa na Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanabukombe wanauliza: Serikali itachukua hatua gani kwa watu waliochakachua pembejeo katika Wilaya ya Bukombe? Kwa sababu watu hao wanafahamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wengi sana katika maeneo ambayo mimi nilikuwa nafika kukagua shughuli walikuwa wanasema kwamba hawakupata pembejeo, hawakupata chochote. Sasa swali ambalo Wanabukombe wamenituma niwaulize ni kwamba Serikali itachukua hatua gani? Kwa sababu watu wamejitajirisha sana. Mahesabu mengi sana haya! Mahesabu niliyoyatoa hapa ni kwa ajili ya Kata moja tu, lakini kuna Kata 29 katika Halmashauri ya Bukombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ambalo nimetumwa ni kwamba Bukombe, sasa hivi kuna njaa kali sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa kwenye ziara yake Kanda ya Ziwa tulimwambia hili, na nasisitiza leo kwamba Wana Bukombe wanaomba msaada wa chakula cha haraka.

La mwisho, linahusu ushirika. Kwa maoni yangu ni kwamba, Wizara hii ina mambo mengi sana. Kuna kilimo na kilimo ni shughuli nzito sana. Kuna chakula, pia ni shughuli nzito sana. Sasa kule Bukombe ushirika kama umeshakwishakufa, kuna Vyama vya Ushirika vilivyoandikishwa 284, lakini vyama hivi haviko hai. Hakuna Mikutano na Maafisa Ushirika hawajitahidi hata

kuitisha Mikutano na wala hawajitahidi kuhakikisha kwamba Katiba za Vyama hivi zinafuatwa. Serikali inaombwa iliangalie hili. Wanaushirika wa Vyama hivi vya Ushirika wananyonywa sana na Viongozi wa Vyama hivi na washiriki wakubwa katika huo unyonyaji, ni Maafisa wa Ushirika. Naomba Serikali iliangalie hili na hayo ni machache ambayo nimetumwa na wananchi wa Bukombe, yapo mengi, lakini mengine nitaandika kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Huyu ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo. Tangazo la kwanza, wanamichezo wote wanatangaziwa kwamba michezo ya mpira wa miguu na *netball* iliyokuwa ichezwe kesho Jumamosi kati ya *CRDB* na Bunge sasa haitachezwa. Pia matembezi *(jogging)* ya *Muungano Sports Club* na Waheshimiwa Wabunge yaliyokuwa yafanywe kesho Jumamosi asubuhi hayatafanyika. Hii ni kwa sababu ya maombolezo ya vifo vya wenzetu waliofariki kwa ajili ya kuzama kwa meli ya *MV. Skagit* iliyotokea huko Chumbe karibu na Zanzibar. Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema Peponi. Amina.

Tangazo lingine la pili, Waheshimiwa Wabunge wote ambao sio Mawaziri, kesho watagawiwa dodoso ambalo limeandaliwa na Wizara ya Habari, Vijana na Michezo ambalo linalenga kupata maoni yao kuhusu mikakati ya maendeleo ya vijana katika maeneo yao

na Taifa kwa ujumla. Tunaomba Waheshimiwa wajaze dodoso hilo na wawasilishe kwa Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge kupitia Wahudumu wa Ukumbi huu.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 28 (8) inasema; “Endapo Spika atakuwa amepokea taarifa ya Mbunge yeyote anayetaka kutoa maelezo binafsi, basi Spika hataliahirisha Bunge bali ataongeza muda usiozidi dakika 30 bila kulihoji Bunge ili kutoa nafasi kwa Mbunge huyo aweze kutoa maelezo yake isipokuwa kwamba, maelezo hayo sharti yawe yameandikwa na kuwasilishwa kwa Spika angalau siku moja kabla hayajatolewa, na Mbunge anayehusika atalazimika kuyasoma kama yalivyowasilishwa.” Sasa mimi kama meza na Mheshimiwa Spika amesharuhusu, kwa sasa namwita Mheshimiwa Mpina aje atoe taarifa yako.

MAELEZO BINAFSI YA MBUNGE

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kwa mujibu wa kifungu cha 28 (8) ambacho umemaliza kukisoma, naomba kutoa maelezo binafsi ya Wabunge kutoka katika Mikoa inayolima zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimu wa pamba mwaka huu ulifunguliwa toka tarehe 2/7/2012 lakini zoezi la ununuzi limekuwa likisuasua sana kutokana na changamoto nyingi zinazolikabili zao la pamba, kwani wakulima hawaridhishwi kabisa na bei ya Sh. 660/= kwa kilo na huku kwa upande mwingine baadhi ya wanunuzi wanaiona bei ya Sh. 660/= ni kubwa na hivyo ni hasara kwao. Wakulima wameamua kuendelea

kushikilia pamba yao kutokana na gharama kubwa za kilimo; kama gharama za kuandaa shamba, gharama za kununua mbegu, kulima, kupanda, palizi mara nne, kupiga dawa mara nne, kuvuna na kusafirisha kupeleka nyumbani na baadaye sokoni, gharama za kupakia na kushusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukikokotoa gharama zote, wakulima wanajikuta wanapata hasara. Inakadiriwa kuwa ekari moja hutoa kilo 300 tu na kuzalisha kilo moja ya pamba kwa sasa ni zaidi ya Sh. 990/=. Gharama za kutunza ekari moja ya pamba ni Sh. 285,000/= wakati mapato yanayotarajiwa katika bei ya Sh. 660/= kwa kilo ni Sh. 198,800/= tu. Hivyo kumfanya mkulima apate hasara ya Sh. 86,200/= kwa ekari moja. Hasara hii ni kubwa, inadidimiza wakulima, inachochea umasikini, wanashindwa kusomesha watoto, wanashindwa kulipa madeni ya pembejeo, wanashindwa kununua chakula cha kujikimu na kujipatia mahitaji mengine muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeainisha mchanganuo wa gharama hizo za ekari moja nyuma ya taarifa hii. Ikiwa jumla ya hekta 560,000 zimelimwa mwaka huu na kukadiriwa kuzalisha tani 300,000 mpaka 350,000 za pamba mbegu wakati jumla ya watu milioni 16 wanategemea zao hili katika Wilaya 42, yaani Mkoa wa Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Tabora, Mara, Morogoro, Singida, Tanga na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Soko la Dunia, mtiririko wa bei ya pamba miaka yote imekuwa ikibadilika kiasi kwamba kila robo ya mwaka ina bei

yake na mbaya zaidi kila wakulima wanapotaka kuuza pamba yao, bei hushuka na msimu unapoelekea mwisho, bei hupanda. Mfano, mwaka 2010 Januari – Machi bei ya pamba ilikuwa senti 71 za Kimarekani. Lakini msimu ulipotaka tu kuanza bei ilishuka na kufikia Senti 69. Lakini msimu ulipomalizika, bei ilipanda na kufikia Senti 82 katika miezi ya Septemba na Desemba.

Mwaka 2011 miezi ya Januari na Machi, bei ilifikia US$ 2, lakini msimuwa miezi ya Aprili na Juni, bei ilishuka na kufika dola 1.7, na mwaka 2012 miezi ya Januari bei ya pamba ilikuwa ni senti 90. Lakini msimu ulipoanza miezi ya Aprili na Juni, bei imeshuka na kufikia senti 62. Kwa mtiririko huu wa bei, Serikali ina wajibu wa kuwakinga wananchi wake kwa madhara yanayotokana na kuyumba kwa bei ya soko la dunia. Masuala iliyoahidi kuyasimamia, ikumbuke kuwa iliwaingiza wananchi katika mkataba na kukopeshwa madawa kwa gharama kubwa wakiahidiwa kuwa bei ya pamba itakuwa nzuri kiasi cha kufikia Sh. 1,000/= kwa kilo. Hata hivyo, hali imekuwa kinyume chake, kwani anguko la mwaka huu ni kubwa kuliko miaka yote na kwamba bei ya pamba ya Sh. 660/= wakulima wengine wataishia kulipa madeni ya pembejeo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani kote Serikali makini zimekuwa zikiwakinga wakulima wake na majanga, yaani *force majeure* kama mafuriko, ukame na bei, hususan katika mazao yanayotegemea Soko la Dunia. Serikali hizo zinafanya hivyo kwa kuwakatia Bima ili kufidia hasara pindi yanapojitokeza majanga. Hata hivyo, hali imekuwa tofauti hapa nchini, kwani Serikali

imewageuzia kisogo wakulima wake na kuendelea kuwapamba kwa nyimbo za Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba mwaka 2008/2009 mabenki na wafanyabiashara waliweza kufidiwa na Serikali trilioni 1.7/= katika kipindi cha mtikisiko wa uchumi. Huku wakulima masikini wakiambulia kiasi kidogo tu cha fidia, kiasi kisichozidi Shilingi bilioni 20 na wengine kudhulumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu sasa Serikali imeshindwa kupata suluhisho la kudumu la bei ya zao la pamba kutokana na kutegema soko la nje ambalo ni la kinyonyaji, kwani viwanda hapa nchini kuchukua asilimia 30 tu ya pamba iliyozalishwa hapa nchini na asilimia 70 hutegemea soko la nje. Hii inasababishwa na Serikali kushindwa kuimarisha na kuanzisha viwanda vya nyuzi ili kuongeza thamani ya pamba. Toka mwaka 2005 Serikali iliahidi kujenga kiwanda cha nguo Mkoani Shinyanga na cha nyuzi Mkoani Simiyu, lakini hadi sasa hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati gharama ya kujenga kiwanda kipya inakadiriwa kwamba ni Dola milioni 38 ambazo ni Shilingi bilioni 60 tu, nadhani kinachokosekana hapa ni nia ya dhati tu, kwani Serikali ingeweza kujenga viwanda na kisha kuuza hisa zake kwa Makampuni na watu binafsi au kudhamini Makampuni na watu binafsi ili waweze kujenga viwanda na kuviendesha hususan kwa wafanyabiashara wa ndani na Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha ubinafsishaji, Serikali iliuza Viwanda vya Nguo vya *Mwatex, Mutex, Sunguratex*, Urafiki na *Manonga Ginnery* kwa bei ya kutupa, tena kwa watu wasio na nia njema na Taifa hili. Viwanda hivi kwa sasa havianyi kazi na vingi vikiwa vimebadilishwa matumizi na kuwa maegesho ya magari na maghala ya bidhaa mbalimbali. Utafiti wa kitakwimu unaonyesha kuwa utoroshaji wa fedha nje kipindi cha ubinafsishaji uliongezeka mara dufu ikidhihirisha wazi kuwa mikataba mingi ilitawaliwa na rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hali ya ununuzi na uuzaji wa pamba ni tete, Serikali iingilie kati suala hili kwa dharura na hivyo tunashauri na kupendekeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango ya muda mfupi na wa dharura sana, kwanza, Serikali ifidie kiasi cha Sh. 340/= ili kuifanya bei ya pamba kufikia Sh. 1,000/= na mkulima anunuliwe pamba yake kwa Sh. 1,000/= kuanzia sasa, ambayo kwa tani 300 itagharibu Shilingi bilioni 102.

Pili, Serikali kupitia Benki Kuu iweke kinga ya bei ya pamba ya Sh. 340/= kwa kilo ili kuwawezesha wanunuzi kununua pamba kwa bei ya Sh. 1,000/=. *Ginners* wafanye kazi ya ku-gin halafu marobota yahifadhiwe kwenye maghala hadi kipindi bei itakapotengemaa.

Tatu, Serikali iwaruhusu wanunuzi wa pamba wanunue pamba kwa bei ya Sh. 1,000/= kwa kilo halafu kupitia Bodi ya Pamba iyanunue marobota yote

na kuhifadhi katika maghala ili baadaye bei ikipanda iyauze. Serikali inaweza ikatumia akiba zake, yaani *reserves* zilizopo Benki Kuu, lakini pia kwa kutumia mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama vile *NSSF, PPF, LAPF, PSPF* na kadhalika.

Nne, kwa kuwa maeneo ya wakulima wa pamba yameathirika sana na ukame na hivyo kupelekea upungufu mkubwa wa chakula, Serikali ipeleke chakula cha msaada na kwa wale wenye uwezo iwauzie kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapendekezo ya muda wakati na mrefu; kwanza, Serikali iimarishe Vyama vya Ushirika nchini kama vile *SHIRECU, MARACOP NA NYANZA*. Kwa kuvihakikishia upatikanaji wa mtaji wa kutosha, waweke wenye riba nafuu na kuimarisha *ginneries* kwa kuzifanyia matengenezo makubwa, kwani ni vya zamani toka miaka 1970 na kwamba viweze kuwekeza kwenye viwanda vya kuchambua na kutengeneza nyuzi na nguo.

Pili, Serikali itafute masoko ya uhakika ya zao la pamba na kisha iwaunganishe wafanyabiashara wake wa ndani, yaani *ginners* kuliko kuendelea kutegemea wanunuzi wadogo wadogo kutoka nchi za China na India. Mabalozi wetu waliotanda kila pembe ya dunia, Mawaziri wa Viwanda na Kilimo wanaweza kuifanya kazi hii vizuri sana na kwa ufasaha.

Tatu, Serikali ijenge viwanda vipya vya kisasa vya nyuzi na nguo, iachane na mawazo kuwa eti ujenzi wa viwanda ni wa sekta binafsi pekee. Pia inaweza

kuwekeza kwa ubia na watu binafsi, yaani *PPP*. Aidha, Serikali inaweza kuwadhamini wanunuzi kupitia Benki Kuu na kutumia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuhakikisha kuwa viwanda vinajengwa vya kutosha na hakuna pamba inayouzwa ikiwa ghafi nje ya nchi.

Nne, Serikali itaifishe viwanda vyote vilivyobinafsishwa vya nyuzi na nguo ambavyo vimebadilishwa matumizi na havijaendelezwa kama *Mwatex, Mutex, Sunguratex*, Urafiki, *Kilitex* na *Manonga Ginnery*.

Tano, Serikali itengeneze mazingira mazuri kwa wafanyabiashara Watanzania waweze kutumia kikamilifu masoko ya nguo ili kuwezesha kuuza nyuzi na nguo katika masoko hayo ambayo kwa sasa hatufanyi vizuri.

Sita, Serikali itekeleze kwa vitendo dhamira yake ya kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo yaani *(TADB)* na kuipatia mtaji wa Shilingi bilioni 500 kwa kuanzia na kuiongezea mtaji Benki ya Rasilimali *(TIB)* wa Shilingi bilioni 500. Hivi sasa Serikali haifanyi vizuri kwa kuwa imekuwa ikitenga fedha pungufu kuliko ilivyokubalika katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano. Serikali isiishie hapo tu, bali izitafutie mtaji benki hizi toka Taasisi mbalimbali za fedha duniani ili ziwe na mitaji ya kutosha. Hii itawezesha wakulima na wafanyabiashara kupata kwa urahisi mikopo yenye masharti na rafiki kwa mkopaji kama riba nafuu na muda mrefu wa kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha kwa niaba ya Wabunge wote wanaotoka kwenye Mikoa inayolima pamba nchini. Ni mimi Luhaga Joelson Mpina. Mbunge wa Kisesa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mpina na tunaishauri Serikali ifuatilie kwa makini mambo haya.

Mimi nilikutana na Balozi wa Japan na nimekwenda Japan, Japan, wako tayari kabisa kuwekeza kiwanda cha nguo Shinyanga, kutengeneza mataulo kwa kutumia pamba ya hapa nchini na tatizo inavyoonekana ni Bodi. Kwa hiyo, mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri jaribuni kuli-s*olve* hili jambo kusaidia wananchi. Kama tatizo ni Bodi, chukueni maamuzi sahihi ili mambo hayo yamalizike.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.55 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumamosi,
Tarehe 21 Julai, 2012, Saa Tatu Asubuhi)